

Bismillahi Ar-Rahmaan Ar-Raheem

NIDHAMU YA UCHUMI KATIKA UISLAMU

Taqiudin An-Nabhani

Chapa ya tano, 1418 Hijri (1998 C.E)

Kimechapishwa na Dar Al-Umma ya kuchapisha, kueneza na kugawanya,
Beirut

وَابْتَغِ فِيمَا آتَاكَ اللَّهُ الدَّارَ
الْآخِرَةَ وَلَا تَنْسَ نَصِيبَكَ
مِنْ الدُّنْيَا وَأَحْسِنْ كَمَا
أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ وَلَا تَبْغِ
الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ إِنَّ
اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ

“Na utafute kwa yale aliyokupa Allah, makazi mazuri ya akhera, wala usisahau sehemu yako duniani, na ufanye wema kama Allah alivyo kufanyia wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi.” (Al-Qasas 77)

UTANGULIZI

Kitabu hichi cha nidhamu ya uchumi katika Uislamu ni utajiri wa fikra ya kiislamu yenyeye thamani kubwa, na mfano wake ni mchache. Ni kitabu cha kwanza kinachoweka wazi uhakika wa nidhamu ya uchumi katika Uislamu katika wakati huu, uwazi wa kifafanuzi ulio mweupe.

Kinabainisha mtazamo wa Uislamu kwa uchumi na lengo lake, vipi mali humiliwi, kuzidishwa kwake, vipi hutumiwa na kutasarruf nayo, vipi kugawanya utajiri kwa watu wa mujtama, na vipi kutengeneza mizani ndani yake.

Kinabainisha sampuli za umilikaji kutoka umilikaji wa kibinafsi, umilikaji wa umma na umilikaji wa serikali, mali inayostahiki Bait ul-Mal ya Waislamu na maeneo ya masrifu yake.

Kinabainisha hukmu za ardhi, ushri na kharaji, na yanayowajibika juu yake katika ushri au kharaj, vipi kutumiwa kwake, kuhuishwa kwake, kutolewa kama zawadi na serikali na kugura kwake kutoka milki ya mmoja hadi mwengine.

Kinafafanua pesa (naqd) na sampuli zake, na yanayopita ndani yake katika riba, kubadilishwa na yanayowajibika ndani yake katika zakaa.

Mwisho wa mzunguko (mutaf) wake ni biashara za kigeni na hukmu zake. Chimbuko la pekee la kuchukua hukmu hizi ni Kitabu cha Allah na Sunna za Mtume wake na yalioelekezwa nazo katika qiyas na Ijma as-Sahaba .Halikuchukuliwa chimbuko lengine lolote wakati wa kuchukua hukmu hizi za kiuchumi.

Kitabu kimetanguliza uhakika wa nidhamu ya uchumi ya kirasilimali, na nidhamu ya uchumi ya kiujamaa inayotokamana nayo ukomunisti, ikazijadili na kubainisha ufisadi woa na kugongana kwao na hukmu za nidhamu ya uchumi katika Uislamu.

Kimeregelewa kitabu kabla ya kuichapisha chapa mpya, na yakafanywa ndani yake marekebisho machache. Bidii kubwa ya umakini imefanywa katika kuregelea kila hadithi ilioko ndani yake, na zikathibitishwa kwa mujibu wa riwaya zake katika vitabu vyaa hadithi.

Kitabu hichi kimekuwa na fadhla kubwa katika kufahamisha Waislamu katika wakati huu nidhamu ya uchumi ya Uislamu .Twamuomba Allah aitandaze fadhla yake kwa watu amma, na kuwamakinisha Waislamu kuziweka hukmu zake katika makao ya kutabikishwa na kutekelezwa katika serikali inayowahukumu na yale aliyo yateremsha Allah .

23 Safar 1410 Hijri
23/9/1979

1:- UTANGULIZI WA NIDHAMU YA UCHUMI

Hakika ya fikra katika umma wowote katika umma nyeginezo ndio utajiri mkubwa utakaopata umma katika uhai wake, ikiwa ni umma unaokuwa, na ndio tunu kubwa inayopokea kikazi kutoka waliopita ikiwa ni umma uliokita katika fikra ya kindani iliyokamilika.

Ama utajiri wa kimada, uvumbuzi wa kielimu, kubuni kwa viwanda na yanayo fanana na hayo ni duni sana kuliko fikra, bali kufikiwa kwake hutegemea fikra, na kuhifadhiwa kwake hutegemea fikra.

Pindi unapobomolewa utajiri wa kimada wa umma, humkinika kwa upesi kuurudisha upya maadamu umma umehifadhi utajiri wake wa kifikra. Ama ukiwacha utajiri wake wa kifikra na kuhifadhi utajiri wake wa kimada tu, kwa haraka hudidimia utajiri huo na kurudi katika hali ya ufukara. Hivyo hivyo kufaulu kielimu ambako kumevumbuliwa na umma, humkinika kufikiwa tena kwa mara nyengine maadamu hawakupoteza njia yao ya kufikiri. Pindi wanapopoteza njia yao ya kufikiri yenye kuzalisha natija, kwa haraka hurudi nyuma na kukosa walichonacho katika uvumbuzi na kubuni. Na kufikia hapa imekuwa hakuna budi ila mwanzo kuwa na pupa juu ya fikra.

Juu ya msingi huo wa fikra na kwa mujiba wa njia ya kufikiri ya kuzalisha natija, huchumwa utajiri wa kimada na kwenda mbio ili kufikia uvumbuzi wa kielimu na kubuni kwa viwanda na yanyo fanana na hayo.

Maana ya fikra ni kuwepo tendo la kufikiri katika umma, katika matukio ya uhai wake, kwa kutumia jumla ya watu wake kwa walio nayo katika maalumati, baada ya kuhisi matukio ili kuhukumu juu ya matukio hayo. Yaani wawe na fikra wanazokusudia kuzitumia katika uhai, ili kuwazalishia kwa kuregelea kuzitumia mafanikio ya njia ya kufikiri yenye kuzalisha natija.

Umma wa Kiislamu leo huchukuliwa kuwa umekosa fikra, basi ni kawaida kukosa njia ya kufikiri inayozaa natija. Kizazi cha sasa hakikupokea kutoka walio tangulia fikra yejote ya Kiislamu wala fikra isiokuwa ya Kiislamu. Na kawaida haukupokea njia ya kufikiri inayozaa natija. Wala kibinafsi haukuchuma fikra wala njia ya kufikiri inayozaa natija. Kwa hivyo umekuwa ni kawaida uonekane katika hali ya ufakiri pamoja na kuwepo utajiri wa kimada katika biladi zake. Hivyo hivyo huonekana katika hali ya kukosa uvumbuzi wa kielimu na kubuni kwa viwanda ingawaje huzisoma nadharia za uvumbuzi huo na kubuni huko, na huzisikia na kuzishuhudia. Hii ni kwa sababu haimkiniki kuzikimbilia mkimbilio wa kuzaa natija, ila ukiwa unamiliki njia ya kufikiri inayozaa natija, yaani wakiwa na fikra wanazoazimia kuzitumia maishani. Na kufikia hapa imekuwa ni lazima kwa Waislamu kuwa na fikra na njia ya kufikiri inayozalisha, kisha juu ya msingi wake humkinika kuelekea katika kuchuma utajiri wa kimada, kuvumbua uvumbuzi wa kielimu na kubuni kwa viwanda. Na wasipofanya hivyo haimkiniki kusonga mbele kwa hatua hata moja, na watabakia wakizunguka mzunguko mtupu, watamaliza katika mzunguko huo hazina ya juhudzi zao za kiakili na kimwili kisha wataishia mahali walipoanza.

Kizazi hichi cha Umma wa Kiislamu hakijakubali fikra zinazogongana na fikra ambayo yatakikana iwepo mpaka

udiriki fikra hii ambayo inapewa na kutokee mgongano baina ya fikra mbili, na kuongozwa kutoka mgongano huo kwa fikra iliyo sawa. Bali ni mtupu kwa kila fikra miongoni mwa fikra na kutohana na njia yejote miongini mwa njia ya kufikiri inayozaa natija. Nao umerithi fikra za Kiisalamu kama falsafa inayowazwa, sawa na Mayunani walivyorithi falsafa za Aristotle na Plato. Na wamerithi Uislamu kama ibada na vitendo vyakidini, kama wanavyorithi Manasara dini ya Kinasara. Wakati huo huo umekuwa ni kipenzi wa fikra za Kirasilimali kwa mujarad wa kushuhudia kufaulu kwake , wala si kwa kudiriki uhakika wa fikra hizo, na kwa kunyenyeka kwake kwa kutabaikishiwa hukmu zake juu yake, wala si kwa kudiriki machimbuko ya suluhisho hizo kwa mitazamo wa Kirasilimali juu ya uhai. Kwa hivyo umekuwa mtupu wa fikra za Kirasilimali kifikra hata kama huendesha maisha kwa mwenendo wake. Pia ni mtupu wa fikra za Kiislamu kivitendo hata kama hufuata dini ya Kiislamu na kusoma fikra zake.

Ama kuvutiwa kwake kwa fikra, kumevuka majaribio ya kupatanisha baina ya Uislamu na hukmu na suluhisho za Kirasilimali. Imefikia kiwango cha kuhisi kushindwa Uislamu kuweka suluhisho za kutatua matatizo mapya ya kimaisha na kuhisi udharura wa kuchukua hukmu na suluhisho za Kirasilimali kama zilivyo bila ya haja ya kuzipatanisha. Wala hauoni madhara yakuwacha hukmu za Kiislamu na kuchukua hukmu nyenginezo ili uweze kusonga mbele katika nyanja za maisha pamoja na ulimwengu ulio tamadunika, na kudandia msafara wa umma za Kirasilimali au kaumu ambayo hutabikisha Ujamaa na kuelekea Ukomunisti kwa kuichukua kama mitazamo ya kaum zilizoendelea. Ama wale walio bakia miongoni mwa walioshikamana na Uislamu, wao pia wanakivitio hicho hicho kwa fikra za Kirasilimali lakini wao hawakuwacha kujaribbu uwezekano kupatanisha baina ya Uislamu na nyenginezo, lakini hawa hawana athari yejote katika nyanja za kimaisha wala hawako katika mujtamaa, yaani hawako katika mafungamano yanayozunguka kiihakika baina ya watu.

Kufikia hapa imekuwa kupeana fikra ya Kiislamu na hukmu za ki-sheria ili kutatua matatizo maishani hugongana na mabongo matupu kwa fikra na njia ya kufikiri. Hugongana na kuvutiwa na fikra za kirasilimali na ujamaa zilizopo kwa wengi. Hivyo hivyo hugongana na uhakika wa maisha ya kivitendo yanayo huhukumiwa na nidhamu ya kirasilimali. Ikiwa fikra haina nguvu kufikia daraja la kutingisha nafsi na akili basi haiwezi kushtuwa watu bali haimkiniki kufikisha katika hali ya kugeuza mtazamo. Kwa sababu ni juu ya fikra hii kubeba mabongo haya mazito yaliyo finyo ili yazame katika kufikiri na kutingisha mvuto wa kimakosa na utamu wa kigonjwa mpaka upatikane mvuto wa kikweli kwa fikra za Kiislamu na hukmu za kisheria.

Kufikia hapa imekuwa ni lazima kwa mbebaji ulinganizi wa Uislamu kukabiliana na misingi ambayo imesimama juu yake hukmu na suluhisho za kirasilimali, abainishe ubaya wake na kuubomoa. Na akusudie uhakika wa maisha ulio mpya, tofauti tofauti, na kubainisha suluhisho zake katika Uislamu kwa kuichukua kama hukmu ya kisheria zinazochuma uwajibu wa kuzichukua kwa hali yake kama hukmu za kisheria zilizovuliwa kutokamana na Kitabu na Sunna au kilichoelekezwa kwayo katika Kitabu na Sunna kutokamana na dalili, wala si kwa upande wa kufaa kwake kwa zama au kutofaa. Yaani abainishe uwajibu wa kuchukuliwa kwake kiitikadi sio kimaslahi, basi hukusudia katika kupeana kwa kubainisha dalili yake ya kisheria ambayo imevuliwa kutokamana nayo, au kwa kutoa sababu yake katika sababu (*illa*) za kisheria iliyokuja nayo au mithali yake katika nnasi za kisheria.

Hakika ya fitna kubwa waliofitinika nayo Waislamu na balaa kali inayowaumiza katika uhakika wa maisha yao ni fikra zinazoambatana na kuhukuma na fikra zinazoambatana na uchumi. Nazo ni fikra ambazo zaidi zimepata upokezi wa kukubaliwa na Waislamu, na nikatika fikra ambazo zaidi zimepata upokezi wa kukubaliwa na Waislamu, na katika fikra ambazo wamaghribi zaidi huzitabikisha na hukesha ili kuzitabikisha kwa kudumu mfululizo. Basi ingawa Umma wa Kiislamu hutawalishiwa kisura na muundo wa nidhamu ya

kidemokrasia kimakusudi kutoka kwa kafiri mkoloni ili aweze kulinda ukoloni wake na nidhamu yake, naye pia huhukumuwa na nidhamu ya kiuchumi ya Kiraslimali kivitendo katika nyanja zake zote za kiuchumi. Kwa hivyo zimekuwa fikra za Kiislamu juu ya uchumi ni mionganini mwa fikra ambazo huathiri zaidi uhakika wa maisha ya kiuchumi katika ulimwengu wa Kiislamu jinsi ambayo itaipindua juu chini, na zitakuwa mionganini mwa fikra zitakazopigwa vita zaidi na kafiri mkoloni na kutoka vibaraka wake waliofitinika na umagharibi mionganini mwa watu walioridhia giza, waliovunjika moyo na watawala.

Kwa hivyo hakuna budi ila kupeana sura ilio wazi juu ya uchumi katika nidhamu ya Kiraslimali ambayo itabainisha fikra za kimisingi ambazo husimama juu yake siasa ya kiuchumi ya wamagharibi mpaka wahisi wapenzi wa nidhamu ya kiuchumi ya kimagharibi ujisadi wa nidhamu hii, na kugongana kwake na Uislamu kisha wazione fikra za Kiislamu za kiuchumi nazozikitatua matatizo ya kiuchumi maishani tatuo lilio sahihi na kufanya kuwa ni muundo wa kipekee katika maisha unao gongana na maisha ya kirasilimali katika msingi na ufanuzi.

Nidhamu ya kiuchumi katika uraslimali

Tunapopeleza nidhamu ya kiuchumi katika mfumo wa Kiraslimali, tutakuta kuwa uchumi kwao ndio unao chunguza mahitaji ya mwanadamu na njia ya kuyashibisha, wala haichunguzi ila katika upande wa kimada katika maisha ya mwanadamu. Nao husimama juu ya misingi mitatu:

Wa kwanza: Tatizo la uhaba wa kulinganisha baina ya bidhaa na huduma zikifananishwa na mahitaji , yaani kutotosha bidhaa na huduma kwa mahitaji mapya mapya tofauti tofauti ya mwaadamu , na hili ndilo tatizo la kiuchumi linaloukabili mujtamaa.

Wa pili: Thamani ya kitu kilichozaaliwa, ndio msingi wa uchunguzi wa kiuchumi na lakusomwa zaidi.

Wa tatu: Bei na nafasi inayosimamia katika uzalishaji, utumiaji na usambazaji nayo ndio jiwe la kiuno katika nidhamu ya kiuchumi wa Kirasilimali.

Ama tatizo la uhaba hulinganishwa na bidhaa na huduma, hilo hupatikana kwa sababu bidhaa na huduma ndio njia ya kushibisha mahitaji ya mwanaadamu. Hilo ni kwa sababu wao husema kuwa mwanaadamu ana mahitaji ambayo lazima yashibishwe, basi hapana budi kuweko njia za kuyashibisha. Ama mahitaji hayo hayawi ila ni mahitaji ya kimada tu, nayo imma ni mahitaji yanayohisika na kushikika na watu kama kuhitajia mwanaadamu chakula na mavazi. Ama ni mahitaji yanayohisiwa na watu lakini hawawezi kuyashika kama mahitaji ya mwanaadamu kwa huduma za tabiu na mwalimu. Ama mahitaji ya kimaanawiya kama ufahari, na mahitaji ya kiroho kama kumtukuza Muumba, hayatabuliki kwao kiuchumi wala hayana mahali kwao wala kutiwa maanani pindi unapofanywa uchunguzi wa kiuchumi.

Ama njia ya kushibisha, hakika wao wamebandika juu yake jins ls bidhss ns hudums. Bidhaa ndio njia ya kushibisha mahitaji ya kushikika na kuhisika, na huduma ndio njia ya kushibisha mahitaji yanayohisika yasioshikika. Ama yale ambayo hushibisha katika bidhaa na huduma, hilo ni katika mtazamo wao ni manufaa ylio ndani yake. Manufaa hayo ni sifa (*khasa*), inapopatikana katika kitu hukifanya kuwa ni chenye kufaa kuwa kishibisha haja. Na kwa kuwamaana ya haja kiuchumi ni kutaka (*raghba*), basi kitu chenye kufaa huwa kiuchumi ni kila ambacho hutakikanwa sawa sawa kiwe cha dharura au kisiwe cha dharura, hata wakikichukua baadhi ya watu kuwa chenye kufaa na wakichukulie baadhi kuwa ni chenye kudhuru; hicho huwa ni chenye kufaa kiuchumi maadamu kuna mwenye kikitaka. Hii ndio inayowafanya kuchukulia vitu ni vyenye kufaa kwa upande wa kiuchumi hata kama maoni jumla hukichukuwa kuwa kisicho cha manufaa au ni cha kudhuru. Basi tembo na hashishi ni vitu vyenye kufaa kwa wanauchumi ikiwa baadhi ya watu wanavitaka. Kwa hili hutizama mwanauchumi kwa njia ya kushibisha yaani kuwa bidhaa na

huduma kwa kuzichukuwa kuwa hushibisha haja bila kujali sababu yelete nyengine yaani hutizama mahitaji na manufaa kama yalivyo wala si kama yanavyo pasa kuwa. Hutizama manufaa kwa upande wake wa kushibisha haja wala havuki mtazamo huu. Huitizama tembo kwa upande wa kuwa kwake na thamani ya kiuchumi kwa sababu hushibisha haja za watu, na humtizama mtengenezaji tembo kama mwenye kutowa huduma kwa upande wa kuwa huduma hiyo ina thamani ya kiuchumi, kwa sababu hushibisha haja za watu.

Haya ndio maumbile ya mahitaji kwao wao, na haya ndio maumbile ya njia ya kuyashibisha. Mwanauchumi wa Kirasilimali hajali inavyopasa kuwa mujtamaa bali hujali mada ya kiuchumi kwa hali yake ya kushibisha haja. Kwa hivyo huwa jukumu la mwanauchumi ni kuleata bidhaa na huduma yaani kuleta njia ya kushibisha kwa ajili ya kushibisha mahitaji ya mwanaadamu bila kujali hali yelete nyengine. Na kwa sababu bidhaa na huduma ambazo ndio njia za kushibisha zina kikomo katika mtazamo wao, basi hizo hazitoshi kutosheleza mahitaj ya mwanaadamu yasiyo na kikomo kwa mujibu wa rai yao. Kuna mahitaji ya kimsingi ambayo mwanaadamu hana budi kushibisha kwa sifa yake kama mwanaadamu, na kuna mahitaji mengi ambayo huzidi kila anapopanda mwaadamu daraja ya juu katika daraja ya *maddniyya*. Haya hukuwa na kuzidi, na huhitaji kushibishwa ushibishaji kamili, na hali hii haipatikani hata bidhaa na huduma zikizidi. Kufikia hapa hutokea msingi wa tatizo la uchumi nalo ni wingi wa mahitaji na uchache wa njia za kuyashibisha, yaani kutotosha bidhaa na huduma ili kushibishsa mahitaji yote ya mwanaadamu ushibishaji kamili. Hukumba mujtamaa wakati huo tatizo la uchumi nalo ni tatizo la uhaba wa kulingana bidhaa na huduma, na natija ya lazima ya uhaba huo ni kubakia baadhi ya mahitaji imma kushibishwa kivipande au kutoshibishwa hata kidogo. Maadamu mambo ni hayo hakuna budi kuweko qaida ambazo watu watazitumia katika mujtamaa ili kuamua ni mahitaji yapi yatakayo shibishwa na yapi yatakayo nyimwa; kwa maana nyengine hakuna budi kwa qaida zitakazo amua jinsi ya kusambaza /kugawanya mapato yalio na kikomo juu ya haja zisizo na kikomo. Basi tatizo kwao

wao ni mahitaji na mazao, yaani ni kuleta mazao ili kushibisha mahitaji wala sio kushibisha mahitaji ya kila mtu kati ya watu. Mambo yalipokuwa hivyo imekuwa hakuna budi ila qaida ambazo zitawekwa, kuwa qaida ambazo zitadhamini kufikia kwa kiwango cha juu kinacho wezekana katika uzalishaji mpaka kuletwe bidhaa na huduma kwa jumuuiya ya watu lakini sio kila mmoja wao. Na kufikia hapa imekuwa la usaambazaji wa bidhaa na huduma limefungamana na tatizo la kuzalishwa kwake. Na limekuwa lengo la juu la utafiti wa kiuchumi ni kufanya kazi ili kuzidisha kinachotumiwa na jumuiyya ya watu mionganoni mwa bidhaa na huduma, basi kwa hayo imekuwa utafiti juu ya sababu ambazo huathiri kiwango cha uzalishaji wa nchi (GDP) huchukua mahala pa kwanza baina ya maudhui yote ya kiuchumi kwa sababu uchunguzi wa kuzidisha uzalishaji wa ncini mionganoni mwa uchunguzi muhimu ili kutatua matatizo ya kiuchumi nayo ni uhaba katika bidhaa na huduma zikilinganishwa na mahitaji. Hii ni kwa sababu wao huitakidi kuwa haimkiniki kutatua tatizo la ufukara na kukosa kuzidisha uzalishaji. Basi tatuo la tatizo la kiuchumi ambalo mujtamaa hukumbana nalo huwa tu katika kuzidisha uzalishaji.

Ama thamani ya kitu kilichozalishwa, nayo humaanisha daraja ya umuhimu wake imma kwa mtu maalum au kwa upande wa kitu chengine. Katika hali ya kwanza huitwa jina la thamani ya manufaa, na katika hali ya pili huitwa jina thamani ya kubadilisha. Thamani ya manufaa ya kitu hufupika kuwa: thamani ya manufaa ya kitu hutokamana na kitu kukadirisha na manufaa yake ya mwisho, yaani kwa kiwango cha kitu kinachoshibisha mahitaji **mandifu** –dhaifu zaidi, na hii ndio wanayoita manufaa ya mwisho au ya kiwango cha mwisho. Yaani manufaa hayakadiriwi kwa mujibu wa mtazamo wa mwenye kuzalisha ili kukadirisha kwa gharama za uzalishaji wake kwa sababu wakati huo huwa imechungwa ndani yake sura ya mtazamo wa kuleta tu sio wa kutaka; wala haikadiriwi kwa sura ya mtazamo wa mtumiaji tu ili kukadirisha kadirio la yaliomo ndani yake ya manufaa na hisia ya kuhitajia kwa manufaa haya pamoja na kutia maanani sababu ya uhaba, kwa sababu wakati huo huo itakuwa imechungwa ndani yake sura ya

mtazamo wa kutaka tu bila ya kuleta. Bali yapasa kuchungwa ndani yake mtazamo wa kuleta na kutaka kwa pamoja, basi huchukuliwa manufaa yake kwa kiwango cha kushibisha ndani yake haja ya mwisho-kwa kiwango cha mwisho cha ushibishaji. Yaani huchukuliwa thamani ya mkate wakati wa mwisho wa njaa sio mwanzoni mwake na katika wakati wa kawaida wa kupatikana mkate sokoni sio wakati wa uhaba wake; hii ndio thamani ya manufaa.

Ama thamani ya kubadilisha, hiyo ni sifa pindi inapopatikana katika kitu hukifanya kuwa kizuri katika kubadilishana. Na huijua kuwa ni nguvu ya kubadiilisha kitu kulingana na chengine, basi thamani ya kubadilsha ngano kulinganisha na mahindi hukadiriwa kwa kima cha mahindi ambayo lazima yapatikane ili kupata uniti moja ya ngano. Na huitwa thamani ya manufaa kwa jina la manufaa tu, na huitwa thamani ya kubadilisha kwa jina la thamani tu.

Kubadilishana hutimia baina ya bidhaa au huduma zinazolingana au kukurubiana katika thamani. Na kufikia hapo imekuwa hapana budi kuchunguza thamani kwa wanauchumi wa Kirasilimali kwa sababu ni msingi wa kubalishana na ni sifa ambayo yamkini kuipima, na ndio kipimo ambacho hupimiwa nacho bidhaa na huduma , na hutofautishwa nayo vitendo vya kuzalisha kutoka visivyo zalisha. Hilo ni kuwa uzalishaji ni kuleta manufaa au kuyazidisha, na hutimia kwa kazi na ili kutofautisha baina ya kazi hizo kwa upande wa kuwa huzalisha au haizalishi, na kujua ipi huzalisha zaidi kushinda nyengine, hapana budi ila kuwepo kipimo barabara cha mazao na huduma tofauti tofauti au kwa maana nyengine ni yale maladirio ya jamii kwa kazi inayojitolea au huduma inayoitoa; na imekuwa makadirio hayo ni jambo la dharura kwa sababu uzalishaji kwa ajili ya kubadilishana imechukua katika jamii za kileo mahala pa uzalishaji kwa ajili ya ulaji na ikawa kila mtu leo hubadilisha kila alicho kizalisha au kiasi kikubwa kwa vitu vingi vyenginevyo vilivo zalishwa na watu wengine. Nakubadilishana huko hutimia kwa kuwepo badili kwa bidhaa au huduma, basi hapana budi kukadiriwa thamani ya bidhaa ili ipate

kubadilishwa. Kwa hivyo imekuwa kujua thamani: ‘Ni nini?’ Ni jambo la dharura kwa uzalishaji na jambo la dharura kwa ulaji, yaani ni jambo la lazima katika kushibisha mahitaji ya mwanaadamu kwa mbunu za kushibisha.

Isipokuwa thamani ya kubadilisha imewtambuliwa katika zama hizi kwa moja wapo wa thamani zake na ikawa ndio ilio zagaa zaidi. Basi katika jamii zilizo endelea kitamaduni hawanasibishi thamani ya bidhaa kwa bidhaa nyengine bali hunasibisha kwa bidhaa maalum inayoitwa fedha. Na imebandikwa juu ya unasibishaji wa kubadilisha kitu kwa fedha kwa jina la bei. Bei ndio thamani ya kubadilisha kitu kikinasibishwa na fedha. Na kwa hayo huwa tofauti baina ya thamani ya kubadilisha na bei, ni kuwa thamani ya kubadilisha ni mnasaba wa kubadilisha kitu na kitu chochote sawa saw kiwe ni fedhs, bidhaa au huduma. Ama bei ni thamani ya kubadilisha kitu kwa fedha maalum. Na hutokamana kwa hapa, uwezekano wa bei hizi zabidhaa kupanda kwa wakati mmoja na zote kushuka kwa wakati mmoja, katika wakati amba ni muhali kupanda na au kushuka thamani ya kuadisha kila bidhaa, baadhi kwa baadhi kwa wakati mmoja. Hivyo hivyo humkinika kubadilika bei za bidhaa bila ya kubadilika katika thamani ya kubadilishwa kwake. Na kwa hayo huwa bei ya bidhaa ni moja wapo wa thamani ya bidhaa hiyo na kwa maana nyengine huwa thamani ya bidhaa kwa kunasibishwa na fedha tu. Na ilipokuwa bei ni moja wapo wa thamani imekuwa kwa tabia ya kawaida iwe ndio kipimo chakuwa kitu ni chenye manufaa au kisichofaa, na kipimo cha kiwango cha manufaa katika kitu. Basi bidhaa au huduma huchukuliwa ni yenye kuzalisha na yenye kufaa ikiwa mujtamaa huithamini bidhaa hiyo au huduma maalum kwa bei maalum. Ama kiwango cha manufaa ya bidhaa hii au huduma, hupimwa kwa bei ambayo itakubalika na wengi wa walaji kulipa, ili kuipata sawa sawa ikiwa bidhaa hiyo ni ktika mazao ya ukulima , sanaa, na sawa sawa ikiwa huduma hiyo ni huduma ya mfanya biashara, shirika la usafiri, tabibu au mhandisi.

Ama kazi ambayo bei inayoifanya katika uzalishaji , ulaji na ugawanyanyaji, hii ni kwa sababu nidhamu ya bei ndio

inayoamua ni yupi ktika wazalishaji ataingia katika mzunguko wa uzalishaji na ni nani watakao kuwa mbali na kundi la wazalishaji, kwa jinsi hiyo hiyo ambao huamua nani katika walaji ataweba kushibisha haja yake nani yupi mahitaji yake yatabakia bila kushibishwa. Na gharama za kuzalisha bidhaa ndio sababu kubwa ambayo huamua kutolewa kwake sokoni, na manufaa ambayo yamo katika ndio sababu kubwa inayoamua kutakikanwa kwake sokoni na yote hayo mawili hupimwa kwa bei. Kwa hivyo imekuwa uchunguzi juu ya kutolewa na kutakikanwa ni uchunguzi miwili ya kimsingikatika uchumi kwa Warasilimali. Muradi kwa kuletwa ni kutolewa sokani na muradi wa kutakikanwa ni kutakikanwa sokoni. Kama ilivyo kutakikanwa hakuwezi kukadiriwa bila kutaja bei, hivyo hivyo kutolewa hakuwezi hskuwezi kukadiriwa bila ya bei. Isipokuwa kutakikanwa hubadilika kinyume na kubadilika kwa bei, basi ikizidi bei hupungua kutakikanwa na ikipungua bei huzidi kutakikanwa. Kinyume na kutolewa inayobadilika kwa kubadilika bei na kwa upande wake yaani kutolewa huzidi kwa kuzidi bei na hupungua kwa kushuka kwake. Na katika hali zote mbili huwa bei ndio inayoathiri zaidi katika kutolewa na kutakikanwa yaani huwa na athari kubwa zaidi katika uzalishaji na ulaji.

Na nidhamu ya bei kwao wao ndio twarika bora kugawanya bidhaa na huduma kwa watu katika mujtamaa. Kwani manufaa ni natija ya juhudhi ambazo mwanaadamu huzitia, basi ikiwa malipo hayako sawa na kazi basi bila shaka kiwango cha uzalishaji kitazorota. Na kwa hilo imekuwa twarika bora ya kugawanya bidhaa na huduma kwa watu katika mujtamaa ile itakayo dhamini kufikiwa katika kiwango cha juu cha uzalishaji; twarika hii ni twarika ya bei ambayo huitwa nidhamu ya bei au mashini ya bei kwa sababu wao huona kuwa twarika hii huleta mizani ya kiuchumi pasina kuangaliwa kama mashini. Kwa sababu imesimama juu kuwachwa huru walaji katika kuamua wenyewe ugawanyaji wa vitu ambavyo humilikiwa na mujtamaa juu ya harakati za kiuchumi tofauti tofauti kwa kukubali kwao kununua baadhi ya vitu na kutokubali kwao vyengine. Basi hutumia mapato yao waliyoyachuma kwa

kununua wanayo yahitaji au kuyataka. Mlaji ambaye hataki tembo atajizuia na kuinunua, na hutumia mapato yake katika kitu chengine, basi ikizidi idadi ya walaji ambao hawataki tembo au wamekuwa watu wote hawaitaki tembo, huwa uzalishaji wa tembo hauna faida kwa kukosekana wanao itaka, basi utasimamakimaumbile uzalishaji wa tembo. Na hivyo hivyo vitu vyote walaji ndio ambao huamua kiwango cha uzalishaji na aina ya kilicho zalistwa kwa kuwachwa na uhuru wao. Na bei ndio ambayo hupelekwa kwa mujibu wake ugawanyanji wa bidhaa na huduma kwa kupatikana walaji au kutopatikana, na kwa kuwalipa wazalishaji au kutowalipa.

Nidhamu ya bei ndio inayo shajiisha uzalishaji na ndio inayopanga ugawanyaji, na ndio chombo kinacho unganisha baina ya mzalishaji na mlaji, yaani ndio ambayo huhakikisha uaswa baina ya uzalishaji na ulaji.

Ama kuwa (bei) ndio inayo shajiisha uzalishaji, hilo ni kwa sababu msukumo mkuu wa mwanaadamu kufanya juhudi yoyote inayozalisha au kujitolea kwa chochote ni malipo yake ya kimada kwa kutia juhudi hiyo au kujitolea huko. Wanauchumi wa Kirasilimali huweka mbali uwezekano wa mwanaadamu kutia juhudi yoyote kwa mdukumo wa uwema au uroho. Na msukumo wa kiakhlaki ambao wanakiri kuwepo kwake, wanaurudisha kwa malipo ya kimada, na huona kuwa juhudi ambazo mwanaadamu huzitia ni kwa ajili ya kushibisha mahitaji yake ya kimada. Na kushibisha huko imma huwa kwa njia ya ulaji wa bidhaa ambazo amezizalisha moja kwa moja au kwa njia ya kupata malipo ya kifedha yanayomuwezesha kupata bidhaa na huduma ambazo zimezalishwa na wengine. Na kwa kuwa mwanaadamu hutegemea katika kushibisha mahitaji yake mengi ikiwa si yote kwaw kubadilisha juhudi za wengine, imekuwa kushibisha mahitaji kumenasibishwa juu ya kupata malipo ya kifedha kwa juhudi zake zisizomwezesha kupata bidhaa na huduma alizozizalisha. Kwa hivyo imekuwa malipo ya kifedha, ambayo ni bei, ndio msukumo wa mwanaadamu katika kuzalisha. Na kufikia hapa imekuwa bei ndio imekuwa

bei ndio inayotia motisha wanaozalisha katika juhudi zao basi bei ndio inayo shajiisha uzalishaji.

Ama kuwa bei ndio ambayo hupanga ugawanyaji, hilo ni kuwa mwanaadamu ataka kushibisha mahitaji yake yote ushibishaji kamili. Kwa hivyo huenda mbio ili apate bidhaa na huduma ambazo zitashibisha mahitaji hayo. Na lau angewachwa kila mtu katika wanaadamu na uhuru wa kkushibisha mahitaji yake asingekoma mpaka apate na kula anachotaka katika bidhaa. Lakini kwa sababu kila mtu miongoni mwa wanaadamu huendea mbio lengo hili, hukuna budi ila kusimama mtu katika kushibisha mahitaji yake katika kikomo ambacho huweza kubadilisha ndani yake juhudi zake kwa juhudi za wengine, yaani katika kikomo cha malipo ya fedha ambazo atazipata kwakutoa juhudi zake, yaani katika kikomo cha bei. Nakufikia hapa imekuwa bei ndio pingu inayowekwa kimaumbile na humfanya mtu kukoma kupata na kula katika kikomo ambacho ni sambamba na mapato yake. Kuwepo bei ndio humfanya mwanaadamu kufikiri na kufadhilisha baina ya mahitaji yake yanayo shindana, ambayo hutaka kushibishwa. Basi huchukua anachokiona kuwa ni cha dharura na kkuwacha kile ambacho huona dharura yake ni chache zaidi. Na ndio inayomlazimisha mtu kutosheka kushibisha baadhi ya mahitaji yake kivipande ili aweze kushibisha baadhi nyengine ambayo huyaona si uchache kiumuhimu na mahitaji ambayo ametosheka kushibisha baadhi yake kivipande. Bei ndio inayopanga nidhamu ya ugawanyaji wa mahitaji anayo yahitaji mtu, hivyo hivyo ndio ambayo huopanga nidhamu ya ugawanyajiwa manufaa yaliyo na kikomo baina ya walaji wengi wanataka manufaa hayo. Basi tofauti ya mapato ya walaji hufanya ulaji wa kila mtu kufungika kwa yale yanyomruhusu mapato yake. Kwa hivyo umekuwa ulaji wa bidhaa umefungwa kwa yule ambaye mmapato yake yamruhusu, na huwa ulaji wa baadhi ya bidhaa ni jumla kwa watu wote ambaao wanamiliki kiwango chachini cha bei. Kwa haya huwa kupanda kwa bei baadhi ya bidhaa na kushuka kwa baadhi yake, na kupatikana malipo ya kifedha kwa baadhi na kutopatikana kwa wengineo, ndio yenye kupanga ugawanyajiwa manufaa kwa walaji.

Ama kuwa bei huhakikisha usawa baina ya uzalishaji na ulaji yaani huwa ni chombo cha kuunganisha baina ya mzalishaji na mlaji, hii ni kuwa mzalishaji ambaye huhakikisah matakwa ya walaji hulipwa kwa kupata faida; na mzalishaji ambaye uzalishaji wake haupokelewi na matakwa ya walaji, hapana budi kumalizika kwa hasara. Na njia ambayo mzalishaji aweza kusimama nayo kwa matakwa ya walaji ni bei tu, basi kwa njia ya bei atajuwa matakwa ya walaji. Basi ikizidi kupokelewa na walaji kwa kununua bidhaa maalum, huzidi bei sokoni na kwa hivyo huzidi uzalishaji wa bidhaa hiyo ili kuhakikishamatakwa ya walaji. Na walaji wakiipa nyongo kununua bidhaa maalum hushuka bei yake sokoni na kwa hivyo hupungua uzalishaji wa bidhaa hiyo. Basi mali iliyotengwa kwa uzalishaji huzidi kwa kuzidi bei na hupungua kwa kupungua bei. Kwa hivyo huwa bei ndio ambayo huhakikisha usawa baina ya uzalishaji na ulaji, na huwa chombo cha kuunganisha baina ya mzalishaji na mlaji, na hili huenda kikawaida pasina kuangaliwa (kama mashini). Kufikia hapaimkuwa bei ndio qaida ambayo husimama juu yake uchumi katika mtazamo wa Warasilimali na ndio jiwe la msingi kaatika uchumi kwao wao.

Huo ndio mukhtasari wa nidhamu ya uchumi katika mfumo wa Kirasilimali na ndio wanaouita siasa ya kiuchumi. Hubainka kuitia kuusoma na kuzama katika kuuchunguza ufisaadi wa nidhamu ya uchumi wa Kirasilimali katika sura nyingi:-

1. Kujumuisha mahitaji na namna ya kuyashibisha

Uchumi kwao wao ndio ambao huchunguza mahitaji ya mwanaadamu na njia ya kuyashibisha, na hufanya njia za uzalishaji bidhaa na huduma ambazo ni mbinu za kushibisha mahitaji pamoja na ugawanyaji wa bidhaa na huduma hizo juu ya mahitaji kama uchunguzi mmoja, yaani wamefanya mahitaji na mbinu za kuyashibisha kuingiliana kwa jinsi na huwa ni kitu kimoja na uchunguzi mmoja, kimoja hakitenganiki na chengine bali hukunjika maja wapo kwa chengine pindi unapokunjwa ugawanyaji wa bidhaa na huduma katika uchunguzi wa kuzalisha bidhaa na huduma hizi.

Vipi nidhamu ya uchumi na uchumi wa kisayansi

Nakujenga juu ya hayo wanautizama uchumi kwa mtazamo mmoja unaokusanya mada ya uchumi na jinsi kuipata bila ya kutofautisha baina yake na bila ya kubagua moja kutoka nyengine, yaaniwanatizama elimu ya uchumi na nidhamu ya uchumi kwa mtazamo mmoja ila ya kutofautisha baina yake pamoja nakuwa kuna tofauti baina nidhamu ya uchumina elimu ya uchumi. Nidhamu ya uchumindio ambaya hubainisha ugawanyaji wa utajiri, kumilikiwa, kutumiwa, na mfano wake. Na katika kubainisha hayo huenda kwa mujibu wa mtazamo maalum katika maisha. Kwa hivyo nidhamu ya uchumi katika Uislamu sio wa Ujamaa na Ukomunisti na sio wa Urasilimali kwa sababu kila nidhamu kati yake huenda kwa mujibu wa mtazamo wa mfumo katika maisha. Kinyume na elimu ya uchumi ambayo huchunguza katika uzalishaji na kukuza, kuweka mbinu zake na kuzikuza. Na hii ni ya kiulimwengu kwa watu wotepasina kuhusishwa na mfumo mmoja bilabial mwengine kama ilivyo elimu nyenginezo. Mfano mtazamo wa umilikaji katika nidhamu ya Kirasilimali hutofautiana na nidhamu ya Kiujamaa na Ukomunisti na katika Uislamu , tofauti na kustawisha uzalishaji ambao ni uchunguzi wa kielimu ambo ni mmoja kwa watu wote kimtazamo hata kama fahamu zao zinatofautiana.

Na kuchanganya huko baina ya mahitaji na mbinu katika uchunguzi, yaani baina ya kuleta mada ya uchumi najinsi ya kuigawanya na kuzifanya kuwa ni kitu kimoja na uchunguzi mmoja ni kosa ambalo natija yake ni mkorogano na kuingiliana katika uchunguzi wa uchumi kwa Warasilimali, kwa hivyo imekuwa msingi wa muundo wa uxumi katika mfumo wa Kirasilimali kuwa ni msingi wa kimakosa.

2. Mahitaji ni ya kimada

Ama kuwa mahitaji ambayo hutaka kushibishwa hayawi ila ni ya kimada tu, hilo ni kosa na hukhalifu uhakika wa mahitaji kwani kuna mahitaji ya kima'anawiya na kuna mahitaji ya

kiroho, na yote huhitaji kushibishwa kama mahitaji ya kimada ,na yote huhitaji bidhaa na huduma iliyashibishwe.

3. Bidhaa na huduma hazihusiani na muundo wa jamii

Ama mtazamo wa wanauchumi wa Kirasilimali kwa mahitaji na manufaa ni kama yalivyo si kama unavyopasa kuwa mujtamaa. Kwani kwa mtazamo huu mwanauchumi wa Kirasilimali humuangalia mwanaadamu kama ni mwanaadamu wa kimada tu aliyevuliwa mwelekeo wa kiroho, fikkra za kiakhlaki na malengo ya kimaanawiya. Wala hajali ipasavyo kuwa mujtamaa katika kunyanyuka kimanawiya kwa kufanya fadhila msingi wa mafungamano yake na yanayo hitajika kumtawala yeze katika upeo wa kiroho kwa ufanya kudiriki fungamano na Allah ndio unao endesha mafungamano, kwa ajili ya kunali radhi za Allah. Na yeze hajali kwa yote hayo bali hamu yake ni mada ambayo hushibisha njaa za kimada tu, basi yeze hadanganyi katika biashara yake iliapate faida na pindi anapopata faida kwa kkudanganya basi itakuwa kudanganya ni halali. Na yeze hawalishi mafukara kwa kuitikia amri ya Allah kwa sadaka, bali huwa lisha ili wasimuibile akini ikiwa kuwaweka na njaa itazidisha utajiri wake basi atasonga mbele na kuwawacha nanjaa. Hivi ndivyo inavyokuwa hamu ya uchumi inayotizama manufaa kama yanavyoshibisha mahitaji ya kimada tu. Mtu huyu ambaye hutizama wanaadamu kupitia mtazamo wa manufaa na kusimamisha maisha ya uchumi juu ya msingi wa mtazamo huu, huchukuliwa kuwa ni mionganoni mwa watu hatari kwa mujtamaa na kwa wanaadamu.

Hii ni kwa upande wa mahitaji na manufaa , na kwa upande mwengine hakika ya mali na juhudhi ambazo wanaziita bidhaa na huduma, mtu huzikimbilia ili kunufaika nazo. Kuzibadilisha kwa watu hujenga mahusiano baina yao yanayojengwa kwa mujibu wake mujtamaa. Basi hapana budi kutizama kwa yale ambayo huwa juu yake mujtamaa katika mafungamano yake kijumla na kifafanuzi pindi anapoangalia mali na mahitaji. Kuwa na hamu kwa mada ya uchumi kwa upande wa kuwa hushibisha mahitaji bila ya kuwa na hamu kwa yanayopasa kuwa juu yake mujtamaa, ni kutenganisha mada ya uchumi

kutokamana na mafungamano yake, na hilo si kawaida. Watu wanapobadilishana mada za uchumi hujenga mujtamaa, basi hapana budi kuwa na mtazamo kwa yale yatakayo pasa kuwa juu ya mujtamaa pindi inapotizamwa mada ya uchumi. Kwa hivyo si sahihi kuchukua kitu kuwa chafaa kwa sababu tu kuna wenye kukitaka sawa sawa hakika yake kiwe ni chenye kudhuru au la, ama chenye kuathiri mafungamano ya watu au la, ama kiwe ni haramu katika itikadi ya watu katika mujtamaa, au kiwe ni halali bali yapasa kuchukua kitu ni chenye kufaa ikiwa uhakika wake hunufaisha kwa kuchukua yanayopasa kuwa juu yake mujtamaa. Na kwa aya si sahihi kuchukua bangi na afyuni na yanayo fanana nayo kama bidhaa inayofaa na kuichukua kama mada ya uchumi kwa sababu tu ya kuwepowanaozitaka , bali yapasa kutambua athari ya mada za uchumi katika mafungamano pindi inapotizamwa manufaa ya vitu , yaani pindi kinapotizamwa kitu kwa kukichukua kama mada ya uchumiau kutokichukua. Yaani yapasa kukitizama kitu kwa kukichukulia kwa yanayopasa kuwa kuwa juu ya mujtamaa wala haijuzu kutosheka katika mtazamo juu ya kitu kama kilivyo tu na kufinya macho juu ya ipasavyo kuwa mujtamaa.

Imekuwa natija ya kuunganisha uchunguzi wa kushibisha mahitaji ndani ya uchunguzi wa mbinu za kuzibisha, na kwa sababu ya mtazamo wa wanauchumi juu ya mbinu za kushibisha kwa mtazamo wake kuwa kushibisha mahitaji tu pasina mtazamo wowote mwengine, imekuwa natija ya hayo ni mtazamo wa wanauchumi umelemea zaidi juu ya kuzalisha utajiri kushinda kuugawanya ili kushibisha mahitaji; bali ukawa mtazamo juu ya ugawanyaji ni jamo la pili. Na juu ya haya hakika ya mtazamo wa uchumi wa Kirasilimali unalenga lengo moja nalo ni kuzidisha utajiri wa biladi kwa jumla na unafanya kazi ili kuikia kiwango cha juu kinacho wezekana katika uzalishaji, na hufanya uhakikishaji wa hali ya juu inayowezekana ya starehe kwa watu katika mujtamaa kama natija ya kuzidishwa mapato katika biladi kwa kuinua ustawi wa uzalishaji katika biladi. Na hilo ni kwa kuweza kwao kuchukua utajiri pindi wanapowachwa huru katika ya uzalishaji na ukusanyaji. Uchumi hauko ili kushibisha mahitaji ya watu

binafsi kwa kumshibisha kila mtu mionganii mwa jamii bali ni fursa ya kuleta yanayoshibisha mahitaji ya mtu binafsi, yaani ni fursa ya kushibisha jamii kwa kunyanya kiwango cha uzalishaji na kuzidisha mapato ya ndani ya biladi. Na kwa ajili ya kuleta mapato ya kindani, hupatikana wakati huo ugawanyaji wa mapato hayo kupitia uhuru wa kumiliki na uhuru wa kazi wa mtu binafsi katika mujtamaa, basi huwachwa watu binafsi na uhuru wa kupata wanayoweza katika utajiri huo kila mmoja kwa mujibu wa anayomiliki katika sababuza uzalishaji. Sawa sawa ikipatikana kushiba kwa watu woteau kupatikana baadhi na kukosa baadhi.

Hii ndio siasa ya uchumi, yaani uchumi wa Kirasilitmali. Na hili ni kosa lililowazi na huhitilafiana na hali wala halifikisha katika kunyanya kiwango cha maisha ya watu wote, wala haihakikishi kutosheka kwa watu wote. Na upande wa makosa katika haya ni kuwa mahitaji amba ya hitaji kushibishwa ni mahitaji ya kibinafsi juu ya pamoja na kuwa ni mahitaji ya kibnaadamu, nayo ni mahitaji ya Muhammad, Salih na Hassan, wala sio mahitaji ya mkusanyiko wa watu, mkusanyiko wa umma au mkusanyiko kwa qaumu. Yule anayekimilia ili kushibisha mahitaji yake ni mtu binafsi sawa sawa iwe kushibisha kwake ni moja kwa moja kama kula au kushibisha kwa njia ya mjumuiko kama ulinzi wa umma, basi imekuwa tatizo la uchumi limesimama juu ya msingi wa ugawanyaji na mbinu za kushibisha mtu binafsi, yaani kugawanya mali na manufaa kwa watu binafsi katika umma au qaumu, sio juu ya mahitaji yanayotokamana na mkusanyiko wa umma au qaumu bila kuangalia kila mtu katika umma pasina kuangalia kila mtu katika watu wake. Na kwa maana nyengine tatizo ni uhaba unaokumba mtu sio uhaba unaokumba jumla ya biladi, na uchunguzi katika nidhamu ya uchumi huwa katika kushibisha mahitaji ya kimsingi ya kila mtu sio uchunguzi katika uzalishaji wa mada za kiuchumi.

Na kufikia hapa haikua kusomwa sababu zinazoathiri katika ukubwa wa uzalishaji wa kindani ndio maudhui ya uchunguzi katika kushibisha mahitaji yote ya kimsingi ya mtu binafsi,

mmoja mmoja, ushibishaji kamili, bali mada ya uchunguzi ni kusoma mahitaji ya mwanaadamu ya kimsingi kwa jinsi yakuwa yeye ni mwanaadamu na kusoma ugawanyaji wa utajiri kwa kils mtu kstiks mujtamaa ili kudhamini kushibshwa mahitaji yake yote ya kimsingi. Na haya ndio yanapasa kuchukua mahala pa kwanza kutatua tatizo la ufakiri wa mtu mmoja mmoja na kugawanywa utajiri wa biladi hushajiisha mjumuiko wa watu wa biladi na kila mmoja wao kufanya kazi ili kuzidisha mapato ya kindani. Ama kusoma sababu ambazo huathiri katika ukubwa wa uzaishajina kuzidisha mapato ya kindani, hakika uchunguzi huo uko katika elimu ya uchumi, yaani katika uchunguzi wa mada ya ki-uchumi na kuizidisha, sio katika kushibisha mahitaji ambayo hupangwa na nidhamu ya uchumi.

Ama kuwa uhaba unaonasibiana na bidhaa na huduma ndio tatizo la uchumi ambalo hukabili mujtamaa na madai kuwa kuzidi kwa mahitaji na uchache wa kuyashibisha , yaani kutosheleza bidhaa na huduma kushibisha mahitaji yote ya mwanaadamu ushibishaji kamili ndio msingi wa tatizo la uchumi. Hilo ni kosa linalokhitilafiana na hali ilivyo. Na hilo ni kuwa mahitaji ambayo kutatuliwa kwake ni jambo la lazima , ni mahitaji ya kimsingi kwa mtu binafsi kwa sifa yake kamamwanaadamu sio mahitaji ya ziada ya kistarehe, hata kama hufanya kazi na kukimbilia mahitaji ya kitarehe. Na kwa haya, hakika mahitaji kimsingi yamefungika na mali na juhud ambazo wanaziita bidhaa na huduma zinazopatikana katika ulimwengu, nazo hutosha kkushibisha mahitaji ya kimsingi na humkinika kushibisha mahitaji yote ya kimsingi ushibishaji kamili kwa watu walaji walahakupatikani matatizo katika mahitaji ya kimsingi licha kulifanya tatizo la uchumi ambalo hukabili mujtamaa. Bali tatizo la uchumi ni ugawanyaji wa mali hizi na juhud kwa kila mtu mionganoni mwa watu ili kushibisha mahitaji yao ya kimsingi ushibishaji kamili na kuwasaidia katika kukimbilia kushibisha mahitaji yao ya kistarehe.

Ama tatizo la kuzidi mahitaji mapya, hakika yake hayaambatani na kuzidi mahitaji ya kimsingi kwa sababu mahitaji ya kimsingi kwa mwanaadamu kama alivyo kama mwanaadamu hayazidi

bali ambalo huzidina kuwa jipya ni mahitaji ya kistarehe. Basi yanayozidi katika mahitaji yanayopatikana kwa kusonga mbele mwanaadamu katika maisha yake ya mjini hufungamana na mahitajiya kistarehe sio mahitaji ya kimsingi. Mtu hufanya kazi kuyashibisha, lakini kukosa kuyashibisha hakusababishi tatizo bali ambalo husababisha matatizo ni kukosa kushibisha mahitaji ya kimsingi. Na swala la kuzidi mahitaji ya kistarehe ni swala lengine linaloambatana na mjumuiko ambao huishi katika chi maalum na sio kwa kila mtu mionganoni mwa watu katika nchi. Na swala hili huleta msukumo kwa mwanaadamu kikawaida ili kushibisha mahitaji yake. Humsukuma na msukumo kwa kuzidi mahitaji ya kistarehe na kufanya kazi ili kuzidisha mbinu za kushibisha imma kwa kuzidisha mapato ya biladi au kwa kufanya kazi katika maeneo mengine au kupanua na kuunganisha biladi kwa nyengine. Swala hili sio tatizo la kushibisha mahitaji ya kimsingi kwa kila mtu katika mujtamaa ushibisahaji ulio kamili, kwa sababu tatizo la ugawanyaji wa utajiri kwa kila mtu mmoja mmoja ili kushibisha mahitaji yote ya kimsingi ushibishaji kamuli na kumsaidia kila mtu katika kushibisha mahitaji ya kistarehe. Na tatizo hili huambatana na mtazamo juu ya maisha, nalo ni maalum kwa umma maalum au mfumo maalum kinyume na swala la kuzidisha mapato ya kindani na kuzidisha uzalishaji ambao huambatana na hali ilivyo inayohisika katika biladi kwa upande wa ujuzi wa kuzidisha utajiri kwa utumiaji au kugura au kupanua au kuungana. Nayo hutabikishwa juu ya hali ilivyo na kila mwanaadamu huisimamia, nayo ni jumla wala haiambatani na mtazamo maalum wala si makhsus kwa umma maalum wala mfumo maalum.

Na kwa haya huwa misingi ya kiuchumi iliyowekwa ndio qaida zinazodhamini ugawanyaji wa utajiri wa biladi wa kindani na kinnje kwa kila mtu katika umma ushibishaji kamili, na humwezesha kila mtu mionganoni mwao kushibisha mahitaji yake ya kiziada. Ama kunyayua kiwango cha uzalishaji basi huhitaji uchunguzi wa elimu, na uchunguzi wake katika nidhamu ya uchumi hautatui tatizo la uchumi ambalo ni kushibisha mahitaji yote ya kila mtu ushibishaji kamili. Kwa sababu kuzidisha

uzalishaji hufikisha kwa kunyayuka kiwango cha utajiri wa biladi, wala hakufikishi kwa kkushibisha mahitaji yote ya kimsingi kwa watu wote, ushibishaji ulio kamili. Huenda ikawa biladi ni tajiri kwa uzalishajiwake kwa mfano kama Iraq na Saudia lakini mahitaji ya kimsingi ya watu wengi huko hayashibishwi ushibishaji ulio kamili. Kwa hivyo imekuwa kuzidi kwa uzalishaji hakutatui tatizo la kimsingi ambalo hulazimisha kutatuliwa kwa haraka kabla ya kila kitu. Nalo ni kushibisha mahitaji ya kimsingi kisha ya kiziada. Kwa hivyo hakika ya ufukara na kukosa kunakotaka kutatuliwa ni kukosa kushibisha mahitaji ya kimsingi ya mwanaadamu kwa sifa yake kama mwanaadamu, sio mahitaji mapya mapya kwa mujibu wa kunyayuka kimiji. Kinacho takikiwa kutatuliwa ni ufukara na kukosa kwa kila mtu miongoni mwa watu katika mujtamaa, mtu mmoja mmoja wala si ufukara na kukosa kwa biadi, bali ni ufukara huu na kukosa huku kunakofahamiwa na kila mtu. Hakutatuliwi kwa kuzidisha uzalishaji bali hutatuliwa kwa jinsi ya kugawanya utajiri kwa kila mtu, kwa hali ambayo hushibisha kila mtu mahitaji yoteya kimsingi ushibishaji kamili na humsaidia katika kushibisha mahitaji yake ya kiziada.

Ama maudhui ya thamani hakika nidhamu ya uchumi ya Kirasilimali huchukulia thamani ni ya kutegemea, wala sio ya uhakika basi nayo kwao ni thamani ya kubuniwa. Kwa hayo huwa thamaniya dhiraa ya kitambara cha sufi huwa ni manufaa yake ya mwisho katika hali ya kupatikana kwake sokoni, na thamani yake ni kiwango kitakacho badilishwa nacho cha bidhaa na juhudi na thamani huwa ni bei ikiwa kitakacho patikana kutokamana na hicho kitambaa ni pesa. Na thamani hizi mbili kwao wao ni vitu viwili tofauti na vina majina mawili yanayo tofautika. Kwanza ni manufaa na la pili thamani ya kubadilisha. Maana hii ya thamani kwa tafsiri hii ni makosa kwa sababu thamani ya bidhaa yejote huwa ni makadirio ya manufaa yaliyo ndani yake pamoja na kutambua upande wa uhaba. Basi mtazamo wa kihakika kwa bidhaa huwa ni mtazamo wa manufaa pamoja na kutambua uhaba wake sawa sawa awe amekimiliki mwanaadamu kiasli, kama kutoka kuwinda au kubadilishana kama kuuza na sawa sawa ikiwa hilo huambatana

na mtu au kitu. Basi thamani ni jina linaloitwa shaksiya maalum ilio na uhakika sio jina la kitu linalokadiriwa, linalobandikwa jina la kukadiriwa wala haichukuliwi juu ya jambo lengine. Basi thamani ni kitu cha kihakika sio kitu cha kutegemea, na juu yake huwa mtazamio wa wanauchumi kwa thamani ni mitazamo ya kimakosa kutoka msingi wake.

Ama kile wanachokiita “thamani ya Mwisho”, hakika yake ni makadirio ya uzalishaji katika hali mbaya ya kusambaza bidhaa. Basi hukadiriwa thamani ya bidhaa katika kiwango cha cini iliuzalishaji uwe ni wenyewe kwenda kwa msingi ulio dhaminiwa. Thamani ya Mwisho si thamani ya bidhaa wala bei, kwa sababu thamani ya bidhaa hukadiriwa kwa makadirio ya manufaa ndani yake wakati wa kukadiriwa pamoja na kutambua uhaba wake wakati huo, wala haipungui thamani yake inaposhuka beibei baada ya hayo kwa sababu thamani huchukuliwa wakati wa kukadiriwa kwake. Na juu ya haya huwa mtazamo wa Mwisho ni mtazamo wa bei wala si mtazamo wa thamani, na kuna tofauti baina ya bei na thamanihata kwa wanauchumi wa Kirasilimali. Bei huhukumu katika kukadiriwa wingi na kutakikana pamoja na uchache wa kuwepo, au wingi wa kuwepo kwake pamoja na uchache wa kutakikanwa, nailo ni jambo linalo ambatana na kuzidisha uzalishaji wala si katika ugawanyaji wake. Ama thamani kukadiriwa kwake ni hakika kwa kipimo ambacho kipo katika bidhaa miongoni mwa manufaa wakati wa kukadiriwa pamoja na kutambua upande wa uhaba bila ya kuchukua katika kukadiriwa, wala kuwepo na kutakikanwa hakuathiri thamani.

Kufikia hapa huwa uchunguzi wa thamani ni wa makosa yaliyo wazi kutoka msingi wake. Na kila kila kilicho pangwa juu yake kutokamana na uchunguzi ni wa makosa yaliyo wazi katika upande mitagaa, isipokuwa thamani ya bidhaa ikikadiriwa manufaa yake kwa manufaa ya bidhaa au juhudhi, itakuwa ndio makadirio sahihi, na itakuwa makadirio yaliyo karibuna uthabiti kwa muda mchache. Ikikadiriwa kwa bei huwa makadirio naya kutegemea wala si makadirio ya kihakika, na huwa wakati huo nui ya kubadilika kila wakati ikifuata soko. Wakati huo hubatilika hali yake kama thamani walw haisadikishwi wakati

na wa'qia wake kwa tamko lathamani, bali huwa ni chombo kinacho patikana ndani yake fedha kwa mujibu wa soko, wala si kwa mujibu wa yaliyomo ndaniyake katika manufaa.

Wanasema wanauchumi wa Kirasilimali kuwa manufaa ni natija ya juhudini ambazo mwanadamu huzitia basi ikiwa malipo si sawa kulingana na kazi basi hapana shaka kiwango cha uzalishaji kushuka. Na kufikia kwa hayo njia ya kipekee ya kusambaza utajiri kwa watu katika mujtamaa ni ile itakayo dhamini kufikia katika mustawa wa juu unaumkinika katika uzalishaji. Msemo huu ni wa kimakosa wazi wazi. Kwani wakia unao shikika, huwa mali ambayo mwenye zi Mungu aliyoiumba katika ulimwengu ndio msingi wa manufaa katika bidhaa, na matumizi ambayo hutumiwa katika ulimwengu ndio msingi wa manufaa katika bidhaa, na matumizi ambayo hutumiwa katika kuzidisha manufaa katika mali haya au kutia manufaa ndani yake pamoja na kazi ndio ambayo imeifanya katika umbo ambalo limefikia kwa manufaa maalum. Kufanya manufaa ni natija ya juhudini tu ni kosa linalokhitilafiana na wakia, na kupuuza mali ghafi, na matumizi ambayo yametumiwa huenda ikawa matumizi hayo ni badala ya mali ghafi na sio badala ya kazi. Na kwa hayo huwa manufaa ni natija ya juhudini za mwanaadamu, na huenda ikawa ni natija ya kuwepo mali ghafi, na huenda ikawa ni natija ya yote mawili pamoja, na siotu natija ya juhudini ya mwanaadamu peke yake.

Ama kuzorota kiwango cha uzalishaji si kwa sababu ya kukosekana usawa wa malipokulingana na kazi tu, huenda ikawaani ntija ya hilo, nahuenda ikawa ni natija ya kumalizika utajiri wote uliopo katika biladi, na huenda ikawa ni natija ya vita, na huenda ikawa ni natija ya mengineo ysio kuwa hayo. Kuzorota kwa uzalishaji katika Uingereza na Ufaransa baada ya vita vikuu vya pili vya ulimwengu sio nayija ya kukosekana usawa wa malipo kulingana na kazi bali ni anatija ya kupungua kwa athari za kila mmoja wao kwa koloni zake zilizokuwa na utajiri, na kumalizwa kwake na vita. Kuzorota kwa uzalishaji Amerika katika vita vikuu vya pili vya ulimwengu sio natija ya kukosekana usawa wa malipo kulingana na kazi bali ni natijaya

kumalizwa na vita dhidi ya Mjerumani. Kuzorota kwa uzalishaji katika ulimwengu wa Kiislamu leo sio natija ya kukosekana usawa wa malipo kulingana na kazi bali niinatija ya kuzorota kifikra ambayo waishi ndani yake umma wa Kiislamu kwa ujumla wake. Kwa hivyo kukosekana kwa malipo kulingana na kazi sio sababu ya kipekee ya kuzorota uzalishaji mpaka ipangika juu ya hayo ndio njia ya kipekee ya usambazajimpaka iwe ndio inayodhamini kunyanyuka kiwango cha uzalishaji. Kufikia kwa kiwango cha juu cha uzalishaji hakina mafungamano yoyotena usambazaji wa utajiri kwa watu.

Wanasema wanauchumi wa Kimagharibi kuwa bei ndio inayo athiri uzalishaji, kwa sababu kinachomsukuma mwanaadamu katika kujitolea, yaani (juhud) ni malipo yake ya kimada. Msemo huu hukhitilafiana na wakia nasio sahihi. Juhudi nyingi anazozitiamwanaadamukwa ajili ya malipo ya kimaanawiya kwa mfano ufahari au malipo ya kiroho kama kupata thawabu za Allah au kujipamba kwa sifa za kiakhlaki kama kutekeleza ahadi. Mahitaji ya mwanaadamu huenda ikawa ni ya kimada, kama faida ya kimada, na huenda ikawa ya kiroho kama kutukuza au ya kimaanawiya kama sifa njema. Kufunga mahitaji kuwa ni mahitaji ya kimada peke yake sio sahihi. Mwanaadamu huenda aktumia mali ili kushibisha mahitaji ya kiroho au mahitaji ya kimaanawiya kwa ukarimu zaidi kuliko kujitoleaa kwake katika kushibisha mahitaji ya kimada. Na kwa haya bei sio pekee inayo athiri uzalishaji, huenda ikawa bei, na huenda ikawa ni jengine. Humoni muashi huenda akashughulisha nafsi yake katika kazi ya miezi katika kukata mawe ya kujenga msikiti, na kiwanda huenda kikafanya uzalishaji wake wa masiku kwa ajili ya kugawanya uzalishaji wake kwa mafukara. Na ummah huenda ukahuisha juhudi zake katika kufukua handaki na kuandaa maandalizi kwa ajili ya kulinda biladi. Jee uzalishaji huo na mfano wakeumeathiriwa na bei? Pamoja na hayo kuna malipo ya kimada yasio fungika kwa bei, huenda ikawa bidhaa nyengine au huduma, basi kufanya bei peke yake ndio inayo athiri uzalishaji sio sahihi.

Na katika la ajabu zaidi mionganoni mwa yaliyotajwa na nidhamu ya uchumi ya Kirasilimali ni kufanya kwake bei ndio pekee

inayopanga usambazaji wa utajiri kwa watu katika mujtamaa. Wanasema kuwa bei ndio pingu ambayo humfanya mwanaadamu kusimama katika kupata na kutumia katika kikomo ambacho hunasibiana na mapato yake, na ndio ambayo hufanya utumiaji wa kila mtu kupungua kwa yale yanayomruhusu mapato yake, na ndio ambayo hufanya utumiaji wa kila mtu kupungua kwa yale yanayomruhusu mapato yae. Kwa hivyo huwa bei kwa kunyanyuka kwake katika baadhi ya bidhaa, na kushuka kwake kwa baadhi ya nyengine, na kupatikana pesa kwa baadhi na kukosekana kwa weGINE, huwa bei kwa hayo ndio yenyE kupanga usmbazaji wa utajiri kwa watumiaji, na huwa sehemu ya kila mtu katika utajiri wa biiladi sio kwa kiwango cha haja zake za kimsingi, bali huwa kwa kiwango cha bei ya huduma ambayo ameitia ndani yake katika kuzalisha bidhaa na huduma, yaani kwa kiwango anachomiliki katika ardhi au rasilimali au kwa kiwango alichosimama nacho katika kazi au kusimamia kwakemiradi.

Kwa msingi huu, nao ni kufanya bei ndio inayo panga usambazaji, huwa nidhamu ya uchumi ya Kirasilimali kuwa imekwisha kiri kuwa hayastahiki maisha ila kwa yule anayeweza kwenda mbio katika kuzalisha bidhaa na huduma. Ama anaeshindwa na hayo kwa sababu ya udhaifu wa kimaumbile, au kwa sababu kumetokea kwake udhaifu wa kighafla basi hastahiki maisha, kwa sababu hastahiki kupata katika utajiriwa biladiyanayo tosha kukidhi haja zake. Hivyo hivyo anastahiki anasa na ubwana na utawala kwa wengine kwa mali yake kila mwenye kuweza kwa haya, kwa sababu ameumbwa na nguvu katika kiwiliwili chake au katika akili yake, na amekuwa na uwezo zaidi kulikko wengineo katika kupata kwa njia yoyote miiongoni mwa njia. Hivyo hivyo huzidisha katika kupata utajiri kuliko wengine kila ikiwa na nguvu mvuto wa mada, na hupungua katika kupata kwake kuliko wengine kila ikiwa na nguvu mvuto wa kiroho na kufungana kwake kwa sifa za kimaanawiyya, ilikumfunga katika kuchuma mada kwa yanayo lazimishwa juu yakena pingu za kiroho, au za kimaanawiyya ambazo amejifunga na fikra zake. Na hili huweka mbali upande wa kiroho na wa kiakhlaki

katika maisha, na huyafanya maisha ni ya kimada, msingi wake ni mapambanoya kimada kwa ajili ya kuchuma njia za kushibisha mahitajiya kimada, na haya ndiyo yanatokea kivitendo katika biladi ambazo zimekubalinidhamu ya Kirasilimali, na biladi ambazo zinaitabikisha..Na imedhihiri katika biladi ambazozimekubali Urasilimali katika nidhamu ya uchumi utawala wa wazalishaji juu ya walaji, na wakawa kipote kidogo miongoni mwa watu kama mashirika makubwa kama mashirika ya mafuta na magari na viwanda vizito na wengineo ndio wanaosimamia wengi wa walaji na wanahukumu juu yao na wanalazimisha juu yao bei maalum ya bidhaa. Na hii ndio iliyo sababisha kuwepo majoribio ya kupiga viraka nidhamu ya uchumi. Wakafanya serikali kuwa na haki katika kuingilia viwango vya bei katika hali maalum ili kuhifadhi uchumi wa nchi, na kuhifadhi walaji, na kufanya kidogo ulaji wa badhi ya bidhaa, na kuweka kikomo kwa utawala wa waliomiliki soko, na wakafanya katika kupanga uzalishaji miraji jumla inayosimamiwa na serikali. Isipokuwa viraka hivyo na mithali yake pamoja na kuwa hugongana na misingi yake pamoja na kuwa hugongana na msingi wa nidhamu ya kiuchumi(nao ni uhuru wa uchumi) hakika yake huwa ni katika hali na dhurufu maalum, zaidi ya hayoni kuwa wengi katika wanauchumi kama watu wa madhab ya ubinafsi hawazitambuina wanazikanusha na wanasema kuwa muundo wa bei peke yake watosha kuhakikisha mapato baina ya maslahi ya wazalishaji na maslahi ya walaji bila ya kuhitajia kwa uangalizi wowote kutoka kwa serikali. Viraka hivyo ambavyo vyalinganiwa na watetezi wa kuingilia kati, hutokea katika dhurufu na hali maalum,pamoja na hilo, hata katika dhurufu na hali hizo hakufanyi usambazaji wa utajiri kwa watu ni wenyе kuhakikisha kushiba kwa mahitaji yote ya watu kushiba kikamilifu.

Kwa hivyo usambazaji mbaya ambao umesimamajuu yake msingi wa uhuru wa kumiliki, na juu ya msingi wa kufanya bei ndio muundo wa kipekee wa usambazaji wa utajiriutasimamia kila mujtamaa unao tabikisha nidhamu ya Kirasilimali. Ama yanayo shuhudiwa ndani ya Amerika kuwa kila mwaamerika amepata utajiri wa kushibisha mahitaji yake yoteya kimsingi,

kushiba kikamilifu, na kushibisha mahitaji mengineo, hilo ni natija ya utajiri mkubwa wa biladi hiyo kiasi cha kuruhusu kila mtu kuweza kushibisha mahitaji yake yote ya kimsingi na baadhi ya mahitaji ya ziada, na sio kwa sababu ya kufanya fungu la mtu kulingana na huduma ambazo amezifanya katika uzalishaji. Kisha kufanya muundo wa bei ndio pingu ya ya uzalishaji kumefanya mashirika ya ukiritimba yaliyoko magharibi kutoka nje ya biladi zao kutafuta masoko mpaka yapate kutokamana nayomali ghafi na masoko ya kuuza bidhaa zao. Yale yanayokumba ulimwengu katika ukoloni wa maeneoya ushawishi na vita vya kiuchumi si kwa jengine ila ni mnatija ya mashirika haya ya ukiritimba, na ni natija ya kufanya bei ndiyo inayo sambaza utajiri. Basi hukusanywa utajiri wa ulimwengu kwa msingi huu na kuwekwa katika mikono ya kirasilimali ya ukiritimba na hayo yote ni kwa ajili ya kaida mbaya zilizo wekwa na nidhamu ya uchumi ya Urasilimali.

Nidhamu ya kiuchumi ya kikomunisti (ujamaa)

Huu ni katika upande wa uchumi wa nidhamu ya Kirasilimali. Ama katika upande wa nidhamu ya uchumi ya Ujamaa na kutokamana nayo Ukomunisti, hakika yake hugongana na nidhamu ya uchumi ya Kirasilimali. Zimedhiihiri rai nyangi za Kiujamaa katika karne ya kumi na tisa, na wakapiga vita wanaujamaa rai za madhhab ya uhuru vita vikali, yaani walipiga vita nidhamu ya uchumi ya Kirasilimali. Ilikuwa kudhihiri Ujamaa kwa nguvu ni natija ya dhulma ambazo zilisibu mujtamaa kutokamana na nidhamu ya uchumi ya Kirasilimali, na kwa ajili ya makosa mengi yaliyomo ndani yake. Tukiangalia madhhab ya kiujamaa hubainika kuwa wana mambo matatu wanayoafikiana, na yanayo watafautisha na wengine mionganimwa madhhab yakiuchumi.

1:- Kuhakikisha aina ya usawa wa kivitendo.

2:- Kupiga marufuku umilikaji wa kibinafsi kijumla au kisehemu.

3:- Kupanga uzalishaji na usambazaji kiujamaa.

Lakini pamojakufikia kwake na mambo haya matatu hukhitilafiana na baadhi yao ikhtilafu iliyo wazi katika maudhui mbali mbali, yaliyo muhimu ya hayo ni:

Kwanza: - Huhitilafiana madhab ya Ujamaa katika upande wa umbo la usawa wa kivitendoambaowanataka kuuhakikisha. Kipote kimoja chasema usawa wa kihisabu, na wanakusudia kwa hayo usawa katika kila kinachonufaisha, basi hupewa kila mtu kutokamana nacho kile kinachopewa wengine. Na kipote chengine chasema usawa wa kijumla , wanakusudia kwayo kuchungwa kazi kwa uweza wa kila na kuchungwa kusambazwa natija kwa mujibu wa mahitaji ya kila mtu. Usawa huhkikishwa kwao wao pindi inapotabikishwa kaida ifuatayo; (Kila mmoja kwa mujibu wa nguvu zake , yaani uweza wake { inakusudiwa kwa haya kazi ambayo anayoifanya} na kila mmoja kwa mujibu wa mahitaji yake{inakusudiwa kwa haya yanayo sambazwa katika uzalishaji}). Na kipote chengine chasema usawa katika mbinu za uzalishaji, kwa upande wa kuwa vitu kiwakia havitoshi kushibisha mahitaji ya kila mtu, basi ni lazima iwe kaida ya usambazaji; (Kila mmoja kwa nguvu zake, yaani uweza wake , naa kila mmoja kwa mujibu wa kazi yake) na uhakikishwa usawa ikiwezekana kupata kila mmoja katika mbinu za uzalishaji kama wanavyopata wengine.

Pili: Huhitilafiana madhab ya Ujamaa kwa upande wa kiwango cha kupigwa marufuku cha umilikaji wa kibinafsi. Kipote kimoja chasema kupigwe marufuku kikamilifu umilikaji wa kibinafsi na huu ndio Ukomunisti. Nakipote chengine chasema kupigwe marufuku umilikaji wa kibinafsi katika upande wa uzalishaji na ndio ambayo huitwa jina la rasilimali. Mfano ardhi, viwanda, reli, migodi na mfano wake , yaani hukatazwa kumiliki kila bidhaa inayo zalisha kitu, basi asimiliki nyumba atakayo ikodisha, wala kiwanda , wala ardhi, wala kinachoshabihiana na hayo. Lakini watabakia watu na umilikaji kwa upande wa utajiri unaoliwa, basi ni sawa wamiliki kila watakacho kila, watamiliki nyumba watakaoishi tu ndani yake, na watamiliki kitakachozaliwa kutokamana na ardhi na viwanda.

Huu ni Ujamaa wa rasilimali. Na kipote chengine chasema kupigwe marufuku umilikaji wa kibinafsi kwa upande wa ardhi ya ukulima na sio nyengine, na hawa ndio wanaujamaa wa wakiukulima. Na kipote chengine chasema; kusomwe kila hali inayo taka maslahi jumla ili kubadilisha umilikaji wa kibinafsikwa umilikaji wa jumla. Na kwa kuzuia watu kumiliki kibinafsi,kwa kuweka kikomo cha mwisho cha faida na kodi, nakikomo duni cha kodi, na kupewa wafanyi kazi sehemu ya rasilimalina mfano wake, na huu huitwa Ujamaa wa Kiserekali.

Tatu:--Hukhitilafiana madhhab ya Kiujamaa katika upande wa mbinu ambazo huzichukua ili kuhakikisha malengo yao. Vyama vya kimapinduzi hutegemea kukomboa wafanyi kazi kwa yale wanayoita kitendo cha moja kwa moja, yaani juhudzi za wafanyi kazi wenyewe kama kwa kuzidisha migomo inayokatiza, uharibifu wa vifaa na kueneza fikra ya migomo jumla baina ya wafanyikazi. Huikuza fikra hiyo mpaka ifike siku watakayo weza kutekeleza matakwa yao kwa kusimama shughuli za kiuchumi na mwishowe kuvunjika nidhamu iliopo ya uchumi.

Ama Ujamaa wa Marx, wao huamini kwa tabia ya kubadilika katika mujtamaa, na wanaitakidi kuwa hilo peke yake latosha kumaliza nidhamu iliopo na kuibadilisha kwa nidhamu nyengine itakayo simama kwa misingi ya Kiujamaa. Ama wenye Ujamaa wa kiserekali mbinu yao katika kutekeleza fikra zao ni kwa kuweka kanuni. Katika kuweka kanuni hutosheleza kulinda maslahi jumla na kutengeneza hali ya wafanyikazi, kam katika kuweka kodi, khasa kodi iliyowekwa juu ya mapato, rasilimali, na mirathi inayo pelekea kupunguza tofauti katika utajiri.

Nne:--Hukhitilafiana madhhab ya Kiujamaa katika upande wa mwili ambao unatakitana kutengenezwa ili kusimamia miradi katika upande wa mwili ambao unatakitana kutengenezwa ili kusimamia miradi katika nidhamu ya Kiujamaa. Mfano wataka wanaujamaa warasilimali kutegemeakupanga uzalishajina usambazaji kwa serikali, katika wakati ambao wanachama wa kimapinduzi wanataka kutegemea usimamiaji kwa kikundi

kilicho pangwa mionganini mwa wafanyakazi wakiongozwa na viongozi wao.

Nadharia za Kiujamaa zilizo maarufu zaidi na kuathiri ni nadharia za Karl Marx ambaye ni Mjerumani. Zimetawala nadharia zake ulimwengu wa Kiujamaa, na kikasimama juu ya misingi yake chama cha kikomunisti, na serikali ya muungano wa Kisovieti katika Urusi, na bado zimebakia nadharia zake ndio zilizo na taathira kubwa mpaka leo.

Na iliyo mashuhuri katika nadharia za Karl Marx ni nadharia ya thamani, ambayo ameichukua kutoka kwa wanachuoni wa uchumi wa Kirasilimali, na kuwashambulia nayo. Adam Smith ambaye huchukuliwa kama kiongozi wa madhhab ya uhuru katika Uingereza na ambayepia huchukuliwa kama ndiye aliye weak siasa ya kiuchumi, yaani nidhamu ya uchumi ya Kirasilimali, amefafanua thamani, akisema: ‘Thamani ya bidhaa yoyote hutegemea kiwango cha kazi iliyotiwa katika kuizalisha.’ Basi thamani ya bidhaa ambayo kuzalishwa kwake kumechukuwa masaa mawili itakuwa marambili ya thamani ya bidhaa ambayo uzalishaji wake hauchukuwi ila saa moja pekee. Akaja baada yake Ricardo na akwa na pupa katika kuweka wazi mtazamo huu wa kazi katika kutambua thamani, akasema; Kinachoweka thamani ya bidhaa sio tu kiwango cha kazi ambayo hutiwa katika uzalishaji wake moja kwa moja, bali hapana budi kuongezwa juu yake kazi ambayo imetiwa zamani katika kuzalisha chombo na ala ambazo hutumiwa katika kazi ya uzalishaji. Yaani Ricardo alikuwa akiitakidi kuwa thamani ya bidhaa hukoma katika matumizi ya uzalishaji wake. Na ameyaweka matumizi hayo kwa sababu moja, nayo ni kazi.

Karl Marx akaja baadaye na akachukuwa mtazamo huu wa Ricardo wa thamani katika uchumi wa Kirasilimali kama silaha ya kuhujumu umilikaji wa kibinagsi, na nidhamu ya Kirasilimali kwa sura yake jumla. Akataja kuwa chanzo cha pekee cha thamani ni kazi inayotiwa katika uzalishaji wake, na kuwa mwekaji rasilimali hununua nguvu za mfanyakazi kwa ujira usiozidi kile ambacho ni cha dharura ili abakie na aweze kazi,

kisha hutumia mwekaji rasilimali nguvu hizo katika kuzalisha bidhaa zinazo pita thamani yake kwa zaidi ya yale anayomlipa mfanyi kazi. Karl Marx amebandika jina kuwa tofauti baina ya anachokizalisha mfanya kazi na anacholipwa kivitendo kuwa ni thamani iliyo zidi, na akaitambua kuwa humathilisha kile anachokiiba mmilikajina wenye kazi katika haki za wafanyi kazi, kwa jina la mapato, faida ya malipo ya rasilimali ambazo hatambui uhalali wake.

Ameona Karl Marx kuwa madhehebu ya Kiujamaa yaliokuja kabla yake hutegemea kufaulu fikra zao kwa yale aliyouumbiwa nayo mwanaadamu kwa kupenda kwake uadilifu na kumsaidia aliyedhulumiwa. Ikawa wanaweka njia mpya wanazo ziitakidi uwezekano wake kutabikishwa katika mujtamaa, na kuzitanguliza kwa watawala, wawekaji rasilimali na tabaka la walio endelea wakiwahimiza kuzitabikisha. Lakini Karl Marx hakujenga madhab yake juu ya hayo wala hakufuata njia waliyoifuata. Amejenga madhab yake juu ya msingi ya falsafa unaojulikana kama mada ya kitarekhe, yaani kinachoitwa mtazamo wa *daelektik*. Akaona kuwa kusimama nidhamu mpya katika mujtamaa kutatimia kwa mujarad wa kutumiwa kanuni za kiuchumi, na kwa mujibu wa kanuni ya kubadilika katika mujtamaa, bila ya kuingiliwa na idara ya uwekaji kanuni au mrekebishaji. Ameuita Karl Marx aina hii ya Ujamaa ‘Ujamaa wa Kisayansi’, ili kuutofautisha na njia za kiujamaa ambazo zimeutangulia na ambazo ameziita ‘Ujamaa wa kindoto’. Kwa ufupi mtazamo wa Karl Marx juu ya Ujamaa ni kama ifuatasvyo:-

Nidhamu ya mujtamaa ambayo inasimama katika zama haiwi illa ni natija ya hali ya uchumi, na kuwa mabadiliko ambayo husibu nidhamu hiyo yote huregea kwa sababu moja, nayo ni mapambano ya tabaka kwa ajili ya kutengeneza hali yake ya kimada. Na tarekhe hutuhadithia kuwa mapambano hayo daima humalizika kwa sura moja, nayo ni ushindi wa tabaka lenye idadi kubwa na hali mbaya kwa tabaka la kitajiri lenye idadi chache na hii ni kile wanachokiita kuwa kanuni ya kubadilika mujtamaa. Nalo katika huambatana na mustaqbal, kama

inavyoambatana na kale. Katika zama za kale yalikuwa mapambano hayo yanapatikana baina ya waungwana na watumwa, kisha baina ya masharifu na watu jumla, na baadaye baina ya masharifu na watu jumla, na baadaye baina ya masharifu na wakulima, na hivyo hivyo baina ya viongozi na machifu katika nidhamu ya kitabaka. Na ilikuwa daima ikikoma kwa kushinda kwa tabaka lililo dhulumiwa na liliona wingi katika idadi juu ya tabakalililo dhulumu lililo chache kiidadi. Lakini baada ya kushinda, hubadika tabaka lililodhulumiwa kuwa ni tabaka linalo dhulumuna kuendeleza ya kale. Tangu mapinduzi ya kifaransa imekuwa mapambano hayo yamesimama baina ya tabaka la kati na kati (Bourgeoisie) na tabaka la wafanyakazi. Lilikuwa la mwanzo ndio mabwana wa miradi ya kiuchumi, na ni wenye kumiliki rasilimalikama inavyokuwa tabaka linalo endeleza ya kale. Na usoni mwake likasimama tabaka la wafanya kazi. Nalo halimiliki chochote katika rasilimali, lakini ni wengi zaidi kiidadi. Huko kuna mgongano baina ya maslahi ya matabaka hayo mawili. NayO huregea katika sababu za uchumi.

Hilo ni kwa nidhamu ya uzalishaji na leo imekuwa haliambatani na nidhamu ya umilikaji. Uzalishaji si wa kibinafsi, yaani kusimamiwa na mtu mmoja peke yake, kama ilivyokuwa katika zama za kale, bali umekuwa ni wakiujamaa, yaani hushirikiana watu ndani yake, wakati ambao nidhamu ya umilikaji haikubadilika kfuatia hayo. Ikabakia umilikaji wa kibinafsi umesimama, wala haijawacha kuwa ni msingi wa nidhamu ya kijamii ya kileo. Ikawa mionganini mwa natija ya hayo ni kuwepo tabaka la nidhamu ya kijamii ya kileo. Ikawa mionganini mwa natija ya hayo ni kuwepo tabaka la wafanyi kazi, nalo lashiriki katika uzalishaji na wala halishiriki katika kumilliki rasilimali na likawa chini ya rehma ya mwenye rasilimali, ambao wenyewe hawashiriki katika uzalishaji katika wakati ambao wanawatumia wafanyi kazi, pindi wasipowalipa katika ujira unaolingana kwa usawa, na mfanyi kazi analazimika kuikubali, kwa sababu hamiliki kazi nyengine. Tofauti baina ya thamani ya uzalishaji na ujira wa mfanya kazi – na hayo ni yale anayo yaita Karl Marx thamani ya bure- huwa ndani yake faida ambayo

hutajirika nayo mrasilimali, pamoja na kuwa uadilifu ni hulazimuisha iwe katika fungu la mfanya kazi. Basi vitabaki vimetangazwa vita baina ya matabaka haya mawili mpaka iwafikiane nidhamu ya umilikaji pamoja na nidhamu ya uzalishaji, yaaani mpaka uwe umilikaji ni wa kiujamaa. Yatakoma mapambano hayo kwa kushinda tabaka la wafanya kazi kwa mujibu wa kanuni ya kubadilika katika mujtamaa kwa sababu ndilo tabaka lililo katika hali mbaya, na lenye idadi kubwa. Ama jinsi litashinda tabaka la wafanya kazina sababu za ushindi wake hilo hutegemea kanuni ya kubadilika kwa mujtamaa. Nidhamu ya maisha ya kiuchumi ya kileo hubebe katika nafsi yake mbegu za majtamaa za amustakbal, nayo imehukumiwa juu yake kuondoka kwa sababu ya kanuni za kiuchumi ambazo yainyenyeka. Basi lilishinda tabaka la kati na kati juu ya tabaka la kisharifuna likatekeleza kazi muhimu katika maisha ya uchumikwa sababu lilikuwa ndilo linalomiliki rasilimali. Lakini leo imekwisha kazi yake na umewadia wakati ambaao litawacha mahali pake kwa ajili ya tabaka la wafanya kazi. Hulazimisha juu yake (kanuni ya kukusanyika pamoja) na kwa vitendo vya ushindani huru. Kwa ajili ya kanuni ya kukusanyika pamoja imekuwa idadi ya wenye rasilimali yapungua na idadi ya wafanyakazi wakuajiriwa inazidi. Vitendo vya ushindani huru huvusha uzalishaji kwa kila kiwango, mpaka idadi ya uzalishaji huzidi yanayo weza kununuliwa na walaji katika tabaka la wafanya kazi ilhali wao wanapokea mishahara isiyo tosha. Litafikisha hilo kwa kutokea mzozo katika tabaka la wafanya kazi. Kila ikisonga mbele nidhamu iliyopo, huzidi athari ya mzozo, na hukaribia wakati wa kutokea kwake, na kila ikipungua idadi ya wenye rasillmali huzidi idadi ya wafanya kazi. Kisha haitochelewa kufika siku itakayo tokea ndani yake mzozo mkubwa kuliko yote iliyo tangulia na itakuwa ni janga kubwa litakalo angusha nguzo za nidhamu uchumi ya Urasilimali, na itasimama juu ya vifusi vyake nidhamu ya Ujamaa. Yuaona Marx kuwa kusimama Ujamaa ndio duru ya Mwisho ya mabadiliko ya kitarekhe. Kwa sababu utakapovunjika umilikaji wa kibinagsi hakutokuwa na mgongano wa kitabaka katika mujtamaa, kwa sababu kutoweka tafauti baina yake.

Ama kanuni ya kukusanyika pamoja ambayo yuwaidekeza Karl Marx ni sehemu katika nidhamu ya Uchumi ya Urasilimali. Na mukhtasari wake ni kuwa kuna harakati zinazo gurisha kazi na rasilimali kutoka baadhi ya miradi mpaka baadhi nyengine, wakati huo hukuwa baadhi yake na huwa midogo baadhi. Hizi zote ni hali zinazo ashiria kutokea mkusanyiko wa pamoja katika uzalishaji. Pindi itakapo chunguzwa miradi ya kutengeneza chokleti utakuta miradi mingi imepungua, katika wakati ambao kila mradi viwango vya nguvu ya uzalishaji vimezidi, ni dalili ya kuwa imetokea mkusanyiko katika kitagaa hichi cha uzalishaji, kwani uzalishaji mkubwa umechukuwa mahala pa mdogo. Kwa mfano, ikiwa idadi ya viwanda ni kumi basi vitakuwa viwanda vinne au vitano, na vitaondoka viwanda vilivyo salia.

Ama mashindano huru yanayo patikana katika maneno yake, humaanisha kaida ya uhuru wa kazi, nayo ni kuwa kila mtu ana haki katika kuzalisha anachokitaka atakavyo.

Ama mizozo ya kiuchumi ambayo yapatikana katika maneno yake, hubandikwa kila msukosuko unaozuka kwa ghafla katika mizani ya uchumi. Mzozo khassa hujumlisha kila aina ya mizozo ambayo hukumba kila kitagaa maalumu mionganoni mwa vitagaa vya uzalishaji na ulaji. Tukio hili hutokea ima katika kuzidisha katika uzalishaji au kupungua kwake, au kuzidi katika ulaji au kupungua kwake.

Ama mzozo jumla wa kiduara hudhihiri kwa umbo la mtingisho mkali unaotingisha nguzo zote za nidhamu ya uchumi, nayo huwa ni nukta ambayo ina tofautisha baina ya kipindi cha nishati na kipindi cha kukwama. Kipindi cha nishati huwa mda wake ni baina ya miaka mitatu na mitano. Na kipindi cha kukwama huwa mda wake hivyo hivyo. Mzozo jumla wakiduara una sifa maalum unaoutafautisha, na muhimu kati yaje ni sifa tatu, nazo ni; sifa jumla inayoiifika nchi moja katika kila upande wa nishati ya uchumi kwa uchache au wingi wake, kisha nayo hudhihiri mwanzo katika biladi moja na kuenea ndani yake,

kisha huenea kutokamana nayo kwa biladi nyengine, ambayo imechukuwa hatua fulani katika maendeleo ya kiuchumi, zilizofungamanishwa na fungamano la kudumu. Sifa ya pili ni sifa ya duara, nayo hutokea kila mara kwa sifa ya kiduara. Na duara ambayo hutofautisha baina ya mzozo mmoja na mwengine huchukuwa baina ya miaka saba na kumi na moja. Isipokuwa kutokea kwake si katika wakati thabiti lakini hutokea kiduara. Ama sifa ya tatu ni kuzidi uzalishaji, huswadifu wenye miradi matatizo makubwa katika kuuza uzalishaji wao, kwa kuzidi viwango juu ya mahitaji kwa wingi wa vilivyozaishwa, basi hutokea mizozo.

Karl Marx aliona mizozo hii hufikisha kwa baadhi ya watu kukosa rasilimali zao, basi itapungua idadi ya wenye rasilimali, na itaidi idadi ya wafanyi kazi, na itafikisha katika kutokea mzozo mkubwa katika mujtamaa utakao angamiza nidhamu ya kale.

Huu ni mukhtasari wa Ujamaa na Ukomunisti ni aina moja miongoni mwa aina zake. Na kutokamana na na mukhtasari huu hubainika kuwa madhehebu yote ya Ujamaa ukiwemo ndani ake Ukomunisti, hufanya kazi ili kuhakikisha usawa wa kivitendo baina ya watu, ima ni usawa usawa wa kimanufaa au usawa katika mbinu za uzalishaji au usawa katika kila kitu. Kila aina ya aina ya usawa huu ni muhali kutokea n ni jambo la kindoto. Hilo ni kuwa usawa katika jinsi ilivyo hauwezekani na haiwezekani kivitendo. Ama kuwa haiwezekani kwa kuwa watu kwa tabia ya maumbile yao hutofautiana katika nguvu za kimwili na kiakili, na hutofautiana katika kusbisha mahitaji. Basi usawa baina yao hauwezi kutokea. Kwani ukifanya usawa baina yao katika kupata bihaa na huduma kwa lazima kinguvu, chini ya nidhamu katili, basi haimkiniki kuwa sawa katika kutumia mali hii katika uzalishaji, wala katika kunufaika nayo, wala haimkiniki kuwa sawa baina yao kiwango cha kushibisha mahitajiyao, basi usawa baina yao ni jambo la kinadharia na ni ndoto.

Pamoja na kuwa usawa wenyewe baina ya watu ilhali wana tofauti katika nguvu, huchukuliwa ni mbali na uadilifu ambao wadai wanaujamaa kuwa wanajaribu kuuhakikisha. Kuzidiana baina ya watu na kutofautiana katika kukusanya manufaa, na katika mbinu za uzalishaji ni jambo la kawaida. Kila jaribio la usawa ni lazima litashindwa kwa sababu hugongana na umbile la kutofautiana lilioko baina ya watu mionganoni mwa banadamu.

Ama kuondoa umilikaji kikamilifu hili hugongana na umbile la mwanaadamu. Kwa sababu umilikaji au kukusanya ni dihirisho mionganoni mwa madhihirisho ya ghariza ya kuhifadhi maisha. Nalo ni lazima liwepo katika mwanaadamu. Kwa sababu ni la kimaumbile ndani yake, na ni sehemu katika muundo wake, na ni dhihirisho mionganoni mwa dhihirisho la nishati yake ya kikawaida, basi haimkiniki kuondolew kwa sababu ni la kighariza. Kila lililo la kighariza haliwezi kung'olewa kutoka mwanaadamu maadamu uhai watambaa ndani yake. Majaribio yoyote ya kuiondoa si lolote bali ni kumgandamiza mwanaadamu, na hilo humfikisha kwa matatizo. Kwa hivyo imekuwa nijambo la kawaida kupangiwa nidhamu ghariza hiyo waa si kuiondoa.

Ama umilikaji wa kisehemu, hilo ni la kuangaliwa. Ikiwa ni kuweka kikomo kiwango cha kumiliki bidhaa kwa kiwango maalim kisichovukwa, basi itakuwa ni kuweka kikomo kwa umilikaji wote, na hili halijuzu kwa sababu huweka kikomo nishati ya mwanaadamu, na huharibu juhudii zake na hupunguza uzalishaji wake. Hakika pindi anapo zuiliwa mtu kukusanya kinachozidi kiwango Fulani, wao humzuia kwenye kikomo hicho na huumharamishiya kuendelezambele nishati yake, na jamii huharamishiwa kunufaika kwa juhudii za watu hawa.

Ikiwa umilikaji wa bidhaa na huduma umefungwa kwa jinsi maalum bila kuweka kikomo jumla, hilo lajuzu kwa sababu haliweki kikomo kwa nishati ya mwanaadamu, na kwa kuwa hilo hupanga ukusanyaji wamalibaina ya watu na husaidia katika juhudii na kuzidisha nishati.

Ikiwa kuondoa umilikaji kisehemu huwekea kikomo mali maalum anayo katazwa mtu kuimiliki, na huruhusiwa kumiliki asokuwa hayo bila kuwekewa kiwango malum, hakika yake haina budi kutizamwa. Ikiwa asli a malihii ambayo yapatikana ndani yake umbile la kunufaika nayo yasiyowezekana kukkusanywa na mtu binafsi eke yake, ila kwa kunyimwa nayo jumla ya watu, tukitizama kushirikiana kwa manufaa ndani yake baina ya watuni jambo la kawaida, kama mabarabara jumla, mabustani ya miji, mito, bahari, nayanayo fanana na hayo. Kumnyima mtu binafsi kuzimiliki peke yake bila wengine ni jambo la kawaida lililokiriwa na asli ya mali, basi hakuna kosa wakati huo katika kumnyima mtu binafsi peke yake kumiliki bila wengine.

Ikiwa asli ya mali hairuhusu hayo hutizamwa ikiwa mali yameungana na yale yaliyo katika asli yake nayo ni kuwa hairuhusu kumiliwi na mtu binafsi ila kwa kunyimwa nayo jumla ya watu kama mali ambayo asli yake haiwezi kumiliwi yote na mtu binafsi, mfano maji na madini yasio katika, hakika hakuna makosa kumnyima mtu binafsi katika kuzimiliki, kwa sababu zimefungana na yale yalio asli yake nayo ni kuwa haimiliwi na mtu binafsi illa kwa kunyimwa jumla yao. Ambayo yamefanya kufungika kwa mali hiyo ni kuwa asili yake haiwezi kumiliwi na mtu binafsi illa kwa kunyimwa jumla yao. Ama ikiwa mali haikufungika kwa hayo kama mali yaliosalia, hakika yake haijuzu kunyimwa mtu kuimiliki. Itakuwa wakati huo ni kuweka kidhulma kikomo katika kumiliki mali, kwa kuruhusukumili baadhi na kunyimwa zengine. Nayo ni kama kuweka kikomo cha kumiliki mali kwa kiwango maalum, na huwa ni kama kuweka kikoo kwa umilikaji wote, na hufikiwa na natija hizo hizo, nayo ni kuwekewa kikomo nishati za mwanaadamu, kuharibu juhud zake, na kpunguza uzalishaji wake, na humzuia kufanya kazi pindi anapofika katika kiwango ambacho ameruhusiwa ye ye kukusanya, pindi anaponyimwa kuzidisha juu yake.

Kuondoa umilikaji kisehemu katika Ujamaa huwa ni kikomo kwa yote, na sio kikomo kwa namna ya umilikaji, nayo ni kuzuia umilikaji wa baadhi ya mali ambazo katika umbile lake na tabia ya asili yake hukusanywa kibinafsi. Ujamaa imma huwekea kikomo umilikaji kwa kiwango, kama kuwekewa kikomo umilikajin wa ardhi kwa masafa maalum, ama kuwekewa kikomo umilikaji wa mali maalumanayo nyimwa mtu binafsi kumiliki kama kuwekewa kikomo katika mbinu za uzalishaji. Pamoja na kuwa mali hizo kwa maumbile yake zaweza kkumilikiwa na mtu binafsi. Kuwekaea vikomo umilikaji katika Ujamaa ni katika aina hii. Nayo ni kunyima umilikaji wa mali ambazo kwa tabia yake humilikiwa kibinafsi, na kunyima umilikaji umilikaji wa mali hizo huweka kikomokwa nishati, sawa sawa zimetengwa mali hizo kikanunikama kunyimwa haki ya kurithi, au kunyimwa umilikaji wa migodi na njia za reli, viwanda na yanayo fanana na hayo, au kuiachia serikali kukataza kila inachoona ni cha maslahi jumla kinacho faa kunyimwa. Hayo yote huweka kikomo kwa nishati za watu maadamu mali ambazo zimenyimwa ni katika maumbile yake kuwa zaweza kumilikiwa kibinafsi.

Kupangilia nidhamu ya uzalishaji na usambazaji kupitia jamaa kwa kuchochea vurugu, hilo haliwachi kuleta mashaka na fujo baina ya watu, na huleta uhasidi na chuki baina yao. Hilo humaanisha kuleta mchafuko, na sio kuweka nidhamu. Wala haiwi kawaida katika kuwaacha wafanyi kazi kuhisi dhulma kutoka kwa wenye mali, kwa sababu huenda wakawa wenye mali ni mionganini mwa wajuzi katika kushibisha mahitaji yote ya wafanyi kazi, kama ilivyo hali ya afanyi kzi wa viwanda America. Hawahisi dhulma inayotokea juu yao kwa sababu ya ukubwa wa matunda ya juhudi zao, na wala haiwi wakai huo kuwa mabadiliko ndio yenye kupanga uzalishaji na ulaji. Kwa hivyo hakuna budi nidhamu hizi kwa hukmu na suluhisho sahihi, zilizo na msingi ulio katikiwa, zinazo afikiana na wakia wa matatizo. Ujamaa wategemea katika kupanga uzalishaji na usambazaji ima kwa kuleta mashaka na fujo baina ya wafanyi kazi au kwa kuweka sheria na kanuni za kutungwa zisizo

tegemea msingi uliokatikiwa. Kwa hivyoimekuwa kupangwa kwake huku ni kwa makosa kutoka msingi wake.

Hii ni bayana ya makosa ya Ujamaa kwa jinsi ilivyo. Ama makosa ya Ujamaa wa Karl Marx kwa aina maalum, hutokea kwa jinsi tatu:

Kwanza: Rai yake katika nadharia ya thamani ni ya kimakosa kutoka msingi wake inayo huhitilafiana na wakia. Hakika kufanya sababu ya kipekee kwa thamani ya bidhaa kuwa ni kazi iliyotiwa katika uzalishaji wake huhitilafiana na wakia, kwa sababu kazi iliyotiwa ni sababu mionganini mwa sababu za thamani ya bidhaa na sio sababu ya kipekee. Kuna vitu ambavyo sio kazi vinavyoingia katika thamani ya bidhaa. Kuna mali ghafi iliyofanyiwa kazi juu yake, na kuna kuhitajia kwa manufaa ya bidhaa hizo. Huenda ikawa mali ghafi akusanya manufaa kuzidi kazi ambayo yatiwa katika kupatikana kwake, mfano kama kuwinda. Huenda ikawa manufaa ya bidhaa hizo hazitakikaniwi sokoni, na hairuhusiwi kuzizalisha kama tembo kwa waislamu. Basi kufanya kazi ndio sababu ya kipekeeya thamani sio sahihi, wala haiambatani na wakia wa bidhaa kwa jinsi ilivyo.

Pili: Msemo wake yakuwa ni nidhamu ya jamii ambayo yasimama katika zama si kitu illa ni natija ya kiuchumi, na mabadiliko tofauti tofauti ambayo yakumba nidhamu hiyo, yote hurudi kwa sababu moja, nayo ni mapambano ya matabaka ya jamii kwa ajili ya kuboesha hali yake ya kimada. Msemo huu ni wa kimakosa unauhitilafiana na wakia, uliojengwa juu ya kufaradhisha nadharia ya kidhana. Ama upande wa makosa yake na kuhitilafiana kwake na wakia dhihirisho lake ni la kitarekhe na ni la kiwakia. Urusi iliyo Sovieti ilipobadlika na kuwa Ujamaa, hayakupatikana hayo kama natija ya mabadiliko ya kimada, na sio kupitia mapambano ya kitabaka yaliyo fikisha kwa kubadilika nidhamu moja kwa nidhamu nengine. Bali kilifikia tawala kikundi kupitia njia ya mapinduzi ya kidamu, kikatabikisha fikra zake juu ya watu na kikabdalisha nidhamu. Hiivyo hivyo ndio hali katika Jamhuri ya watu wa China. Utabikishaji katika Ujerumani Mashariki wala si Ujerumani

Magharibi, na juu ya nchi za Uropa mashariki wala si Uropa magharibi, hayo hayakutokea kama natija ya mapambano yoyote baina ya matabaka bali iliatikna kupitia kutawla serikali ya Kiujamaa juu ya nchi hizo na ikatabikisha juu yake nidhamu yake. Kama inavyo patikana katika nidhamu ya Kiraslimali na ilivyo tokea katika nidhamu ya Kiislamu, na kama inavyo tokea katika nidhamu yoyote nyengine. Pamoja na kuwa biladi ambazo zilitarajiwa kubadilisha nidhamu iliyopo kupitia mapambano ya kitabka, nazo ni Ujeruman, Uingereza, na America ni bladi za Kiraslimali ambazo wameithiri ndani yake wenye rasilimali na wafanyi kazi. Haikuwa Urusi a Kiaisiri wla Uchina ambazo zote zilikuwa ukulima ndani yake ni zaidi kuliko viwanda, na ambazo tabaka la wafanya kazina warasilimali ni kidogo pindi inapolinganishwa na nchi za kimagharibi. Pamoja na kuwepo matabaka baina ya warasilimali na wafanyi kazi katika nch za Uropa magharibi na katika America hazikugura kwa Ujamaa, na zote zimebakia zikitabikisha nidhamu ya Kiraslimali, bila ya kuathirika na taathira oyote pamoja na kuwepo tabaka la wafanyi kazi na tabaka la wamilikaji rasilimali katika nidhamu yake, na hii peke yake yatosha kuvunja mtazamo huo kutoka msingi wake.

Upande wa tatu unao bainika ndani yake makosa ya mtazamo wa Karl Marx ni katika anachokisema juu ya kanuni ya kubadilika mujtamaa, na kwa nidhamu ya maisha imehukumiwa kumalizika kwa sababu ya kanuni ya kiuchumi inayo inyenyekea, nakuwa tabaka la kati na kati ambalo limeshinda juu ya tabaka la kimasharifu, na likawa ndio lenya kumiliki rasilimali, imewadia wakati ambao litawacha mahali pake kwa tabaka la wafanyi kazi na hulazimisha hil juu yake kwa kanuni ya kukusanya. Ama upande wa ksa hili ni kuwa nadharia ya Karl Marx katika kukusanya uzalishaji ambao amejenga juu yake kuzidi kwa idadi ya wafanyi kazi na kupungua wenye rasilimali ni mtazamo wa kimakosa. Kwani kuna kikomo kisicho vukwa na uksanyaji wa uzalishaji. Inapofikia kikomo maalum husimama, basi si sawa maadiliko anayo yatazamia Karl Marx. Inapatikana katika mkusanyiko sababu tofauti tofauti za uzalishaji kwa kikomo inacho simama kwake bila kukivuka.

Juu ya yote hayo hakika kukusanya uzalishaji kattu hakupatikani katika kitagaa cha uzalishaji nacho ni ukuima. Basi viyi yaeza kupatikana katika mujtamaa? Pamoja na kuwa Karl Marx adhania kukusanya uzalishaji hufuatwa na kukusanywa utajiri hali inayo punguza idadi ya wafadhili ambao wana athirika na rasilimali, na kuzidi idadi ya wafanyi kazi ambao hawamiliki kitu chochote. Hili I kosa kwa sababu kukusanywa uzalishaji huenda ikazuka kutokamana na kuzidi idadi ya wenyewe rasilimali, na huenda ikazuka kutokamana nayo wafanyi kazi kuwa wenyewe rasilimali. Katika mashirika ya hisa ambayo huchukuwa ada za miradi mingi mikubwa huwa wanahisa wengi ni wafanyi kazi basi viyi hutokea kukusanywa uzlishaji? Juu ya hilo hakika katika viwanda kuna wafanya kazi walio na mishahara mikubwa kama wahandisi, wanasayansi na wakurugenzi, na waweza kuwejka akiba kiasi kikubwa cha ishahara yao wanayotmia kufadhili vitu vyengine visivyo kuwa vya kimahitaji na kuanzisha miradi ya siku za usoni. Wakati huo haitabikishiki juu yao nanayo yasema kwayo Karl Marx juu ya wafanya kazi katika kubadilika.

Huu ni mfano wa msingi ambao umesimama juu yake nidhamu ya uchumi ya Urasimali, na msingi ambao umesimama juu yake nidhamu uchumi ya Ujamaa na kutokamana nayo Ukomunisti, na ishara ya kiufupi kwa yale yaliyomo katika misingi hiyo katika ubovu na makosa. Hi kwa upande mmoja na kwa upande mwengine ni kuwa huhitilafiana na njia ya Uislamu katika kuchukwasuluhisho, na hugongana na Uislamu.

Ama katika upande wa kuhitilafiana kwake na njia ya Uislamu katika matatizo ya mwanaadamu. Ama katika upande wa kuhitilafiana kwake na njia ya Uislamu katika matatizo ya mwanaadamu, uislamu namna yake ya kusuluhisha matatizo ya kiuchumi ni njia moja ile ile inayotumika na uislamu kusuluhisha matatizo ye yote yale ya kibinadamu. Kama kawaida uislamu huangalia ukweli hasa wa wa tatizo la uchumi, kulielewa na kulitafutia suluhisho kutoka kwa **shariah** baada ya kusoma marudio yetu ya sheria na kuhakikisha kwamba inafaa kuchukuliwa kama hatua ya kufuata katika kusuluhisha. Kwa

hana ndio hutofautiana baina yake uraslimali na ujamaa. Uraslimali, hali iliyopelekea kusababisha tatizo, ndio inayo tumika kama chimbuko la suluhisho. Ujamaa suluhisho huchukuliwa kutoka kwa nadharia za kufikiriwa kama kielelezo cha tatizo na suluhisho linawekwa kutokana na fikra hizo. Kwa hivyo kila moja katika hizo ni tofauti na njia za kiislamu na haifai mwislamu yeyote kuchukua kutoka na na suluhisho hizo za kikafiri.

Ikhtilafu ya uraslimali na ujamaa ambayo kwake ni ukumunisti, uchumi kwa uislamu ni kwamba uislamu huchukuasuluhisho kutoka kwa wahyi (*akhkam shariah*). Hali uraslimali na ujamaa suluhisho zake ni kutokamana na ukafiri. Kulingana na wao kuhukumu ni kutumia sheria zisizotoka kwa Allah SWT ambayo haikubaliwi kiislamu na mwislamu hafai kuitumia kwa njia yeyote ile. Kuzifuata ni ufasiqi kwa yule asiyeziamini. Na ikiwa anaziamini kuwa ni sheria sawa na kuwa uislamu hauwezi kuhukumu katika zama za sasa (modern age) na hauwezi kutoa suluhisho kwa matatizo ya uchumi wa kileo basi huyo amekufuru, Ewe Allah SWT tuhifadhi kutokamana na fikra hizo. Amin.

2. Uchumi

Neno uchumi (iqtisaad) limetolewa kutoka kwa neno la kizamani la kireno limaanishalo mpangilio wa kinyumbani (*home affairs*) kwa namna kwamba wahusika mahiri (active members) hujumuika katika kukutengeneza bidhaa na huduma na wote katika wahusika hugawanya kile walicho miliki. Ikaendelezwa maana hiyo hadi kufikia kumaanisha jamii inayo tawaliwa na dola.

Hawakukusudia kulitumia neno uchumi (iqtisaad) kwa maana yake ki neno kumaanisha vyombo miliki (*property*) ima kwa kuongezeka kwake au ama kuhifadhi utengenezaji wake, ambayo imezungumziwa katika uchumi wa kisayansi ama kwa namna ya ugawaji wake ilivyozungumziwa katika nidhamu ya uchumi.

Ingawa uchumi wa kisayansi na nidhamu ya uchumi zote zahusika na uchumi lakini maana yake si sawa. Nidhamu ya uchumi haiathiriki na panda shuka za ungi wala uchache (*fluctuation*) wa mali. panda shuka hizi wala haziathiri muundo wa nidhamu ya uchumi. Kwa hivyo ni makosa kuliangalia suala la uchumi kama somo moja na kulijadili kama kipengee kimoja, inayosababisha kutojua tatizo la uchumi linalostahili suluhisho au kutofahamu sababu zinazo changia kuongezeka kwa mali katika nchi. Hii ni kwa sababu usimamizi wa mambo ya kijamii kwa mujibu wa kuzalisha mali ni kipengee kimoja na usimamizi wa mambo ya kijamii ni kipengee kingine. Kwa hivyo mas'ala ya usimamizi wa uchumi lazima yatofautishwe na mas'ala ya usimamizi wa ugawaji wake. Ya kwanza inahusika na mbinu na ya pili yahusika na fikra. Nidhamu ya uchumi yatakiwa izungumziwe kama fikra iliyotegemezewa kwa mtazamo wa maisha na uchumi wa kisayansi upewe mtazamo usio kuwa na uhusiano wowote na mtazamo wa maisha.

Jambo muhimu sana katika mas'ala haya ni nidhamu ya uchumi, kwa sababu nidhamu ya uchumi huashiria/huzungukia mahitaji ya kibinadamu, namna ya kuyashibisha na namna ya ufuatiliaji. Kwa sababu mbinu zitele kila mahali mbinu hizi ndizo zinazo msukuma mwanadamu kuzitunga. Aidha tatizo lililoko katika mahusiano ya watu ima katika jamii inayopelekea kuwabana watu kutokamana na kuzitumia mbinu hizi. Hii ni kwa sababu ya mwanadamu kumiliki mbinu hizi. Na huundio msingi wa matatizo ya uchumi ambao sharti yasuluuhishwe. Kwa hivyo tatizo la uchumi hupatikana kutoka kwa kipengee cha kumiliki manufaa wala sio kubuni mbinu za kuleta manufaa.

Msingi wa nidhamu ya uchumi

Manufaa ya kitu huhusisha uzuri wake wa kushibisha mahitaji ya mwanadamu. Manufaa ni mambo mawili. **Kwanza** ni ghariza za mwanadamu kutimiza lengo. **Pili** uzuri wa kukuwa ndani yake na kushibisha mahitaji ya mwanadamu kinyume na mahitaji ya mtu binafsi. Manufaa haya hupelekea ima juhudzi za kibinadamu, bidhaa au zote. Neno juhudzi za kibinadamu humaanisha fikra na vitendo anavyojiendezea kuanzisha kukuza

mali au kunufaika nayo. Neno bidhaa huhusha kila kitu kinachomilikiwa katika kutumiwa kutaka kuuza au kukopa ima katika matumizi ya kikawaida kama tunda au gari ama katika matumizi kama kukopa mashini au nyumba. Mali huhusisha pesa kama dhahabu fedha bidhaa kama nguo vyakula vitu visivyo songeshwa kama nyumba na viwanda na vyote vinavyomilikiwa. Kwa sababu mali yejote ile hushibisha mahitaji ya kibinadamu na juhudzi za kibinadamu ni mbinu ya kupata mali na manufaa yake, halafu mali ni msingi wa manufaa, hali juhudzi ni humuwezesha tu kupata mali. Asli ya mwanadamu ni kutaka kumiliki mali. Kwa hivyo juhudzi mwanadamu na mali ndizo silaha zitumiwazo kushibisha mahitaji yake. Kwa hivyo mali ni **bidhaa (maal) na juhudzi pamoja**.

Imma kwa kutumia mpaka imalizike kama tufaha au kwa kutomalizika kama gari, na imma kwa kunufaika nayo kama kuazima kifaa, na kuishi nyumba ya kupangisha. Na hujumuisha mali za kifedha kama dhahabu na fedha, na bidhaa kama nguo na vyakula, na majengo kama nyumba na viwanda, na yasio kuwa hayo mionganoni mwa zinazo milikiwa. Na kwa kuwa mali ndio ambayo hushibisha mahitaji ya mwanaadamu, na haikuwa juhudzi ya mwanaadamu illa ni chombo cha kuifikia mali yenye na kunufaika nayo, kwa hivyo imekuwa mali ndio msingi wa manufaa. Amma juhudzi ya mwanaadamu nayo ni mionganoni mwa mbinu, ambazo humuezesha kufikia mali. Na kufikia hapa amekuwa mwanaadamu kwa maumbile yake huenda mbio ili kupata mali. Huwa juhudzi za mwanaadamu na mali ni vyombo ambavyo hutumiwa ili kushibisha mahitaji ya mwanaadamu, na ndizo utajiri ambao mwanaadamu huenda mbio ili kuifikia na kukusanya. Basi utajiri ni mkusanyiko wa mali na juhudzi.

Kukusanya watu utajiri huwa imma kutoka watu wengine kama kupata mali kuitia tunu na imma sio kutoka watu kama kukusanya mali moja kwa moja kutoka mali ghafi, na huwa imma dhati yake ili kuitumia na kunufaika kama kupata tufaha na kumiliki nyumba na imma kuikusanya ili kunufaika na dhati yake kama kupangisha nyumba na imma kuikusanya ili

kunufaika na natija inayotokamana na juhudi ya mwanaadamu kama ramani ya nyumba kutoka kwa muhandisi.

Kukusanya huku mali kwa njia zake zote imma huwa kwa malipo kama kuuza, kukodisha kitu na ujira wa aloajiriwa na imma bila malipo kama tunu, urathi na kuazima. Na kwa hayo huwa tatizo la kiuchumi ni katika kukusanya utajiri na sio katika kuleta utajiri. Nao hutokea kutokamana na matatizo juu ya kukusanya yaani umilikaji, na kutokamana na utumiaji m'baya wa umilikaji huo, na kutokamana na usambazaji m'baya wa utajiri baina ya watu, wala kata kata hautokamani na yasiokuwa hayo. Kwa hivyo imekuwa kutatua upande huo ndio msingi wa nidhamu ya kiuchumi.

Kwa hayo huwa msingi ambao umejengwa juu yake nidhamu ya kiuchumi imesimama juu ya nguzo tatu nazo umilikaji, utumiaji na milki na usambazaji wa utajiri baina ya watu.

MTAZAMO WA UISLAMU KWA UCHUMI

Hukhitalifiana mtazamo wa uislamu kwa mada ya utajiri na mtazamo wake wa kunufaika nayo, na kwake ni mbinu ambazo huleta manufaa ni kitu, na kukusanya manufaa ni kitu chengine. Basi mali na juhudi za mwanaadamu ni mada ya utajiri, nazo ni mbinu ambazo huleta manufaa, na kueka kwake katika mtazamo wa uislamu kwa upande wa kuwepo kwake katika maisha ya duniani na kwa upande wa kuwa uzalishaji wake hukhitalifiana na hali ya kunufaika nazo, na jinsi ya kukusanya manufaa hayo. Nao huenda ikaingilia katika kunufaika na utajiri kuingilia kuliko wazi, basi ikaharamisha kunufaika na baadhi ya mali, kama tembo na mfu, kama pia imeharamisha kunufaika na baadhi ya juhudi za mwanaadamu kama kucheza dansi za umalaya. Ikaharamisha kuuza kilicho haramishwa kuliwa kwake katika mali, na ikaharamisha kuajiri kilicho haramishwa kitendo chake miongoni mwa vitendo. Hii ni katika pande wa kunufaika na mali juhudi za mwanaadamu. Amma katika upande wa jinsi ya kukusanywa kwake hakika imekwisha weka hukmu tofauti tofauti za kukusanya utajiri kama hukmu za kuwinja, kuhuisha

ardhi na kama hukmu za kuajiri na kuunda viwanda na kama hukmu za urathi, tunu na wasiya.

Hii ni kwa upande wa kunufaika na utajiri na jinsi ya kuukusanya. Amma kwa upande ya mada ya utajiri katika hali ya uzalishaji wake uislamu umehimiza uzalishaji wake, na ikashajiisha wakati ilipo shajiisha kuchuma kwa sura yake jumla wala haikuingilia katika kubainisha jinsi ya kuzidisha uzalishaji na kiwango cha kuzalisha, bali liliwaacha hilo kwa watu wenye kulihakikisha kama wanavyotaka. Amma katika upande wa kuwepo mali katika maisha ya duniani hilo huwa kimaumbile, Allah (swt) viumbe vyake amevidhalilishia mwanaadamu. Asema Allah Ta'ala:-

{ هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا }

“*Ndiye yeye aliyekuumbeni vyote vilivyomo katika ardhi*” (Al-Baqarah 29) Na asema:

{ اللَّهُ الَّذِي سَخَّرَ لَكُمُ الْبَحْرَ لِتَجْرِيَ الْفُلُكَ فِيهِ بِأَمْرِهِ وَلَتَبْغُوا مِنْ فَضْلِهِ }

“*Allah ndiye aliyekutiishieni bahari ili humo zipite marekebu kwa amri yake na ili muzitafute fadhila zake*” (Al-Jathiya 12) Na Asema:-

{ وَسَخَّرَ لَكُمْ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مِنْهُ }

“*Na amekutiishieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini vyote vimetoka Kwake*” (Al-Jathiya 13). Na Asema:-

{ فَلَيَنْظُرْ إِلَيْنَا إِلَى طَعَامِهِ - أَنَّا صَبَبْنَا الْمَاءَ صَبَّاً - ثُمَّ شَقَقْنَا الْأَرْضَ شَقَّاً - فَأَنْبَبْنَا فِيهَا حَبَّاً - وَعِنْبَاً وَقَضْبَاً - وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا - وَحَدَائِقَ عَلْبَانًا - وَفَاكِهَةَ وَأَبَانًا - مَتَاعًا لَكُمْ وَلَا نَعِمَّكُمْ }

“*Hebu mwanaadamu naatazame chakula chake. Hakika sisi tumemimina maji kwa nguvu. Tena tukaipasua ardhi kisha tukaotesha humu (vyakula vilivyo) chembe chembe. Na mizabibu na mboga. Na mizeituni na mitende. Na mabustani (mashamba) yenye miti iliyosongana barabara. Na matunda na malisho. Kwa ajili ya kukustarehesheni nyinyi na wanyama wenu*” (Abasa 24-32). Na Asema:-

{ وَعَلَمْنَاهُ صَنْعَةَ لَبُوْسٍ لَكُمْ لِتُحْصِنَكُمْ مِنْ بَأْسِكُمْ }

“*Na tukamfundisha (Daud) matengenezo ya mavazi ya vita kwa ajili yenu ili yakuhifadhini katika mapigano yenu*” (Al-Anbiyaa 80). Na Asema:-

{ وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنَافِعٌ لِلنَّاسِ }

“Na tumekiteremsha (tumekiumba) chuma, chenye nguvu nyingi na manufaa Kwa watu” (Al-Hadid 25)

Akabainisha katika ayah hizi zinazo shabihiana nazo kuwa yeye ndiye aliyeumba mali, na akaumba juhud ya mwanaadamu na wala hakugusa jambo lolote jengine linalo ambatana nalo, hali inayoonyesha kuwa haikuingilia mada ya mali, na wala katika juhud za mwanaadamu, isipokuwa yeye amebainisha kuwa ndiye aliyeviumba ili watu wanufaikie nayo. Hivyo hivyo haikuingilia katika kuzalisha utajiri, wala haipatikani adili ya kisheria inayoonyesha kuwa Uislamu umeingilia katika uzalishaji wa utajiri, bali kinyume na hilo twakuta dalili za kisheria zinazoonyesha kuwa sheria imeliwacha jambo hilo kwa watu katika kutoa mali, na katika kuboresha juhud za mwanaadamu. Imepokelewa kuwa Mtume Rehema na Amani zimfikie, amesema katika maudhui ya utungani mbegu za mtende **“nyinyi ni wajuzi kwa mambo ya dunia yenu”** na imepokelewa kuwa yeye Rehma na Amani zimfikie amewatuma wawili kati ya Waislamu kwenda Jurash Al-Yaman ili wajifunze kutengeneza silaha. Hii ni dalili ya kuwa Sheria imeliwacha jambo la uzalishaji mali kwa watu, waizalishe kwa mujibu wa ujuzi wao na maarifa yao.

Kwa haya hubainika kuwa uislamu hutizama nidhamu ya kiuchumi na sio elimu ya kiuchumi, na imefanya kunufaika na utajiri, na jinsi ya kukusanya manufaa hayo kuwa ni maudhui ya uchunguzi, wala haikuwekea vikwazo uzalishaji wa utajiri wala juu ya mbinu za manufaa kata kata.

SIASA YA KI-UCHUMI KATIKA UISLAMU

Siasa ya ki-uchumi ndio lengo ambalo lililokusudiwa na hukmu ambazo hutatua upelekaji mambo ya mwanaadamu.

Siasa ya ki-uchumi katika uislamu ni kudhamini kushibishwa mahitaji yote ya kimsingi ya kila mtu kushiba kikamilifu, na kumwezesha kushibisha mahitaji ya kiziada kwa kadri ya uweza wake, kwa kumchukulia kuwa yuwaishi katika mujtamaa maalum, olio na mtindo wake maalum wa kimaisha, nao

humuangalia kila mtu kwa jicho lake, na wala sio kwa mkusanyiko wa watu wanaoishi katika biladi. Humtizama yeze mwanzo kama mwanaadamu ambaye hana budi kushibisha mahitaji yake yote ya kimsingi kushiba kikamilifu, kasha pili kwa kumuangalia kwa utu wake wa kipekee kwa kumwezesha kushibisha mahitaji yake ya kiziada kwa kadri anavyoweza. Na humtizama wakati huo huo kwa kuwa amefungika pamoja na wengine kwa mafungamano maalumu, unaopelekwa kwa mwenendo maalumu kwa mujibu wa mtindo maalumu. Na kwa haya hakika ya siasa ya ki-uchumi katika uislamu sio tu kuinua kiwango cha maisha katika biladi bila ya kutizama katika kudhamini kunufaika kila mtu katika maisha haya, na wala sio kuwafanya watu wajitosheleze na kuwawacha huru katika kuchukua kwao kutokamana nayo kwa kadri ya uweza wao, bila ya kutizama katika kudhamini haki ya maisha ya kila mtu kati yao yejote atakae kuwa, bali ni kutatua matatizo ya kimsingi ya kila mtu kwa kumchukuwa kuwa ni mwanaadamu anaeishi kwa mujibu wa mafungamano maalumu, inaomuezesha kumnyanyua kiwango chake maishani, na kumhakikishia kujitosheleza nafsi yake kwa mujibu wa mtindo maalumu maishani. Kwa haya hukhitalifiana (Uislamu) na nyenginezo katika siasa za ki-uchumi.

Uislamu katika wakati ambao imeweka hukmu za kiuchumi kwa mwanaadamu, imefanya sheria juu ya mtu. Na katika wakati ambao yafanya kazi ili kudhamini haki ya kuishi na kumwezesha kujitosheleza, imefanya hilo kuhakikishwa katika mujtamaa maalumu, iliyona mtindo maalumu maishani. Nao huangalia kwa yale yanayopasa kuwa juu yake mujtamaa, katika wakati ambao huangalia katika kudhamini maisha na kumwezesha kujitosheleza, na imefanya mtazamo wake kuwa yale yanayopasa kuwa juu yake mujtamaa kuwa ni msingi wa mtazamo wake juu ya maisha na kujitosheleza, kwa hivyo utakuta hukmu za ki-Sheria zimekwisha dhamini uweza na kushibisha mahitaji yote ya kimsingi, kushiba kikamilifu kwa kila mtu mionganoni mwa raia na serikali ya Kiislamu, katika vyakula, mavazi na maskani, hilo ni kwa kumfaradhishia kazi kila mwanamume muweza mpaka aweze kuishibisha nafsi yake

kwa mahitaji yake ya kimsingi na kwa wale ambao yampasa ye ye kuwaangalia. Kwa haya Uislamu imedhamini kwa kila mtu kushibisha mahitaji ambayo hana budi mwanaadamu kama hali ya kuwa mwanaadamu kuzishibisha, nayo ni vyakula, mavazi na maskani. Kasha ikahimiza kila mtu kujifurahisha na vivilyo vizuri, na kuchukuwa katika mapambo ya dunia kwa kadri ya anavyoweza. Ikazuia serikali kuchukuwa kodi katika mali yake, kwa yale ambayo ni faradhi kwa waislamu wote, isipokuwa kilichozidi baada ya kutoshleza mahitaji yake, ambayo hushibisha kivitendo maisha yake ya kikawaida, hata kama ni mahitaji ya kiziada. Kwa hivyo imedhamini kuwezesha haki ya kuishi kila mtu kwa dhati yake, na ikampa fursa ya kujitosheleza maishani. Nayo wakati huo huo imedokeza kuchuma mali kwa mtu huyu katika kushibisha mahitaji yake ya kimsingi nay a kiziada katika mipaka maalumu. Na ikafanya mafungamano yake kwa kila muislamu, wala haichukulii kuwa ni mada ya ki-uchumi. Ikaharamisha kila Riba na kuamiliana nayo kwa kila mwenye kubeba uraia wa ki-Islamu, wala haichukulii kwao wao kuwa ni mada ya ki-uchumi, sawa sawa wawe ni waislamu au la, ikafanya hali ambayo yapasa kuwa juu yake mujtamaa pindi inapojinufaisha kwa mali kuwa ni jambo la kimsingi wakati wa kunufaika na mada ya ki-uchumi.

Na kutokamana na hayo hubainika kuwa uislamu haumtenganishi mtu kutoka sifa yake kama mwanaadamu, wala hautenganishi sifa yake kama mwanaadamu na utu wake, wala hautenganishi yale yapasayo kuwa juu yake mujtamaa katika kudhamini kushibisha mahitaji ya kimsingi kwa kila mtu na kummakinisha katika kushibisha mahitaji yake ya kiziada, bali imefanya kushibisha mahitaji na yale yampasayo kuwa juu yake mujtamaa ni mambo mawili yaliyo ya lazima, halitenganiki mojawapo kutokamana na jengine, lakini kwa jinsi inayofanya yale yanayopasa kuwa juu yake mujtamaa kimsingi ili kushibisha mahitaji kwa ajili ya kushibisha mahitaji yote ya kimsingi kushiba kikamilifu na kumakinisha katika kushibisha mahitaji ya kiziada, hapana budi kuwepo mada ya ki-uchumi kwa watu, mpaka waweze kushibisha mahitaji, wala haiwezi kupatikana kwao ila wakienda mbio kuichuma, kwa hivyo

uislamu umehimiza kuchuma, na kutafuta rizki, na kwenda mbio, na ikafanya kwenda mbio ili kuchuma Rizki ni faradhi, Asema Ta'ala:-

{ فَامْشُوا فِي مَنَاكِبِهَا وَكُلُوا مِنْ رِزْقِهِ }

“Basi nendeni katika pande zake zote na kuleni katika riziki yake” (Mulk 15)

Isipokuwa haimaanishi maana hiyo kuwa itaingilia katika uzalishaji wake au kiwango cha kuzalishwa, kwa sababu haina mafungamano na hayo, bali yeye amehimiza kwa kazi, na juu yetu kuchuma mali, zimepokwa hadithi nyingi zinazo himiza kuchuma mali na katika hadithi “**kuwa Mtume Rehma na Amani amempa mkono wa maamkuzi Sa'ad bin Muadh Radhi za Allah zimfikie, akakuta mikono yake imemea sugu, Mtume Rehma na Amani zimfikie akamuuliza juu ya hayo, akasema: Napiga sururu na shoka ili kusimamia jamii yangu, Mtume Rehma na Amani zimfikie Aliubusu mkono wake kasha akasema: Mikono miwili anayoyapenda Allah Ta'ala**” na akasema Amani zimfikie “**hajala mmoja wenu kattu chakula kizuri kuliko kile anachokula kutokamana na kazi ya mkono wake**” na imepokelewa kuwa Umar alipita penye watu wa kusoma, akawaona wamekaa na wameinamisha vichwa vyao, akasema: “Nani hawa?” akajibiwa: hawa ni wanaomtegemea Allah, Akasema: LA hawa ni walaji wanaokula mali za watu. Je siwajulishi ni nani wanaomtegemea Allah? Akaambiwa ndio, akasema: ni yule ambaye hupanda mbegu katika ardhi, kasha humtegemea **Mola wake aliyetukuka**. Na hivi tutakuta ayah na Hadithi juu ya kwenda mbio katika kutafuta riziki na juu ya kufanya kazi ili kuchuma mali hayo, na kula vizuri, Asema Ta'ala:

{ قُلْ مَنْ حَرَمَ زِينَةَ اللَّهِ الَّتِي أَخْرَجَ لِعِبَادِهِ وَالطَّيِّبَاتِ مِنْ الرِّزْقِ }

“Sema ni nani aliyearamisha mapambo ya Allah ambayo amewatolea waja wake na vizuri katika riziki.” (Al-Aaraf 32)
Na Asema Ta'ala

{ وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْخَلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ هُوَ خَيْرًا لَهُمْ بَلْ هُوَ شَرٌّ لَهُمْ
سَيْطَرُوْفُونَ مَا بَخِلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ }

“Wala wasione wale ambao wanafanya ubakhili katika yale aliyowapa Allah katika fadhila zake kuwa ni bora kwao, la ni vibaya kwao. Watafungwa kongwe (*Madude Ya kunasa shingoni*) za yale waliyoyafanya ubakhili siku ya qiyama.” (Al-Imran 180) Na Asema Ta’ala:

{ كُلُوا مِنْ طَيِّبَاتٍ مَا رَزَقْنَاكُمْ }

“Kuleni katika vizuri tulivyowaruzuku nayo” () Na Asema Ta’ala:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَنْفَقُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُمْ مِنْ الْأَرْضِ }

“Enyi mliaoamini toeni katika vile vizuri mlivyovichuma na katika vile tulivyokutoleemi katika ardhi” (Al-Baqarah: 267) Na Asema Allah Ta’ala:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُحَرِّمُوا طَيِّبَاتٍ مَا أَحَلَ اللَّهُ لَكُمْ }

“Enyi mliaoamini msiharamishe vizuri alivyo kuhalalishieni Allah” (Al-Maaidah87) Na Asema Allah Ta’ala:

{ وَكُلُوا مِمَّا رَزَقْنَا اللَّهُ حَلَالًا طَيِّبًا }

“Na kuleni katika vile alivyokuruzukuni Allah vilivyo halali na vizuri” (Al-Maaidah 88)

Ayah hizi na zinazoshabihiana nazo ni dalili wazi inayoonyesha hukumu ya kisheria inayoambatana na uchumi inayolenga uchumaji mali, na kufurahika na vizuri. Basi Uislamu umemfaradhishia mtu kuchuma mali, na ukawaamrisha kunufaika na utajiri ambao wanaouchuma, na hilo ni kuhakikisha kutengulia uchumi katika biladi, na kushibisha mahitaji ya kimsingi kwa kila mtu, na kumwezesha kushibisha mahitaji yake ya ki-ziada, na kwa ajili ya kuchunga Muislamu kupata mali utakuta Uislamu pindi ilitoweka hukmu zinazoambatana na jinsi ya kukusanya utajiri ili chunga isije ikatatiza katika jinsi ambayo mwanaadamu hukusanya mali, basi ikafanya ni rahisi sana. Pindi ilipoweka sababu za kumiliki na ikawa mikataba ambayo hutumiwa katika kubadilisha umilikaji, na ikamwachia mwanaadamu kuvumbua mbinu na vifaa, ambazo atachuma nazo, wala haikuingilia katika uzalishaji wa utajiri. Ikafanya mbinu na mikataba kuwa ni mipaka yaliyopana, inayokusanya nguzo za kisheria na hukmu za kisheria, huingia chini yake mas’ala tofauti tofauti. Basi ikalazimisha kazi na ikabainisha hukmu zake, ikamwacha mwanaadamu kufanya kazi

kama Seremala, Mshonaji viatu, Fundi, Mkulima na yasiyokuwa hayo, ikafanya zawadi kwa sura ambayo hupimwa juu yake kupewa, mfano katika kuifanya kwake kuwa ni sababu ya kumiliki, ikafanya kuajiriwa katika hali ambayo hupimwa juu yake uwakilishaji mfano katika kuhakikisha ujira wa wakili. Na hivyo hivyo twakutasababu za kumiliki, mikataba imekwisha bainishwa na Mtungaji Sheria (Allah) s.w.t na akaidokezea katka maana jumla, na hufanya ni yeye kukusanya kila katakachokuwa kipyta katika matukio lakini haziwi upya kwa kuwa upya Muamalah, kwa uwajibu wa kujifunga watu na muamala ambazo zimepokelewa kutoka Sheria. Lakini hutabikishika juu ya kila kitakacho kuwa kipyta katika matukio, jinsi litakavyo kuwa na kutofautika. Kwa haya huenda muislamu katika kuchuma mali mwenendo ulio murwa bila ya kusimama katika njia yake vizuizi vinyomzuia baina yake na baina ya kuchuma, pamoja na pupa ya kufanya chumo chake ni kizuri na halali. Kwa hivyo huweza kila mtu kupata chenye kushibisha mahitaji amabayo yataka kushibishwa. Haukutosheka Uislamu kwa kumhimiza mtu wala kufanya kushiba kupungue juu ykuchuma kwa watu, bali ikafanya Bait-ul-Maal ni ya raia wote hupewa kutokamana nayo, na kafanya kusimamia aloshindwa kujisimamia ni faradhi kwa serikali, na kukidhi haja za Ummah ni wajibu miongoni mwa uwajibu wake, kwa sababu ni juu yake kuchunga haki za raia, amepokea Bukhari kutoka kwa Ibnu Umar, Asema: Asema Rehma na Amani zimfikie “**Imam ambaye ni juu ya watu ni mchungaji nay eye ataulizwa juu ya alichokichunga.**” Na kuwa ili iweze serikali kusimamia yale yaliyowajibishwa juu yake na sheria, imejaalia uweza wa kukusanya mali maalumu kama Jizya na Kharaj, na ikafanya mali ya Zaka katika Bait-ul-Maal, na ikaijaalia haki ya kukusanya yale yaliyo faradhishwa kwa Uislamu wote kama kutengeneza njia, kujenga mahospitali,kumlisha alio na njaa na yanayofanana na hayo, ikafanya milki za aamma chini ya idara yake na yeye ndio inayoisimamia, na imezuia watu binafsi kuzisimamia, na ikaikataza kuwapa umilikaji wake au kuwapa kuzisimamia. Kwa sababu usimamizi jumla ni kwa walii wa Amri, wala haijuzu kwa mtu yejote katika raia kuzisimamia illa kwa kutawalishwa

(kuteuliwa) na walii wa Amri. Na milki hizi aamma katika petroli, chuma, shaba na yanayo fanana na hayo ni mali ambayo hakuna budi illa kuzitumia na kuzikuza, ili kuhakikisha kutangulia uchumi wa Ummah, kwa sababu mali hii ni ya Ummah, na serikali ndiyo inayosimamia kukuzwa kwake na kuzisimamia.

Basi itakaposimama serikali kuleta mali, itaweza kubeba mizigo ya kuangalia mambo ya raia, na atasimama kila mtu katika kuchuma mali, na kuendea mbio riziki. Basi itapatikana utajiri ambao utatosheleza kushibisha mahitaji yote ya ki-msingi kushiba kikamilifu, na kushibisha mahitaji ya ziada. Isipokuwa kutangulia huko ki-uchumi ni kwa kuhimiza kila mtu kuchuma mali, na ikafanya mali ya serikali, na kukuzwa milki amma huwa kwa ajili ya kutumia mali kama chombo cha kushibisha mahitaji na sio kwa dhati ya mali, wala si kujifakhirisha nayo, wala si kwa kuitoa juu ya maasia au kwa kiburi na ujeuri, kwa hivyo asema Rehma na Amani zimfikie **“Anaetafuta Dunia (kwa kuchuma cha) halali ili kujitosheleza atakutana na Allah Ta’ala kama mwezi katika siku nyeupe, na mwenye kuitafuta ili ajifakhirishe na kurundika atakutana na Allah ilhali amemkasirikia.”** Asema Amani zimfikie, **“Na je unao mwanaadamu katika mali yako ila ulichokula ukakimaliza, au ukakivaa kikaparara au ukatoa sadaka ukakibakisha.”** Asema Allah Ta’ala:

{ وَلَا تُسْرِفُوا إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ }

“Wala musifanye israfu hakika yeye papendi wenyewe kufanya israfu” (Al-A’raf 31)

Sio lengo la kuchuma mali ili iwe ni chombo cha kushibisha mahitaji, sio kujifakhirisha ambao uislamu haikufanya tu kutafutwa kwake, bali Uislamu imefanya uchumi wote upelekwe kwa mujibu wa maamrisha ya Allah na makatazo yake kuwa ni jambo la lazima. Ikamuamrisha Muislamu kutafuta katika chumo chake maisha ya Akhera na wala asisahau fungu lake Duniani. Asema Ta’ala:

{ وَابْتَغِ فِيمَا آتَكَ اللَّهُ الدَّارَ الْآخِرَةَ وَلَا تَنْسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا وَأَحْسِنْ كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ وَلَا تَنْبُغِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ }

“Na utafute kwa yale aliyokupa Allah, makazi mazuri ya akhera, wala usisahau sehemu yako duniani, na ufanye wema kama Allah alivyo kufanya wala usitafute kufanya ujisadi katika ardhi.” (Al-Qasas 77)

Ka hivyo imefanya falsafa ya ki-uchumi ni kupeleka mambo ya ki-uchumi kwa mujibu ya maamrisho ya Allah na makatazo yake, ikijengewa juu ya kudiriki fungamano na Allah, yaani kuifanya fikra ambayo imejengwa juu yake upelekaji wa mambo ya muislamu katika mujtamaa maishani, nayo ni kuzifanya vitendo vya ki-uchumi kwa mujibu ya matakwa ya hukmu za ki-Sheria ikizichukulia kuwa ni dini, na ikafanya kupelekwa mambo ya raia kwa wale wanaobeba uraia kuzifunga vitendo vyao vya ki-uchumi kwa kuzichukulia kama sheria. Watafanyiwa Mubah yale ambayo Uislamu imefanya ni Mubah na itawafunga na yale waliofunga nao Uislamu. Asema Ta’ala:

{ وَمَا آتَكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا }

“Na alichokupeni Mtume basi pokeeni na anachokukatazeni jiepusheni nacho” (Al-Hashr: 7) Na asema Ta’ala:

{ يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمْ مَوْعِظَةٌ مِّنْ رَبِّكُمْ وَشِفَاءٌ لِمَا فِي الصُّدُورِ }

“Enyi watu yamekujeni mawaidha kutoka kwa Mola wenu na poza la yale yaliyomo vifuani.” (Yunus: 57) Na Asema Ta’ala:

{ فَلَيَحْذِرُ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ }

“Basi wajihadhari wale wanaokaidi amri yake, wasije wakapatwa na msiba au ikawafika adhabu iumizayo” (An-Nur: 63) Na Asema:

{ وَأَنْ احْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ }

“Na hukmu baina yao Kwa yale aliyoyateremsha Allah” (Maida: 49)

Imekwisha dhaminiwa kujifunga Waislamu na watu kwa hukmu hizo kwa mwelekeo ambao Uislamu umeifunga ni yenye kutekeleza siasa hizo kwa msukumo wa uchaji Mungu, na kwa Sheria ambazo hutekelezwa na serikali juu ya watu. Asema Ta’ala:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذَرُوا مَا بَقِيَ مِنْ الرِّبَا إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ }

“Enyi mliaoamini mcheni Allah na acheni yaliyobakia katika Riba, ikiwa mumeamini” (Al-Baqarah: 278) Na Asema:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا تَدَاءَيْتُم بِدِيْنِ إِلَى أَجَلٍ مُسَمًّى فَاكْتُبُوهُ }
 “Enyi mliaoamini mnapokopeshana deni kwa muda uliowekwa
 basi liandikeni” (Al-Baqarah Ayah 282) Mpaka Aliposema:
 { إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً حَاضِرَةً تُدِيرُونَهَا بَيْنَكُمْ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَلَا تَكْتُبُوهَا }
 “Illa ikiwa ni biashara iliyohudhuria mnayo peana baina yenu,
 basi si vibaya kwenu msipoianidika” (Al-Baqarah: 278)

Yeye yuwatubainishia jinsi ya kuzitekeleza hukmu hizo, na akabainisha jinsi ya kudhamini kujifunga na hukmu hizo.

Hivi ndivyo inavyoshuhudiwa siasa ya ki-uchumi katika uislamu kuwa imejengwa juu ya kushibisha mahitaji ya kila mtu, ikimchukulia kama mwanaadamu anayeishi katika mujtamai maalumu, na juu ya kuchuma utajiri ili kupata yatakayo shibisha mahitaji. Imesimama juu ya fikra moja nayo ni kupeleka mambo kwa mujibu ya hukmu za kisheria inayotekelawa na kila mtu kwa msukumo wa uchaji mungu na kutekelezwa na serikali kwa kuelekeza na kwa kuweka sheria.

MISINGI JUMLA YA KI-UCHUMI

Hubainika baada ya kuzidadisi hukmu za kisheria zinazoambatana na uchumi katika uislamu kuwa zatatuwa maudhui ya kumwezesha mtu kunufaika na utajiri, na kuwa hilo ndilo tatizo la ki-uchumi kwa mujtamai katika mtazamo wake. Nayo pindi inapochunguza uchumi hakika huchunguza katika kukusanya utajiri na katika utumiaji wake na watu, na katika usambazaji wake baina yao. Juu ya haya hakika ya hukmu zinazoambatana na uchumi zimejengwa juu ya misingi mitatu nayo, umilikaji, utumiaji wa milki na usambazaji wa utajiri baina ya watu.

Amma umilikaji katika upande wa kumiliki, nazo ni za Allah kwa upande yeye ndiye anayemiliki Ufalme Wote, na kwa kuwa ashadokeza kuwa mali ni yake. Asema Ta’ala:

{ وَآتُوهُم مِنْ مَالِ اللَّهِ الَّذِي آتَاكُمْ }

“Na wapeni katika mali ya Allah aliyokupeni” (Nur: 33)

Basi mali yote ni ya Allah (swt) peke yake, isipokuwa Allah (swt) amemfanya mwanaadamu ni msimamizi juu ya mali, na kawapa wao hizo (mali), na akafanya ni haki yao kumiliki, Asema Ta'ala:

{ وَأَنْفَقُوا مِمَّا جَعَلَكُمْ مُسْتَحْلِفِينَ فِيهِ }

“Na toeni katika yale aliyokupeni” (Hadiid: 7) Na Asema:

{ وَيُمْدِدُكُمْ بِأَمْوَالٍ وَبَنِينَ }

“Na atakupeni mali na watoto” (Nuh: 12)

Kufikia hapa twakuta kuwa Allah pindi alipobainisha asili ya kumiliki mali aliisifu kuwa mali ni yake akasema:

{ مَالِ اللَّهِ }

“Mali Ya Allah” Na pindi alipobainisha kugura kwa mali kwa watu aliisifu kuwa ni milki yao akasema:

{ فَادْفَعُوا إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ }

“Wapeni mali zao” (AN-Nisaa: 6)

{ خُذُّ مِنْ أَمْوَالِهِمْ }

“Tukua Katika Mali Zao” At-Tauba Ayah 103,

{ فَلَكُمْ رُءُوسُ أَمْوَالِكُمْ }

“Basi mtapata rasilimali zenu” Al-Baqarah Ayah 279,

{ وَأَمْوَالَنَّا افْتَرَقْنَاهَا }

“NA mali mlizozichuma” At-Taubah 24,

{ وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ }

“Na mali yake hayatamfaa atakapokuwa anadidimia (motoni)”
(Al-Layl: 11)

Isipokuwa haki hii ya kumiliki ambayo imekuwa kwa usimamizi imekuja kwa jumla kwa wanaadamu wote wana haki ya kumiliki, wala si umilikaji wa kivitendo, wao tu ni wasimamizi katika haki ya kumiliki. Amma umilikaji wa kivitendo kwa mtu maalum Uislamu umekwisha shurutisha kwa idhini kutoka kwa Allah kwa mtu kumiliki (mali). Kwa hivyo mali hakika ya kumiliki kivitendo ni kwa idhini itokayo kutoka kwa Mtungaji Sheria (Allah) kumiliki kwake. Itakuwa idhini hii ni dalili maalumu kwa mtu huyo kuwa sasa imekuwa wake umilikaji wa mali. Basi usimamizi wa watu wote katika umilikaji umekuja kwa usimamizi jumla, na imefaidisha kuwepo haki ya kumiliki na usimamizi wa mtu maalumu katika umilikaji wa kivitendo

umekuja kwa idhini maalumu ambao imekuja kutoka Mtungaji Sheria (Allah) kwa mtu katika kumiliki.

Sheria imekwisha bainisha kuwa kuna milki ya kibinafsi, basi kwa kila mtu kumiliki mali kupitia sababu za kumiliki, amepokea Abu Daud kutoka Samurah (ra) kutoka kwa Mtume Rehma na Amani zimfikie asema: “**atakaye zungusha kizuizi katika ardhi basi (ardhi) hiyo ni yake.**” Na milki amma kwa Ummah wote, amepokea Ahmad kutoka mtu mionganini mwa Muhajireena asema: amesema Mtume Rehma na Amani zimfikie, “**watu hushirikiana katika matatu: Maji, Malisho na Moto.**” Na kuna milki ya serikali, basi kila atakaye kufa katika waislamu na asiwe na warithi basi mali yake itakuwa ni ya Baitul-Maal. Kila kilicho cha Baitu-Maal ni milki ya serikali isipokuwa Zakat. Serikali ina kхиari kutumia mali anayomiliki popote inapotaka, kwa mujibu ya hukmu za ki-Sheria. Sheria imebainisha sababu ambazo mtu huzitumia ili kumiliki, na hali ambazo humiliki nazo Ummah na sababu ambazo humiliki nazo serikali, na ikakataza yasiyo kuwa hayo.

Amma utumiaji wa milki hilo ni kwa upande wa milki amma imewachiwa serikali, kwa sababu yeye ni naibu ya Ummah, lakini sheria imekataza, yaani serikali, kutumia milki amma kufadhilisha au kuunganisha. Na ikaruhusu kutumia katika yasiyokuwa hayo kwa mujibu wa hukmu ambazo sheria imebainisha. Amma kwa mujibu ya milki ya serikali, na milki ya kibinafsi utumiaji wake ni wazi katika hukmu za Baitul-Maal. Hukmu za Muamalah katika kuuza, rahani au yasiyokuwa hayo. Sheriah imeruhusu serikali na mtu binafsi kutumia anayomiliki kwa kubadilisha na kuungusha, na yasiyokuwa hayo kwa mujibu ya hukmu ambayo imebainishwa na Sheria. Amma usambazaji wa utajiri baina ya watu hilo huingia kikawaida katika sababu za kumiliki na katika mikataba. Isipokuwa tofauti katika watu kinguvu, na katika haja ya kushibisha huleta tofauti katika usambazaji wa utajiri baina ya watu na hufanya uwezekano wa kuwepo usambazaji mbaya, basi hufikisha usambazaji mbaya kwa kukusanya mali katika mikono ya kipote na kukosekana kwake na kipote chengine,

kama pia hufikishia ukiritimba wa chombo thabiti cha kubadilishana, nayo ni dhahabu na fedha. Kwa hivyo sheria imekuja kuzuia kubadilishana utajiri tu baina ya matajiri na ikawajibisha kubadilishwa kwake baina ya watu wote, ikakataza kukiritimba dhahabu na fedha hata kama imetolewa zakat yake.

3. AINA YA MILKI

MILKI YA KIBINAFSI

Ni katika maumbile ya mwanaadamu kwenda mbio ili kushibisha mahitaji yake, kwa hivyo imekuwa ni ya kimaumbile kukusanya mali ili kushibisha mahitaji hayo, na ni katika maumbile yake kwenda mbio katika kukusanya huko. Kwa sababu kushibisha mwanaadamu njaa yake ni jambo la lazima, wala hamkiniki akae bila hilo. Kufikia hapa imekuwa kukusanya kwa mwanaadamu utajiri pamoja na kuwa ni jambo la kimaumbile bali pia ni jambo la lazima asokuwa na budi nalo. Kwa hivyo yamekuwa kila majaribio ya kumzuia mwanaadamu kukusanya utajiri ni kinyume na maumbile, na kila majaribio ya kuweka kikomo ya ukusanyaji wake kwa kiwango maalumu hivyo hivyo hukhitalifiana na maumbile. Kwa hivyo imekuwa ni kawaida kusiwe na kizuizi baina ya mwanaadamu na baina ya kukusanya utajiri, wala baina yake na baina ya kwenda mbio katika kukusanya huko, isipokua haifai kuwachwa mwanaadamu kukusanya huko jinsi atakavyo, na kuiendea mbio jinsi atakavyo, na kuzitumia kama atakavyo, kwa sababu hili hufikishia katika fujo na kuchanganyikiwa na husababisha shari na ujisadi, kwa sababu watu hutofautiana katika nguvu na haja na kushiba, basi wakiwachwa na mambo yao watakusanya wenye nguvu na watanyimwa wanyonge, wataangamia wagonjwa na wenye punguwani na watazitumia wenye kuvuka mipaka katika Anasa. Kwa hivyo hakuna budi ila kuwezesha watu kupata utajiri, na kuiendea mbio kwa sura ambayo itadhamini mahitaji ya kimsingi kwa watu wote, na itadhamini kuwawezesha wao kufikia kushibisha mahitaji yasiyokuwa ya kimsingi. Kwa ajili ya hayo hakuna budi ila kudokezea ukusanyaji huo kwa jinsi maalumu, itakayohakikisha ndani yake usahali, kwa jinsi ambayo itakayo kuwa karibu kwa watu wote, pamoja na tofauti za nguvu zao na mahitaji yao, na kwa

kufikiana na maumbile katika hali ya kushibisha mahitaji ya kimsingi, na kumwezesha katika kufikia kushibisha mahitaji yasiyokuwa ya kimsingi. Kufikia hapa imekuwa hapana budi kuweka umilikaji uliodokezewa kwa jinsi, na imekuwa hakuna budi kupiga vita unyimaji wa kumiliki, kwa sababu hugongana na maumbile na kupiga vita kudokeza umilikaji kwa jumla kwa sababu huvunja mbio za mwanaadamu katika kukusanya utajiri nao hugongana na maumbile na kupiga vita uhuru wa kumiliki, kwa sababu yake hufikisha kwa fujo katika mafungamano baina ya watu, na husababisha shari na fisadi. Umekuja uislamu na ukafanya Mabda umilikaji wa kibinafsi na ukadokezea jinsi na sio kwa jumla. Juu ya hilo ni maumbile na hupanga mafungamano baina ya watu na kumpa fursa mwanaadamu kushibisha njaa yake yote.

Utambuzi Wa Milki Ya Kibinafsi

Milki ya kibinafsi ni hukmu ya kisheria iliyokadiriwa kwa dhati au manufaa, huhusisha kumwezesha aliyotegemezewa nayo kunufaika na kitu, na kuchukua fidia yake, hilo ni kama kumiliki mwanaadamu kipande xha mkate na nyumba, hakika yeye yuwaweza kwa kumiki kwake kipande cha mkate kukila, na kukiiza na kuchukuwa thAmani yake, na kumwezesha kwa kumiliki kwake nyumba kuishi ndani yake, na kuiiza na kuchukua thAmani yake. Basi kipande cha mkate na nyumba kila mmoja ina Dhati yake, na hukmu ya kisheria iliyokadiriwa juu yake ni idhini ya Mtungaji Sheria katika kunufaika nazo kwa kuzila, kunufaika na kubadilisha. Na idhini hii ya kunufaika yawajibisha kumwezesha mmilikaji, nay eye ndiye aliyotegemezewa idhini hiyo, katika kula kipande cha mkate, na kuishi ndani ya nyumba, kama pia kumwezesha kuziuza. Basi kwa upande wa kipande cha mkate, hukmu ya kisheria iliyokadiriwa juu ya dhati yake ni idhini ya kuliwa kwake. Na kwa upande wa nyumba, hukmu ya kisheria iliyokadiriwa juu yake ni katika kunufaika, nayo ni idhini ya kuishi ndani yake. Kwa hayo huwa umilikaji ni idhini ya Mtungaji Sheria (Alla) kwa kunufaika na dhati. Kwa hayo basi haitubutu umilikaji illa kwa kuthibitishwa na Mtungaji Sheria (Allah), na kwa kukiru kwakena sababu zake. Basi haki ya kumiliki dhati haitokAmani

na dhati yenyewe, na kutokamana na tabia yake yaani kwa hali yake ni yenyeye kunufaisha au isiyonufaisha, bali hutokamana na idhini ya Mtungaji Sheria (Allah), na kwa kufanya sababu ambao ni Mubah kumiliki dhati kama natija ya sababu, ambao humiliki kisheria. Kwa haya huwa idhini ya kumiliki baadhi ya vitu na ikazuia kumiliki baadhi yake, ikaidhinisha baadhi ya mikataba na ikakataza baadhi yake, ikakataza kwa muislamu kumiliki tembo na nguruwe, kama ilivyomkataza kumiliki mali ya Riba na mali ya kamari kwa mtu yeote katika Raia wa serikali ya Kiislamu, ikaidhinisha biashara basi ikahalalisha na ikakataza riba na ikaifanya kuwa ni Haramu, ikaidhinisha shirika la INAAN ikakataza vyama vyta ushirika na mashirika ya hisa na Bima.

Umilikaji uliokubaliwa na sheria una sharuti kama ilivyokuwa na utumiajikatika milki na pingu kwa hali ambayo milki haitoki katika maslahi ya jamaa, na maslahi ya mtu binafsi huchukuliwa kama sehemu ya Jamaa na wala sio mtu alotengwa, na kwa kuchukuliwa kama mwanaadamu katika mujtamai maalumu. Kunufaika na dhati iliomilikiwa ikiwepo uweza kutoka Mtungaji Sheria, yaani Asili ya kila milki ni ya Mtungaji Sheria (Allah), na yeye ndiye alompa mtu binafsi kwa utaratibu kutoka kwake yeye juu ya sababu za kisheria, nao ni kumilikishwa kutoka Mtungaji Sheria (Allah) kwa mtu binafsi katika jamaa ni kitu maalum, isinge kuwa ni haki yake kumiliki huko lau si kama kumilikishwa huko.

Pamoja na kuwa kumiliki dhati ni kumiliki dhati yenyewe, na kumiliki manufaa yake, na sio tu kumiliki manufaa, makusudio ya kiuhakika katika kumiliki ni kunufaika na dhati kunufaika ki-maalumu iliyobainishwa na Sheria.

Kwa mwangaza huu juu ya utambuzi na milki ya kibinafsi humkinika kufahamika kuwa kuna sababu za kisheria za kumiliki na humkinika kufahamika kuwa hali maalum za kutumia milki hiyo, na humkinika kufahamika kuwa kuna njia maalumu za kunufaika kwa yale anayomiliki, na humkinika kufahamika matukio ambayo huchukuliwa kuwa ni uadui kwa

haki ya milki ya kibinagsi. Hii humkinika kufahamika katika utambuzi wa maana ya kihakika ya ukusanyaji ambao Mtungaji Sheria (Allah) amefanya ni Mubah, na maana ya kwenda mbio katika kukusanya huko na kunufaika nay ale aliyoyakusanya. Kwa maana nyengine huonyesha utambuzi kwa maana ya kihakika ya umilikaji.

Maana ya umilikaji

Haki ya kumiliki ya kibinagsi ni haki ya mtu kisheria, ni kwake yeye kumiliki mali yanayoweza kugurishwa na yasyoweza kugurishwa, na haki hii imehifadhiwa na imedokezewa na sheria na muelekeo. Haki hii ya kumiliki pamoja na kuwa na maslahi yaliyo na thAmani ya kimali iliyodokezwa na Sheria, hilo humaanisha kuwa maana ya umilikaji wa kibinagsi huwa ni kwa mtu alona uweza wa kumiliki na kuzitumia, pamoja na kuwa na uweza juu ya kazi ya ki-khiyari, kwa hivyo twakuta kuwa kudokezwa haki ya kumiliki ni jambo wazi katika mipaka ya maamrisho ya Allah na makatazo yake.

Hakika imedhihiri umilikaji huo katika sababu za kisheria za kumiliki ambazo kwa mujibu wake zakiri haki ya kumiliki, katika hali ambazo zimepangwa juu yake adhabu na hali ambazo haikupangwa juu yake adhabu, mfano utambuzi wa uwizi, na lini huitwa uwizi na utambuzi wa unyakuzi na utambuzi wa utekaji nyara mpaka mwisho... Kama inavyo dhihiri pia katika udokezaji huo haki ya kutumia milki na hali ya Mubah katika utumiaji huo, na hali ambayo hukatazwa ndani yake utumiaji huo na katika utambuzi wa hali hizo na kubainisha matukio yake, uislamu ulipodokeza umilikaji haukudokeza kwa jumla bali ilidokeza kwa jinsi na hudhihiri kudokeza huku katika jinsi ilivyowazi katika mabo yafuatayo:-

1:-Kwa kudokeza kwake katika upande wa sababu za kumiliki, na kukuza milki na wala sio katika kiwango cha mali ya kumilikiwa.

2:-Kwa kudokeza jinsi ya ktumia.

3:-Hali ya kuwa shingo ya Ardhi ya Kharaj ni milki ya serikali wala sio ya mtu binagsi.

4:-Hali ya kufanywa milki ya kibinafsi kuwa ni milki Amma kwa nguvu katika hali maalumu.

5:-Kumpa yule ambaye zimeshindwa mbinu zake kupata ya kutosha katika haja zake katika mipaka yake.

Kwa haya hudhihiri maana ya milki ya kibinafsi nayo ni kumpa uweza mtu katika yale anayomiliki, kwa jinsi maalumu iliyomo mipaka, imefanywa milki ni haki ya mtu ki-sheria, na imeweka sheria kuchunga haki ya mtu binafsi kumiliki kuwa ni wajibu wa serikali, na ikafanya kuheshimiwa na kuhifadhiwa na kutofanyiwa uadui ni jambo la lazima. Kwa hivyo imeweka adhabu kali kwa kila mwenye kuharibu haki hiyo, sawa sawa kwa uwizi au unyakuzi au kwa njia yoyote mionganoni mwa njia zisizokuwa za ki-sheria. Hakika zimewekwa sheria na adhabu kali, na zikawekwa muongozzo wenyewe kuzuia nafsi katika kuchukuwa kisichokuwa na haki katika haki za kumiliki, katika yale yaliyo milki ya watu wengine. Basi mali ya Halali ndio ambayo huambatana juu yake maana ya milki na mali ya Haramu sio milki, wala haiambatani juu yake maana ya milki.

Sababu za kumiliki mali

Mali ni kila chenye kumilikiwa vyovyyote itakavyo kuwa dhati yake, na kilicho kusudiwa katika sababu ya kumiliki ni sababu ambayo humpa mtu umilikaji wa mali, baada ya kuwa hana wa kuimiliki, amma kubadilisha kwa aina zozote hio sio katika sababu ya kumiliki mali, bali ni sababu ya kumiliki aina yake, pindi inapomiliki aina maalumu ya mali kwa aina nyengine isiyokuwa mali. Basi mali asili ni yenyе kumilikiwa na kilichotokea ni kubadilisha aina yake. Hivyo hivyo haingii kukuza mali kama faida ya biashara, kodi ya nyumba, mavuno na ukulima na yanayoshabihiana nayo katika sababu za kumiliki mali. Hakika yake hata kama imetokea ndani yake baadhi ya mali mpya, lakini imetokea kutoka mali nyengine basi hiyo ni sababu ya kukua mali na sio mionganoni mwa sababu ya kumiliki mali. Maudhui ni kumiliki mali ya kukua, kwa maana nyengine ni kupata asili ya mali. Kukuza milki ni kuzidisha mali ambayo yuwaimiliki, basi mali ipo, basi kuikuza na kuizidisha. Hakika imekuja sheria kwa kila milki na kuikuza milki kwa Ahkaam

zenye kuambatana nayo. Basi mikataba ya kibiashara na ujira ni katika Ahkaam zenyenye kuambatana na kukuza mali. Kazi ya kuwinja na ushirika wa mudharaba ni katika Ahkaam zenyenye kuambatana na milki. Basi sababu za milki ni sababu za kukusanya asili, na sababu za kukuza milki ni sababu za kuzidisha asili ya mali, ambayo imetangulia kuipata kwake kwa sababu mionganoni mwa sababu za kumiliki.

Kumiliki mali ina sababu za ki-sheria ambayo sheria imefunga katika sababu maalumu, wala hajuzu kuivuka, basi sababu ya umilikaji imefungwa kwa yale yaliyobainishwa na sheria. Utambuzi milki iliyotangulia, ni kuwa ni hukmu ya ki-Sheria iliyokadiriwa kwa dhati au manufaa inayolazimu kuwepo idhini ya Mtungaji Sheria mpaka kupatikana umilikaji. Na idhini hapana budi kwa sababu aloidhinisha Mtungaji Sheria (Allah) ili kupata milki. Basi ikipatikana sababu ya ki-Sheria hupatikana umilikaji wa mali, na isipokuwepo sababu ya kisheria haipatikani umilikaji wa mali. Sheria imekwisha dokeza sababu za kumiliki katika hali maalumu, iliyobainisha katika idadi maalumu, wala haikumwacha mkono, ikawekea mipaka mipana iliyowazi huingia chini ya sehemu tofauti tofauti, nayo ni kitagaa chake na ni suala katika hukmu zake. Wala haikuwekea sababu (ILLAH) kwa sababu (illah) jumla maalumu, basi haifanywi Qiyas juu yake kwa jumla zozote nyengine. Hilo ni kwa sababu zinazokuwa mapya katika mahitaji ila ni tukio katika mali, na sio katika Muamalati, yaani sio katika nidhamu ya fungamano, bali ni katika maudhui yake. Basi imekuwa hakuna budi ili kufunga Muamalati katika hali maalumu, inayotabikishika juu ya mahitaji mapya na yalotofauti, juu ya mali kwa jinsi ya kuwa ni mali, na juu ya juhud kwa kuwa ni juhud. Katika haya kuna kidokezo kwa umilikaji wa kibinafsi kwa sura ambayo huwafikiana na maumbile na huiweka ndhamu milki hiyo mpaka mujtamai ulindwe kutokana na hatari ya kuwachwa mkono. Hakika ya milki ya kibinafsi n dhihirisho mionganoni mwa dhihirisho la hisia ya kuhifadhi maisha, kama ilivyokuwa Ndoa ni dhihirisho mionganoni mwa dhihirisho la kijinsia, na kama ilivyo ibadaati ni dhihirisho mionganoni mwa dhihirisho la hisia ya kuabudu. Basi zikiwachwa mkono

dhihirisho hizo katika kushibisha kinacho takakushibishwa hilo litafikisha kwa fujo na kuchanganyikiwa na kushiba kivibaya au kushiba kimakosa, kwa hivyo imekuwa hakuna budi kudokeza jinsi ambayo mwanaadamu atakavyopata mali, mpaka wasihukumu watu wachache katika Ummah njia ya mali, wala wasinyimwe walio wengi katika kushibisha baadhi ya mahitaji yao, mpaka asiendee mbio mali kwa sababu ya mali na akose mwanaadamu utamu wa maisha mazuri, na hunyimwa watu kupata mali na kufichwa katika mahazina. Kwa hivyo imekuwa hakuna budi ila kudokeza sababu za kumiliki.

Kwa kuzichunguza hukmu za ki-Sheria ambazo hulazimu milki ya kibinafsi kwa mali hubainisha sababu za kumiliki kuwa zimefungwa katika sababu tano nazo ni:-

A: -Kazi

B:-Urathi

C:-Haja ya mali kwa ajili ya uhai

D:-Ruzuku za mali ya serikali kwa raia

E:-Mali anayoyapata mtu bila ya kutoa mali au juhudii.

4:- SABABU YA KWANZA MIONGONI MWA SABABU ZA KUMILIKI (KAZI.)

Hubainika tunapotazama katika aina yejote miongoni mwa aina ya mali, sawa sawa ikiwa imepatikana kimaumbile kama kiyoga, amma kimepatikana kwa kazi ya mwanaadamu kama kipande cha mkate na gari. Hakika kupatikana kwake huhitaji kazi.

Ilipokuwa tamko la kazi ni dalili pana, imekuwa imekuwa kazi ni aina tofauti tofauti, kwa umbo tofauti na yenye natija tofauti tofauti. Hakika ya Mtungaji Sheria (Allah) hakuliwachia mkono tamko la kazi, wala haikuweka (Nasi) dalili juu ya kazi kwa umbo la kijumla bali imeweka dalili kama kazi maalumu zilizo na vikomo, ikabainisha katika dalili hizo juu ya kazi hizo na kwa aina ya kazi ambazo hufaa kuwa ni sababu za kumiliki. Tukichunguza hukmu za ki-Sheria zilizodokeza juu ya kazi

hubainika kuwa aina za kazi zilizoruhusiwa na sheria kuwa ni sababu za kumiliki mali ni kazi zifuatavyo:-

- 1:-kuhuisha ardhi mwitu**
- 2:-kutoa yaliyo ndani ya ardhi au katika hewa**
- 3:-kuwinja**
- 4:-uwakili na udalali**
- 5:-ushirika wa mwili na rasilimali (Mudharabah)**
- 6:-ukulima wa mimea**
- 7:-kufanyia wengine kazi kwa ujira.**

Kuhuisha Ardhi Mwitu

Mwitu ni ardhi ambayo hakuna anayemiliki, wala hakuna anayenufaika nayo, kuhuyisha kwake ni kulimwa kwake au kupandwa miti au kujengwa juu yake, kwa maana nyengine ni kutumiwa kwake kwa aina yejote miongoni mwa aina ya utumiaji, ambayo hufaidisha uhai, na kuhuisha mtu ardhi ni kwa kuifanya ni milki yake, Asema Rehma na Amani zimfikie “**atakaye huisha ardhi mwitu basi hiyo (ardhi) ni yake.**” Imepokewa na Bukhari, kutoka Umar na Asema “**atakaye jenga kuta juu ya Ardhi basi hiyo (ardhi) ni yake.**” Na Asema “**mtu yejote atakaye tangulia (ardhi) ambayo hakutanguliwa katika (ardhi) hiyo na muislamu yejote basi hiyo (ardhi) ni yake.**” Wala hakuna tofauti baina ya Muislamu na Dhimmi, kwa sababu ya uwazi wa hadithi, kwa sababu anachokichukua Dhimmi kutoka matumbo ya mabonde, misitu na vilele vya majabali ni milki yake, wala haijuzu kumpokonya kutoka kwake, basi ardhi mwitu ni awla kuwa ni milki yake. Hii ni jumla kwa kila ardhi sawa sawa ikiwa ni Darul-Islam au Darul-Harb, sawa sawa ikiwa ni ardhi ya Ushri au ardhi ya Kharaj. Isipokuwa sharuti ya kumiliki ni kuitumia ardhi kwa muda wa miaka mitatu tangu alipoweka mkono wake juu yake, na kuendelea kuhuyishwa kwake kwa kuitumia. Basi ikiwa haitumii kwa muda wa miaka mitatu mfululizo kutoka tarehe ya kuweka mkono wake juu yake, au kuipuza baada ya hilo kwa muda wa miaka mitatu mfululizo hupomoka haki yake ya kumiliki, Asema Umar Bin Al-Khattab “**Hana haki mwenye kuzuia (ardhi) baada ya miaka mitatu.**” Hakika amelitamka

Umar na akalitendea kazi ilhali masahaba wakiona na wakasikia wala hawakukanya basi imekuwa ni Ijmaa.

Kutoa Yaliyo Ndani Ya Ardhi

Kaika aina za kazi ni kutoa yaliyo ndani ya tumbo la ardhi, kati yaliyokuwa ya dharura kwa jamaa nayo ni hazina (Rikaaz), yaani yale ambayo waislamu jumla hawana haki nayo, kama katika Tafsiri ya Ki-Fiqhi, mwenye kutoa (yaliyo ndani ya Ardhi) khumusi NNE na huitolea Zaka khumusi moja. Amma ikiwa mionganini mwa dharura za jamaa, yaani ni haki ya waislamu jumla, hakika huingia katika miliki Amman a kudhibiti chake ni kuwa hazina hiyo imezikwa ndani ya ardhi kwa kitendo cha mwanaadamu au ikiwa kiwango chake ni chenye kikomo ambacho hakifiki kuwa jamaa wana haja nayo basi hivyo ni hazina (Rikaaz). Yanayokuwa ya asili na jamaa wana haja kwake kama timbo ambazo hutolewa ndani yake mawe ya kujenga na mengineo haiwi ni hazina (Rikaaz) wala milki amma, bali huingia katika milki ya kibinagsi. Kumiliki hazina (Rikaaz) na kutoa khumusi ndani imethibiti kwa hadithi tukufu, hakika amepokea An-Nisai kutoka Amru Bin Shuaib kutoka kwa babake kutoka kwa babu yake asema: aliulizwa Mtume Rehma na Amani zimfikie juu ya cha kuokotwa, akasema: “**kitakacho okotwa katika njia inayopitiwa au kijiji kilichoamirishwa basi kitangaze mwaka mmoja, ni cha mwenyewe akija waila basi ni chako, kisichokuwa kaika njia inayopitiwa wala si katika kijiji kilichoamirishwa basi ndani yake ni ndani ya hazina (Rikaaz) khumus.**” Hivyo hivyo hufanyiwa aina zote zinazotolewa ndani ya ardhi na yanayo tolea hewa kama (Oxygen) anayoipumua mtu na (Nitrogen) ambayo hutumiwa na mimea. Hivyo hivyo kutoa kila kitu ambacho Sheria imeifanya ni Mubah katika yale aloyaumba Allah na akuwachia kunufaika nayo.

Kuwinja

Katika aina ya kazi ni kuwinja. basi kuvua samaki, lulu, marijani na mdoya na mengineo yanayovuliwa baharini kumiliki yanayovuliwa, kama ilivyohali katika kuwinja ndege na

wanyama, na yaliyomo katika kuwinja cha bara huwa ni milki ya aliyokiwinja, Asema Ta'ala:-

{ أَحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ الْبَحْرِ وَطَعَامُهُ مَتَاعًا لَكُمْ وَلِسَيَارَةٍ وَحُرْمَ عَلَيْكُمْ صَيْدُ الْبَرِّ مَا دُمْتُمْ
حُرُمًا }

“Nyinyi mehalalishiwa kuvua vinyama vya baharini na kuvila, kwa faida yenu na kwa wasafiri, na mmeharamishiwa mawinjo ya wanyama wa bara maadamu mmeharimia hijja” (Al-Maaidah: 96). Na Asema:-

{ وَإِذَا حَلَّتُمْ فَاصْطَادُوا }

“Na mkisha toka hijja yenu basi winjeni” (Al-Maaidah: 2). Na Asema:-

{ يَسْأَلُونَكَ مَاذَا أَحِلَّ لَهُمْ قُلْ أَحِلَّ لَكُمُ الطَّيَّبَاتُ وَمَا عَلِمْتُمْ مِنْ الْجَوَارِحِ مُكَلِّبِينَ
تُعَلِّمُونَهُنَّ مِمَّا عَلِمْتُمُ اللَّهُ فَكُلُّوا مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَادْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ }

“Na wanakuuliza wamehalalishwa nini? Sema: mmehalalishiwa kila vilivyo vizuri na mllichowafundisha wanyama kukiwinja, mnawafundisha alivyo kufunzeni Allah, Basi kuleni walichokukamatieni na, kisomee jina La Allah.” (Al-Maaidah: 4).

Amepokea Abu tha'laba Al-khushni Asema “nimemjia Mtume Rehma na Amani zimfikie, nikasema ewe Mtume wa Mwenyeesi Mungu twaishi katika ardhi ya kuwinja, nawinja kwa uta wangu na nawinja kwa mbwa wangu alofunzwa (kuwinja), na nawinja kwa mbwa ambaye hakufunzwa, basi nipashe habari niipi inayo nifaa? Akasema: “Amma kuhusu ulichokitaja kuwa muko katika ardhi ya kuwinja basi ulichokiwinja kwa uta wako na ukataja jina la Allah basi kile, na ulicho kiwinja kwa mbwa wako uliomfunza (kuwinja) na ukataja jina la Allah basi kile, na kilichowinjwa na mbwa wako ambaye hakufunzwa (kuwinja) ukamkuta (kiwinjo ni hai) kichinje na ukile” imepokewa na An-Nisaai na Ibnu Maajah.

Uwakili Na Udalali (As-Samsarah)

Wakili ni jina la yule anayemfanyia kazi mwengine kwa ujira, kuuza na kununua, hilo pia huambatana na dalali ambaye humfanyia kazi mwengine huuza na hununua kwa ujira. Uwakili

ni aina mojawapo katika kazi ambayo mtu humiliki mali kwa mujibu wake kisheria. Hakika amepokea Abu Daud kutoka Qays Bin Abi Ghurza Al-Kinany Asema: Tulikuwa wakati wa Mtume Rehma na Amani zimfikie tukitwaa Samasira, akapita mbele yetu Mtume Rehma na Amani zimfikie akatuita kwa jina ambalo ni bora kuliko hilo akasema: **“Enyi mkusanyiko wa wafanyi biashara hakika ya biashara huingia ndani yake urongo na kuapa basi isafisheni na sadaka”** maana yake ni yeze huzidisha katika kusifu bidhaa yake mpaka yuwasema urongo na huenda akaapa ili kukiiza bidhaa yake. Basi ni Sunnah kutoa sadaka ili kufuta athari ya hayo, hapana budi iwe kazi ambayo aliyoajiriwa juu yake kuuza na kunuwa iwe ni yenye kujulikana, imma kwa bidhaa au kwa muda. Basi ameajiriwa kumuuzia au kumnumunulia nyumba Fulani au kitu Fulani huwa ni sahihi, hivyo hivyo akimuajiri kumnumunulia au kumuuzia kuanzia mchana mpaka usiku huwa ni sahihi, amma akimuajiri kwa kazi isiyojulikana huwa ni fisidifu.

Sio katika uwakili (Samasira) yale yanayo fanywa na baadhi ya wanaoajiriwa, nao ni tajiri humtuma mtumishi amnunulie bidhaa kutoka kwa mtu mwengine, na huyo mtu mwengine ampe mali ili anunuwe kutoka kwake, wala haihisabu katika bei bali huichukuwa kwake uwakili wa tajiri, hii ndio wanayoiita (Commission) hii haitambuliwi kuwa ni (Samsarah) kwa sababu mtu ni wakili wa tajiri ambaye amemtuma kumnumunulia. Basi itakachopunguwa katika bei ni cha mnunuaji na sio mtumwa, kwa hivyo ni haramu kwake yeze kuichukua, bali hiyo ni juu ya aliyomtuma amruhusu aliyemtuma na itakuwa yajuzu kwake yeze, hivyo hivyo lau kama amemtuma mtumishi wake au rafiki yake amnunulie kitu na mwenye kuuza akampa mali yaani (Commission) akanunua kwake kitu, basi haijuzu kwake yeze kuichukua kwa sababu hiyo sio (Simsarah) bali ni uwizi wa mali ya aliyomtuma, kwani yeze ni wa aliyemtuma na sio mtumwa wa aliyotumwa kwake.

Mudharaba

Mudharabah ni kushirikiana wawili katika biashara, huwa mali ni ya mmoja wao na kazi ni kwa mwengine, yaani kushiriki kwa

mwili wa mtu na mali ya mwengine. Basi huwa kwa mmoja wao kufanya kazi na mali ni ya mwengine. Juu yao kuafikiana kwa kiwango maalumu cha faida au nusu yake, mfano atoe mmoja wao elfu moja na azifanyie kazi mwengine na wagawanye faida baina yao. Hakuna budi kusalimisha mali kwa mwengine kufanya kazi, na kuwachwa baina yake na baina ya mali, kwa sababu Mudharaba hulazimisha kusalimisha mali kwa Mudharib. Mwenye kuzifanyia kazi kumshurutisha mwenye mali kumpa thuluthi ya faida, au nusu yake au wanayowafikiana juu yake, baada ya kuwa hilo kujulikana sehemu yake, kwa sababu ya kustahiki Mudharib kwa faida ya kazi yake, basi yajuzu yale waliowafikiana juu yake ikiwa ni kidogo au kingi kama ujira katika kuajiri, na sehemu ya matunda katika kugawanya mimea. Basi Mudharaba ni aina kati ya aina ya kazi ambayo huwa ni sababu ya kisheria ya kumiliki, basi humiliki mudharib wa mali ambayo amepata faida kutoka Mudharaba wa kazi yake, kwa mujibu ya yale walifikiana juu yake. Mudharaba ni aina moja kati ya aina ya shirika kwa sababu yake ni ushirika wa mwili na mali, shirika ni katika muamalati ambao dalili ya sheria imeiruhusu basi kutokamana na Abi Hurairah Asema: Asema Rehma na Amani zimfikie “**Asema Allah Mimi ni watatu wa washirika wawili maadam hatomkhini mmoja wao menziwe, na akimkhini mmoja wao mwengine noandoka (Allah) baina yao.**” Na asema Amani zimfikie “**Mkono (msaada) ya Allah uko na washirika wawili maadam hawatokhiniana**” na imepokelewa kuwa Al-Abbass Bin Abdul-Muttalib Radhi za Allah zimfikie alikuwa akitoa mali kwa ajili ya mudharaba kwa sharuti kuwa Mudharib (mwenye kuzifanyia kazi) hatovuka nazo bahari, na wala asipitie bonde, wala asinunue mifugo, basi akifanya hayo atadhamini (Mudharib) hasara. Likamfikia hilo Mtume wa Allah Rehma na Amani zimfikie na akalikubali. Masahaba Radhi za Allah ziwafikie waliwafikiana juu ya kujuzu Mudharaba. Alikuwa Umar akitoa mali ya mayatima kwa ajili ya Mudharaba, pia amempa **Uthman mtu mali kwa ajili ya Mudharaba**. Katika Mudharabah huwa Mudharib (mwenye kuzifanya kazi) ana milki kwa ajili ya kazi yake kwa mali ya mwengine. Basi Mudharabah kwa upande wa Mudharib ni kazi

na sababu kati ya sababu ya kumiliki, lakini kwa upande mwengine mali sio sababu kati ya sababu ya kumiliki bali ni sababu kati ya sababu ya kukua milki.

Al-Musaqaat (Kugawanya Matunda)

Katika aina ya kazi ni Musaqaat, nayo ni mtu kumwachia mtu mwengine asimamie kunyunyiza maji miti yake na kufanya mengineo yanayohitajia kwa malipo ya kupaya matunda maalumu. Imeitwa musaqaat kwa sababu ya kitendo cha (saqiyi) kunyunyiza maji, kwa sababu watu wa Hijaz miti yao yahitaji sana kunyunyiziwa mali, kwa sababu wao hunyunyiza kutoka visima ndio ikaitwa hivyo. Musaqaat ni kazi ambao sheria imedokeza kujuzu kwake. Hakika amepokea Muslim kutoka Abdullah bin Umar Radhi za Allah zimfikie yeye na babake, asema “**Amefanyisha kazi Mtume wa Allah Rehma na Amani zimfikie watu wa Khaybar kwa sharuti ya kuwapa sehemu ya matunda au mimea**” yajuzu musaqaat katika mitende, miti na mizabibu kwa malipo ya sehemu maalumu anayopewa mfanyi kazi katika matunda - hii ni katika mti ulio na matunda. Amma miti yasio kuwa na matunda kama miti yanayomea karibu na maji au yenye matunda yasiokusudiwa kama Msunodari na Mwerezi basi hajuzu ndani yake Musaqaat, kwa sababu Musaqaat huwa katika sehemu ya matunda, na haya yasiokuwa na matunda yanayokusudiwa. Isipokuwa hukusudiwa ndani yake majani yake kama Mforsadi na waridi. Hakika hujuzu ndani yake Musaqaat, kwa sababu huvunwa kila mwaka na humkinika Musaqaat juu ya sehemu yake. Basi huthubutu kwa mfano huu hukmu yake.

Kuajiri Muajiriwa

Uislamu umeruhusu mtu kuajiri waajiriwa yaani wafanyi kazi watakaomfanyia kazi, Asema Ta’ala:

{ أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَةَ رَبِّكَ نَحْنُ قَسَمْنَا بَيْنَهُمْ مَعْبُشَتَهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَرَفَعْنَا
بَعْضَهُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِيَتَّخِذَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا سُخْرِيًّا }

“Kwani wao ndio wanaogawa rehema za Mola wao? Sisi tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani, na tukawanyanyua baadhi yao juu ya wengine kwa daraja

nyinyi kua hivyo baadhi yao wanawafanya wenginewe wawatumikie" (Az-Zukhruf: 32).

Amepokea kuwa Ibn Shihab Asema: Amenipasha habari Urwah Bin Zubair kuwa Aisha Mama wa Waumini Radhi za Allah zimfikie Asema: "**Mtume wa Allah Rehma na Amani zimfikie na Abu Bakar wamemuajiri mtu kutoka Bani Dayl kama kiongozi wa njia aliye na ujuzi ilhali yeye yuko ndani na dini ya makafiri wa Quraish wakampa ngamia wao wawili na wakasikizana naye kwenye pango la jabali Thawr baada ya usiku mitatu aje na ngamia wao wawili asubuhi ya siku wa tatu.**" Na asema Allah Ta'ala:

{ فِإِنْ أَرْضَعْنَا لَكُمْ فَاتَّوْهُنَّ أُجُورَهُنَّ }

"*Na wakikunyonyesheeni, basi wapeni ujira wao*" (At-Talaaq: 6).

Amepokea Bukhari kutoka kwa Abi Hurairah Asema: Asema Rehma na Amani zimfikie, "**Asema Allah aliye na Izza aliye Tukuka: watu watatu Nitakuwa mpizani wao siku ya Qiyama, mtu aliyetoa (kilma) kasha akaenda kinyume, na mtu aliyemuza mtu huru kasha akala thamani yake na mtu alomuajiri muajiriwa aliomfanyia (kazi yake) kikamilifu na asimpe ujira wake.**" Kuajiri ni kumiliki muajiri manufaa ya muajiriwa na kumiliki muajiriwa mali kutoka muajiri, nayo ni mkataba wa kutoa manufaa kwa (malipo) ridhaa. Mkataba wa kuajiri muajiriwa imma ni kwa manufaa ya kazi anayoifanya muajiriwana imma kwa manufaa ya muajiriwa mwenyewe, basi ikipatikana mkataba juu ya manufaa ya kazi huwa kilichofungwa juu yake mkataba ni manufaa ambao hupatikana kutoka kazi, kama kuajiri wafanyi kazi za mikono na wajuzi wa kazi maalumu kama kuajiri mpakaji rangi, mfuaji chuma na Seremala. Ikifungwa mkataba juu ya manufaa ya mtu huwa mkataba ni juu ya mtu kama kuajiri mtumishi na mfanyi kazi. Muajiriwa huyo ni imma tu amfanyie kazi mtu kwa muda maalumu, kama mwenye kufanya kazi katika kiwanda au bustani au shamba la mtu kwa ujira maalumu, au mfanyi kazi wa serikali katika nyanja zote, na imma afanye kazi maalumu kwa watu wote kwa ujira maalumu kama Seremala, mshonaji

nguo, mshonaji viatu na mfano wake. Wa kwanza ni muajiriwa khasa na wapili ni muajiriwa kishirika au muajiriwa jumla.

5:- KAZI YA MUAJIRIWA

Kufafanua Kazi

Uajir ni kunufaika kwa manufaa ya kitu kilichoajiriwa nayo kwa upande wa muajiriwa ni kunufaika na juhudi zake. Hapana budi katika kuajiri muajiriwa katika kufafanuliwa kazi, kufafanuliwa muda, kufafanuliwa ujira na kufafanuliwa juhudi. Basi hapana budi ila kubainisha aina ya kazi, mpaka isiwe ambao haijulikani, kwa sababu kuajiriwa kusijulikana ni fisadi. Basi hapana budi ila kufafanuliwa muda wa kazi, kwa siku, au mwezi au mwaka, na hapana budi ila kufafanuliwa ujira wa mfanyi kazi. Kutoka kwa Ibn Mas'ud Asema: Asema Rehma na Amani zimfikie **“anapoajiri mmoja wenu muajiriwa basi amjulishe kwa ujira wake.”** Hapana budi kufafanuliwa juhudi ambazo atazitoa mfanyi kazi wala hakalifishwi mfani kazi ila kwa kazi anayoiweza. Asema Allah Ta'ala:

{ لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا }

“Haikalifishi Allah nafsi ila kwa uweza wake.” (Al-Baqarah: 286).

Asema Rehma na Amani zimfikie, **“Nikiwaamrisha jambo lifanyeni kwa kadri ya uweza wenu.”** imepokewa na As-sheikhani (Bukhari na Muslim kwa njia ya Abi Hurairah). Basi haijuzu kumuomba mfanyi kazi kutoa juhudi ila kwa kadri ya uweza wake wa kikawaida. Kwa kuwa haiwezekani kupima juhudi kwa vipmo vya ki-hakika imekuwa kufafanukiwa saa za kazi ndio mizani ya kipekee ya kileo ya kuidhibiti. Basi kufafanuliwa saa za kazi ni kidhibiti cha juhudi. Na hufafanuliwa pamoja na yake aina ya kazi, kama kuchimba ardhi ngumu na laini, kuketa chuma au kuketa mawe, au kuendesha gari au kufanya kazi katika mgodi, hakika yake hubainisha pia kiwango cha juhudi. Kwa hilo huwa kazi imekwisha kufafanuliwa kwa aina yake, muda wake, ujira wake na juhudi ambayo itatiwa ndan yake. Kwa haya hakika sheria ilipofanya Mubah kumtumisha mfanyi kazi ililazimisha kufafanuliwa kazi yake, aina, muda, ujira na juhudi. Ujira huu

anaouchukuwa muajiriwa ni ridhaa kwa kazi aloifanya ni milki yake kwa juhudhi alotoa.

Aina ya kazi

Yajuzu kuajiri juu ya kila kazi iliyohalali. Basi yajuzu kuajiri katika biashara, ukulima na usanii wa kiviwanda, na juu ya utumishi, juu ya uwakili, juu ya kunukulu jawabu ya mpizani, mshtaki au mshtakiwa, juu ya kutaka ushahidi na kuibeba kwa hakimu, juu ya kuomba haki, na juu ya kuhukumu baina ya watu, juu ya kuchimba visima na ujenzi, kuendesha magarina ndege, juu ya kazi imma itukie juu ya kazi maalumu, au juu ya kazi iliyosifiwa sifa zake. Basi ikitukia uajiri juu ya kazi maalumu, au muajiriwa maalumu mfano kama Khalid kumuajiri Muhammad kufanya kazi ya kushona nguo hii, au aendeshe gari hili, basi humpasa aloajiriwa kufanya kazi hiyo mwenyewe, wala haijuzu kata kata kuwa mtu mwengine mahala pake, basi akiugua au akishindwa kufanya kazi hasimami mahala pake mtu mwengine, kwa sababu muajiriwa amekwisha fafanuliwa, na ikiharibika nguo maalumu au kuharibika gari maalumu haimpasi kwake yezekufanya kazi kwengineko, kwa sababu aina ya kazi imekwisha fafanuliwa. Amma ikitukia uajiri juu ya kitu maalumu kilichosifiwa sifa yake, au muajiriwa aliosifiwa kwa kazi maalumu, au kwa kazi iliyosifiwa, basi wakati huo hukmu huwa tofauti katika hali hii yajuzu kwa muajiriwa kufanya kazi na yajuzu kwa mwengine kusimama mahala pake. Anapouga au kushindwa yampasa aweke mtu atakaefanya kazi yake. Hivyo hivyo yampasa kuendesha gari, au kushona nguo, gari lolote au nguo yejote atakayompa muajir, maadamu yaambatana na sifa ya kazi ambayo kwa mujibu wake mkataba wa uajiri umefungwa juu yake. Kwa sababu ufanuzi haukuwa juu ya dhati, basi haiwi ni ufanuzi wake bali huwa ufanuzi ni wa aina na huwa kwa jinsi yake, yaani kitu chochote maadamu ni aina ya jinsi hiyo. Katika hali hii huwa ufanuzi kwa sifa wala si kwa dhatiinayowacha khiyari kwake katika kuleta dhati yejote katika jinsi hiyo ambayo imefungwa juu yake mkataba. Kufafanua aina ya kazi humjmulisha mfanyi kazi ambao atakaofanya kazi kwa kubainisha juhudhi yake mfano kama mhandisi, na hujumisha kazi ambayo ataifanya kwa

kubainisha juhudi ambayo atatia ndani yake mfano kama kuchimba kisima, juu ya hayo huwa kufafanua kazi kama sifa ni kama kuifafanua kwa dhati, basi hupelekwa ufanuzi wake kwa sifa kama ufanuzi wake kwa dhati. Hutosha kuwa katika sifa hata kama hayuko hayuko, na huwa kama alohuduria na kushuhudia. Pia yajuzu kumuajiri Muhandisi fulani basi ufanuzi huwa ni yeye, hivyo hivyo yajuzu kumuajiri Muhandisi alio na sifa kadha, kama inavyojuzu kumuajiri mtu ili ashone nguo fulani, hivyo hivyo kumuajiri mtu ili ashone nguo ilio na sifa kadha.

Basi atakapokubali mtu kazi miongan mwa kazi na akampa mwengineo kwa malipo machache kuliko hayo, na kilichobakia ikawa ni faida yake hiyo yajuzu, sawa sawa amemsaidia wa pili kwa kitu au la, kwa sababu yajuzu kwake yeye kumuajiri mwengineo kwa ujira sawa na wa kwanza, au chini yake au kwa zaidi yake kwa hayo ndivyo wanavyofanya wenyewe viwanda kama washonaji, waseremala na mithali yao kati ya wanaoajiri wafanyi kazi ili kufanya kazi pamoja nao, hivyo hivyo hufanya Mwunzi katika kuajiri wafanyi kazi ili kufanya kazi ya Mwunzi, hiyo pia hujuzu, sawa akiwapa kiwango ambacho amekichukuwa au zaidi au kidogo, kwa sababu kuajir huko sawa sawa ikiwa juu ya kazi maalumu, au ikiwa kwa muda maalumu nayo ni aina ya muajiri khasa inavyojuzu kisheria.

Amma kuajiri wafanyi kazi juu ya kuchukua kitu katika ujira wao au kuweka msimamizi juu yao kwa sehemu ya ujira wao hilo halijuzu, kwa sababu wakati huo itakuwa amekwisha iba sehemu ya ujira wao ambao amekadiria, amekwisha pokea Abu Daud kutoka Abi Saeed Al-Khudhriy kuwa Mtume Rehma na Amani zimfikie Asema: “**Tahadharini na kugawanya, akasema: Tukasema na nini kugawanya? Akasema: kupunguzwa kitu ambacho ni baina ya watu.**” Na katika riwaya nyengine kutoka Attaa kutoka kwa Mtume Rehma na Amani zimfikie Asema: “Mtu aliye na usimamizi juu ya watu na akachukua kutoka sehemu ya huyu na huyu.” Hata kama Mwunzi amemwambia mtu alete wafanyi kazi mia, kila mfanyi kazi akalipwa kwa Dinari moja na akawapa wafanyi kazi chini

ya Dinari moja hilo hajuzu, kwa sababu kiwango ambacho wamekubaliana juu yake huchukuliwa ni ufanuzi wa ujira wa kila mfanyi kazi. Basi akipunguza ndani yake huwa amechukuwa haki yao. Amma akisikizana naye juu ya kuleta wafanyi kazi mia wala hakutaja ujira wao na akawapa ujira wao chini ya yale aliyosikizana na Mwunzi hilo lajuzu, kwa sababu atakuwa hakupunguza katika ujira wao waliokadirwa noa. Ni sharuti kufafanua aina ya kazi ufanuzi ambao huondoa ujinga/kutokujua, mpaka uwe ujira ni wenye kujulikana, kwa sababu uajiri juu ya ujingga ni fisidifu. Lau angesema nimekuajiri ili unibebee sanduku hili la bidhaa mpaka Misri kwa Dinari kumi basi huwa ni uajiri ulio sahihi au nimekuajiri unibebee kila tani kwa Dinari moja huwa ni sahihi au unibebee tani moja kwa Dinari na kitakachozidi kitakuwa kwa hesabu ya hilo pia hilo hujuzu, hivyo hivyo kila tamko lenye kuonyesha kutaka kubebewa wote. Amma akimwambia nibebee kait yake tani moja kwa Dinari na kitakachozidi kitakuwa kwa hesabu ya hayo akikusudia chochote kitakachobakia hilo halisihi, kwa sababu mkataba uliofungwa juu yake baina yao hakijulikani. Amma lau akisema nibebee kila tani kwa Dinari hilo husihi, kama pia lau akimuajiri kumtolea maji kwa kila mita moja kwa tani moja hilo lajuzu. Basi ni sharti uajiri ujulikane na ikiingia ujingga hilo halisihi.

Muda wa kazi

Lisilokuwa na budi katika kuajiri si tu kutaja kazi ambayo atakayoajiriwa juu yake kama kushona na kuendesha gari mpaka mahali kadhaa, wala isitajwe ndani yake muda, na mionganoni mwake n yale yasiokuwa na budi tu kutajwa ndani yake muda ambao atakayeajiriwa juu yake na wala isitajwe kiwango cha kazi, kama kumuambia nakuajiri kwa mwezi mmoja unichimbie kisima au mtaro, wala asihitaji kujua kiwango, basi ni juu yake kuchimba katika mwezi huo, akichimba kidogo au kingi. Mionganoni mwa yasiokuwa na budi kutajwa ni muda wa kazi kwa mfano kujenga nyumba, kubuni kinu cha kusafisha mafuta na yanayofanana nayo. Kila kazi ambayo haijulikani ila ka kutajwamuda basi hapana budi ila kutaja muda. Kwa sababu uajiri lazima uwe ni maalumu, kutotaja muda katika baadhi ya

kazi huifanya ni Majhul isio julikana. Na ikiwa uajiri haujulikani basi haijuzu. Ikitokea uajiri juu ya muda maalumu kama mwezi na mwaka basi haiwi kwa mmoja wao kuivunja ila baada ya kumalizika muda. Akimuajiri kwa muda unaoendelea kama amemuajiri mfanyi kazi kila mwezi kwa Dinari ishirini, basi mfanyi kazi kila mwezi atajifunga na mkataba kwa kufanya kazialoajiriwa kuifanya. Hapana budi kutajwa muda katika mkataba wa kuajiri kufuata mkataba, bali lau kama amemuajiri katika mwezi wa Rajab na yeye yuko katika mwezi wa Muhamarram basi huwa ni sahihi, na inapotajwa muda katika mkataba au ikawa kutajwa kwake katika mkataba ni dharura ili kuondoa kutojua basi yapasa kufafanuliwa muda kwa kipindi cha wakati kama dakika au saa au wiki au mwezi au mwaka.

UJIRA WA KAZI

Ni sharti kuwa mali ya uajiri iwe ni yenyе kujulikana kwa ushahidi na kwa sifa ambayo itaondoa kutojua, kwa sababu Mtume Rehma na Amani zimfikie asema: “**atakapo ajiri mmoja wenu muajiri basi amjulishe kwa ujira wake.**” Kulipia uajiri yajuzu iwe kwa pesa, na yajuzu isiwe kwa pesa, na yajuzu iwe kwa mali, na yajuzu iwe kwa manufaa. Kila kinachojuzu kuwa na thamani yajuzu kuwa ni malipo sawa sawa ikiwa ni dhati au manufaa, kwa sharti iwe ni yenyе kujulikana. Amma ikiwa haijulikani basi haijuzu. Lau kama amemuajiri mvunaji kwa malipo ya sehemu ya mavuno hilo si sahihi kwa sababu ya kutojulikana (malipo) kinyume na lau angemuajiri kwa pishi moja au kwa kibaba kimoja hilo husihi, yajuzu kumuajiri kwa chakula chake au mavazi yake, au kumpa ujira pamoja na chakula chake na mavazi yake, kwa sababu hilo lajuzu kwa myonyeshaji. Asema Ta’ala:

{ وَعَلَى الْمُؤْلُودِ لَهُ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ }

“*Na juu ya baba chakula cha kina mama, na nguo zao kwa mujibu wa ada*” (Al-Baqarah: 233).

Basi akajaalia kwao nao chakula na mavazi kwa ajili ya kunyonyesha, ikijuzu hilo kwa mnyonyeshaji basi hujuzu kwa wengineo kwa sababu wote ni uajiri, nalo ni suala mionganii mwa mas’ala ya uajiri.

Kwa ufupi yapasa uajiri uwe maalumu elimu inayoondoa kutokujua mpaka aweze kuitekeleza bila ya kuwepo mzozo, kwa sababu asili ya mikataba yote ni kuondoa mzozo baina ya watu. Hapana budi kuwafikiana juu ya ujira kabla ya kuanza kazi na ni makruhu kutumia muajiri kabla ya kuafikiana naye juu ya ujira. Ikitokea uajiri juu ya kazi inayostahiki ujira wa mfanyi kazi kwa mkataba, lakini haipasi kuipokea ila baada ya kazi, basi yapasa wakati huo haraka haraka kuipokea kwa msemo wake Rehma na Amani zimfikie, “**watu watatu Mimi ni mpizani wao Siku ya Kiyama, mtu alotoa kwa ajili yangu kasha akakhini, na mtu alomuajiri muajiri aliyotekeleza kazi yake kasha asimpe ujira wake.**” Imepokelewa na Bukhari kutoka kwa Abi Hurairah. Amma akiweka sharti ya kuakhirisha kwa ujira kwa muda, akiweka sharti ya kumlipa kwa siku au mwezi au chini ya hapo au zaidi ya hayo ni kwa mujibu ya masikilizano yao. Si dharura kwa muajiri kupata manufaa kivitendo bali yatosha kummakinisha yeye kwa manufaa hali inayofanya ujira ulazimike juu yake. Lau kama amemuajiri muajiriwa khasa ili amtumishe nyumbani kwake kasha akaja nyumbani akaiweka nafsi yake chini ya amri yake basi astahiki ujira kwa ajili ya muda ambao humkinika kunufaika na muajiri. Kwa sababu hata kama mkataba ni juu ya manufaa na kivitendo asiyepata lakini kumwezesha yeye kutekeleza nay eye kutomtumia ili kupata manufaa yatosheleza kustahiki ujira. Kwa sababu upungufu watoka kutoka upande wa muajiri na sio kutoka upande wa muajiriwa. Amma muajiri na shirika au muajiri amma hakika yeye anapoajiriwa juu ya kazi maalumu, basi ni lazima imma awe chini ya muajiri kama mpakaji rangi anayepaka rangi duka, na mshonaji nguo dukani kwake, jukumu lake la kazi haliondoki mpaka aisalimishe kazi kwa alomuajiri, wala hastahiki ujira mpaka amsalimishie baada ya kuimaliza, kwa sababu mkataba uliofungwa juu yake ni kuwa jukumu haliondoki maadamu hajamsalimishia aliyefanya mkataba naye. Imma itokee kazi katika milki ya muajiri mfano muajiri amweke katika nyumba yake mshonaji nguo ili ashone ndani yake, au aipake rangi basi jukumu la kazi litaondoka na atastahiki ujira kwa mujibu wa

kazi yake kwa sababu ye ye yuko chini ya mikono ya muajiri, basi hapo kwa hapo huwa amepokea kazi.

JUHUDI AMBAYO HUITIA KATIKA KAZI

Hutokea mkataba katika ujira wa muajiri juu ya manufaa ya juhudil alioitoa. Hukadiriwa ujira kwa manufaa. Amma juhudil yenyewe sio kipimo cha ujira, wala si kipimo cha manufaa. Ingekuwa ni hivyo basi ingekuwa ujira wa mchongaji mawe ni zaidi kuliko mhandisi, kwa sababu juhudil yake ni zaidi lakini waqiah ni kinyume na hayo. Kwa hayo ujira huwa ni badili ya manufaa, na sio badili ya juhudil, kama pia hukhitalifiana ujira kwa kutofautika kazi tofauti. Hakika hivyo hivyo hutofautika ujira wa kazi moja kwa kutofautika kiwango cha manufaa wala sio kwa kutofautika juhudil. Mkataba katika hali hizi mbili juu ya manufaa ya muajiriwa wala si kwa juhudil ya muajiri. Basi kinachozingatiwa ni manufaa, sawa sawa manufaa na waajiriwa hukhitalifiana katika kazi tofauti, amma manufaa ya waajiriwa tofauti katika kazi moja wala si kwa kuzingatiwa tu juhudil. Ndio kuwa manufaa ya kazi ni matunda ya juhudil sawa sawa ikiwa katika kazi tofauti, au katika kazi moja inayofanywa na watu tofauti, lakini muradi wake ni manufaa yake wala si mujarad wa kutoa juhudil hata kama chenye kuonekana ni juhudil. Mtu akimuajiri mjengaji kumjengea basi hapana budi ila kukadiria uajiri huo kwa wakati au kazi, basi akikadiria kwa kazi basi kinachodhiihirika ni manufaa katika kuibainisha mahala pake, urefu wake, upana wake, urefu wake na mada ya kujengea mpaka mwisho, ikikadiria kwa wakati basi manufaa huzidi ndani yake kwa kuzidi mada na hupungua kwa kupunguka kwake. Basi huwa kusifu kazi na kutaja wakati ni kipimo cha manufaa na ikikadiria kwa wakati basi hatofanya kazi zaidi ya uweza wake wakikawaida, wala halazimishwi kwa mazito yasiyokuwa ya kawaida.

HUKMU YA KUAJIRI JUU YA MANUFAA YALIYO HARIMISHWA

Sharti ya kusihi uajiri ni uwe juu ya manufaa yaliyo Mubah, wala haijuzu kuajiri muajiri kwa manufaa ambayo yameharamishwa. Basi haijuzu kuajiri muajiri juu ya kubeba

tembo mwenye kulinunua, wala juu ya kulikamua, wala juu ya kubeba nguruwe wala mmmfu. Amekwisha pokea Tirmidhi kutoka Anas Bin Malik asema: “**amelaani Mtume Rehma na Amani zimfikie katika tembo watu kumi: mwenye kulikamua, mwenye kukamuliwa, mwenye kulinywa, mwenye kulibeba, mwenye kubebewa, mwenye kulinywesha, mwenye kuliiza, mwenye kula thAmani yake, mwenye kulinunua na mwenye kununuliwa.**” Hivyo hivyo haijuzu kuajiri juu ya kazi ya riba, kwa sababu ni kuajiri juu ya manufaa yaliyo harimishwa, kwa sababu amekwisha pokea Ibm Maajah kutoka kwa njia ya Ibn Mas’uod kutoka kwa Mtume Rhma na Amani zimfikie “**kuwa ye ye amlaani mlaji riba na mwenye kumwakilisha na weny kushuhudia na mwenye kuliandika.**” Amma mfanyi kazi wa Banki, idara za kuchapa sarafu na mashirika yote yanayofanya kazi kwa riba hakika hiyo huangaliwa ikiwa kazi ambayo ameajiriwa juu yake ni sehemu katika kazi za riba sawa sawa iwe natija yake ya pekee ni riba au natija yake ni ya mengineo pamoja na kazi za riba, hakika ni haramu kwa muislamu kufanya kazi hii na hilo kama meneja, muhisabu na mchungaji na kila kazi ambayo manufaa yake hufungamana na riba, sawa sawa ikiwa fungamano lake ni moja kwa moja au si moja kwa moja. Amma kazi ambazo hazifungamani na riba kwa sura ya moja kwa moja na kwa sura isiyokuwa ya moja kwa moja kama Bawabu, Mlinzi, mfagiaji na yanayofanana na hayo hilo hujuzu, kwa sababu ni uajiri juu ya manufaa yaliyo Mubah na kwa kuwa haiambatani na yale yanayo ambatana na mwandishi wa riba na shahidi wake, mfano ni mfanyi kazi wa benki na wafanyikazi wa serikali, ambao hushughulika na kazi za riba, mfano ni wafanyi kazi ambao hushughulika katika kuwapa wakulima mikopo ya riba, na wafanyi kazi katika mashirika ya kifedha ambao hufanya kazi ambazo ni katika kazi za riba na wafanyi kazi wa idara ya mayatima ambao hukopeshwa mali kwa riba. Basi kazi zote hizo zimeharamishwa na huchukuliwa mwenye kufanya kazi ndani yake huwa amefanya dhambi kubwa mionganini mwa madhambi makubwa, kwa sababu huambatana juu yake kuwa ye ye ni mwandishi wa riba au shahidi, na hivi ndivyo kila kazi

mionganoni mwa kazi ambazo Allah Ta'ala ameziharamisha huwa ni haramu kwa muislamu kuwa ni muajiriwa ndani yake.

Amma kazi ambazo faida yake ni haramu au kushiriki kati yake ni batili kisheria kama mashirika ya Bima, mashrika ya Hisa, jumuia ya Ushirika na yanayofanana na hayo, hakika hutizamwa notani yake. Basi ikiwa kazi anayoifanya mfanyi kazi ni katika kazi ambazo Sheria imebatilisha ikiwa ni mikataba iliyobatili au fisidifu au ni kazi ambazo zilizoratibishwa kati ya kazi ambayo haijuzu kuzifungia mikataba au kazi ambazo hukhitalifiana na hukmu za kisheria, basi huwa ni haramu kwake kuwa ni muajiriwa ndani yake. Hilo ni kama mfanyi kazi anayeandika mikataba ya bima hata kama hazikubali, au yule ambaye hujadiliana juu ya sharuti za bima au yule ambaye hukubali bima. Mfano mfanyi kazi ambaye hugawanya faida kwa mujibu ya mauzo katika jumuia la ushirika na mfano wa mfanyi kazi anayeza Hisa za mashirika au ambaye yuwafanya hesabu za fungu la Hisa, mfano mfanyi kazi anayesimamia matangazo ya kibiashara kwa jumuia ya ushirika na yanayofanana nayo. Wafanyi kazi wote na mashirika ambayo yajuzu kisheria kazi yake basi yajuzu kuwa ni mfanyi kazi ndani yake. Na ikiwa kazi hiyo haijuzu kwake binafsi kuifanya basi haijuzu kuwa ni mfanyi kazi ndani yake kwa sababu haijuzu kuwa ni muajiri ndani yake. Yale ambayo ni haramu kuyafanya katika kazi basi huwa ni haramu kuajiriwa juu yake hata akiwa muajiri.

HUKMU YA KUAJIRI ASIYEKUWA MUISLAMU

Amma muajiri na muajiriwa si sharuti kwao wao kuwa ni waislamu, au mmoja wao kuwa ni muislamu. Basi yajuzu kwa muislamu kata kata kuajiri asiyekuwa muislamu, kwa sababu ya alivyofanya Mtume Rehma na Amani zimfikie, na ijmaa –us – Sahaba juu ya kuajiri asiyekuwa muislamu katika kazi ye yote iliyo Mubah, na katika kazi za serikali ambayo ameajiriwa kusimamia juu yake. Hakika alimuajiri Mtume wa Allah Rehma na Amani zimfikie amemuajiri Myahudi kama muandishi na akamuajiri myahudi mwengine kama mkalimani, akamuajiri mushirikina kama kiongozi wa njia, na Abubakar na Umar waliwaajiri manasara ili wafanye hesabu za mali kama

inavyojuzu kwa muislamu kumuajiri asiyekuwa muislamu hivyo hivyo yajuzu kwa muislamu kuajiriwa na asiyekuwa muislamu ilikufanya kazi isiyokuwa ya haramu. Amma kazi ya haramu basi hilo haijuzu, sawa akiwa muajiriwa ni muislamu au asiwe ni muislamu. Kwa hayo yajuzu kwa muislamu kuajiriwa na mnasara ili amfanyie kazi. Hii haimaanishi muislamu awe mfungwa anaedhalilishwa na kafiri, bali ni kuajiriwa nafsi yake kwa mengine hilo lajuzu. Uislamu haikuweka uislamu kama sharuti ya kuajiriwa wala uislamu kuwa ni sharuti ya kuajiri. Hakika Ali Radhi za Allah zimfikie ameajiriwa na myahudi, akimchotea maji kila ndoo moja kwa tende na Mtume Rehma na Amani zimfikie akapashwa habari juu ya hilo wala asimkataze, kwa sababu mkataba wa malipo haihusishi kumdhalilisha muislamu. Amma kazi ambazo ndani yake kuna kujikurubisha kwa Allah Ta'ala hilo huwa ni sharuti muajiriwa ndani yake awe ni muislamu. Hayo ni kama Uimamu, Uadhini, Hijjah, kutekeleza Zakat, Kufundisha Qur'an na Hadithi, kwa sababu hilo halisihi ila kwa muislamu basi haijuzu kusimamiwa illa na muislamu. Sababu yake ni kuwa halisihi illa kwa muislamu. Amma ikiwa ni katika kazi ambazo ndani yake kuna kuajikurubisha kwa Allah husihi kutekelezwa na asiyekuwa muislamu kwa sababu husihi kuajiriwa ili kusimamia. Kwa ufupi kazi ambazo muajiriwa hujikurubisha ndani yake kwa Allah basi haichukuliwi katika yale yanayo mkurubisha muajiri kwa Allah hilo huangaliwa hata ikiwa halisihi ila kwa muislamu. Kama Uqadhi hakika yake haijuzu ndani yake kuajiriwa asiyekuwa muislamu. Hata kama yasihi kwa asiyekuwa muislamu, kama vita hilo haijuzu kuajiri asiyekuwa muislamu. Basi dhimmi yajuzu kuajiri kwa ajili ya vita na kupewa ujira wake kutoka kwa Baitul-Maal.

KUAJIRI JUU YA IBADATI NA MANUFAA

Ufafanuzi wa uajiri ni kuwa ni mkataba juu ya manufaa kwa malipo, na sharti kuwa ni manufaa inayomuezesha muajiriwa kunufaika nayo. Hutuongoza pale tunapoitabikisha juu ya matukio kuwa uajiri wajuzu juu ya kila manufaa inayomuezesha muajiriwa kunufaika kutoka muajiri, sawa sawa ikiwa manufaa ya kibinagsi kama mtumishi. Amma manufaa ya kazi kama fundi

maadamu haikuthubutu makatazo ya manufaa hayo kwa dalili ya kisheria, kwa sababu asili ya hukmu juu ya vitu ni Ibahah, na manufaa ya kitu ni katika vitu wala hapa haisemwi kuwa ni mkataba, au muamalati na asili ya (hukmu) ndan yake ni kujifunga (na hukmu) walka si Ibahah, kwa sababu mkataba ni uajiri na sio manufaa. Amma manufaa hlo ni kitu hutokea juu yake muamalati na hufungwa juu yake mkataba, na sio muamalati au mkataba. Kwa hayo yajuzu kuajiri juu ya manufaa ya wote ambazo haikuthubutu makatazo yake sawa sawa imethubutu dalili ya kujuzu kwake au la. Basi yajuzu mtu kuajiri mwanamume au mwanamke kumchapia katika ala ya kupiga chapa (typewriter) kurasa Fulani kwa malipo maalumu, kwa sababu hilo ni uajiri juu ya manufaa maalumu haijathubutu makatazo yake. Basi yajuzu kuajiri juu yake hata kama haijathubutu dalili ya kuijuzisha. Yajuzu kuajiri mtu kupima kwa mizani juu ya kazi maalumu kwa muda maalumu, kwa yale yaliyopokewa katika Hadithi ya Suwaya Bin Qays, amekuja kwetu sisi Mtume wa Allah kwa kutembea tukabadiishana naye na tukamuuzia, na kuna mtu anayepima kwa ujira, akasema Mtume wa Allah Rehma na Amani **zimfikie “pima na uweke sawa”** imepokewa na Abu Daud. Uajiri huu hujuzu kwa kuwa imethubutu dalili ya kuijuzisha. Amma ibadati sawa sawa ikiwa ni faradhi au Nafila hilo hutizamwa ndani yake na ikawa haivuki manufaa ya mtendaji wake kama kujihijia mwenyewe, kutoa zaka zake, basi haijuzu kuchukua ujira juu yake kwa sababu ujira ni malipo ya manufaa, wala hapa mwengine hapati manufaa. Basi kuajiriwa kwake haijuzu kwa sababu ya hiyo, kwa sababu ni faradhi juu yake. Amma ikiwa ibada hiyo huvuka manufaa ya mtendaji wake basi basi hujuzu kuajiriwa juu ayke, hilo kama kuadhania wengineo, kama kuwa imamu kwa wengineo au kuajiri mtu ili amhijie maiti yake au kumtolea zaka zake. Hakika hayo yote hujuzu kwa sababu ni mkataba juu ya manufaa kwa malipo. Ujira hapa ni malipo ya kunufailka, na imetokea kwa mwengine basi hujuzu kuajiri. Amma aloyapokea Tirmidhy kutoka kwa Uthman Bin Abil-A'as kuwa Amesema **“Hakika katika ya mwisho aliyoahidi ya kwayo Mtume Rehma na Amani zimfikie ni kuweka Muadhini asiyechukua ujira kwa adhana yake.”** Katika hadithi Mtume Rehma na

Amani zimfikie akataza kuchukua muadhini anayechukuwaujira kama Muadhini wake wala hakumkataza muadhini kuchukuwaujira. Hii ni dalili ya kuwa kuna waadhini wanaochukuaujira wa wengine hawachukuwiujira, na akamkataza kumchukua muadhini anayechukuwaujira. Katika makatazo yake haya muna kutopendeza kuchukuwaujira kwaajili ya adhana, inayoleta hisia ya kuchukiza kuchukuwaujira juu yake, isipokuwa hiyo si dalili ya kuharimisha uajiri juu yaadhabali ni dalili ya kujuzu kwake pamoja na karaha.

Amma kfundisha, hilo lajuzu kwa mtu kuajiri mwalimu wa kuwafundisha watoto wake au amfundishe yeye, au amfundishe amtakae katika wale anaotaka kuwafundisha kwa sababu kufundisha ni manufaa iliyo Mubah, na yajuzu kuchukuwa malipo kwa ajili yake. Basi ayjuzu kuajiri juu yake. Sheria imejuzisha kuchukuwaujira juu ya kufundisha Qur'ani. Ikawa ikijuzu kuchukwaujira kwa ajili ya kufundisha Qur'ani ni katikamilango bora. Hakika amepokea Al-Bukhari kutoka kwa Ibnu Abbass kutoka kwa Mtume Rehma na Amani zimfikie kuwa amesema "**ujira mlionna haki zaidi kuchukuwaniju ya kitabucha Allah.**" Na amepokea kuwa Mtume Rehma na Amani zimfikie **amemuozesha mtu mke kwa (mahari) ya yale aliyonayo katika Qur'ani** yaani ili amfundishe nayo, amepokea Bukhari kutoka Sahl Bin Sa'ad As-Saideyn. Hakika imefungwa Ijma'a us-Sahabah juu ya kujuzu kuchukuwariziki juu ya kufundisha kutoka Bait-ul-Maal, basi ikajuzu kuchukuwaujira juu yake. Hakika imepokewa kwa njia ya Ibn Abi Shayba kutoka Sadaqa Al-Dimashqy kutoka Al-Wadhy Bin Ataa asema: **kulikuwako Madina walimu watatu wanaofundisha watoto, na alikuwa Umar Bin Al-Khattab akimlipakila mmoja wao (Dinari) kumi na tano kila mwezi.** Yote hayo ni dalili ya kujuzu kuchukuaujira juu ya kufundisha. Amma kwyale yaliyopokewa katika hadithi zinazokataza katika mlangohuu hakika zote huonyesha kutopendekeza kuchukuaujira juu ya kufundisha Qur'ani wala sio kukataza kuajiri juu ya kufundisha, nazo ni dalili ya ukaraha (kuchukiza) kuchukuaujira juu ya kufundisha Qur'ani, wala si juu ya uharamu wa kuajiri ili kuifundisha. Na karaha ya kuchukuaujira hauondowi

kujuzu kwake basi huwa ni karaha kuchukua ujira juu ya kufundisha Qur'ani pamoja na kujuzu kuajiriwa juu yake.

Amma kuajiri Tabibu (Daktari) hilo lajuzu kwa sababu ni manufaa yanayomkinika kunufaika nayo, lakini haijuzu kumuajiri ili kuponyesha kwa sababu kuajiri juu ya hilo au jambo lisilojulikana. Yajuzu kumuajiri tabibu (Daktari) ili kumpima, kwa sababu hilo ni manufaa maalumu yajuzu kuajiri huduma za Tabibu (Daktari) kwa siku maalumu, kwa sababu ni kazi yenye mipaka, yajuzu amuajiri ili ampoze kwa sababu kupoza kwake inajulikana kwa elimu inayoondoa ujinga, hata kama hajui aina ya maradhi, kwa sababu yatosha ajue kuwa tu yeye ni mgonjwa. Hakika yajuzu kuajiri tabibu kwa sababu tiba ni manufaa na yamkinika kunufaika nayo basi yajuzu kuajiriwa juu yake. Kwa sababu imepokewa kutoka kwa Mtume Rehma na Amani zimfikie yale yanayoonyesha kujuzu kuajiriwa juu ya tiba. Amekwisha pokea Al-Bukhari kutoka kwa Anas kuwa asema: “**aliumika Mtume wa Allah Rehma na Amani zimfikie na aliomuumika ni Abu Taybah na akamlipa pishi mbili za chakula na akazungumza na mabwana wakamchaffishie (kazi).**” Ilikuwa kuumika siku hizo ni dawa inayotumiwa kutibu nayo. Basi hii ni dalili inayochukuliwa kama dalili ya kujuzu kumuajiri Tabibu. Amma kauli yake Rehma na Amani zimfikie “**chumo cha kuumika ni khabithi kichafu.**” Ambayo amepokea Tirmidhi kutoka Rafi'i Bin Khadeej, haionyeshi kukataza uajiri juu ya kuumika, bali ni dalili inayoonyesha ukaraha (kuchukiza) kuchuma kupitia kuumika pamoja na kuwa ni Mubah kwa dalili kua **Mtume (saw) ailiita kitunguu thomo na kitunguu maji kua ni khabithi pamoja kuruhusiwa (mubah) kwake.** Amepokea Muslim kutoka Ma'adan Bin Abi Twalha. Haya yote ni katika uajiri ambao manufaa yake ni ya khasah.

Amma uajiri ambao manufaa yao ni amma hakika huduma yake huchukuliwa ni katika maslahi ambayo ni wajibu wa serikali kuwaletea watu. Hilo ni kwa kuwa kila manufaa ambao huvuka manufaa ya mtu binafsi mpaka jamaa, huwa jamaa ni lenye kulihitajia, huwa manufaa hayo ni kwa maslahi ya jumla

ambazo ni wajibu na Baitul – Maal kuwatolea watu wote. Hilo ni kama Amir aajiri kadhi kwa mshahara ili ahukumu baina ya watu, kama kuajiri mfanyi kazi wa idara ya maslahi, kama kuajiri waadhini na maimamu. Huingia katika maslahi ambayo yapasa serikali kuwaajiria watu wote elimu na matibabu. Amma kufundisha kuna Ijmaa-us-Sahabah juu ya kupewa waalimu ruzuku kwa kadri maalumu kutoka Baitul – Maal kama ujira wao **kwa sababu Mtume alifanya fidya ya mateka wa kikafiri kuwafundisha watoto kumi wa kiislamu. Akabadilisha fidya yake badala ya Ghanima.** Nayo (Ghanima) ni milki ya waislamu wote. Amma tiba kwa sababu **Mtume Rehma na Amani zimfikie alitunukiwa tabibu kama zawadi na akamfanya ni wa waislamu.** Basi kule kujiliwa Mtume na zawadi, wala asitumie, wala asiichukue bali akaijaalia kuwa ya waislamu, hii ni dalili ya kuwa zawadi hii ni ya waislamu wote na wala si yake.basi Mtume alipojiliwa na kitu kama zawadi na akaliweka ni la waislamu wote huwa kitu hicho ni cha waislamu wote, kwa hilo hakika ya riziki ya matabibu (madaktari) na waalimu ni kutoka Baitul – Maal, hata kama yajuzu kwa mtu binafsi kuajiri tabibu na kuajiri mwalimu. Isipokuwa ni wajibu wa serikali kuweka tiba na elimu kwa raia wote, wala hakuna tofauti baina ya Muislamu na Dhimmi wala baina ya tajiri na faqih kwa sababu hayo ni kama adhana na uqadhi, hayo ni katika mambo ambayo huvuka manufaa yake na huhitajiwa na watu nayo ni katika maslahi ya jumla na ni katika mambo ambayo ni wajibu wa kuwapa raia na kudhaminiwa na Baitul – Maal.

NI NANI MUAJIRIWA

Hakika ya sheria ya kiislamu humaanisha muajiriwa kuwa ni kila mtu anayefanya kazi kwa ajili ya ujira sawa sawa akiwa ameajiriwa na mtu binafsi au kuhusisha mfanyi kazi bila ya kutofautishiwa na sheria baina ya muajiriwa na serikali na aloajiriwa na mwengineo. Basi mfanyi kazi wa serikali, mfanyi kazi wa jamaa, mfanyi kazi wa kibinafsi kila mmoja wao ni mfanyi kazi na hutekelezwa juu ya hukmu za kazi, yaani kila mmoja wao ni muajiriwa na hutekelzwa juu yake hukmu za kuajiriwa. Basi mkulima nimuajiriwa, mtumishi ni muajiriwa,

mfanyi kazi wa viwanda ni muajiriwa, makarani wa wafanyi biashara ni waajiri mfanyi kazi wa serikali ni muajiri na kila mmoja wao ni mfanyi kazi kwa sababu mkataba wa uajiri imma ikusudiwe manufaa ya mtu. Basi ikipatikana juu ya manufaa ya kitu maingi ndani yake uchunguzi wa muajiriwa kwa sababu yeze hasa mahusiano nayo na ikipatikana juu ya manufaa ya kazi kama kuajiri fundi wa kazi za mikono na mafundi wa kazi maalumu. Au imepatikana juu ya manufaa ya mtu kama kuajiri watumishi na wafanyi kazi haya ndio yanayo ambatana na muajiriwa au hawa ndio yanayo tabikishwa juu yake kuwa yeze ni muajiriwa.

MSINGI AMBAO JUU YAKE HUKADIRIWA UJIRA.

Uajiri ni mkataba juu ya manufaa kwa malipo. Sharuti ya kufungwa kwa mkataba wa uajiri ni kuwa wanastahiki, na kuwa kila mmoja wao ni mwenye kutofautisha baina ya zuri na baya, na sharti ya kusihi kwake na kuridhika kwa wenyе mkataba. Na sharuti ya ujira uwe wajulikana kwa msemo wake Rehma na Amani zimfikie “**Anapoajiri mmoja wenu muajiri basi amjulishe ujira wake.**” Imepokewa na Ad-Dariqutny kutoka kwa Ibn Mas’oud, na aliyoyapokea Ahmed kutoka kwa Abi Said **kuwa Mtume Rehma na Amani zimfikie amekataza kuajiri muajiriwa mpaka abainishiwe ujira wake.** Isipokuwa hata kama ujira haujulikani hufungika uajiri na husihi. Hurudi wakati wa ikhtilafu kwa kiwango chake kwa ujira wa mithali. Basi ikiwa ujira haukutajwa wakati wa kufungwa mkataba wa uajiri au kukhitalifiana muajiri na muajiriwa katika ujira uliotajwa basi hurudi kwa ujira wa mithali yake. Hakika kurudi kwa ujira wa mithali ni Qiyas. Kwa mahari hakika hurudi kwake pale isipotajwa, au kukhitalifiana juu ya kutajwa kwa mahari ya mithali yake. Kwa aliyoyapokea Ahmad kutoka kwa Abdallah kuhusu mwanamume aliyomuoa mwanamke kisha akafa bila ya kumuingilia bila ya kumtajia mahari, akasema haki yake (mwanamke) mahari na juu yake eda na haki yake (mwanamke) mirathi, akasema Ma’aqal Bin Sinan “nimemshuhudia Mtume Rehma na Amani zimfikie akihukumu nayo kuhusu Barwa’ a Binti Washiq mwanamke kati yetu kama ulivyo hukumu. Maana ya kauli yake kuwa haki yake ni mahari ya wanawake wake,

yaani mahari yake ni mirathi ya mahari ya wanawake wake. Mtungaji Sheria (Allah) amewajibisha mahari ya mithali kuwa yule ambaye mahari yake haikutajwa na kwa mfano wa hilo watakapo khitalifiana katika kutajwa mahari ilipokuwa mahari ni malipo katika mkataba wa ndoa hakika hupimwa Qiyas juu ya kila malipo katika mkataba. Hakika huhukumiwa ndani yake malipo ya mithali katika hali ya kutotajwa malipo katika mkataba au kukhitalifiana juu ya malipo yaliyotajwa. Kwa hivyo huhukumiwa ujira wa mithali katika uajiri na kwa bei ya mithali katika biashara pale isipotajwa wakati wa mkataba na wakati wa kukhitalifiana katika kilichotajwa. Juu ya haya huhukumiwa ujira wa mithali wakati muajiri anapo khitalifiana na muajiriwa juu ya ujira uliotajwa na wakati isipotajwa ujira wakati wa kufunga mkataba. Basi ikijulikana ujira au kukhitalifiana juu ya ujira uliotajwa huwa ujira ni ujira wa mithali. Kwa hayo huwa ujira ni vigawanyo viwili; ujira uliotajwa na ujira wa mithali. Amma ujira uliotajwa ni sharuti kuchukuliwa kuridhika juu yake wafungaji wa mkataba, basi wakiridhika wafungaji wawili wa mkataba juu ya ujira maalumu huwa ujira huo ndio ujira uliotajwa wala muajiri halazimishwi kutoa zaidi ya hilo kama pia muajiriwa halazimishwi kupokea kidogo kuliko hicho, bali ndio ujira uliowajibishwa kisheria. Amma ujira wa mithali nao ni ujira wa kazi iliyo mithali yake ima mithali ya mfanyi kazi kwa mkataba ni uajiri ushapatikana juu ya manufaa ya kazi huwa ujira wa mithali ya ujira tu wa mfanyi kazi mithali yake. Ikiwa mkataba wa uajiri umepatikana juu ya manufaa ya mtu.

Ambaye hukadiriya ujira ni yule aliye na ujuzi katika kuweka ujira na sio serikali, na sio desturi ya mji bali ni wenye ujuzi kuhusu ujira wa kazi, muradi ni kukadiria ujira wake au ni mfanyi kazi, muradi ni akadirie ujira wake.

Amma msingi ambao juu yake hukadiriwa ujira kwa upande wa wajuzi nao ni manufaa. Sawa sawa ikiwa ni manufaa ya kazi au manufaa ya mfanyi kazi, kwa sababu mkataba wa uajiri hutokea juu ya manufaa, basi huwa ni msingi ambao husimama juu yake makadirio ya ujira wala haukadiriwi ujira kwa uzalishaji wa

muajiriwa wala si kwa kiwango cha maisha baina ya jamaa. Basi haingii uzalishaji wa muajiriwa wala kunyanyuka kiwango cha maisha katika kukadiriwa kwake bali hurudi kukadriwa kwake kwa manufaa. Basi kwa mujibu wa makadirio ya wajuzi kwa kiwango cha manufaa hayo katika mujtamai ambao wanaishi ndani yake, kwa kukadiria ujira wa muajiriwa, na pindi wajuzi wanapo kadiria ujira wa kazi na ujira wa mfanyi kazi, huitazama thAmani ya manufaa hayo katika mujtamai. Basi huikadiria kwa thAmani ya manufaa ambayo hutekelezwa na mfanyi kazi au kazi. Basi ikitokea ikhtilafu katika makadirio ya thamani ya manufaa katika mujtamai, basi haijuzu kukadiriwa kwa ushahidi wa hoja, bali hutosheka kwa rai ya mjuzi, kwa sababu suala ni kujua thamani ya manufaa wala si kusimamisha ushahidi wa kukadiriwa kwake.

Huu ndio msingi ambao hupelekwa juu yake makadiro ya ujira, nayo ni manufaa kwa mujibu wa makadirio ya wajuzi. Isipokuwa pindi mjuzi anapokadiria ujira wa mithali na sio ujira wa kazi, au tu mfanyi kazi. Basi yapasa juu yao kumtizama mtu aliyemfano wa muajiri kwa kazi hiyo, yaani waitazame kazi na mfanyi kazi, na wakati huo huo waitizame wakati pamoja na zama za uajiri na mahala pake, kwa sababu ujira hutofautika kwa kutofautika kazi, mfanyi kazi, zama na mahali.

Asili ya wajuzi ambao hukadiria ujira au ujira wa mithali katika kuchaguliwa kwao na wafungaji mkataba yaani muajiri na muajiriwa, ikiwa hawakuchagua mjuzi au kuhitalifiana juu yao basi mchakama au serikali ndio ilio na uweza katika kuchagua wajuzi hawa.

KUKADIRI UJIRA WA MUAJIRIWA

Kikawaida mwanaadamu huchangamka katika kutoa juhudhi ili kuzalisha mali ambao atakidhi kwayo mahitaji yake. Na mahitaji ya mwanaadamu ni mengi, wala hawezi kuzikidhi kwa upweke bila ya wengine. Kwa hivyo yamekuwa maisha ya mwanaadamu ni katika mujtamai, hubadilishana na pamoja na wengine natija ya juhudhi zao ni jambo la lazima. Kwa hayo hakika mwanaadamu ambaye huishi katika mujtamai hutia

juhudzi zake ili kuzalisha mali ili hapo hapo aitumie na aibadilishe wala hatii tu juhudzi zake ili aitumie kwa sababu mahitaji yake ni mengi, na yeye na haja kwa mali yasiopatikana kwake, kuhusu haja ya kunufaika na juhudzi ya mwengine moja kwa moja, kama kufundisha na tiba, kwa hivyo imekuwa aina ambayo huizalisha vyovyyote itakavyo kuwa aina yake na idadi yake isipokuwa haitoshi kushibisha mahitaji yake yote, kwa sababu yeye hawezu kuzalisha kitakacho zalisha mahitaji yake yote kwa juhudzi yake ya kibinagsi, bali hapana budi ila kutegemea juhudzi za wengine. Basi yeye anahaja kwa kubadilishana juhudzi za wengine kwa yaliyo ya lazima kwake imma kwa juhudzi au kwa mali. Kufikia hapo imekuwa hapana budi kuwepo ubadilishanaji wa juhudzi za watu kwa kuwa juhudzi hizi huenda zikawekwa juhudzi zengine au mali, imekuwa hapana budi kwa kipimo kitakacho weka thAmani ya juhudzi zilizotiwa kwa malinganisho kwa baadhi yake ili iweze kubadilishwa na kuwekwa thamani ya mali inayo kusudiwa kupatikanwa ili kushibisha, ili aweze kuibadilisha kwa baadhi yake, au kwa juhudzi, kwa hivyo hapana budi kuwa kipimo ambacho chaweka kiwango cha thAmani ya juhudzi na thAmani ya mali kuwa ni moja, mpaka iwezekane kubadilisha mali kwa baadhi yake, na kubadilisha mali kwa juhudzi na juhudzi. Kwa hivyo wakawafikiana juu ya malipo ya fedha ambayo yamuwezesha mwanaadamu kupata mali ya lazima ili kushibisha na kupata juhudzi za lazima za kushibisha. Nayo kwa upande wa bidhaa huwa ni bei na kwa upande wa juhudzi huwa ni ujira. Kwa sababu katika kubadilisha bidhaa kwa bidhaa na kubadilisha juhudzi kwa manufaa ya juhudzi hatoweza mwanaadamu.

Kwa hivyo mwanaadamu hana budi kwa muamalati wa biashara, kama alivyokuwa hana budi kwa muamalati wa kuajiri. Isipokuwa haipatikani fungamano baina ya biashara na uajiri ila kwa sifa yake kuwa ni muamalati baina ya watu kati ya wanaadamu. Wala uajiri haukomi juu ya biashara, wala uajiri haukomi juu ya bei. Kwa hivyo imekuwa kukadirwa uajiri isiyokuwa makadirio ya bei wala moja haliwi mafungamano na jengine. Hilo ni kwa sababu bei ni badili ya mali, nayo ni lazima

kuwa mali kwa mali, sawa iwe mali imekadiriwa kwa thAmani au bei. Ama ujira nao ni kutoa juhudhi nayo si dharura kwa juhudhi hiyo kuzalisha mali, bali huenda ikazalisha mali na huenda isizalishe mali, kwa sababu manufaa ya juhudhi haikomi juu ya uzalishaji wa mali bali kuna manufaa mengine isiyokuwa mali. Basi juhudhi zitiwazo katika ukulima au biashara au viwanda vyovoyote itakavyo kuwa aina yake, vyovoyote kutakavyokuwa kidigo au kingi kiwango chake, huzalisha mali, na huzidisha moja kwa moja utajiri wa nchi. Ama huduma ambazo hutolewa na tabibu (Daktari), mhandisi, wakili, mwalimu na anayefanana nao, hakika juhudhi zao hazizalishi mali, wala hazizidishi moja kwa moja utajiri wa Ummah. Basi akiwa fundi akichukuwa ujira wake basi atakuwa amechukuwa mali kulingana na alichokizalisha, lakini mhandisi atakuwa amechukuwa ujira hachukuwi kulingana na mali kwa sababu hajazalisha mali yejote. Kwa hivyo huwa ni lazima kukadiriwa bei kulingana na mali, kinyume na kukadiria manufaa ya juhudhi, nao haulinganishi na mali bali kulinganisha manufaa huwa ni kwa mali na huenda ikawa bila mali. Kufikia hapa hukhitalifiana biashara na ujira wa muajiri na hukhitalifiana bei na upande wa makadirio ya kivitendo kwa ujira. Pamoja na kuwa haimaanishi kukhitalifiana biashara na uajiri na bei na ujira kuwa ni kukosekana fungamano baina yao, bali maana ya kukhitalifiana ni kuwa uajiri haujengwi juu ya biashara wala biashara juu ya uajiri wala bei haikadirwi juu ya makadirio ya bei, kwa sababu kujengea mojawapo na jengine hufikisha katika kuzihukumu bei za bidhaa, ambazo muajiriwa huzizalisha kwa ujira ambao hulipwa. Pamoja na kuwa thAmani za bidhaa huhukumiwa na muajiri na sio muajiriwa, basi ikiwa itafanya ihukumiwe na muajiriwa basi hilo litafikisha muajiri kuhukumiwa na muajiriwa. Atashukisha na atapandisha ujira kile atakacho kwa hoja ya kushuka bei au kupanda kwake na hili halijuzu, kwa sababu ujira wa muajiriwa ni badili ya manufaa ya kazi yake. Nayo huwasawa na thAmani ya manufaa yake maadamu ujira umeshakadiriwa baina yao. Basi ujira wa muajiriwa haufungAmani na bei za bidhaa anazozizalisha wala haisemwi amelazimishwa muajiri kutoa ujira uliokadirwa katika hali ya kushuka bei za bidhaa ambazo amezalisha kufikisha kwa kupata

hasara, na hii hufikisha kwa kumtoa kazini mfanyi kazi, kwa sababu hilo hupatikanwa pale inapotokea kushuka kwa bidhaa katika soko zima. Hii hurudi kwa makadirio ya wajuzi juu ya manufaa ya mfanyi kazi na sio muajiri, kwa sababu wao hutizama mkusanyiko wa manufaa ya muajiriwa kwa sura ya kijumla, wala si juu ya hali moja, kwa hivyo makadirio ya ujira haufungamani na bei ya bidhaa bali hufungamana na makadirio ya wajuzi.

Juu ya hayo hakika ya kujengea uajiri juu ya biashara, na biashara juu ya uajiri hufikisha kwa kuhukumu bei za bidhaa zinazohitajiwa kwa ujira wa muajiri. Pamoja na kuwa bei za bidhaa zinazohitajiwa huhukumiwa na kutosheka kwa muajiriwa wala si ujira wake. Basi itakapo fanywa kuwa bei za bidhaa zinazohitajiwa ni zenye kuhukumiwa na ujira wa muajiriwa hufikisha kwa kutosheka kwa muajiriwa na muajiri ni yeye kudhaminiwa kwake, pamoja na kuwa kutosheka kwa kila mwanaadamu huwa ni katika sehemu ya kuangaliwa mambo yake, nayo ni juu ya serikali na wala sio juu ya muajiri. Wala haijuzu kufungAmanisha kata kata kutosheka kwa muajiriwa kwa ajili ya uzalishaji wake, wakati huo huwa muajiriwa ni kiwiliwili kidhaifu hawezi ila kuzalisha kidogo ambacho ni chini ya mahitaji yake, basi itakapo fungAmanishwa ujira wake na uzalishaji wake au kwa mahitaji yake ambayo yuwahitaji hunyimwa kuishi maisha mazuri, na hili halijuzu, haki ya kuishi ni wajibu kuwepo kwa kila mwanaadamu katika raia wa serikali, sawa sawa akiwa ni mweza juu ya uzalishaji au la. Basi ujira wake hukadiriwa kwa thamani ya manufaa yake, sawa sawa zikimtosheleza mahitaji yake au la. Juu ya hayo huwa ni makosa kukadiria ujira wa mfanyi kazi kwa bei ya bidhaa anazozizalisha au kwa bei ya mahitaji anayoyahitajia. Basi huwa ni makosa kujenga ujira juu ya biashara na biashara juu ya ujira, wala si kujengea ujira juu ya bei na bei juu ya ujira. Basi haijuzu kujengewa moja juu ya nyengine, kwa hivyo haijuzu kujengewa bei juu ya ujira wala kujengea ujira juu ya bei. Basi kukadiria ujira ni kitu na kukadiriwa bei ni kitu chengine, na kila mojawapo zina sababu zake maalumu, na huchukuliwa khasa katika kukadiriwa. Basi ujira hukadiriwa kwa kukadiriwa

manufaa ambayo hupatikana kwa juhudi, basi makadirio huwa kila kitu kwa manufaa na sio kwa juhudi, hata kama manufaa hupatikana kwa juhudi ambazo mtu anazozitia. Manufaa hayo hukadiriwa na wajuzi kwa mujibu ya kunufaika na manufaa hayo. Na makadirio yake sio ya milele, bali zinufaike kwa muda ambao wamewafikiana juu yake, au kwa kazi ambao wamewafikiana kuifanya. Basi utakapo kwisha muda au kutimiza kazi huanza kukadiria upya ujira, imma kutoka kwa waliostaifu na imma kutoka kwa wajuzi wa kubainisha ujira wa mithali. Huenda muda ukawa wa kila siku na huenda ukawa kwa mwezi, na huenda ukawa kwa mwaka. Amma bei nayo ni kiwango kinacho nasibishwa kubadilishwa kwake na kiasi cha fedha na kiasi cha bidhaa moja maalumu katika zama maalumu. Amma kukadiria kwake hakika huwa kwa kukiriwa kwa kawaida na soko kwa bidhaa zikichukuliwa kama mahitaji yanayo hitajiwa na watu. Ndio huenda ikakadiria bei kwa kiwango cha haja ya mnunuaji wa bidhaa, basi ataichukua vyovyyote itakavyo kuwa bei yake, na huenda ikawa kwa kukadiria haja ya muuzaji basi aiuze kwa bei yoyote, lakini hilo halijuzu, nalo ni jambo la hatari kwa mujtamai wala haruhusiwi kwa hilo, nayo huitwa (Ghubn) kwa hivyo linalochukuliwa katika hali hiyo ni kwa wauzaji na wanunuaji sokoni na sio wauzaji na wanunuaji waliostaifu. Kwa ibara nyengine ni makadirio ya bidhaa yanayo kadiriwa na soko. Basi kukubali mnunuaji kwa bei ya soko imekuwa ni lazima na hivyo hivyo muuzaji kwa bei ya soko imekuwa ni lazima, na yule ambaye aloweka bei hiyo na kumlazimisha muuzaji na mnunuaji kuinyenyekea na haja kwa manufaa ya bidhaa katika mujtamai ambayo utauziwa bila ya kuangalia matumizi ya uzalishaji wake, kwa hayo hutofautika makadirio ya bei na makadirio ya ujira wala hakuna mafungamano baina yao. Kwa hivyo haijengwi makadirio ya ujira juu ya makadirio ya bei. Bei huwekwa na mahitaji kwa bidhaa. Na huwa uhaba ni sibabu inayoathiri makadirio yake wala haimkiniki kupimwa bei kwa matumizi ya uzalishaji. Huenda isiwe bei sawa na matumizi ya uzalishaji, huenda ikawa kidogo na huenda ikawa kingi kwa mujibu wa hali kwa muda mfupi na imma kwa muda mrefu, hupatikana kwa kawaida usawa baina ya bei ya soko na

matumizi ya uzalishaji, lakini hilo halifanyi uajiri kuwa ni lenye kufungika kwa bei ya bidhaa. Hakika ya wanunuzi kwa muda mfupi na muda mrefu hawaangalii kununua bidhaa kwa gharama zake bali hukiri bei yake katika hali mbili, haja ya bidhaa pamoja na kuchunga sababu ya uhaba.

Hakika wamekhitalifiana warasilimali na wakomunisti katika kukadiria ujira wa muajiriwa ikhtilafu iliyowafanya kugongana. Basi warasilimali huitia sababu ya uajiri kuwa ni kawaida na ujira wa kawaida kwao wao ni yale yanayo hitajia sibabu kati ya sababu za maisha katika kiwango chake cha chini. Huzidi uajiri inapozidi gharama za maisha katika kiwango chake cha chini, na hupunguza inapopungua, kwa hayo uajiri ni sababu inayo kadiriwa kwa mujibu wa gharama za maisha bila ya kuangalia manufaa ambayo yameletwa na juhudzi za mtu na mujtamai. Amma kile ambacho wanakichukua wafanyi kazi Uropa na Amerika katika za ki-urasilimali hakika ya marekebisho ya nidhamu ya kirasilimali katika kumpa mfanyi kazi haki zilizozidi ya hayo yake na kwa kumpa uhuru wa kumiliki pamoja na hilo hakika marekebisho hayo yamebakia yale anayoyachukua mfanyi kazi ni kiwango cha chini cha maisha ambayo yuwaweza kuishi katika kiwango cha kutosheka sio kiwango ambacho kinachozaliwa na viwanda. Pamoja na kuwa kunyanyuka kiwango cha maisha katika mujtamai katika Uropa na Amerika hufanya kiwango cha chini anacho kichukua humwezesha kuridhika kwa dhihirisho zuri lakini yeye hachukui kiwango anachokizalisha. Basi kukadiria ujira wa mfanyi kazi katika Uropa na Amerika hata kama haimfanyi mfanyi kazi kuwa faqiri kulinganisha na sisi, na humfanya ni mwenye kushibisha mahitaji yake ya kimsingi na baadhi ya haja zake za kiziada, lakini ikipimwa kiwango cha maisha ya jamaa ambayo yuwaishi baina yake huwa kiwango chake ni cha chini ikilinganishwa na chake, hata kama kiwango chake ni cha juu kulinganisha na sisi. Kwa hali ye yeyote hakika pamoja na kunyanyuka kiwango cha wafanyi kazi katika Uropa na Amerika hakika kukadiria ujira huko ni katika kila biladi ya kirasilimali hubakia kuwa ni kiwango cha chini ya maisha kulingana na mujtamai wake.

Kwa hali yejote ile maadamu makadirio huwa kwa yale ambayo mfanyi kazi yuwazihitaji miongoni mwa mbinu za kimaisha kwa kiwango cha chini, hakika yatokea kutokamana na hayo ni kubakia mfanyi kazi na milki kidogo yanayo koma kwa yale wanayoyahitaji kutosheleza mahitaji yake katika kiwango chake cha chini kulingana na jamaa anayoishi baina yao. Sawa sawa ikiwa maisha yao ni kutosheleza tu mahitaji yao ya kimsingi kama ilivyo hali ya wafanyi kazi katika biladi zilizobakia nyuma kifikra, kama biladi za kiislamu. Amma kutosheleza mahitaji ya kimsingi na kiziada kama ilivyokuwa hali ya wafanyi kazi katika biladi zilizotangulia kifikra kama Uropa na Amerika, hakika wafanyi kazi wake wote umilikaji wao umefungika kwa kiwango cha chini cha maisha kulinganishwa na mujtamai wanaoishi ndani yake, jinsi itakavyo tofautika kiwango cha maisha kwa kunyanyuka na kushuka, na maadamu makadirio yale anayoyahitajia mfanyi kazi miongoni mwa sababu za kimaisha katika kiwango cha chini.

Amma wakomunisti hakika wao waona kuwa kazi ambayo anayoifanya mfanyi kazi humpa ubora wa mwanzo katika kuzalisha bidhaa na kutimiza kuundwa kwake. Na kuwa kazi au uweza wa kazi unacheza mchezo wa kimsingi katika uzalishaji. Basi huwa ujira wa mfanyi kazi ni kile anachokizalisha na kuwa mapato yote ya uzalishaji hurudi juu ya sababu moja nayo ni kazi.

Sababu hii hukhitalifiana na wakia. Waka unaohsiwa ni kuwa mali ambao Allah ameumba katika ulimwengu ndio msingi wa thAmani ya bidhaa, na matumizi ambayo hutolewa katika kuzidisha manufaa ya mali hayo, au kuleta manufaa ndani yake pamoja na kazi, ndio ambayo huifanya katika umbo ambalo limekuwa juu yake, hufikisha kwa manufaa maalumu. Basi kufanya kazi ndio msingi ni kosa linalokhitalifiana na wakia, nakufanya bidhaa iliyozalishwa kuwa ni ujira wa mfanyi kazi ni kupuuza mali ghafi na matumizi ambayo yametiwa, na huenda ikawa kutiwa kwake ni sababu nyengine ya kuchukuwa ujira wake. Basi mfanyi kazi aliyoko hazalishi bidhaa wala kata kata

uzalishaji haurudi kwa kazi yake mpaka apewe bidhaa kwa ujira wake. Hata kama tutalazimisha kuwa lengo ni aina ya kazi, hakika hubakia mali ghafi nayo imeumbwa na Allah, basi haisihi kupuuzwa wala kuhisabiwa hisabu. Pamoja na kuwa kumchukua mfanyi kazi kama aina inayo kadiriwa ndani yake ujira ni kosa, kwa sababu wafanyi kazi n watu maalumu na ujira huwa ni kwa watu hawa. Basi kuchukuwa jinsi ya mfanyi kazi haifikishi kwa makadirio ya ujira bali hufikisha kwa kuondolewa ujira na kuondoaa umilikaji na hili hugongana na maumbile ya mwanaadamu na ni fikra ya kimakosa, wala haina wakia inayohisiwa. Wakia inayohisiwa hujulisha kuwa mwanaadamu huenda mbio kibinagsi ili kushibisha mahitaji yake. Basi msukumo huo humfanya yeeye aende mbio ili ayakusanye kutoka ulimwengu, au kwa kuongeza juhudii kutoka kwake kwa yale yaliyopo katika ulimwengu ili iwe mali inayofaa kushibisha mahitaji yake. Kwa hivyo mtazamo wa kukadiria ujira kwa wakomunisti kuwa ni bidhaa anayoizalisha ni la kimakosa. Hivyo hivyo kufunga ujira kwa yale aliyyoyazalisha hupungua juu ya mali ghafi pia ni kosa, kwa sababu vifaa ambavyo amevitumia na matumizi aliyyoyatoaimeathiri katika kuundwa bidhaa, nayo si sehemu ya kazi ya mfanyi kazi. Ikichukuliwa kama sehemu ya kazi ya mfanyi kazi kwa kuchukuliwa jinsi ya kazi, hufikisha hilo kwa kuondoliwa ujira wa mfanyi kazi hafungi kwa bidhaa wala thamani, wala juhudii hiz za mtu na jamaa. Sawa sawa ikiwa manufaa hayo hupatikana katika mali ghafi kama kiyoga na Tufaha, ama hupatikana kwa kazi ya mfanyi kazi kama gari la moshi. Hakika ya kukadiria juhudii huwa katika manufaa haya, na sio katika bidhaa ambazo amezizalisha. Kwa hivyo imekuwa kudokeza ujira wa mfanyi kazi kwa kiwango maalumu vyovvyote itakavyo kuwa kipimo chake, kosa linalokhitalifiana na waqiah unaohisiwa na htosha kuwa ujira ni maalumu wala haukufungwa kwa kiwango maalumu. Kwa hayo hakika ya mtazamo wa makadirio ya ujira kwa warasilimali na wakomunisti na wanaujamaa ni kosa linalokhitalifiana na waqiah na husababisha kuharibika kwa mafungamano ambayo yapasa kusimama baina ya watu ili kushibisha mahitaji yao.

Hurudi ikhtilafu hii katika kukadiria ujira wa mfanyi kazi kwa ikhtilafu katika maana ya thamani ya bidhaa yaani katika kudokeza thamani ya bidhaa. Wametambua baadhi ya warasilimali kuwa thamani ni yale yanayoilazimisha bidhaa katika wakati, juhudhi na mada za mwanzo mwanzo, kama gari la moshi thAmani yake ni zaidi kuliko thAmani ya balskeli. thamani hii ni kwa mujibu ya uhaba wake kwao. Wakasema wengine kuwa thAmani ya kitu hukoma juu ya manufaa yake yaani nguvu yake juu ya kushibisha mahitaji. Wakasema wengine ni kuwa thamani ya bidhaa ye yote hukoma juu ya kiwango cha kazi kinachohitajika katika uzalishaji wake, na huengenza juu yake kiwango cha kazi ambacho hutia uzalishaji wa mashine na vifaa ambazo hutumiwa katika kazi ya uzalishaji. Isipokuwa mtazamo huu wa kisasa ambao huitia nadhariya ya kikomo inayoitizama thamani kwa upande wa mzalishaji na mlaji kwa pamoja yaani katika upande wa kuweka na kutaka. Nayo hukoma juu ya kila kuweka na kutaka. Basi manufaa ya kikomo ambayo huhukumu kutaka yaani ni kikomo cha nguvu cha kitu katika kushibisha mahitaji kwa jinsi ambayo hupungua baada yake uweza wa kushibisha au huwa ni dhara. Gharama za kikomo cha uzalishaji ndio ambao huhukumu katika kuweka, yaani ndio kikomo cha kiwango cha kazi inayotiwa katika kuzalisha bidhaa kwa jinsi ambayo huwa kutiwa kwango chenyewe cha uzalishaji huwa ni hasara na kuwa thamani hubadilika kwao katika nukta ambayo huhakikishwa usawa baina ya hali hizi mbili.

Amma thAmani kwa wakomunisti hakika Karl Max ametaja kuwa chanzo cha pekee cha thamani ni kazi iliyotiwa katika uzalishaji wake. Na kuwa mwekaji rasilimali hnunua nguvu za mfanyi kazi kwa ujira usiozifi yale ya dharura ya kumbakisha hai mweza kazi, kisha huzitumia nguvu hizo katika kuzalisha bidhaa zinazopita thAmani ya yale anayotoa kwa mfanyi kazi. Karl Max ameita tofauti baina ya anayoyazalisha mfanyi kazi na yale anayopewa kihakika kwa jina thamani ya ziada na akakariri kuwa humathilisha yale yanayo nyakuliwa na mwenye kumiliki na mwenye kazi katika haki za wafanyi kazi, kwa jina la

mapato na faida, na faida ya rasilimali ambayo hatambui usharia wake.

Uhakika ni kuwa ni fikra iliyo na waqiah katika hisia, nayo ni kuwa thAmani yaani bidhaa ndio makadirio ya manufaa yaliyomo pamoja na kutambua sababu uhaba. Pamoja na kuwa manufaa hayo huwa ni kazi ni njia ya kuifikia. Huenda ikawa ni njia ya uzalishaji wake, lakini hilo katu halitambulikani wakati wa kubadilishana, wala akati wa kunufaika nayo. Kwa hivyo umekuwa mtazamo kwa manufaa pamoja na kutambua sababu za uhaba, sawa ameimiliki mwanaadamu mwanzoni mwake kama kwa mfano uwinjaji au kubadilisha kama biashara, wala hakuna tofauti katika hilo baina ya mujtamai katika Moscow na mujtamai katika Paris na mujtamai katika Al-Mdinatul-Munawwarah. Hakika ya mwanaadamu katika kila mahali pindi anapokwnda mbio ili apate bidhaa hukadiriwa ya kikomo ndani yake katika manufaa pamoja na kutambuliwa uhaba. Hii ndio thamani yake kwa upande ilivyo kwa mwanaadamu. Na ndiyo thamani ya kihakika ya bidhaa. Amma thamani ya kivitendo ya bidhaa hakika hukadiriwa kwa makadirio ya kitu chengine badala yake katika bidhaa au fedha. Hubakia thAmani yake hii juu ya sura thabiti vyovyote itakavyo badilika zama, mahala na dhurufu. Amma bei ya bidhaa nayo ni anachopewa katika fedha badili ya bidhaa moja maalumu katika zama maalumu, mahala maalumu na dhurufu maalumu. Hubadilika kwa kubadilika zama, mahala na dhurufu kwa ibira nyengine ni kiwango cha kubadilisha baina kiwango cha pesa kwa kiwango cha bidhaa badala yake.

Lau kama mwanaadamu atamuoa mwanamke na akafanya mahari yake ni kabati maalumu iliyo sifiwa akataja bei yake ni dinari hamsini na kivitendo akasalimisha kabati, huwa thamani ya kabati kwa kusalimisha kabati lenyewe. Lau kama atalichukuwa kutoka kwake baada ya hilo na akamundai (mwanamke) hakika ni juu yake kulisalimisha kabati lenyewe na sio thamani yake. Ikithubutu kuharibika kwa kabati au kudaiwa kuharibika kwake ni lazima atoe dinari khamsini kwa sababu hiyo ni thamani ya kabati, sawa sawa ikiwa ni mithali ya kabati

kwa wanaodai ni sawa na zaidi ya Dinari hamsini au kidogo, kwa sababu kivitendo ni thamani iliyokadiriwa, wala haichukuliwi thamani ya kabati mithali yake, kinyume na lao asingetaja katika aqdi kuwa thamani yake ni Dinari hamsini na kivitendo akasalimisha kabati, kisha akaichukua kutoka kwake (mke) na akamshtaki juu yake basi ni juu yake kusalimisha kabati na juu yake kununua kabati kwa Dinari hamsini, sawa sawa ikiwa kabati kwa mwenyekudai hulingana na hamsini au kidogo. Hakika la wajibu juu yake ni thamani ya kabati nayo ni Dinari hamsini katika kila wakati.

Hilo ni kwa sababu thamani haibadiliki na bei yabadilika. Basi thamani ya kivitendo kwa bidhaa ni makadirio ya kubadilishwa kwake wakati wa kukadiriwa. Bei ya bidhaa ni kinachotolewa badili yake sokoni. Tofauti hii baina ya thamani na bei huwa katika biashara na aina zote za kubadilishana. Amma ujira wa muajiriwa nao ni kiwango ambacho imekadiriwa manufaa ya juhudhi wakati na mkataba, na hukadiriwa mara nyengine wakati wa kukoma muda na uajiri. Kufikia hapa hudihiri kuwa hakuna mafungamano baina ya ujira wa muajiriwa na thamani ya bidhaa, wala baina ya ujira wa muajiriwa na gharama za uzalishaji, wala baina ya ujira wa wa muajiriwa na kiwango cha maisha bali kitu chengine tofauti, kwani hiyo ni makadirio yanayostahiki manufaa ambayo hupata kutoka kwake muajiri. Huwa kukadiriwa manufaa hayo haurudi kwa muajiri bali hurudi kwa haja ya manufaa hayo. Basi makadirio ya pekee ya ujira wa muajiriwa huwa ni manufaa yaliyosifiwa kwa sifa hizi. Ujira huo hukhitalifiana na kazi na hutafautiana kwa kutofautika uzoefu wa kazi moja. Basi ujira wa muhandisi hutofautika na ujira wa seremala na ujira wa seremala hodari hutofautika na ujira wa seremala wa kawaida. Kinacho nyanyua ujira wa watu katika kazi moja ni kwa mujibu wa uzoefu wa manufaa ya juhudhi wala hii haichukuliwi kuwa ni mapendeleo bali ni ujira wao ambao wanaostahiki kwa mujibu wa ubora wa manufaa yao.

6 SABABU YA PILI YA KUMILIKI

URATHI

Miongoni mwa sababu za kumiliki mali ni urathi, nayo imethubutu kwa nasi ya Qur'aani isiyo na shaka, nayo ni ahkaam maalumu za kukoma wala hazina sibahi, nayo hata kama imekwisha kuja nasi kivipande isipokuwa vipande hivyo ni misingi mipana. Basi Allah Ta'ala pindi aliposema:-

{ يُوصِّيْكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِذِكْرِ مِثْنَ حَظَ الْأَنْثَيْنِ فَإِنْ كُنَّ نِسَاءً فُوقَ اثْتَتِينِ فَلَهُنَّ ثُلَثًا مَا تَرَكَ }

“Allah amekuusieni juu ya watoto wenu: fungu la mwanamume ni kama mafungu mawili ya mwanamke, na ikiwa wanawake ni zaidi ya wawili basi watapata thuluthi mbili za alichokiata maiti” (An-Nisaa 11).

Twafahamu katika kauli yake hii hukmu tofauti tofauti. Twafahamu kuwa watoto wa kiume huchukua mara mbili ya watoto wa kike, na twafahamu kuwa mtoto wa mtoto huamiliwa muamala wa mtoto ikiwa hakuna watoto, kwa sababu watoto wa mtoto wa kiume huingia chini ya tamko la watoto, kinyume na mtoto wa binti haamiliwi muamala mtoto wa mtoto katika hali ya kukosekana watoto kwa sababu watoto wa binti ki-lugha hawaingii chini ya tamko la watoto. Twafahamu pia kuwa watoto wakiwa ni wanawake zaidi ya wawili hakika wao (hugawanyana) washirika katika thuluthi ya kilichowachwa. **Hakika Mtume Rehma na Amani zimfikie amewajaalia mabinti wawili hukmu ya waliozidi, na masahaba wamewafikiana juu ya hilo** kuwa huwa hukmu wa mabinti wawilikwa kilichozidi. Hukmu hizi zimefahamika kutoka maana jumla iliyotajwa na Ayah. Kwa hukmu hizi hustahiki warithi sehemu ya kilichowachwa. Juu ya hilo imekuwa urathi ni miongoni mwa sababu za kumiliki kwa mujibu wa hukmu fafanuzi katika Kitab, Sunnah na Ijmaa-us-Sahabah.

Urathi ni mbinu ya kugawanya urathi na kugawanya urathi hauna sababu bali ni bayana ya Waqiah. Hilo ni kuwa utajiri ushafanywa mubah umilikaji wake, huenda ukakusanyika katika mikono ya watu kwa hali ya kuikusanya ili isiendelee kukusanyika huko baada ya kufa kwao imekuwa hapana budi kwa mbinu ya kuigawanya baina ya watu. Na imeshuhudiwa

kiwaqiah kuwa mbinu ya kugawanya urathi huu kikawaida nayo ni mirathi katika uchunguzi hubainisha kwa hali ambazo hugawanywa urathi katika hali tatu nazo:-

A:-hali ya kwanza kuwa warithi wakichukuwa mali yao kwa mujibu wa hukmu za urathi, wakati huo husambazwa kwao wao mali yote.

B:-Hali ya pili ni kuwa hakuna warithi wakuchukuwa mali yote kwa mujibu wa hukmu za urathi kama anapokufa maiti aliye tu na mke na maiti aliye tu na mume. Hakika ya mke atachukuwa to robo na huwa baki ya mirathi kwa Baitul-Maal na ikiwa mume atachukuwa tu nusu na huwa iliyobakia ni ya Baitul-Maal.

C:-Wakati hakuna mrithi wowote. Katika hali hii huwa mali yote ni ya Baitul-Maal yaani Serikali.

Kwa hayo hugawanyika utajiri hugura mali kwa warithi na huanza tena kubadilishwa mali katika mzunguko wa ki-uchumi baina ya watu wala hatozuia mtu maalumu mkusanyiko wa utajiri.

Urathi ni sababu ya kisheria ya kumiliki, basi mwenye kurithi kitu humiliki umilikaji wa kisheria. Basi huwa urathi ni sababu mionganoni mwa sababu za kumiliki ambazo zimeruhusiwa na sheria za kiislamu.

7 SABABU YA TATU MIONGONI MWA SABABU ZA KUMILIKI HAJA YA MALI KWA AJILI YA UHAI

Miongoni mwa sababu za kumiliki mali ni haja ya mali kwa ajili ya uhai, hilo ni kwa sababu maisha ni haki ya kila mwanaadamu. Basi ni wajibu na apate maisha haya kama haki wala sio zawadi wala si huruma. Sababu ambayo humdhamini mtu kati ya Raia wa serikali ya kiislamu kupata chakula chake nayo ni kazi. Basi ikiwa hakupata kazi huwa ni juu ya serikali kumtafutilia yaya (kazi) kwa sababu yeye (Serikali) ni mchungaji wa raia hawa, na ni mas'oul wa kuwapa mahitaji yao.

Asema Rehma na Amani zimfikie:- “**Imamu ambaye ni juu ya watu ni mchungaji na ni mas’oul juu ya Raia wake.**” Imepokewa na Bukhari kutoka kwa Ibnu Umar. Basi ikiwa hakupata kazi au kushindwa kufanya kazi kwa sababu ya maradhi, au uzee au sababu yejote katika sababu za kushindwa huwa maisha yake ni wajibu juu ya yule ambaye Sheria imemwajibisha kumsimamia. Basi ikiwa hayupo yule ambaye ni wajibu kwake kumsimamia, au amepatikana lakini hawezi kumsimamia, huwa usimamizi wake ni juu ya Bait-ul-maal yaani juu ya Serikaki. Zaidi ya hilo huwa na haki katika Baitul-Maal katika haki nyengine, nayo ni zakat. Asema Ta’ala:

{ وَالَّذِينَ فِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَعْلُومٌ - لِلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ }

“*Na ambao katika mali yao iko haki maalu – kwa mwenye kuomba na anaejizuilia kuomba*” (Al-maarij 24-25). Haki hii ya faradhi kwa matajiri kuitoa. Asema Ta’ala:-

{ إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ }

“*Wa kupewa sadaka (zakat) ni mafakira na masikini.....*”
(Tauba Ayah 60)

{ فَرِيضَةٌ مِّنْ اللَّهِ }

“*Huu ni wajibu uliofaradhishwa*”

Yaani haki iliofaridhiwa. Hata kama serikali itapunguza katika hilo na ikapunguza jamaa wa kiislamu katika kuihisabu, katika kuwasimamia wanaohitaji na haitegemewi kuwa jamaa ya waislamu itapunguza. Huwa kwa mtu huyo kuchukua anachokihitaji ki-maisha popote atakapokipata, sawa sawa ikiwa ni mlki ya kibinaksi au milki ya serikali. Katika hali hii si mubah kwa mwenye njaa kula mfuu (mzoga) madamu kuna chakula kwa watu, kwa sababu yejote hahesabiwi kuwa amelazimika kula mfuu, pamoja na kuwepo atakacho kula katika mkono wa mtu yejote. Amma ikiwa hawezi kupata cha kukila, hakika ni juu yake kula mfuu ili kuokoa maisha yake. Ilipokuwa maisha ni sababu mionganii mwa sababu za kupata mali, Sheria haichukulii kuchukuwa kwake chakula kwa mwaka wa ukame kuwa ni uwizi onaokatwa mkono juu yake kutoka kwa ummah. Kutoka kwa Mtume Rehma na Amani zimfikie kuwa asema:- “**Haukatwi (mkono) katika zama za njaa.**” Kama pia hudhamini sheria haki ya mtu katika kumiliki mali kwa ajili

ya uhai kwa kuweka sheria zinazotoa haki hii kwa kuongoza. Amepokea Imam Ahmad kuwa Mtume wa Allah Rehma na Amani zimfikie asema:- “**Watu wa kijiji chochote atakayepambaukia kati yao mtu aliye na njaa basi huwa mbali na dhimma ya Allah Ta’ala.**” Na amepokea Al-bazaar kutoka kwa Anas kuwa Mtume wa Allah Asema:- “**Hajaniamini yule ambaye amelala huku ameshiba na jirani yake ubavuni mwake ana njaa na yeye yuwajuwa.**”

8 SABABU YA NNE MIONGONI MWA SABABU ZA KUMILIKI

KUTOA SERIKALI MALI YAKE KWA RAIA

Miongoni mwa sababu za kumiliki ni kutoa serikali kutoka kwa mali ya Baitul-Maal kwa raia ili kukidhi haja zao, au kunufaika na milki yao. Amma kukidhi haja zao kama kuwapa mali ili kupanda (mimea) ardhi zao, au kulipa madeni yao. Hakika aliwapa Umar bin Al-Khattab wakulima wa iraq kutoka Baitul-Maal, mali aliowasaidia nao juu ya kupanda ardhi zao, kukidhi haja zao bila ya kuzirudisha kutoka kwa sheria imemjaalia mwenye madeni haki katika mali ya zaka, hupewa kutokamana nayo ili walipe madeni wao wakishindwa kuyalipa, Asema Ta’ala:-

{ وَالْغَارِمِينَ }

“..Na wenye madeni...” (At-Taubah: 60)

Amma haja ya jamaa ya kunufaika na milki ya kibinagsi, basi huwa katika kumilikisha serikali kwa wau katika ummah miongoni mwa milki zake na mali zisizoumia ziolio na manufaa. Kama kupeyana kwa serikali kipande cha ardhi ambayo hakuna wa kumiliki kama alivyofanya Mtume wa Allah pindi alipofika **Madinah akamganyia Abu Bakar na Umar kama alivyomganyia Az-Zubair ardhi kunjufu. Akamganiya Urathi wa Mbiu wa Farasi wake katika Ardhi mwitu wa An-Naqeer, na akamgawanyia ardhi iliyo na miti na mitende. Kama pia walivyo gawanya Al-Khulafaa Ar-Rashideen waliokuja baada yake kutoka ardhi ya waislamu.** Hii (ardhi) ambayo serikali humgawanyia mtu binagsi huwa ni milki yake. Kwa sababu jamaa wanahaja katika milki ili

kunufaika nayo, na kumrahisishia mtu huyo ili anufaike na kutumia nishati yake ya kiakili au kimwilikwa jamaa kwa sababu ya milki hiyo na utumiaji wa tamko la (iqtaa) hapa kuna matumizi ya kilugha na ki-fiqhi wala haina mafungamano kwa nidham ya (Feudalism) amabyo Uislamu hautambui.

Na yale ambayo serikali humpa mtu binafsi katika yale inayoyagawanya kwa wapiganaji katika ngawira (ghanima) na yale anayoidhinisha Imam kuchukuliwa katika ngawira (Salab).

9 SABABU YA TANO MIONGONI MWA SABABU ZA KUMILIKI

MALI AMBAYO MTU HUICHUKUWA BILA MALI AUJUHUDI

Miongoni mwa sababu za kumiliki ni baadhi ya watu kuchukuwa mali ya baadhi bila mali au juhud. Na hii hukusanya mambo matano:-

1:- Fungamano la baadhi ya watu kwa baadhi. Sawa sawa ikiwa ni fungamano katika maisha ya kama tunu na zawadi, ama baada ya kufa kwao kama wasiya. Amepokea An-Nasai na Ibn Is-Haq katika sera ya Mtume kutoka kwa Amru Bin Shuaib kutoka kwa babake kutoka kwa nyanyake kuwa ujumba la Hawazin lilipokuja kumuomba Mtume wa Allah awarudishie yale aliyochukuwa kama (Ghanima) ngawira kutoka kwao, Mtume wa Allah akasema:- “**kile ambacho ni changu na cha Banu Abdul-Muttalib basi hilo ni chenu.**” Yaani ni tunu kutoka kwangu kwenu. Amepokea Ibn Asakir kutoka kwa Abu Hurairah asema:- “Asema Rehma na Amani zimfikie “**peaneni, (zawadi) mtapendana.**” Akasema Rehma na Amani zimfikie “**Si katika sisi aliye na mfano mbaya, ambaye huirudia zawzdi yake kama mbwa anayerudisha matapishi yake.**” Imepokewa na Bukhari kutoka kwa Ibn Abbass. Wala hakuna tofauti katika tunu na zawadi baina ya kafiri na Muislamu. Basi kumpa kafiri ni mubah na kupokea alichokitoa ni kama kukubali alichokitoa Muislamu. Amepokea Muslim kutoka Asmaa Bint Abu Bakar, Asema:- amekuja kwangu mamangu ilhali yeye ni mushrikina walio ahidiwa (na Mtume katika Hudaibiya) basi

nikamuuliza Mtume wa Allah, nikasema:- **amenijilia mamangu ilhali yeye yuwanipenda, jee naweza kumpa mamangu zawadi?** Akasema:- “Ndio.” Amepokea Al-Bukhari kutoka Aby Humaid As-Saidiy. Asema **mfalme wa Ayla alimpa zawadi Mtume Rehma na Amani zimfikie, farasi mweupe na akamvisha mavazi.** Kama ilivyo tunu na zawadi ni kujitolea kwa hali na mali katika uhai, hivyo hivyo wasiya ni kujitolea kwa mali baada ya kufa. Asema Ta’ala:-

{كُتِبَ عَلَيْكُمْ إِذَا حَضَرَ أَحَدُكُمُ الْمَوْتُ إِنْ تَرَكَ خَيْرًا الْوَصِيَّةَ لِلَّوَادِينَ وَالْأَفْرَادِينَ}

“Mmefaradhishiwa juu yenu anapofikiwa mmoja wenu na mauti, kama akidai mali, afanye wasiya kwa wazazi na jamaa zake” (TMQ:2:180). Amepokea Al-Bukhari kutoka Saad Bin Aby Waqqas, asema:- **“Niliugua nikiwa Makkah maradhi ambayo nilichelea kifo, akaja Mtume Rehma na Amani zimfikie kunizuru nikasema:- ewe Mtume wa Allah, mimi nina mali nyingi na sina wa kunirithi ila binti yangu, jee nitoe sadaqa Thuluthi ya mali yangu? Akasema “La.” Nikasema:- Basi Nusu? Akasema “La.” Nikasema:- Thuluthi? Akasema “Thuluthi ni nyingi. Hakika yako kumwacha mtoto wako tajiri ni bora kuliko kuwaachia maskini wanaoomba watu.”**

Humiliki mtu kwa sababu ya zawadi au tunu au wasiya kitu kilichotolewa tunu au cha zawadi au kilichousiwa nacho.

2:- Kustahiki mali kama Ridhaa kwa ajili ya dhara mionganoni mwa madhara ambayo yamefika. Hilo ni kama fidya ya aliyouliwa na fidya ya jaraha. Asema Ta’ala:-

{ وَمَنْ قَتَلَ مُؤْمِنًا خَطًّا فَتَحْرِيرُ رَقْبَةِ مُؤْمِنَةٍ وَدِيَةٌ مُسْلَمَةٌ إِلَى أَهْلِهِ }

“Na mwenye kumuua muislamu kimakosa basi amkomboe mtumwa alie mumin na atoe fidiya kuwapa jamaa za maiti” (An-Nisaa: 92).

Amepokea An-Nisai kuwa Mtume wa Allah Rehma na Amani zimfikie aliwaandikia watu wa Yaman barua na akamtuma nayo Amru Bin Hazim, yaliyo kuja ndani yake:-

“Hakika fidya ya nafsi ni ngamia mia moja.” Amma fidya ya jaraha hakika amepokea An-Nisai kutoka Az-Zuhayri kutoka kwa

Abu Bakar Bin Muhammad Bin Amru Bin Hazim kutoka kwa babake kutoka kwa nyanyake kuwa Mtume wa Allah Rehma na Amani zimfikie alimuandikia barua:- “**Na kila pua iliyokatwa kuna fidya, na katika ulimi kuna fidya na katika midomo miwili kuna fidya na katika mayai mawili ya pumbu kuna fidya na katika dhakari kuna fidya na katika uti wa mgongo kuna fidya na katika macho mawili kuna fidya na katika mguu mmoja kuna nusu fidya na katika yaliyo ndani ya kichwa kuna thuluthi ya fidya na katika yaliyo ndani ya matumbo kuna thuluthi ya fidya na katika mifupa iliyofungwa ni ngamia kumi na tano.**”

Katika fidya ya aliyouliwa, hustahiki fidya hiyo warithi wake kutoka kwa muuwaji aliyeuwa kwa kusudi. Asema Rehma na Amani zimfikie:- “**Hafanyi mtu kosa ila juu ya nafsi yake.**” Imepokewa na Ibn Majah kwa njia ya Amru Bin Al-Ahwas. Amma bila ya kukusudia kama inayofanana na kusudi na makosa, basi hustahiki warithi wa aliyeuliwa fidya kutoka kwa muuwaji. Amepokea Bukhari kutoka kwa Abu Hurairah Asema, “**Walipigana wanawake wawili kutoka Hudhayl mmoja wao alimpura mwengine kwa jiwe akaamuua na kilichoko katika tumbo lake. Wakamshtakia hilo kwa Mtume Rehma na Amani zimfikie, akahukumu,** “**Fidya wa mtoto wake ni mtumwa wa kiume au wa kike na fdya ya mwanamke ni ya wakaribu wake.**” Na ‘Aql’ hapa ni mwenye kubeba ‘aql’ na ‘aql’ hapa ni fidya. Na wenye kutoa ‘aql’ ni jamaa wake na huingia ndani yake babake aliyeuwa na watoto wake, ndugu zake, ammi zake na watoto wao. Ikiwa aliyeuwa hana jamaa wa kutoa Aql basi fidya hutolewa na Baitul-Maal. **Kwa sababu Mtume Rehma na Amani zimfikie alitoa fidya ya muansari aliyeuwawa Khaybar kutoka Baitul-Maal.** Imepokelewa kuwa mtu aliuwawa katika zahma katika zama za Umar na asijulikane muuwaji wake, Ali akamwambia Umar: **Ewe Amirul-Mu’mineen haipotei damu ya Muislamu, basi diya yake ni kutoka kwa Baitul-Maal.**

Amma diya ya jaraha, nalo ni kupasuka kichwa au sura au kukatika kiungo au kukatika nyama au kupotea manufaa kama

kupotea kusikia, kuona na akili. Basi mtu akipata jeraha mionganoni mwa majeraha haya hustahiki diya juu ya jeraha hilo kwa mujibu wa hukmu fafanuzi ya kila kiungo katika ya kiungo, na kila hali katika hali zozote. Humiliki mtu mali kwa sababu ya diya inayomhusu kutoka diya ya aliyeuliwa au kwa diya ya kiungo ambacho amekikosa au manufaa yaliyopotezwa.

3:- Kustahiki mahari na yanayoyafuata katika aqdi ya nikah, hakika mwanamke humiliki mali hayo kwa sura iliyofafanuliwa katika hukmu za ndoa. Mali hayo sio badili ya manufaa. Hakika ya manufaa yanayo badilishwa baina ya mume na mke hustahiki kwa dalili ya kisheria. Asema Ta'ala:

وَآتُوا النِّسَاءَ صَدْقَاتِهِنَّ نِحْلَةً {

“*Na wapeni wanawake mahari yao*” (An-Nisaa: 4) yaani wapeni kwa kuridhika kama faradhi ambayo Allah Ta’ala ameifaradhisha. Na “**NIHLA**” ni kipewa yaani hupewa kwa sababu kila mmoja kati ya mume na mke hustarehe na mwenziwe. Amepokea Ahmad kutoka Anas asema amekuja **Abdulrahman Bin Auf** huku amevaa nguo ya **Za’farani Mtume (saw)** akasema una mahaba akasema (**Abdulrahman Bin Auf**): **Ewe Mtume wa Allah nimeoa mwanamke. Akasema (saw) nini mahari yake? Akasema: dhahabu uzani wa konde ya tende. Akasema (saw) “fanya walima angalau kwa kondoo mmoja.”**

4:- Kilichoookotwa: mtu akiokota kitu huangaliwa ikiwa yawezekana kuhifadhika na kutambuliwa kama dhahabu, fedha, vyombo vya thamani na nguo na ikiwa si mionganoni mwa haramu basi yajuzu kukiokota na kukimiliki, kwa yale aliyyapokea Abu Daud kutoka Abdalla Bin Amru Bin Al-Aas kuwa Mtume Rehma na Amani zimfikie aliulizwa juu ya kilichoookotwa Akasema: **ikiwa ni mionganoni mwa (yaliyookotwa) katika njia inayoptiwa au kijiji basi kitangaze mwaka na akija mwenyewe mpe na ikiwa hakuja basi ni chako. Na (yaliyookotwa) katika magofu basi hutolewa ndani yake na kaitika hazina khumusi.** Amma kilichoookotwa ni cha haramu basi hakihisabiwi katika ya kilichoookotwa, kwa sababu kilichoookotwa cha haramu ni

Haramu. Kama ilivyokuja katika hadithi iliyopokelewa kwa njia ya Abdulrahman Bin Uthman kuwa "**Mtume Rehma na Amani zimfikie amekataza mwenye kuhiji kuokota wala haijuzu kukichukua illa kwa kuhifadhia mwenyewe kwa msemo wa Mtume Rehma na Amani zimfikie wala haokoti kilichoanguka ila mwenye kukitafuta.**" Imepokewa na Bukhari.

Amma ikiwa katika vile visivyomkinika kuhifadhiwa kwa kuwa ni katika visivyobakia kama chakula, tikiti na yanayoshabihiana nayo basi yeye ni mwenye kukhiyarishwa baina ya kuvila na atamlipa mwenyewe gharama zake akipatikana na baina ya kuviuza na kuhifadhi thAmani yake kwe muda wa mwaka. Haya yote ikiwa cha kuokotwa kwa kawaida huombwa. Ikiwa kina thamani basi mwenyewe hatakiwacha kikipotea. Amma ikiwa mionganoni mwa matunda kama tende, na tonge na yanayofanana nayo hakika hilo halitangazwi sifa yake na atakimiliki mara moja.

5:- Ridha anayopewa Khalifa na wanaochukuliwa kazi yao ni ya utawala. Hilo hawapewi kama badala ya kazi yao bali ni badala ya kufungika kwao na kufanya kazi zao. Hawa humiliki mali kwa mujarad wa kuichukuwa kwa sababu Allah amewahalalishia. **Hakika Abu Bakar mali kama ridha ya kufungika kwake kutoka biashara pindi alipoombwa kutoa wakati wake kwa ajili ya mambo ya waislamu, na masahaba wakakiri juu ya hayo.**

Basi mali hayo matano – fungamano, ridhaa kwa ajili ya dhara, mahari, kilichoookotwa, ridhaa kwa watawala – mali anayoyachukua mtu bila mali wala juhudhi. Kuchukua katika sura hizi ni mionganoni mwa sababu za kumiliki za kisheria ambao mtu humiliki mali aliyooyachukuwa.

10 JINSI YA KUTUMIA MALI HAKI YA KUTUMIA

Inajulikana umilikaji kuwa ni hukmu ya kisheria iliyokadiria kitu au manufaa inayomuezesha mwenye kukimiliki kunufaika

na kitu au kuchukuwa mali kwa ajili yake. Kwa haya huwa umilikaji ni hukmu ya kisheria juu ya kitu au manufaa yaani ni idhini ya kisheria. Basi huwa kuitumia ni ndani ya yale yaliyopangwa na hukmu hii ya kisheria , yaani kwa idhini itakayomuezesha mwenye kumiliki kunufaika na kitu na kuchukua malipo kwa ajili yake. Basi kutumia (Tasarufu) ni kunufaika na kitu ilipokuwa mali ni ya Allah na Allah amemfanya mja kuwa ni msimamizi juu yake kwa idhini yake. Imekuwa mtu kukusanya mali ni kama kazi yake. Yuwatekeleza hilo ili kunufaika na mali na kuikuza, kupitia kuimiliki kwake. Kwa sababu pindi anapomiliki mtu mali huwa ameimiliki ili anufaike nayo, na yeye huwa amefungika kwa mipaka ya kisheria , wala hakuwachwa huru katika kutumia kitu, ahta kama yeyendiye mwenye kumiliki kitu, kwa dalili yakuwa lau yaya ataitumia kwa kunufaika kwa mali hayo kwa njia isiyokuwa ya kisheria, kwa usafihi na ubadhirifu huwa ni juu ya serikali kumzuia na kumkataza kutumia huko, na kumpokonya uweza huo aliopewa. Kwa hayo huwa kutumia kitu na kunufaika nayo ndiyo maana iliyokusudia katika kumiliki, au ndio athari ya kumiliki huko. Haki ya kutumia kitu kilichomilikiwa hujumuisha ya kutumia katika kukuza milki ni haki ya kutumia katika kusimamia kizazi na matumizi.

KUKUZA MILKI

Kukuza mali kumefungika kwa mbinu na vyombo, ambayo hutumiwa ili kuzalisha. Amma kukuza umilikaji wa mali hii hilo huambatana na jinsi ambayo mtu hupata kuzidisha milki hiyo. Kwa hivyo nidhamu ya kiuchumi haingii katika kukuza mali, bali huingia katika umilikaji. Wala uislamu haupingi kukuzwa kwa mali na ukamuachia mwanaadamu aikuze kwa mbinu na vifaa ambavyo anavyoviona kuwa zitafikisha kwa kukua kwake. Na itaingia umilikaji huu wa mali na ikabainisha hukmu zake. Kufikia hapa imekuwa kukua kwa milki umefungika kwa mipaka ambayo sheria imeziweka, wala haijuzu kuzivuka. Mtungaji sheria amekwisha bainisha misingi mipana ya jinsi ya kukuza nazo umilikaji na ikamuachia Mujtahid ufanuzi wake ili avue hukmu zake kutoka misingi haya mipana, kwa mujibu ya kufahamu hali halisi, kisha akadokeza juu ya jinsi maalumu

aliyoiharamisha na kuikataza. Basi akabainisha Muamat na mikataba ambayo hukua ndani yake milki kwa njia maalumu.

Sheria imekwisha bainisha hukmu za kilimo ilipobainisha hukmu za ardhi na yanayo fungamana nayo, ikabainisha hukmu za biashara ilipobainisha hukmu za kuuza shirika na yanayo fungamana nayo. Ikabainisha hukmu za viwanda ilipobainisha hukmu za kuajiri na kuunda. Amma yaliyozaliwa na viwanda yaani yaliozaa huingia katika biashara, kwa hivyo imekuwa kukuza umilikaji umefungika kwa hukmu ambayo sheria imekuja nazo, nazo ni hukmu za ardhi na yalioambatana nayo. Hukmu za kuuza na shirika na yanayoambatana nayo, hukmu za uajiri na uundaji.

11 HUKMU ZA ARDHI

Ardhi ina koo na manufaa. Koo yake ni asli yake, na manufaa yake ni kuitumia kwake katika kilimo na mengineo. Uislamu umefanya Mubah kumiliki koo ya ardhi kama ilivyofanya Mubah kumiliki manufaa yake. Na ikaweka hukmu kwa kila moja wake. Amma kumiliki koo ya ardhi hiyo huangaliwa, ikiwa biladi ambayo ardhi hiyo imefunguliwa kivita itakuwa koo ya ardhi ni milki ya serikali na huchukuliwa kuwa ni ardhi ya Kharaj, isipokuwa bara arabu.

Ikiwa imefunguliwa kwa sulhu huangaliwa ikiwa sulhu hiyo huifanya ardhi hii ni yetu, na wenyeji wazikalie kwa mkabala wa kutoa Kharaj. Hakika Kharaj juu ya ardhi hubakia milele. Na hubakia ardhi yake kuwa ni ardhi ya Kharaj mpaka siku ya Qiyamah hata kama (ardhi hiyo) itagura kwa waislamu kwa kusilmi au kununua au kwa sababu nyengineo.

Imma ikiwa sulhu ni kuwa ardhi ni yao na itabakia kwa mikono yao, na watakubaliwa kubakia humo kwa kharaji maalumu wanaolipishwa basi kharaji hino itachukuliwa kuwa kama jizya inaoanguka kwa kusilmi kwao au kuuza kwao aradhi kwa Muislamu. Amma wakiuza ardhi kwa mkafiri basi kharaji itabakia wala haianguki kwa sababu mkafiri ni mwenye kulipa kharaji na jizya. Ikiwa watu wa biladi walislimu humo mfano

wa Indonesia, au ipo katika Bara la Arabu, shingo la ardhi ni milki ya watu wake na huchukuliwa kuwa ardhi ya ushri. Sababu ya hayo ni daraja ya mali na huchukuliwa kama ngawira inaokusanywa katika vita; basi huwa ni halali na ni milki ya Bait al-Mal. Hafs bin Ghiyath amesimulia kumpitia Abu Dhi'b kutoka Zuhri aliesema: **“Mtume wa Allah (saw) alikubali jizya kutoka Majusi wa Bahrain. Zuhri akasema: Aliyesilimu mionganoni mwao, Uislamu wake ulikubaliwa. Na Uislamu wake ulimhifadhia nafsi na mali yake ila ardhi iliokuwa ni fai (ngawira) kwa Waislamu kwa sababu hakusilimu kutoka mwanzo alipokuwa na nguvu.”** Tofauti baina ya ardhi na mali nyenginezo katika ngawira ni kuwa mali hugawanywa, hufanyiwa tasarruf na hugawanya kwa watu ilhali shingo la ardhi hubakia chini ya tasarruf ya Bait al-Mal kihukmu hata kama itabakia chini ya mikono ya wenyewe wakinufaika nayo. Kwa kubakia ardhi kwa Bait al-Mal pasina shingo yake kugawanywa ila tu watu wake humakinishwa kunufaika nayo, huwa ni dhahiri kuwa ni ngawira amma ya Waislamu wote sawa sawa waliokuwepo wakati wa ukombozi au waliokuja baadaye. Amma Bara la Arabu, ardhi yake nzima ni ya ushri kwa sababu Mtume (saw) alikomboa Makka kinguvu na akaiwacha kwa wenyeji wake bila kulazimisha kharaji juu yake. Na pia kwa sababu kharaji juu ya ardhi ni kama jizya juu ya watu basi haithubutu juu ya ardhi ya (Bara la) Arabu kama jizya haithubutu juu ya vicha vyao. Hii ni kwa sababu mionganoni mwa sharti ya kuweka kharaji juu ya biladi ni kuwacha watu wake na wanaoamini na kuabudu kama katika biladi ya Iraq. Ilhali haikubaliwi kutoka washirikina wa kiarabu ila Uislamu au panga (kuuwawa). Allah ta'ala asema:

{ فَإِذَا انسَخَ الْأَشْهُرُ الْحُرُمُ فَاقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدُّتُمُوهُمْ وَخُذُّوْهُمْ وَاحْصُرُوهُمْ
وَاقْعُدُوا لَهُمْ كُلَّ مَرْصَدٍ فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوْا الزَّكَةَ فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ }

“Na ile miezi mitukufu itakapokwisha, basi wauweni washirikina popote munapowapata, wakamateni mateka, wazungukeni na wakalieni katika kila njia. Lakini wakitubu na kusimamisha swala na kulipa zakaa basi waacheni” [TMQ 9:5].

Na asema:

{ سَتُدْعَونَ إِلَى قَوْمٍ أُولَيْ بَأْسٍ شَدِيدٍ ثُقَاتُهُمْ أَوْ يُسْلِمُونَ }

“*Karibuni hivi mutaitwa (kupigana) na watu wenyе mapigano makali; mutapigana nao au watasilimu*” [TMQ 48:16]. Madamu jizya haichukuliwi kutoka kwao, basi kadhalika kharaji haichukuliwi kutoka ardhi zao.

Kwa hayo huwa shingo la ardhi katika biladi zote Uislamu ulizikomboa kwa nguvu, au kwa sulhu kwa sharti ardhi ni yetu, huwa ni milki ya serikali na ardhi yake huchukuliwa kuwa ni ya kharaji sawa sawa baado iko mikononi mwa Umma wa Kiislamu kama Misri, Iraq na Turkia au imegura kushikwa na mikono ya makafiri mfano wa Uhispانيا, Ukraine, Al-Qaram (Crimea), Albania, Bilad al-Hind na Yugoslavia. Na kila ardhi waliposilimu watu wake kama Indonesia pamoja, na kila ardhi katika Bara la Arabu, ni milki ya wenyeji wake na huchukuliwa kuwa ni ardhi ya ushri.

Amma manufaa ya ardhi, hayo ni milki ya kibinagsi sawa sawa iwe ni ardhi ya kharaji au ushri na sawa sawa serikali imewapa ardhi hiyo, wamebadilisha baina yao, kuhuisha au kuiwekea mipaka/kuizuia (*tahjeer*). Mwenye kutasarruf na ardhi hupewa haki kupitia manufaa haya kama mwenye kumiliki (shingo ya) ardhi yenye; basi aweza kuuza manufaa haya, kuyatoa kama zawadi na hurithiwa kutoka kwake. Hii ni kwa sababu serikali yaweza kukata (yaani kutoa) ardhi kwa watu binagsi sawa sawa iwe ni ardhi ya ushri au kharaji, lakini kutoka ardhi ya kharaji ni kumilikisha manufaa ya ardhi ilhali shingo lake hubakia kwa Bait al-Mal. Amma katika ardhi ya ushri, hiyo ni kumilikisha shingo pamoja na manufaa ya ardhi.

Tofauti baina ushri na kharaji ni kuwa ushri ni juu ya mazao (*naatij*) ya ardhi yaani serikali huchukuwa kutoka wakulima wa ardhi kiasi cha ushri (10%) juu ya mazao yake ya kihakika ikiwa ardhi hunyunyizwa kimaumbile na maji ya mvua. Na huchukua nusu ushri (5%) ikiwa ardhi hunyunyizwa kisanii kupitia (*saaqiya*) au mbinu nyengine. Muslim amesimulia kutoka Jabir akisema: Mtume (saw) amesema: “**Ushri ni juu ya (ardhi) inaonyunyizwa na mito na mawingu (ghaim), na nusu ushri ni juu ya inaonyunyizwa na (saaniya).**” Ushri hino

huchukuliwa kama zakaa na inawekwa katika Bait al-Mal wala haitumiwa ila kwa mojawapo wa makundi manani yaliotajwa katika aya:

{إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ}

“*Hakika sadaqa (zakaa) ni kwa mafaqiri na masikini...*” [TMQ 9:60]. Al-Hakim, Bayhaqi na Tabarani wamesimulia kutoka hadithi ya Abu Musa na Muadh kwamba Mtume (saw) alisema pindi alipowatuma Yemen kuwafundisha watu dini yao: “**Musichukue sadaqa ila kutoka hizi (vitu) vinne: Shayiri, ngano, zabibu na tende.**”

Amma kharaji juu ya ardhi, serikali huchukua kutoka mwenye ardhi kiwango maalumu ambayo serikali imepima kwa mujibu ya mazao ya kawaida ya ardhi iliokadiriwa, wala sio mazao ya kihakika. Hupimwa juu ya ardhi kwa kiwango cha kutarajiwa ili asidhulimiwe mwenye ardhi wala Bait al-Mal. Kharaji huchukuliwa kutoka mwenye ardhi kila mwaka sawa sawa ilipandwa/ililimwa (*zuri’at*) au la, na sawa sawa ilizaa au haikuzaa (*ajdhab*). Abu Yusuf amesimulia katika ‘*Al-Kharaj*’ kutoma Amru bin Maimun na Haritha bin Mudhrib: ‘**Umar bin Al-Khattab alimtuma Uthman bin Hanif kwenda As-Siwad (ardhi ya Iraq/Iran) na alimwamrisha aipime masafa (masaha). Na akaweka dirham na (qafeez) juu ya kila jareeb, ilioamiriwa au (ghamir) ikiwa mithali yake huamiriwa.**’ Na Al-Hajjab bin Arta’ a amesimulia kutoka ibn Awf ‘**kwamba Umar bin Al-Khatib alipima As-Siwad, chini ya (ma duna) mlima wa Hilwan, na akaweka dirham na qafeez moja juu ya kila jareeb ilioamiriwa au kuwa na mafuriko (ghamir) yenye kupata maji kupitia ndoo au kwa mbinu nyengine, sawa sawa imepandwa au imeachwa**’ (Abu Yusuf ameisimulia katika ‘*Al-Kharaj*’). Kharaji huwekwa katika Bait al-Mal tofauti na mlango wa zakaa, na hutumiwa katika njia zote serikali huona ni sawa kama mali nyengine inavyotumiwa.

Ardhi iliombolewa kinguvu na kulazimishwa kulipa kharaji hubakia ni ardhi ya kharaji milele. Watu wake wakisilimu au kumuuzia Muislamu, kharaji yake hubakia kwa sababu sifa yake ya kuwa imekombolewa kinguvu itabakia mpaka siku za

mwisho. Na watalazimika kulipa ushri pamoja na kharaji kwa sababu kharaji ni haki iliowajibika juu ya ardhi na ushri ni haki iliolazimika juu mazao ya ardhi ya Muislamu kupidia aya na hadithi. Haki hizi mbili hazifutiani kwa sababu zimewajibika kwa sababu mbili tofauti. Amma ile hadithi iliosimuliwa kwa Mtume wa Allah (saw) waliostadili nao watu wa madhabu ya kiHanafi: "**Ushri na kharaji hazichangamani katika ardhi ya Muislamu**" hino si hadithi wala Al-Huffadh (wenye kuhifadhi hadithi) hawakuithibitisha kuwa ni maneno ya Mtume (saw).

Kharaji hulipwa mwanzo kisha zakaa huchukuliwa ikibakia baada kulipa kharaji mimea na matunda yanofikia nisabu ya kulipa zakaa. Kama yaliobakia hayafiki nisabu, hakuna zakaa juu yake.

KUHUISHA ARDHI

Ardhi maiti ni ardhi isiodhihirisha kwamba ilitangulia kumilikiwa na mtu yoyote. Haidhirishi athari ya chochote mionganoni mwa (*ihaata*), mimea, kuamiriwa au mifano yake. Kila ardhi maiti huwa ni milki ya mtu mwenye kuhuisha. Shar'a imemilikisha mwenye kuihuisha kupidia aliosimulia Bukhari kumpitia Aisha kwamba Mtume wa Allah (saw) alisema: "**Mwenye kuamirisha ardhi isiokuwa ya mtue ana haki zaidi (juu yake)**." Na Abu Dawud amesimulia kwamba Mtume (saw) alisema: "**Mwenye kuweka mipaka (*hait*) juu ya ardhi, hiyo (ardhi) ni yake**." Na Bukhari amesimulia kutoka Umar kwamba Mtume wa Allah (saw) alisema: "**Mwenye kuhuisha ardhi maiti, hiyo (ardhi) ni yake**." Muislamu na dhimmi wako sawa (kwa hukmu hino) kwa sababu ya kutofungika (*itlaaq*) hadithi.

Kuhuisha ni tofauti na kutolewa (*iqtaa'*). Tofauti baina yake ni kuwa kuhuisha huhusika na ardhi maiti isiodhihirisha kwama ilitangulia kumilikiwa na mtu yoyote; haidhirishi athari ya chochote mionganoni mwa (*ihaata*), mimea, kuamiriwa nk. Na kuhuisha ardhi hino ni kuiamirisha kwa kitu chochote kinacho dhihirisha kuhuisha. Amma kutolewa ardhi, hino ni kutolewa ardhi ilioamiriwa inaofaa kwa ajili ya ukulima sasa hivi yaani inadhihirisha kwamba ilitangulia kumilikwa na mute. Amma

kuiwekea mipaka/kuizuia (*tahjeer*) ardhi, hino ina usawa kama kuhuisha (katika kumilikisha) kupitia msemo wake (saw): "**Mwenye kuweka ukuta (hait) juu ya ardhi, hiyo (ardhi) ni yake.**" Na msemo wake (saw): "**Mwenye kuzungusha ukuta (hait) juu ya kitu, hicho (kitu) ni chake.**" Na pia kwa sababu mwenye kuizuia (*tahjeer*) humiliki kupitia kwayo tasarrufi kwa msemo wazi wa hadithi. Na mwenye kuizuia aweza kumzuia anayetaka kuhuisha kile alichokizua. Lau mwengine amzidi nguvu na kuhuisha ardhi alioizuia, huyo mwengine haimiliki ardhi na itaregeshwa kwa mwenye kuizuia. Na pia kuzuia ni kama kuhuisha katika kutasarruf na ardhi na kuweka mkono juu yake. Basi mwenye kuzuia akiuza ardhi alioizuia, atamiliki bei ya kuiuza kwa sababu hiyo ni haki inaobadilishwa kwa pesa basi yajuzi kupewa malipo/ridha juu yake. Lau mwenye kuizuia atakufa, milki yake hunukuliwa kwa warathi wake kama mali nyengine; na hawa warathi watatasarruf nayo na kugawanyiwa kwa mujibu ya mafungu ya kiSheria kama mali nyengine inavyogawanywa. Kuzuia haimaanishi kuweka mawe juu yake; bali maana yake ni kuweka chochote kinachoonyesha kuweka mkono juu yake yaani kumiliki. Basi kuzuia itakuwa kwa kuweka mawe kwa mipaka yake au kisichokuwa mawe kama kuweka majani yaliokauka, kusafisha ardhi na kuchoma miba ndani yake, kukata yaliyomo ndani yake ya hashishi au miba na kuyaweka ubavuni mwake ili kuzuia watu kuingia, kuchimba mito yake (*wa lam yasqiha*) na mifano yake. Haya yote ni kuzuia.

Dhahiri ya hadithi ni kuwa kuzuia kama kuhuisha hutokeea tu juu ya ardhi maiti si ardhi nyengine. Msemo wa Umar: "**Mwenye kuzuia hana haki baada miaka mitatu**" humaanisha mwenye kuzuia katika ardhi maiti. Amma ardhi isiokuwa maiti, haimiliwi kupitia kuzuia wala kuhuisha bali humiliwi kwa kutolewa/kupewa na Imam. Hini ni kwa sababu kuhuisha na kuzuia imekuja kwa ardhi maiti na alisema (SAW): "**Mwenye kuhuisha ardhi maiti.**" Na maiti ni sifa ilio na ufahamu (*mafhum*) basi huamiliwa nayo na huwa ni kizuizi/kipingu (*qayd*). Pia Bayhaqi amesimulia kutoka Amru bin Shuaib "**kwamba Umar alijaalia kuzuia kuwa miaka mitatu, na**

akiwacha mpaka ikapita miaka mitatu na akaja mwengine kuihuisha, huyo ana haki zaidi juu yake" Maana yake ni kuwa ardhi isiokuwa maiti haimiliwi kupitia kuzuia au kuhuisha.

Tofauti hino baina ardhi maiti na isiokuwa maiti huonyesha kwamba Mtume aliwaruhusu watu kumiliki ardhi maiti kupitia kuhuisha na kuzuia basi ikawa katika mambo mubah. Kwa hivyo kuhuisha au kuzuia haihitaji ruhusa ya Imam kwa sababu mambo ya mubah hayahitaji ruhusa ya Imam. Amma ardhi isiokuwa maiti, haimiliwi mpaka Imam aitoe kwa sababu sio katika mambo ya mubah; bali ni katika yale Imam ana nguvu juu yake na huitwa ardhi za serikali. Kwa kudokezea hayo, **Bilal Al-Muzni alimwomba Mtume wa Allah kumpa ardhi na hakuimiliwi mpaka Mtume alipompa**. Lau ingemilikiwa kupitia kuhuisha au kuzuia basi angeliizungusha na alama kuonyesha kumiliki kwaka, na ingelikuwa milki yake pasina kuomba apewe.

Mwenye kuhuisha ardhi maiti, Muislamu au kafiri, katika ardhi za ushri humiliyi shingo na manufaa yake. Muislamu atawajibika kulipa ardhi kama zakaa juu ya mimea na matunda inaowajibika zakaa juu yake ikifika nisabu. Amma kafiri, halazimishwi ushri au kharaji juu yake kwa sababu yeye si mionganoni mwa wenyewe kulipa zakaa mpaka iwajibishwe juu yake, na kwa sababu kharaji haiwajibiki juu ya ardhi ya ushri.

Mwenye kuhuisha ardhi maiti katika ardhi za kharaji ambayo haikutanguliwa kulipishwa kharaji humiliyi shingo na manufaa yake akiwa Muislamu, na manufaa yake tu akiwa kafiri. Muislamu atawajibika kulipa ushri juu yake wala hakuna kharaji juu yake. Kafiri atawajibika kkulipa kharaji kama ilivyolipishwa juu ya watu wake makafiri pindi waliporuhusiwa ilipokombolewa kubakia juu yake kwa malipo ya kharaji.

Mwenye kuhuisha ardhi maiti katika ardhi ya kharaji iliotanguliwa kulipishwa kharaji kabla kubadilika kuwa ardhi maiti humiliyi manufaa yake tu bila shingo lake, Muislamu au

kafiri. Kharaji itawajibika juu yake kwa sababu husimama juu yake kwamba ilikuwa ardhi iliokombolewa na kulipishwa kharaji; kwa hivyo ni wajibu kharaji ibakie juu yake milele sawa sawa ni Muislamu au kafiri anaimiliki. Hino ikiwa imehuishwa kwa ajili ya ukulima lakini ni kwa ajili ya nyumba au kusimamisha viwanja, mahazina au (*hadhair*), hakuna ushri au kharaji juu yake pasina tofauti hapo baina ardhi ya ushri au kharaji. Masahaba waliokomboa Iraq na Misri walibuni Kufa, Basra na Fustat na wakaishi humo paomja na wengine siku za Umar bin Al-Khattab wala hawakulipishwa kharaji au zakaa kwa sababu zakaa hailipishwi juu ya nyumba au majengo

KUTASARRUF KATIKA ARDHI

Kila mwenye kumiliki ardhi hulazimishwa kuitumia, na mwenye kuhitaji usaidizi hupewa inaomwezesha kuitumia kutoka Bait al-Mal. Lakini akiachia miaka mitatu pasina kuitumia hypokonywa na kupewa mwengine. Umar bin Al-Khattab alisema: "**Mwenye kuzuia hana haki baada miaka mitatu.**" Na Yahya bin Adam amesimulia kumpitia Amru bin Shuaib aliosema: "**Mtume (SAW) aliwagawanya watu kutoka Muzaina au Juhaina ardhi na wakaiwacha pasina kuitumia, basi wakaja watu na wakaihuisha.** Umar akasema: Lau ingelikuwa mimi nimeigawanya au Abubakar ningeliirudisha lakini ni kutoka Mtume (SAW). Akasema: Umar alisema: **Mwenye kudharau ardhi miaka mitatu pasina kuiamirisha kisha akaja mwengine kuiamirisha, ardhi hiyo ni yake.**" Maana yake ni kwamba yashapita zaidi ya miaka mitatu yaani lau kama ilikuwa kutoka Abubakar au mimi basi ingekuwa hazijapita miaka mitatu lakini ni kutoka Mtume (SAW) kwa hivyo imepita miaka mitatu basi haiwezi kurudishwa. Na Abu Ubayd alisimulia katika '*Al-Amwal*' kumpitia Bilal bin Al-Harith Al-Muzni "**kwamba Mtume (SAW) alimpa (ardhi ya) Al-'Aqeeq nzima.** Akasema: **Ilipokuwa wakati wa Umar, yeye alisema kwa Bilal: Mtume (SAW) hakukupa ili uizuie kwa watu bali alikupa ili uifanyie kazi. BAsi chukua kutoka kwayo unaoweza kuiamiri na rudisha inaobakia"** Na ijma ya masahaba imesimama

kwamba mwenye kuacha ardhi yake miaka mitatu hupokonywa na kupewa mwengine.

Kwa hayo, mwenye ardhi afaa kulima ardhi yake kupitia vyombo, mbegu, wanyama na wafanyakazi wake. Na aweza kuilima na wafanyakazi anaowaajiri kuifanyia kazi; akishindwa, serikali itamsaidia. Lau mwenye ardhi hailimi basi ampe mwengine kuilima kama zawadi bila malipo. Na lau hafanyi hivo na aishike, hupewa miaka miaka mitatu; akiidharau muda wa miaka mitatu, serikali huichukua na kumpa mwengine. Yunus amesimulia kutoka Muhammad bin Ishaq kutoka Abdullah bin Abubakr aliesema "**Bilal bin Al-Harith Al-Muzni alikuja kwa Mtume (SAW) kumwomba ardhi na akampa ardhi ndefu na pana. Alipotawazwa Umar akambwambia: Ewe Bilal, ulimwomba Mtume (SAW) ardhi ndefu na pana na yeye alikupa, na alikuwa Mtume (SAW) hakatai chochote aulizwacho ilhali ardhi mikononi mwako imekuzidi. Akasema: Ndio. Akasema: Angalia unachokiweza ili ubakie nacho kisha turudishie kwetu usichokiweza au kilichokuzidi nguvu ili tukigawanye baina Waislamu. Akasema: Sifanyi, wallahi! Ni kitu Mtume (SAW) amenipa. Umar akasema: Wallahi utafanya! Basi akachukua kutoka kwake kilichomshinda kukiamiri na kukigawanya baina Waislamu**" (Yahya bin Adam ameisimulia katika kitabu cha '*Al-Kharaj*') Hino ni wazi kwamba ardhi ambayo mwenyewe hushinda kuilima na kuidharau miaka mitatu, serikali humpokonya na kumpa mwengine kama alivyofanya Umar bin Al-Khattab na Bilal Al-Muzni katika machimbo ya *Al-Qabaliya*.

Mwisho, ardhi humilikwa kupitia kuzuia, kutolewa na Khalifa, kuhuisha, mirathi na kununua. Dalili/nususi (*nusus*) zilizokuja kutaja kupokonywa ardhi kutoka mwenye kuidharau kwa miaka mitatu zilitaja mwenye kuzuia na mwenye ardhi na Khalifa; wengine wenye kumiliki ardhi—yaani wenye kuirithi, kuhuisha na kununua—hawakutajwa. Basi je Khalifa aweza kumpokonya ardhi kila mwenye kumiliki ardhi kisha akaidharau ardhi miaka mitatu na kumpa mwengine, au hiyo ni khusisi kwa mwenye kuzuia na mwenye kupewa ardhi na Khalifa? Jawabu yake ni

kuwa mwenye kuchunguza huona kwamba kuzuia ardhi ni kama kuinunia, kuirithi au sababu yoyote nyengine yakumiliki ardhi katika kutasarruf nayo na kuweka mkono juu yake. Lau mwenye kuzuia ardhi auze ardhi alioizuia, mnunuzi huimiliki kwa sababu ni haki iliobadilishwa kwa mali basi yajuzu malipo/ridha juu yake. Na lau mwenye kuzuia ywafa, milki ya ardhi hunukuliwa kwa warathi wake kama mali nyengine zinazofanyiwa tasarruf, na hugawanywa kwa mujibu ya mafungu yao ya kisheria. Kadhalika kwa wale Khalifa aliowapa ardhi. Kwa hivyo hakuna sifa maalumu kwa ardhi ya mwenye kuzuia na aliopewa ardhi ili kuhusishwa na kuchukuliwa ardhi ikiwachwa miaka mitatu tofauti na wamiliki wengine wanaomiliki kupitia sababu nyengine za kumiliki ardhi. Au kuwafanya mwenye kuzuia na mwenye kupewa ardhi kuwa ni kizuizi (*qayd*) cha kufunga wenyewe kupokonywa ardhi ikipita miaka mitatu. Amma kuwa dalili huwataja wao tu wala sio wengine, haifahamiki maana ya kufungwa kwa sababu si sifa yenye ufahamu (*wasf m'alum*) kwamba hupokonywa mwenye kudharau kwa sababu ye ye ni mwenye kuzuia au kupewa ardhi; bali hino ni katika jinsi ya kutajwa moja wapo ya vitu vingi nayo ni kuchukua ardhi kutoka mwenye kuimiliki akiidharau. Basi dalili ni jumla ('aam) na kutajwa mwenye kuzuia na mwenye kupewa ni kutajwa moja wapo ya vitu vingi wala sio kizuizi inaozua vyengine. Ikija dalili juu ya tukio, hutizamwa; ikiwemo ndani yake usababu ('illiyya) basi huwa ni dalili jumla juu ya yale iliofungika kisababu nayo. Dalili hapa hufahamika na usababu nayo ni kuwa ardhi hupokonywa baada miaka mitatu kwa kudharau kuilima basi kudharau ardhi miaka mitatu ndio sababu ('illa) ya kupokonywa. Kwa hivyo sababu ya kupokonywa ardhi mwenye kuzuia ni kuwa ameidharau miaka mitatu wala sio kuwa ye ye ni mwenye kuzuia au kupewa kwa sababu kuzuia ardhi haileti maana ya kuwa ndio sababu ya kupokonywa kwake, sio kipekee wala sio ikiunganishwa na kudharau. Bali kudharau pekee yake ndio inaoleta usababu ya kupokonywa. Basi kudharau ardhi ni sababu inaozunguka na kile kitu kilichofanyiwa usababu kwa kuweko na kutokuweko. Kwa hivyo pindi hutoka mwenye kumiliki ardhi kuidharau miaka mitatu, hupokonywa sawa sawa ameimiliki kwa kuzuia, kupewa, mirathi au njia nyengine. Na

lau mwenye kuizua asiidharau asiidharau kwa miaka mitatu, hapokonywi. Kisha kuzuia ardhi katika msemo wa Umar: "**Wala mwenye kuzuia ardhi**" ni (lughya) kinaya inaomaanisha kumiliki kwa sababu ilikuwa ni kawaida kwamba mwenye kumiliki ardhi alikuwa akizuia ardhi yaani kuweka mawe kwa mipaka yake kuonyesha kwamba yeye anamiliki na ili aitofautishe na milki ya mwengine. Wala si sharti kuweka mawe kwa mipaka ili aitwe mwenye kuzuia; bali lau aweke mimea au miti kwa mipaka ya ardhi, au achimbe mipaka yake au afanye chochote inaoonyesha kuwa ameitia mkononi, yote haya yatosha ili iitwe kuzuia na mwenye kufanya hivo aitwe mwenye kuzuia. Kwa hivyo alisema Mtume katika hadithi nyengine: "**Anayezungusha ukuta juu ya ardhi**" (Abu Dawud ameisimulia) hudokeza kuwa kuzuia ardhi ni mithali juu ya kumiliki kama maana ya neno '*ihtajara*' katika lugha hongoza kwayo. Hakika lugha yasema ku-'*ihtajara*' kitu ni kuiweka katika chumba yaani kuikumbatia. Basi ku-*ihtajara* ardhi yaani kuikumbatia kwa maana ya kuimiliki. Kwa hivyo maana ya hadithi: "**Hakuna kwa mwenye kukumbatia ardhi yaani kuimiliki haki baada miaka mitatu**" sawa sawa ameweke mawe kwa mipaka yake, kuzungusha ukuta au kufanya chochote inaodokeza kuimiliki.

Hino ni kwa mnasabaa wa nasi. Amma kwa mnasaba kwa aliyoifuata Umar na waliosalia katika masahaba kuinyamazia, Umar alihukumia ardhi—ambayo Mtume (SAW) alimpa Muzaina kisha wengine wakaiamiri—kwa mwenye kuiamiri na kumzuia Muzaina kumpokonya akisema: "**Mwenye kuipuuza ardhi miaka mitatu pasina kuiamiri kisha akaja mwengine na akaiamiri, basi hiyo ni yake.**" Huu msemo wa Umar ni wa kijumla: "**Mwenye kupuuza ardhi**" na akasema kwa Bilal bin Al-Harith Al-Muzni: "**Mtume (SAW) hakukupa kuizua kwa watu. Bali alikupa tu ili ufanye kazi basi chukua kiasi unachoweza kukiamiri na rudisha kinachobakia**" (Abu Ubaid ameisimulia katika '*Al-Amwal*'). Na akamnyang'anya kivitendo alichoshindwa kukiamiri. Kukhusisha hino kwa kupewa (ardhi) pekee yake bila kitu wazi cha kuikhusisha (hapa tu) haijuzu, bali hubakia jumla. Amma kuwa tukio kilitokea juu

ya mwenye kupewa ardhi, hino ni msemo wa hali ilivyokuwa wala sio kizuizi katika tukio hino.

Kwa hivyo kila mwenye kumiliki ardhi hupokonywa akiidharau miaka mitatu na kupewa mwengine pasina kujali sababu ya kumiliki ardhi kwa sababu muhimu ni kudharau ardhi wala sio sababu ya kumiliki. Wala haisemwi kwamba hino ni kuchukua mali za watu pasina haki kwa sababu *Shar'a* imejaalia kumiliki ardhi kuwa na maana tofauti na maana ya kumiliki isiokuwa ardhi au kumiliki majumba; imefanya kuimili ni kuilima. Basi ikidharauliwa kwa muda uliotajwa na *Shar'a*, maana ya kumiliki hupotea kutoka mwenye kumiliki. *Shar'a* imejaalia kumiliki ardhi kwa ajili ya kulima kwa kuamiri, na kuimili kuipitia kupewa, mirathi, kununua au (sababu) tofauti na hayo na ikaijaalia kupokonywa kutoka mwenyewe ni kupertia kuipuuza. Haya yote ni kwa ajili ya kudumisha ardhi kulimwa na kutumiwa.

KUZUILIWA KUKODISHA ARDHI

Haruhusiwi kabisa mwenye ardhi kukodisha ardhi yake sawa sawa awe ni mwenye kumiliki shingo na manufaa yake au amiliki manufaa yake tu yaani sawa sawa ikiwa ardhi ni ya kiushri au kharaji na sawa sawa kodi iwe ni pesa au tofauti na hicho. Kadhalika haijuzu kabisa kukodisha ardhi ya shamba kwa ajili ya chochote kinachozalisha miongoni mwa vyakula au vyengineo, wala chochote kinachotokamana nacho kwa sababu haya yote ni kukodisha, na kukodisha ardhi ya shamba hairuhusiwi kabisa.

Imekuja katika Sahih Al-Bukhari kwamba Mtume (SAW) alisema: "**Mwenye ardhi ailime au ampe zawadi ndugu yake. Akikataa basi ardhi yake ishikwe**" Na ikaja katika Sahih Muslim: "**Mtume (SAW) alikanya kodi au fungu ichukuliwe katika ardhi.**" Na ikaja katika Sunan ya An-Nisai: "**Mtume (SAW) alikanya kodi ya ardhi. Tukasema: Ewe Mtume, basi tutaikodisha kwa fungu la ngano/mbegu? Akasema: La. Akasema: Na tulikuwa tukiikodisha kwa rabi'a as-saqiy. Akasema: La, ilime au mpe zawadi ndugu yako.**" Na *rabi'a*

ya mto mdogo humaanisha bonde, yaani tulikuwa tukiikodisha kwa kulima kipande kilicho kwa bonde yaani ubavuni mwa maji. Na imeswihi kutoka Mtume (SAW) "**kwamba alikanya kuchukua kodi au fungu kwa ardhi, au ikodishwe kwa thuluthi au robo**" na Abu Dawud amesimulia kutoka Rafi bin Khudaij kwamba Mtume (SAW) alisema: "**Aliye na ardhi ailime au ndugu yake ailime wala asiikodishe kwa thuluthi wa la robo wala vyakula viliotajwa.**" Na Al-Bukhari alisimulia kutoka Nafi kwamba Abdullah bin Umar alisimulia kutoka Rafi bin Khudaij "**kwamba Mtume (SAW) alikanya kukodisha mashamba. Basi ibn Umar alikwenda na nilifuatana naye kumuuliza, naye akasema: 'Mtume (SAW) alikanya kukodisha mashamba.'**" Na Al-Bukhari alisimulia kutoka Salim kwamba **Abdullah bin Umar aliwacha kukodisha ardhi.**

Hizi hadithi ni wazi kwamba Mtume (SAW) alikanya kukodisha ardhi. Na kukanya, hata kama hudokeza tu mujaradi yaukomba kuwacha (kitendo), lakini kidokezo hapa huonyesha kwamba ombi ni la kukatikiwa kwa sababu wakamwambia Mtume: Tuikodishe kwa fungu la ngano/mbegu. Akasema: La. Kisha wakamwambia: Tuikodishe kwa majani makavu. Akasema: La. Kisha wakasema: Tulikuwa tukiikodisha kwa *rabi'a*. Akasema: La. Kisha akaitilia mkazo kwa msemo wake: "**Ilimeni au mpe zawadi ndugu yako.**" Hino ni wazi katika kudumu (kwake) juu ya kukanya ambayo ni kutilia mkazo. Pamoja na kuwa kutilia mkazo katika kiarabu imma ni kupitia maneno kwa kukariri maneno au kimaana; hapa neno la kukanya limekaririwa inaokodeza kutilia mkazo. Amma Mtume kukodisha Khaibar kwa nusu (kinachopatikana), hino sio katika mlango huu kwa sababu ardhi ya Khaibar ilikuwa ya ya miti wala si ardhi tupu kwa dalili ya yaliosimuliwa na ibn Ishaq katika Sera kutoka Abdullah Abubakr "**kwamba Mtume (SAW) alikuwa akimtuma Abdullah bin Rawaha kama mwenye kupima baina Waislamu na mayahudi, basi aliwapimia...kisha Abdullah bin Rawaha alisibiwa (kuwa) katika (vita vya) Mut'a. Basi akawa Jabbar bin Sikhr bin Umayya bin Khansa, ndugu wao Banu Salama, ndiye aliye kuwa**

akiwapimia baada Abdullah bin Rawaha." Mpimaji ni yule mwenye kupima matunda zikiwa kwa mitagaa zake kabla hazijatoka. Hino ni wazi kwamba ardhi ya Khaibar kuwa ni ya miti wala sio ardhi tupu. Amma yaliyomo ndani yake ya mimea, yalikuwa duni ya masafa ya miti basi yalikuwa yakiyafuata. Kwa hivyo ardhi ya Khaibar haikuwa katika mlango wa kukodisha ardhi bali ilikuwa katika mlango wa *musaaqaat* (kukodisha ardhi ya miti) na *musaaqaat* yajuzu. Na juu ya hayo, **baada ya Mtume (SAW) kukanya, masahaba walizua kukodisha ardhi akiwemo Abdullah bin Umar.** Hino ikadokeza uharamu wa kukodisha ardhi. Isipokuwa uharamu wa kukodisha ardhi ni ikiwa imekodishwa kwa ukulima. Amma ikiwa imekodishwa sio kwa ukulima hino yajuzu kwa sababu yajuzu kumkodishia ardhi ili iwe malishi, pahala pa kutulia, hazina ya bidhaa au kunufaika nayo kwa chochote tofauti na ukulima. Hii ni kwa sababu kukanya kukodisha ardhi imebuniwa juu ya kuikodisha kwa ukulima kama ilivyochukuliwa kutoka hadithi sahihi. Hizi hukmu za ardhi na yanaohuka nayo hubainisha vipi Mwenye Sheria (*As-Shari'*) humfunga Muislamu akifanya kazi kuzidisha umilikaji wake kupitia njia ya ukulima.

12 BIASHARA NA UTENGENEZAJI/UTENDAJI (*Istisna'*)

Biashara

Kwa hakika Allah *Subhaanahu wa Ta'ala* amejaalia mali kuwa sababu ya kusimamisha maslahi ya waja katika dunia, na amehalalisha njia ya biashara ili kuchuma maslahi hayo. Kwa sababu *kinachohitajiwa* na kila mtu hakipatikani kwa uepesi kila mahali, na pia kuichukua kwa njia ya nguvu na kimabavu ni ufisidifu, basi hakuna budi kuwepo nidhamu ya kumakinishia kila mmoja kuchukua anachokihitaji si kwa njia ya nguvu na mabavu. Hiyo ni biashara na hukmu za biashara. Allah *Ta'ala* asema:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً عَنْ تَرَاضٍ مِنْكُمْ }

"Enyi mlolioamini, musile mali baina yenu kwa ubatili ila ikiwa biashara kwa maridhiano baina yenu" [TMQ 4:29] Biashara ni sampuli mbili: Halali ambayo Shar'a huiita *al-bay'u* na haramu

inayoitwa *riba*; kila moja wapo ni biashara. Allah amejulisha juu ya makafiri kukanusha tofauti baina biashara na riba kiakili aliposema '*Azza wa Jalla*:

{ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا }

"*Hii ni kwa sababu wao wanasema: 'Biashara ni kama riba'*" [TMQ 2:275] kisha akatofautisha baina yao kwa uhalali na uharamu kwa msemo wake *Ta'ala*:

{ وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَمَ الرِّبَا }

"*Allah amehalalisha biashara na kuharamisha riba*" [TMQ 2:275] Akatujulisha kwamba kila mmoja yao ni biashara, na cha halali kilichoruhusiwa mionganini mwa hizo mbili ni biashara. Kutekeleza biashara hino ni kwa lafdhi mbili mojawapo ikidokeza kutaka na nyengine ikidokeza kukubali; nazo ni 'Nimeuza' na 'Nimenunua' au yaliofanana nayo kimsemo na kivitendo. Mwenye bidhaa aweza kusimamia biashara au awakilishwe na mwakilishi au mjumbe anayesimamia biashara kwa niaba yake. Pia yajuzu kumwajiri mfanyakazi kusimamia biashara kwa niaba yake kwa sharti mshahara wake uwe maalumu. Ikiwa atamwajiri kwa sehemu ya faida atakuwa na mshirika wa *ki-mudharaba*, na hukmu ya *mubharib* itasamama juu yake wala sio hukmu ya mfanyakazi. Kadhalika yajuzu anunue mali kibanafsi au kumpitia mwakilishi, mjumbe au amwajiri mwenye kumnunulia.

Mwishowe, biashara yajuzu nayo ni mionganini mwa sampuli za kuzisidisha mali, na ni wazi katka hukmu za biashara na ushirika. Biashara imekuja katika Qur'an na Hadith. Asema *Ta'ala*:

{ إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً حَاضِرَةً تُدْرِرُونَهَا بَيْنَكُمْ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَلَا تَكْتُبُوهَا }

"*Ila ikiwa ni biashara iliohuduria mnayopeana baina yenu, basi si vibaya kwenu musipoandika*" [TMQ 2:282] Na Rufa'ah amesimulia kwamba "**alitoka pamoja na Mtume (SAW) kwenda kwa musalla**. Akaona watu wakifanya biashara na akasema: 'Enyi wafanyaji biashara.' Wakamwitika kwa kuinua mashingo na macho yao kwake. Akasema: 'Wafanyaji biashara watafufuliwa kama watu waovu Siku ya Qiyama ila mwenye kumcha Allah, kutenda mema na kutoa sadaqa.'" Na Abu Said amesimulia kwamba Mtume

(SAW) alisema: "**Mfanyaji biashara mkweli mwaminifu yuko pamoja na Mitume, masidiki na mashahidi**" (At-Tirmidhi amezisimulia zote mbili).

Biashara ni vigawanyo viwili: Biashara ya kindani na biashara ya nje. Amma biashara ya ndani, hiyo ni kuuza na kununua inaotokea baina ya watu kuhusika na bidhaa walizo nazo sawa sawa iwe mazao yao ya kiukulima au uzalishaji au ni mazao ya wengine lakini zipo katika biladi zao na wanazibadilisha baina yao. Biashara ya kindani haina vizuizi ila yaliokuja katika hukmu zinazohusika na biashara. Amma bidhaa na sampuli za bidhaa, na kunukuliwa kwao ndani ya nchi kutoka biladi mpaka biladi, hino huachiliwa kila mtu kufanya biashara ndani ya hukmu ya *Shar'a*; na serikali haina jukumu katika biashara ya kindani ila haki ya usimamizi tu. Amma biashara ya nje, hiyo ni kununua bidhaa kutoka nje ya nchi na kuuza bidhaa za nchi nje yake sawa sawe bidhaa hizi zikiwa ni za ukulima au uzalishaji. Biashara hino hunyenyekoa usimamizi wa moja kwa moja wa serikali ambao hutawala usimamizi wa moja kwa moja juu ya kuingia na kutoka bidhaa, na biashara za harbi na mu'ahid.

UZALISHAJI

Hino ni mtu kumzalishia mwengine chombo, gari au chocote kinachoingia katika uzalishaji. Uzalishaji yajuzu na imethhibitika katika Sunna. Mtume (SAW) alizalisha pete (kumpitia mwengine). Anas alisema: **Mtume (SAW) alizalisha pete**. Na kutoka ibn Masoud kwamba **Mtume (SAW) alizalisha pete ya dhahabu** (zimesimuliwa na Bukhari). Na pia alizalisha minbar. Kutoka Sahl aliesema: **Mtume (SAW) alituma kwa mwanamke: 'Mwamrishe mtumwa wako mseremala kunitengenezea mabao kuyaketia** (Bukhari ameisimulia). **Na watu walikuwa wakizalisha katika zama za Mtume (SAW) naye aliwanyamazia** na kunyamaza kwake ni kukiri juu ya uzalishaji wao. Na kukiri kwa Mtume (SAW) na kitendo chake ni dalili ya kiSunna. Na chenye kufanywa mkataba juu yake ni kinachozalishwa yaani pete, minbar, kasha, gar ink. Basi kwa sura hino huwa ni jinsi ya biashara wala sio jinsi ya kuajiri. Lakini lau mtu amletee mzalishaji kitu cha kutengenezewa vitu

vyengine na kuwomba amzalishie kitu maalumu, hino itakuwa katika jinsi ya kuajiri.

Uzalishaji kiasli ni msingi muhimu katika misingi ya maisha ya kiuchumi ya umma yoyote ile, na wau wowote katika mujtama wowote ule. Uzalishaji ulikweko ukifungika kwa mitambo ya uzalishaji ya kimkono tu lakini pindi mwanadamu aliongoka kutumia bukhari (steam) katika kupeleka mitambo yakaanza mitambo yakupelekwa kimashini kuchukua nafasi ya mitambo ya kimkono. Na pindi ilipokuja uvumbuzi wa kileo yakatokea mapinduzi ya kiajabu katika uzalishaji mpaka mazao yakazidi kwa kiwango kisichoweza kutarajiwa. Na mitambo ya kujiendesha kimashini yakawa msingi wa misingi wa maisha ya kiuchumi.

Hukmu zinazohusika na viwanja vya kimashini au vya kimkono haitoki imma kuwa hukmu za ushirika, kuajiri, au biashara ya kindani na nje. Kwa upande wa kubuni viwanja, huwa ni mali ya kibinafsi na hino ni nadiri. Aghlabu ni mali ya watu binafsi wanaoshiri kuzibuni, na hapa hutabikishwa hukmu za shirika za Kiislamu. Amma kwa upande wa kufanya kazi ndani humo katika idara, kazi, kuzalisha nk hutabikishwa hukmu za kumwajiri mfanyakazi. Amma kwa upande wa kutasarruf na mazao yake, hutabikishwa hukmu za biashara na pia biashara za nje; na urongo, kuhadaa na ukiritimba zitazuiliwa humo kama kupanga bei itazulikwa mionganoni mwa hukmu za biashara. Amma kuagizia mazao yanaozalishwa, madago au makubwa, hutabikishwa hukmu za uzalishaji. Na Shar'a huamua katika kumlazimu mwenye kuagazia na alichozalishiwa au kutomlazimu.

13 HUKMU ZA MASHIRIKA

Shirika katika Uislamu

Shirika kilugha ni kuchangamanisha fungu mbili au zaidi kiasi ya kwamba haitambuliki moja kutoka mwenzake. Shirika kiSheria ni mkataba baina wawili au zaidi wanaowafikiana ndani yake kutenda amali ya kimali kwa makusudio ya faida. Mkataba wa shirika huhitaji kuwepo kutaka (offer) na kukubali

(acceptance) pamoja kama mikataba mengine. Kutaka ni mmoja wao kumwambia wa pili: 'Nimekushirikisha katika katika kadha' na yule mwengine kusema: 'Nimekubali.' Lakini maneno yaliotajwa si lazima ila maana yake yaani hapana budi kuhakikishwa katika kutaka na kukubali maana inaodokeza kwamba mmoja wao amkhutubu mwengine moja kwa moja au kwa kuandika kushirika katika kitu, na yule wa piloi akubalie hilo. Kukubaliana juu ya kushiriki tu haitambuliwi kama mkataba, na kukubaliana tu juu ya kulipa mali ili kushiriki haitambuliwi kama mkataba; bali ni lazima mkataba ikusanye maana ya kushiriki juu ya kitu. Sharti ya kuswihi mkataba wa shirika ni kwamba yaliokubaliwa iwe ni tasarruf, na tasarruf hino iliokubaliwa iwe ni mkataba wa shirika inaokubali kuwakilisha ili yanaopatikana kutoka tasarruf iwe ya ushirika baina wao wawili.

Ushirika yajuzu kwa sababu alipotumwa Mtume (SAW), watu walikuwa wakiamiliana nazo na Mtume aliyakiri. Basi ikawa kukiri kwake (AS) kwa watu kuamiliana nazo ni dalili ya kiSheria juu ya kujuzu kwao.

Bukhari amesimulia kwamba Abu Al-Minal alisema: "**Mimi na mshirika wangu tulinunua kitu mkono kwa mkono na kwa mkopo. Al-Bara bin Azib alituikia na tukamuulizia.** Akasema: '**Mimi na mshirika wangu, Zaid bin Arqam, tulimuuliza Mtume (SAW) juu yake naye** akasema: '**Chukueni kila ambacho ni mkono kwa mkono, na kiregesheni kile ambacho ni mkopo.**' Na Al-Daraqutni alisimulia kutoka Abu Hurayra kwamba Mtume (SAW) alisema: "**Yaani Allah ta'ala asema: 'Mimi ni wa tatu wa washirika wawili maadamu mmoja wao hamkhini sahibu wake. Lau akhini, Mimi nawawacha'**"

Ushirika yajuzu ya Waislamu baina yao, ya madhimmi baina yao, na baina Waislamu na madhimmi. Yaswihi Muislamu kumshirikisha mkristo, majusi au dhimmi mwengine. Muslim asimulia kutoka Abdullah bin Umar aliesema: "**Mtume (SAW) aliwaamili watu wa Khaybar—nao ni mayahudi—kwa nusu**

ya yanaotoka ya matunda na mimea." Na Bukhari alisimulia kumpitia Aisha: "**Mtume (SAW) alinunua chakula kutoka myahudi na akaweka rehani vazi lake la kivita.**" Na Tirmidhi amesimulia kutoka ibn Abbas aliesema: "**Mtume (SAW) alifariki na vazi lake la kivita ilikuwa ni rehani kwa pishi ishirini za chakula ya ahli wake.**" Na Tirmidhi amesimulia kutoka Aisha: "**Mtume (SAW) alituma kwa mayahudi kuomba nguo mbili mpaka (siku za) nafasi/hali nzuri.**" Kwa hivyo yajuzu kuwashirikisha mayahudi, manasara na wengineo mionganoni mwa madhimmi kwa sababu yajuzu kuamiliana nao. Lakini haijuzu kwa madhimmi kuuza tembo na ngurue ilhali wako katika shirika na Muislamu; amma tembo na ngurue waliouza kabla kumshirikisha Muislamu, bei yake ni halali katika shirika. Shirika haijuzu ila kutoka mwenye kuruhusiwa kutasarruf kwa sababu ni mkataba juu ya kutasarruf katika mali, basi haiswihi kutoka yule asiyeruhusiwa kutasarruf katika mali. Ndio maana hairuhusiwi shirika ya mwenye kuwekaw chini ya usimamizi (guardianship) wala shirika ya kila asiyeruhusiwa kutasarruf.

Shirika amma ni shirika la kumiliki au shirika za mikataba. Shirika ya kumiliki ni shirika la kitu chenyewe kama shirika katika kitu kilichorithiwa na wau wawili, au wameinunua au mtu amewapa zawadi nk. Shirika la mikataba ndio inaotambuliwa katika uchunguzi wa kuzidisha umilikaji. Hudhihirika baada kuchunguza kwa makini na kufuutilia shirika za mikataba katika Uislamu, na kufuutilia hukmu za kiSheria zinazohusika nazo na dalili za kiSheria zilizokuja juu yake, kwamba shirika za mikataba ni tano nazo ni: Shirika la '*al-'inan*', shirika la viwiliwili (*al-abdan*), shirika la mudharaba, shirika la '*nyuso*' (*al-wujooth*) na shirika la '*mufawadha*'. Na haya ndio jumla ya hukmu zao.

Shirika la 'Al-'Inan'

Hino ni viwiliwili viwili vikishiriki na mali yao yaani watu wawili washiriki na mali zao kwa sharti wafanye kazi nazo na viwiliwili zao, na faida ni baina yao. Huitwa shirika la *al-'inan* kwa sababu wako sawa katika kutasarruf kama watu wawili

wenye kupanda farasi wakiwa sawa kwa farasi wao na katiko mwendo, basi *al-'inan* ni sawa. Shirika hili lajuzu kwa Sunna na Ijma as-Sahaba, na watu washirikiana nao kutoka zama za Mtume (SAW) na masahaba.

Sampuli hino ya shirika ambayo hufanya pesa kuwa ni rasilimali kwa sababu peas ni thamani ya mali na bei za vinaonunuliwa. Amma ardhi, haijuzu shirika juu yake ila ikikadiriwa kithamani wakati wa mkataba na kufanywa thamani yake kuwa rasilimali wakati wa mkataba. Ni sharti kwamba rasilimali iwe maalumu na iwezekane kutasarruf nayo moja kwa moja. Shirika juu ya rasilimali isiojulikana, mali isiokweko au deni haijuzu kwa sababu hakuna budi kuiregelea rasilimali wakati wa kutengana. Na pia kwa sababu haimkini kutasarruf na deni moja kwa moja ilhali hio ndio makusudio ya shirika. Haishurutishwi usawa wa mali hizo kiviwango wala mali hizo mbili kuwa sampuli moja; lakini ni wajibu zikadiriwe kwa thamani moja ili mali mbili ziwe mali moja. Yaswihi washiriki kwa pesa za kiMisri na kiSyria lakni lazima zikadiriwe kwa thamani maji, makadirio yanaoondosha tofauti zao na kuzifanya kitu kimoja kwa sababu ni sharti rasilimali ya shirika iwe mali majo inaoenea kila kitu (hadi) mshirika mmoja asijue mali yake kutoka mali ya mwenzake. Na ni sharti mikono ya washirika wawili yawe juu ya mali. Shirika la *al-'inan* imebuniwa juu ya kuwakilisha na uaminifu kwa sababu kila mmoja wao kwa kuumpa mwenzake sahibu wake huwa amemwamini, na kwa kumpa ruhusa kutasarruf huwa amemwakilisha. Na pindi inapotimia shirika huwa mali kitu kimoja na ni wajibu kwa washirika kusimamia kazi wao wenyewe kwa sababu shirika imetukia juu ya viwiliwili vyao. Haijuzu kwa mmoja wao kumwakilisha mtu ili mwili wake usimame badala yake katika kutasarruf katika shirika. Bali shirika litaajiri inaowataka na kutumia mwili wa inaomtaka kama mfanyakazi wa shirika wala sio badala wa mmoja wa washirika.

Yamjuzu kila mshirika, wawe ni wawili au zaidi, kuuza na kununua kwa sura anayoiiona ni maslaha kwa shirika. Pia aweza kupokea pesa na bidhaa zilionunuliwa, kushtaki juu ya deni na

kushtakiwa, kunukulu madai ya pesa na kunukuliwa, na kureegesha mali kwa sababu ya aibu. Na aweza kukodi na kukodisha kutoka rasilimali ya shirika kwa sababu manufaahufuata mwendo wa vitu venyewe basi huwa kama kununua na kuuza. Anaweza kununua bidhaa kwa mfano gari na aweza kuikodisha kwa kuchukuliwa kwake kuwa ni bidhaa ya kuuzwa basi manufaa yake katika shirika ni kama kitu chenyewe na hufuata mwendo wake. Haishurutishwa usawa wa washirika katika mali bali hushurutishwa usawa katika tasarruf. Amma mali, yaswihi kuwa sawa au kwa tofauti na faida itakuwa kama walivyoshurutisha. Ni sawa washurutishe usawa katika faida au kwa tofauti. Ali (RA) alisema: "**Faida ni vile walivyokubaliana**" (Abdurrazaq ameisimulia katika *Al-Jami'*). Amma hasara katika shirika la '*al-'inan*, hiyo ni kwa makadirio ya mali tu; ikiwa mali ni sawa kiviwango basi hasara itagawanya baina yao kinusunusu na ikiwa kwa thuluthi basi hasara itagawanya kithuluthithuluthi. Wakishurutisha tofauti na hayo, sharti yao haina uzito na hutekelezwa hukmu ya hasara bila sharti yao nayo ni kugawanya hasara kwa mujibu ya fungu za mali. Hii ni kwa sababu mwili haina hasara kimali basi hasara yake ni ile juhudi tu iliotumia. Basi hasara hubakia kwa mali na hugawanywa kulingana na fungu za washirika. Hiyo ni kwa sababu kushiriki ni kuwakilisha na hukmu ya uwakili ni kwamba wakili hadhamani bali hasara hutukia tu juu ya mali ya mwenye kuwakilisha. Abdurrazaq amesimulia katika *Al-Jami'* kutoka Ali aliesema: "**Kutukia (*al-wadhi'yya*) ni juu ya mali na faida ni walivyosikizana.**"

Shirika la Miwiliwili (Al-Abdaan)

Hino ni wawili au zaidi kushiriki kwa miwiliwili yao tu bila mali zao yaani juhudi zao katika kazi maalumu sawa sawa iwe ya kifikra au kimwili. Hino ni kama wasanii wanaoshirikiana kufanya kazi katika usanii wao na faida wanaopata igawanye baina yao. Mfano ni wahandisi, madakatari, wawindaji, mahamali, waseremala, wapelekaji magari nk. Haishurutishwi kukubaliana wasanii mionganoni mwa washirika wala kwamba wote wawe wasanii. Lau wasanii wanaotengeneza vitu tofauti watashiriki, hino yajuzu kwa sababu wanashiriki katika

kuchuma kilichoruhusiwa basi huswihi, na kadhalika lau wasanaii wanakubaliana baina yao. Na lau wanashirikiana ju ya kazi maalumu ili mmoja wao asimamie idara ya shirika, mwengine apokee mali, na wa tatu afanye kazi na mikoni yake, shirika huswihi. Kwa hivyo yajuzu kushirikiana wafanyikazi katika kiwanda, sawa sawa wote wajue usanii au baadhi wanajua na wengine hawajui kwa hivyo wanashiriki kama wasanii, wafanyikazi, makarani na maaskari, na wote wawe washirika katika kiwanda. Lakini ni sharti kwamba kazi wanaoshiriki kuitenda kwa makusudio ya faida iwe ni kazi inaoruhusiwa (*mubah*); imam kazi ikiwa ni haramu, haijuzu kushirikiana juu yake.

Faida katika shirika la kiwiliwili hulingana na walivyowafikiana katika kuwa sawa sawa au kwa tofauti kwa sababu kazi yastahiki faida na yajuzu wanashirika kushirikiana kitofauti katika kazi; kwa hivyo yajuzu wawe tofauti katika faida inaopatikana. Kila mmoja wao huweza kudai ujira wote kutoka aliowaajiri pamoja na bei ya bidhaa wanoiunda kutoka mwenye kuinunua. Na mwenye kuwaajiri au kununua bidhaa walizozienda aweza kulipa yote au bei yote ya bidhaa kwa yoyote mionganini mwa mwao; na huwa hana makosa kwa kumpa yoyote mionganini mwao. Na mmoja wao akifanya kazi bila washirika wake, anayochuma hugawanya baina yao kwa sababu kazi inadhaminiwa na wote; na kwa kudhaminiwa na wote ujira hulazimika basi huwa ni yao pamoja kama dhamana ni yao. Hakuna mmoja wao anayeweza kujiwakilisha na mwengine kama mshirika na mwili wake, kama hakuna mmoja anayeweza kumwaajiri mtu mwengine kama mfanyikazi atakaye kuwa mshirika kwa mwili wake. Hino ni kwa sababu mkataba imetukia juu yake khasa basi ni lazima yeye mwenyewe asimamie kazi moja kwa moja kwa sababu mshirika kiwiliwili ni yeye na amehusishwa katika shirika. Lakini yajuzu kumwaajiri mmoja wao kama mfanyikazi na hapo kuajiriwa itakuwa kutoka shirka na kwa ajili ya shirika hata kama mmoja wa washirika huisimamia wala sio kama wakili wake au mfanyikazi wake. Tasarruf ya kila mshirika ni tasarruf ya shirika

na kila mmoja wao hulazimika na zile kazi mshirika wake alizikubali.

Shirika hili lajuzu kwa yaliosimuliwa na Abu Dawud na Al-Athram kwa isnadi zao kutoka Abu Ubaid kutoka Abdulla bin Masoud aliesema: “**Nilishiriki mimi, Ammar bin Yasar na Sa'd bin Abi Waqqas kwa yale tatakaonali katika vita vya Badri. Basi S'ad alikuja na watekwa wawili ilhali mimi na Ammar hatukuja na chochote.**” Na Mtume (SAW) alikiri waliotenda. Na Ahmad bin Hanbal alisema: “**Mtume (SAW) alishirikisha baina yao.**” Hadithi hino ni wazi katika kushiriki jamii ya masahaba kwa miwiliwili yao kwa kazi wanoitekeleza, nayo ni kupigana na maadui na kugawanya wanaonali katika ngawira baina yao lau wanafaidika katika uwanja wa vita. Imma wanaosema ya kwamba hukmu ya ghanima huhalifu shirika hili, hino haikuja katika hadithi hino kwa sababu hukmu ya ngawira iliteremka baada ya vita hivi vya Badri basi hukmu ya ngawira haikweko pindi ilipotekea shirika hili. Na hukmu ya ngawira iloteremka baadaye haikufuta shirika iliotokea, bali iliabinisha tu fungu za ngawira; basi hukmu ya shirika la kiwiliwili hubakia kuthibitishwa na hadithi hino.

Shirika la Mudharaba

Pia huitwa “*qaradh*” nayo ni kushiriki mwili na mali. Maana yake ni mtu kutoa mali yake kwa mwengine ili afanye biashara nayo kwa sharti faida inaopatikana igawanye baina yao kulingana na walivyokubaliana. Lakini hasara katika mudharaba haifuati makubaliano ya washirika bali yaliokuja katika Shar'a. KiSheria hasara katika mudharaba hutukia mali tu wala haimtukii mwenye kushiriki kiwiliwili tu. Hata lau mwenye mali na mshiriki kimwili wakubaliane kwamba faida na hasara ni baina yao, faida itakuwa baina yao na hasara juu ya mali. Hii ni kwa sababu shirika ni kuwakilisha na hukmu ya wakili ni kwamba yeche hadhamini, na hasara humtukia mwenye kuwakilisha tu. Abdurazaq amesimulia katika ‘*Al-Jami*’ kutoka Ali (RA) aliesema: “**Hasara ni juu ya mali, na faida ni walivyokubaliana.**” Mwili haupati hasara ya kimali bali

huhasirika ile juhudini iliotumia tu; basi hasara hutukia juu ya mali.

Mudharaba haiswihi mpaka mali isililimishwe kwa mtendakazi na kumwacha nayo kwa sababu mudharaba hulazimisha kusilimishwa mali kwa mwenye kutenda kazi. Na mudharaba hulazimu kukadiri fungu la mtendakazi, na mali ambao mudharaba imesimama juu yake iwe ni kiwango maalumu. Wala haiswihi mwenye mali kufanya kazi pamoja na mudharaba na haitoswihi ikishurutishwa kwa sababu hamiliki tasarruf na mali iliotiwa katika shirika. Wala mwenye mali hamiliki tasarruf yoyote katika shirika bali mshirika kimwili ndio mwenye kutasarruf, kufanya kazi na kuwa na mkono juu ya mali. Hii ni kwa sababau mkataba wa shirika imetukia juu ya mali wa mshirika kimwili pamoja na mali ya mwenye mali, wala haikutukia juu ya mwili wa mwenye mali; basi yeze huwa ni kama mgeni kwa shirika asiyemiliki tasarruf yoyote humo. Lakini mshirika kimwili hufungika kwa ile tasarruf alioruhusiwa na mwenye mali wala haruhusiwi kuihalifu kwa sababu atasarruf kwa ruhusa. Lau aruhusiwa kufanya biashara ya sufi tu au amzuia kusafirisha bidhaa baharini, (mwenye mali) aweza kufanya hivo. Lakini haimaanishi kwamba mwenye mali atasarruf katika shirika bali ni kwamba mudharaba afungwa ndani ya mipaka alioruhusiwa na mwenye mali. Juu ya hayo tasarruf katika shirika hufungika kwa mtendakazi tu wala mwenye mali hana uwezo wowote katika tasarruf.

Na katika mudharaba ni kushirikisha mali mbili na mwili wa mmoja wao. Kwa hivyo lau kuna elfu tatu, mmoja wao ni elfu na mwengine ni elfu mbili kisha mwenye elfu mbili amruhusu mwenye elfu moja kutasarruf nazo kwa sharti faida iwe baina yao, shirika itaswihi na mtendakazi ni mwenye elfu moja na mwenye mali ni mwenye elfu mbili ambaye ni mshirika wake. Kadhalika katika mudharaba ni kushiriki mali mbili na mwili wa mwengine asiyekuwa mmoja wao; hizi zote huingia katika mlango wa mudharaba.

Mudharaba yajuzu kiSheria kwa sababu imesimuliwa “**kwamba Al-Abbas bin Abdulmuttalib alikuwa akitoa mali kimudharaba na kushurutisha shuruti maalumu. Haya yalimfikia Mtume (SAW) naye akayaona kuwa ni sawa.**” Na Ijma as-Sahaba imesimama juu ya kuruhusu mudharaba. Na ibn Abi Sheeba amesimulia kutoka Abdulla bin Hamid kutoka babake kutoka babu yake “**kwamba Umar bin Al-Khattab alimpa mali ya yatima kimudharaba. Akaifanyia bidii na kufanikiwa, basi Al-Fadhl akaigawanya**” Na ibn Qudama alitaja katika ‘*Al-Mughni*’ kutoka Malik bin Al-‘?Ala bin Abdurrahman kutoka babake kutoka babu yake “**kwamba Uthman alifanya qaradh na yeye.**” Na pia alitaja kutoka ibn Masoud na Hakim bin Hazzam “**kwamba walifanya qaradh pamoja.**” Na hayo yalikuwa mbele ya macho ya masahaba wala haikupokewa yoyote kuihalifu au kuipinga, basi hino ikawa ni **ijma yao** juu ya mudharaba.

Shirika la Nyuso (Al-Wujooh)

Hino ni watu wawili kushiriki na mali ya mtu mwengine yaani mtu mmoja atoe mali yake kwa wawili au zaidi kimudharaba. Kwa hivyo wawili watakuwa washirika kiwiliwili wanaoshiriki katika faida katika mali ya mtu mwengine. Wanaweza kukubaliana kugawanya faida kithuluthi, kila mmoja katika wawili apate thuluthi na mali ipate thuluthi; au wakubaliane kuigawanya kirobo ili mali ipate robo, mmoja wa wawili apata robo na wa pili apate nusu. Au wanaweza kukubaliana juu ya shuruti nyengine. Kwa shuruti hizi zinazoweza kutokea yamkinika faida igawanye kitofauti baina ya washiriki kiwiliwili ili kushiriki kwao iwe kwa fungu tofauti kutegemea uso ya mmoja wao au wawili imma kwa ajili ya uhodari wake katika kazi au uhodari wake katika kutasarruf kiidara juu ya kwamba tasarrufa ya kiSherika wanaoimiliki ni katika mali moja. Kwa hivyo shirika hino huwa ni kigawanyo cha sampuli ya shirika tofauti na shirika ya mudharaba juu ya kwamba hakika yake yaregelea mudharaba.

Katika shirika la nyuso ni kushiriki wawili au zaidi kwa wanaoyanunua kupidia wanabiashara kuwaamini na nyuso zao

zinazotegemea imani hino pasina wao kuwa na rasilimali. Wanakubaliana kwamba kumiliki kwao kwa yale wanaonunua itakuwa kinusunusu, kithuluthi, kirobo nk. Kisha wanauza bidhaa hizo na kugawanya wanachopata kinusunusu, kithuluthi, kirobi nk kutegemea walivyokubaliana wala si kutegemea wanavyomiliki bidhaa. Amma hasara, hino itakuwa kwa mujibu ya kumiliki kwao bidhaa kwa sababu hio ni kama mali zao wala sio kwa mujibu ya walivyokubaliana juu ya hasara wala kwa mujibu ya faida, sawa sawa ikiwa faida baina yao ni kwa mujibu ya bidhaa zao au tofauti na hayo.

Shirika la nyuso kwa vigawanayo vyake yaruhusiwa kwa sababu wakishiriki kwa mali ya mwengine itakuwa sampuli ya shirika ya mudharaba ilithubutu kupertia Sunna na Ijma. Na wakishiriki kwa wanaochukua kutoka mali ya mtu mwengine yaani wanaonunua kupertia nyuso zao na imani ya wanabiashara juu yao, itakuwa ni sampuli ya shirika la kimwili iliothubutu kupertia Sunna. Kwa hivyo shirika la nyuso imethubutu kupertia Sunna na Ijma.

Lakini ni lazima ijulikane kwamba maana ya imani hapa ni imani ya kimali nayo ni imani ya kulipwa (deni) wala sio kuwa na jaha au kujulikanwa kwao. Kwa hivyo mtu aweza kuwa ni mwenye jaha lakini haaminiwi kupia basi haaminiwi kimali wala hatambuliwi kuwa na imani katika mambo ya biashara na shirika. Aweza kuwa ni waziri au tajiri mkubwa lakini haaminiwi kulipa basi haaminiwi kimali wala kuaminiwa na chochote; hawezi kununua bidhaa bila kulipa bei zake. Na mtu mwengine aweza kuwa maskini lakini wanabiashara wanaamini uweza wake kuwalipa basi anaweza kununua bidhaa bila kulipa bei zake. Kwa hivyo shirika la nyuso hutegemea imani ya kulipa wala sio jaha. Basi yanaotokea katika baadhi ya shirika ya kumwingiza waziri kama mwanachama wa shirika, kumpa fungu maalumu katika faida bila kuchangia mali yoyote au kushirika na juhud yoyote ila kushiriki kwake na daraja yake katika mujtama ili kusahilishia kazi za shirika; hino sio katika sampuli ya shirika la nyuso wala taarifa ya shirika katika Uislamu haitabikishwi juu yake. Sampuli hino ya shirika

hairuhusu wala mtu huyu hatakuwa mshirika wala si halali kwake yeze kuchukua chochote kutoka shirika hino.

Na yanaotokea katika nchi kadha kama Saudia na Kuwait ya kuwa asiyekuwa msuudi au mkuwaiti hana ruhusa kufanya biashara au kazi basi humwingiza msaudi humo Saudia au mkuwaiti humo Kuwait na kumpa fungu katika faida bila msaudi huyu au mkuwaiti huyu kulipa mali au shirika kufungwa juu ya mwili wake; bali huhisabiwa mshirika kwa sababu ya ruhusa iliochukuliwa kwa jina lake na kupewa fungu la faida kwa ajili ya hiyo. Hino pia sio katika shirika la nyuso wala sio shirika inaoruhusiwa kiShar'a. Na msaudi huyu au mkuwaiti huyu hahisabiwi kuwa mshirika wala si halali kwake kuchukua chochote kutoka shirika hino kwa sababu hamiliki shuruti ziliowajibishwa na Shar'a kumilikiwa na mshirika ili awe mshirika kiShar'a nayo ni kushirika kimali au kimwili au imani ya kulipa ya kibiashara ili yeze mwenyewe asimamie kazi kwa yale anaochukua katika bidhaa kutegemea imani hino.

Shirika la Masikizano (*Al-Mufawadha*)

Hino ni kushiriki washirika wawili katika jumla za sampuli za shirika zilizotangulia kutajwa, mfano wajumuisha wawili baina shirika la *al-'inan*, viwiliwili (*al-abdan*), mudharaba na nyuso (*al-wujooth*). Hino ni kama mtu kutoa mali kwa wahandisi wawili kushiriki pamoja nayo kimudharaba ili hawa wawili wajenge nyumba kuuza na kufanya biashara nazo, na wakubalie hao wawili kufanya kazi na zaidi na walizo nazo ya mali kwa kuchukua bidhaa bila kulipa bei zake moja kwa moja kutegemea imani wanabiashara walio nayo juu yao. Kushiriki wahandisi wawili pamoja na miwiliwili yao ni shirika la *al-abdan* kulingana na kujenga kwao, na kulipa kwao mali kutoka mali zao kufanya kazoo nazo ni shirika la mudharaba, na kushiriki kwao katika bidhaa wanazozinunua kutegemea imani ya wanabiashara juu yao ni shirika la nyuso; basi shirika hino imejumuisha kila sampuli ya shirika katika Uislamu basi yajuzu kwa sababu kila mojawapo yajuzu kipekee basi yajuzu pamoje na mwenzake. Faida ni walivyosikizana kwa hivyo yajuzu faida iwe kwa mujibu ya mali, na yajuzu faida iwe sawa juu ya tofauti

zao kuchangia mali au kutofautika juu ya kuwa sawa katika kuchangia mali.

Sampuli hino ya shirika ya masikizano yajuzu kwa kuja nasi juu yake. Amma iliotajwa na baadhi ya mafuqaha katika sampuli nyengine za shirika la masikizano kama watu wawili washiriki kwa kuwa sawa katika mali, tasarruf na deni hadi kila mmoja amwakilishe mwengine juu ya haya yote bila kizuizi, hino haijuzu kabisa kwa sababu haikuja nasi ya kiSheria kama dalili juu yake. Na kwa sababu hadithi wanaoshuhudia nayo: “**Mukisikizana, sikizaneni vizuri**” au: “**Sikizaneni kwa sababu hiyo ina baraka zaidi**”; haikusihi yoyote katika hadithi hizi mbili wala maana zake lau mtu adhania mafhumu yake yamesihi. Isitoshe hino ni shirika juu ya mali isiojulikana na vitendo visiojulikiana, na hino pekee yake yatosha kutosihi shirika hino. Na pia mionganini mwa mali yake ni mirathi inaowawasilia baada kufa mwenye kurithiwa ilhali mmoja wao aweza kuwa dhimmi kwa hivyo vipi atapewa fungu katika mirathi? Kadhalika shirika hukusanya maana ya kuwakilisha na kuwakilisha juu ya kisicho julikana jinsi yake haijuzu. Kwa hivyo yote haya huleta maana ya kutosihi sampuli hino la shirika la masikizano.

Kuvunja Shirika

Shirika ni katika mikataba yanaoruhusia kisheria. Itabatilishwa kwa kufa mmoja wa washirika wawili, uwendazimu wake, kufungiwa mmoja kutotasarruf kwa sababu ya usafihi wake au kuvunjwa na mojawapo wa washirika wawili ikiwa shirika imeundwa na washirika wawili kwa sababu hino ni mkataba unaojuzu basi hubatilishwa na hayo kama kuwakilisha. Akifa mojawapo wa washirika wawili naye ana mrathi anayefaa anaweza kusimamia shirika na kuruhusiwa na mshirika kutasarruf; auaweza kudai mgawanyiko. Akiomba mojawapo wa washirika wawili kuvunja shirika, mshirika mwenzake lazima ajibu ombi hilo. Wakiwa washirika ni wengi kushinda wawili na mojawapo aomba kuvunja shirika ilhali waliobaki wapendelea kubakia kwake, shirika iliokweko huvunjwa na itaundwa upya baina waliobakia. Lakini hutofautishwa baina

kuvunjwa shirika baina shirika la mudharaba na nyenginezo. Katika shirika la mudharaba, akiomba mwenye bidii kuuza na mwenye mali atake kugawanya, ombi na mwenye bidii huitikiwa kwa sababu haki yake ipo katika faida wala faida haitopatikana ila katika kuuza. Amma katika shirika zilizobakia, mmoja akiomba mgawanayo na mwengine aombe kuuza, ombi la kugawanya huitikiwa badala la ombi la kuuza.

14 MASHIRIKA YA KIRASILIMALI

Shirika katika nidhamu za kirasilimali ni mkataba inaodhamini kuwalazimu watu wawili au zaidi kushiriki katika mradi wa kimali kwa kuchangia hisa ya kimali au kitendo ili kugawanya yanaotokea ya faida au hasara kutoka mradi huu. Nazo ni vigawanyo viwili: Shirika za watu, na shirika za mali.

Amma shirika za watu, hizo ndizo zinazodhirisha upande wa kibinadamu aliye na athari katika shirika na katika kupima thamani ya kihisa. Hiyo ni kama shirika la kudhamamiana (*tadhaamun*) na shirika la (*at-tawsiyya al-baseeta*). Tofauti na shirika za kimali ambazo upande wa kibinadamu haupo wala hautambuliwi au kuwa na athari yoyote. Bali husimama juu ya kupotea kuwepo upande wa kibinadamu na kubakia upande wa kimali kipekee katika kuunda shirika na kuipeleka; hizo ni kama shirika la hisa na shirika la (*tawsiyya al-asham*).

Shirika la Kudhaminiana Kikamilifu (Unlimited Liability Partnership)

Hino ni shirika baina watu wawili au zaidi wakiwafikiana kufanya biashara pamoja kwa jina maalumu, na kila mmoja wao hulazimika na deni za shirika juu ya mali zao zote kwa kudhaminiana bila kizuizi chochote. Kwa hivyo hawezi mshirika wowote kurudi nyuma katika haki zake kwa mtu mwengine ila kwa ruhusa ya washirika waliobakia; na shirika huvunjwa kwa kifo cha mmoja wa washirika, kuzuiliwa kwake na kutumia mali yake kwa sababu ya ubadhifuru au kafilisika kwake madamu hakuna makubaliano yanaokhalifiana na hayo. Wanachama wa shirika hino wanadhamini katika ahadi yake mbele yaw engine kutekeleza kila ahadi ya shirika na

mas'uliyya yao juu ya hayo hayana kikomo; kwa hivyo kila mshirika aweza kudaiwa kulipa deni zote za shirika si tu kutoka mali za shirika bali kutoka mali yake pia. Kwa hivyo ni lazima atimize na mali yake binafsi kilichopunguka kutoka deni za shirika baada shirika kutumia mali zake. Na shirika hili halikubali kupanuliwa mradi, na huundwa na watu wachache ambao kila mmoja amuamini mwenziwe na kumjua kikamilifu. Na kitu muhimu zaidi ndani yake ni shakhsiya ya shirika, si kwa kuwa kwake mwili tu bali kupitia nafasi yake ya kimsingi na athari yake katika mujtama.

Shirika hino ni fisidifu kwa sababu shuruti zilizotajwa ndani yake huhalifu shuruti za shirika katika Uislamu. Hii ni kwa sababu hukmu ya kiSheria haishurutishi kwa mshirika ila kuwa aruhusiwa kutasarruf tu. Na pia shirika laweza kupanua amali zake basi wakikubaliana washirika kupanua shirika imma kwa kuzidisha rasilimali zao au washirika wengine, wana uhuru wa kutasarruf na kufanya wanavyopenda. Na kwa sababu washirika hawana mas'uliyya wa kibinafsi ila kulingana na hisa yao ndani ya shirika, na pia mshirika ana haki kuwacha shirika wakati wowote anapopenda pasina haja ya mwafaka wa washirika. Na shirika haivunjwi kwa kifo cha mmoja wa washirika au kufungiwa kwake kutotasarruf bali kushiriki kwake pekee yake humalizika na shirika la washirika waliosalia hubaki ikiwa imeundwa na zaidi ya wawili. Hizi ni shuruti za kiSheria ilhali shuruti za shirika la kudhaminiana huhalifu shuruti hizo bali ni kinyume nazo basi huifanya shirika fisidifu na hajuzi kushiriki nayo kiSheria.

Shirika la Hisa (Limited Liability Company)

Shirika za hisa ni shirika inaoundwa na washirika ambao hawajulikani na jumla ya watu. Mwanzilishi wa shirika la hisa ni kila aliosahihisha mkataba wa kuanzilisha shirika kwa sababu mkataba wa kuanzilisha ndio huunda baina wenye kuisahihisha mafungamano/ahadi za kufanya kazi ili kuhakikisha lengo la ushirikiano nayo ni shirika. Kujiandikisha kwa shirika ni mtu kujihusisha na mafungamano kwa kununua hisa moja au zaidi katika mradi wa shirika kwa kulipa bei yako ya kutajwa. Nayo

ni mfano wa tasarruf kwa matakwa ya mtu mmoja yaani hutosheleza mtu kununua hisa ili kuwa mshirika pasina kujali kuridhia washirika waliobakia au la. Kujiandikisha hutokea kupitia mbinu mbili: Mwanzo huwahusisha waanzilishi wa hisa za shirika wakizigawanya baina yao bila kuziuba kwa watu jumla; hiyo (kupitishwa) kanuni ya kupangia nidhamu ya shirika inaokusanya shuruti zitakaopeleka shirika, kisha kuisahihisha baina yao. Kila mwenye kusahihisha kanuni huchuliwa ni mwanzilishi na mshirika, na pindi wote wanapoisahihisha ndipo shirika imeanzilishwa. Mbinu ya pili ya kujiandikisha nayo ndio ilioenea ulimwenguni ni baadhi ya watu kusimama kuanzilisha shirika, kupanga nidhamu kisha kuuza hisa moja kwa moja kwa watu jumla ili kujiandikisha. Kisha inapotimia kipindi cha kujiandikisha katika shirika, mkutano wa kuanzilisha shirika huitwa ili kuangalia suala la kupitisha nidhamu ya shirika na kuteuwa kikao lake la usimamizi. Kila mshirika ana haki kuhudhuria mkutano wa kuanzilisha pasina kujali idadi ya hisa zake, hata lau amiliki moja tu. Shirika huanza kazi yake inapomalizika wakati uliopangwa kufunga nafasi ya kujiandikisha.

Mbinu zote mbili ni sura moja nayo ni kulipa mali. Wala shirika halichukuliwi kuwa limesihi ili kwa kumaliza waanzilisha kusahihisha katika mbinu ya kwanza, na kwa kumalizika kipindi cha kujiandikisha katika mbinu ya pili. Mkataba wa shirika ni mkataba baina mali tu wali upande wa kibinadamu haina nafasi yoyote; mali ndizo zenye kushirika wala sio wenye kumiliki mali. Hizi mali zashiriki bila kuwepo upande wa kibinadamu kwa hivyo hana mshirika wowote—pasina kujali idadi ya hisa zake—kutawala vitendo vyta shirika kwa sifa yake kama mshirika, wala kufanya kazi ndani yake au kupeleka chochote katika vitendo vyake kwa sifa yake kama mshirika; bali mwenye kutawala vitendo vyta shirika, kufanya kazi ndani yake, kupeleka na kusimamia vitendo vyake vyote ni mtu anayeitwa mudiri aliyechaguliwa aliyeetuuliwa na kikao cha idara. Kikao hichi cha idara huchaguliwa na mkutano wa kijumuiyya (general meeting) ambayo kila mshirika ana kura kulingana na mali anayomiliki wala sio sifa yake ya kibinagsi kwa sababu mshirika ni mali

inayopanga idadi ya kura. Kila hisa ina kura wala sio kila mtu kuwa na kura; hakuna upande wa kibinadamu katika shirika ya hisa bali muhimu ni rasilimali tu. Shirika ya hisa ni ya kudumu wala haifungwi na uhai wa watu; mshirika aweza kufa bila kuvunja shirika na aweza kufungwa kutotasarruf ilhali shirika litabakia. Amma rasilimali ya shirika, hino hugawanya kwa idadi ya hisa na thamani zinazolingana zinazoitwa ‘hisa’ (shares). Mshirika mwenye hisa ha(*taqtasiyy*) sifa yake ya binadamu na mas’uliyya yake ina kikomo kulingana na hisa zake katika rasilimali basi washirika hawafungwi na hasara ila kwa kiwango cha hisa zao ndani yake. Aweza kuzungusha hisa yake; aweza kuiuza na kumshirikisha mwengine ndani yake bila ruhusa ya washirika waliosalia. Hisa zinazomilikiwa na kila mtu ni karatasi za kimali zinazowakilisha rasilimali; zinaweza kuwa kwa majina au kwa mwenye kuibeba, nazo hunukuliwa kutoka milki ya mtu kwa mwengine. Tajiri anayeandikishwa katika hisa halazimishwi ila kulipa thamani yake iliotajwa; hisa ni sehemu isioweza kutenganishwa katika umbo la shirika wala sio sehemu ya rasilimali yake. Karatasi za kimali ni mfano wa karatasi iliosajiliwa katika hisa hino, na thamani yake si moja bali hubadilika kulingana na faida au hasara ya shirika. Faida au hasara hino si moja kwa kila mwaka; yaweza kuhalifiana au kutofautika. Kwa hivyo hisa haiwakilishi rasilimali inaolipwa kuanzisha sherika, bali huwakilisha rasilimali ya shiriki pindi inaponunuliwa yaani katika wakati maalumu; basi huwa kama karatasi ya pesa ambao bei yake huanguka ikiwa soko la hisa limerudi nyuma, na hupanda pindi soko la hisa limepanda. Baada shirika kuanza kazi, hisa hupoteza sifa yake kuwa rasilimali na hugeuka kuwa karatasi ya pesa na thamani maalumu inaopanda na kushuka kulingana na soko, kulingana na faida au hasara ya shirika, au kulingana na watu kuitaka au kutoitaka. Basi huwa ni bidhaa inaonyenyekea soko la kuuzwa na kutakikana. Hisa hunukuliwa baina mikono ya watu kama karatasi za pesa hunukuliwa baina yao bila haja ya kuandikisha katika makaratasi za shirika ikiwa hisa humilikiwa na mwenye kuzibeba, au kwa kuandikishwa na shirika ikiwa hisa zinabeba jina la mshirika.

Shirika huchukuliwa ni yenyе faida ikiwa mali za shirika huzidi mali ya madeni yake ikipita mwaka; inaozidi ndio faida. Faida hugawanywa kila mwaka baada kupita mwaka wa kimali wa shirika; thamani za mali za shirika zikipanda kwa sababu ya dhurufu zisizotarajiwa bila kuwepo faida, haizuiliwi kugawanya ziada hino. Lakini yaktokea kinyume na hayo na thamani za mali za shirika kushuka ilhali shirika limepata faida lakini faida hino ikiunganishwa na thamani ya mali yake baado haizidi thamani ya madeni yake, hakuna nafasi ya kugawanya faida. Pindi faida inapogawanywa, huhifadhiwa fungu la faida kama akiba na yaliosalia hugawanywa baida washirika. Shirika hutambuliwa kama mtu binafsi kikanuni (corporate personality) ilio na haki ya kudai na kudaiwa kwa jina lake binafsi mbele ya mahakama kama ina eneo rasmi la kuketi na jinsi maalumu ya kitaifa. Hakuna mshirika au mwanachama wa idara ya shirika anayezungumza kwa niaba ya shirika, si kwa sifa yake kama mshirika au ya kibinafsi, bali mwenye uwezo huo ni aliye wakilishwa na shirika kuzungumza kwa jina lake. Kwa hivyo mwenye kutasarruf ni shirika yaani shakhsiya ya ya kimajazi ya kikanuni (corporate personality) wala sio mtu binafsi mwenyewe anaye tasarruf.

Hino ndio shirika la hisa, na ni mionganii mwa shirika batili kiSheria na ni katika vitendo vya maingiliano asieruhusiwa Muislamu kutenda. Amma sababu za ubatili wake na uharamu wa kushirika ndani yake, hino hubainishwa na yanaofuata:-

1:- Istilahi ya shirika katika Uislamu ni: Mkataba baina wawili au zaidi wanaokubaliana ndani yake kusimamia kitendo cha kimali kwa lengo la faida. Ni mkataba baina wawili au zaidi kwa hivyo haisihi mwafaka wa upande mmoja tu; bali lazima kuwepo mwafaka baina upande mbili au zaidi. Mkataba huo lazima utegemee kusimamia amali ya kimali kwa lengo la faida. Hairuhusiwi kutegemea kulipa mali tu wala haitoshi kwamba lengo ni kushirikiana tu. Kusimamia amali ya kimali ndio msingi wa mkataba wa shirika, na kusimamia amali ya kimali imma kutoma watu wawili wenye kukubaliana au mmoja wao na mali ya mwenzake. Wala mkataba hauwezi kuwa baina yao

ili mwengine asimamie amali ya kimali kwa sababu haitokuwa mkataba wala haitomfunga yoyote. Mkataba humfunga mwenye kujiingiza katika mkataba na huhusisha tasarruf zake yeye wala sio mwengine, kwa hivyo ni lazima usimamizi wa amali ya kimali ifungwe baina wale wawili wenyе kujiingiza katika mkataba imma baina yao au mmoja wao na mali ya mwengine. Na kwa kuwa kusimamia amali ya kimali kupitia mmoja wa wale wawili wenyе kujiingiza katika mkataba ni jambo la kilazima—ili kutimie kusimama shirika na kuwepo kwake—hino hulazimisha kwamba hakuna budi kuwepo mwili katika shirika inotukia mkataba juu yake. Kuwepo mwili ni shuruti ya shirika katika Uislamu, nalo ni jambo la kimsingi katika kusimamisha shirika. Mwili ukiwepo ndipo shirika litasimama, na lau hakuna mwili basi shirika halisimami wala kuundwa kimsingi.

Warasilimali hutambua shirika la hisa kama mkataba inaolazimisha kufungwa watu wawili au zaidi kushiriki katika mradi wa kimali kwa kutanguliza hisa za mali ili kugawanya faida au hasara inaotokamana na mradi huu. Kutoka istilahi hino, na kutoka uhakika wa shirika kupitia mbinu zake mbili zilizotangulia, hubainika kwamba hiyo si mkataba baina watu wawili au zaidi kulingana na hukmu za Sheria ya Kiislamu. Hino ni kwa sababu mkataba kiSheria ni mtu kutaka na mwengine kukubali baina watu wawili au zaidi yaani hakuna budi kuwepo upande mbili katika mkataba: Mmoja wao akisimamia kutaka kwa kuanza kuvutia kwa mkataba kwa kusema kimfano: ‘Nimekuowa’, ‘Nimekuuzia’, ‘Nimekukodishia’, ‘Nimekushirikisha’, ‘Nimekupa zawadi’ au mfano wa hayo. Na mwengine asimamia kukubali kwa kusema kimfano: ‘Nimekubali’, ‘Nimeridhia’ au mfano wa hayo. Mkataba ukikosa kuwepo upande mbili, au kukosa kutaka na kukubali, haitopita wala haitoitwa mkataba kiSheria. Imma katika shirika la hisa, waanzilishi hukubaliana juu ya shuruti za shirika wala hawajiingizi moja kwa moja kivitendo katika ushirikiano pindi wanakubaliana juu ya shuruti za shirika; bala wanasisizana na kukubaliana juu ya shuruti tu. Kisha wanachora maandishi ambayo ni nidhamu ya shirika, kisha baada hapo

husahihishwa maandishi haya na kila mwenye kutaka kushirika ikichukuliwa kusahihisha kwake tu ndio kukubaliana nayo. Hapo ndipo atahisabiwa ni mwanzilishi na mshirika yaani ushirikiano wake hutimia kwa kutima kusahihisha au kumalizika wakati wa kujiandikisha. Hino ni wazi ya kwamba hakuna upande mbili zilizopitisha mkataba pamoja, wala hakuna kutaka na kukubali. Bali ni upande mmoja inaokubaliana juu ya shuruti na kwa kukubali kwake hubadilika kuwa ni mshirika. Shirika la hisa si mwafaka baina wawili, bali ni mwafaka kutoka wa mtu mmoja tu juu ya shuruti. Kwa hivyo wanauchumi wa kirasilimali, na wanasheria wa kimagharibi, husema kwamba kujifunga nayo ni mfano wa tasarruf kupitia matakwa ya mtu mmoja tu. Matakwa ya mtu mmoja ni kila mtu anaojifunga na jambo kutoka upande wake mbele ya jumla ya watu au mtu mwengine, pasina kujali kukubali au kutokubali wale watu wengine au yule mtu mwengine kama mfano wa ahadi ya kutoa zawadi. Shirika la hisa kwao wao na katika uhakika wake humfunga mshirika, mwanzilishi au msahihishi wa maandishi kwa shuruti ziliomo, pasina kujali kuwepo mwengine aliokubali au la; na wameihisabu mfano wa tasarruf kwa matakwa ya mtu mmoja. Kwa hayo mkataba wa shirika la hisa ni mkataba wa matakwa ya mtu moja ambayo ni mkataba batili kiSheria kwa sababu mkataba kiSheria ni kufungamanisha kutaka iliotokamana na mmoja wa wanaofunga mkataba pamoja na kukubali mwenzake kwa sura inaodhihirisha athari yake katika yale waliokubaliana juu yake. Mkataba wa shirika la hisa haijatekeleza haya. Haijatokea ndani yake makubaliano baina watu wawili au zaidi, bali humfunga tu kwa mujibu yake mtu mmoja kushiriki katika mradi wa kimali. Na kiasi wanavyozidi wenye kujifunga na washirika, huchukuliwa kwamba mwenye kujifunga ni mtu mmoja. Yaweza kusemwa kwamba washirika wamekubaliana juu ya shuruti za shirika kwa hivyo makubaliano yao huchukuliwa kuwa kutaka na kukubali, na kuandika maandishi huchukuliwa kama jambo rasmi tu kusajili mkataba waliokubaliana juu yake. Kwa hivyo kwa nini haiitwi mkataba?

Jibu lake ni kuwa washirika wanakubaliana baina yao juu ya shuruti za shirika, lakini kwa mujibu wa makubaliano yao hawajihisabu kwamba wameshiriki kivitendo wala hawajafungwa na makubaliano juu ya shuruti. Bali yajuzu kwa kila mmoja wao kuwacha na kutoshiriki baada makubaliano juu ya shuruti na baada kuandikwa maandishi. Hafungwi na makubaliano juu ya shuruti kulingana na istilahi zao na makubaliano yao ila baada kusahihisha maandishi. Anaposahihisha maandishi ndipo huwa amefungwa, amma kabla ya hapo hajafungwa na chochote. Kwa hayo makubaliano yao juu ya shuruti kabla kusahihisha maandishi haihisabiwi kuwa ni mkataba baina yao. Na pia si mkataba kiSheria kwa sababu makubaliano juu ya shuruti za ushirikiano, na juu ya kushirikiana, haihisabiwi kuwa mkataba wa shirika kwa sababu kulingana na makubaliano yao hawafungwi nayo kabla kusahihisha ilhali mkataba ni kile kinachowafungwa wenye kukubaliana juu yake. Kwa hivyo makubaliano yao juu ya shuruti za shirika, na juu ya kushirikiana, kutaka na kukubali, basi haichukuliwi kama mkataba kwa mujibu ya hukmu za Sheria pasina hata kutaja kwamba wao wenyewe hawaichukui kama mkataba.

Mtu aweza kusema kwamba mshirika kukubali kusahihisha mkataba huchukuliwa kama kutaka kwake kwa mwengine, na kusahihisha anayemfuata huchukuliwa kama kukubali; kwa hivyo kwa nini haichukuliwa kupewa maandishi ni kutaka na kusahihisha ni kukubali? Jibu lake ni ni kwamba kila mshirika aliyesahihisha atakuwa amekubali tu basi ni kukubali, na kutaka haikufanywa na mtu yoyote maalumu yaani kutaka haitokei kutaoka mtu yoyote maalumu. Hakuna mwenye kutaka, sio waanzilishi wala msahihishi wa kwanza, bali inaopatikana ni kukubali kutoka kila mshirika. Msahihishi akubali shuruti na kujifunga nazo kibinagsi pasina mtu yoyote mwenye kutaka kutasarruf kwa kutaka kwa yoyote yaani bila mtu yoyote kumwambia: ‘Nimekushirikisha.’ Amma kupewa kwake maandishi kusahihisha haihisabiwi kuwa ni tasarruf ya kutaka. Kwa hayo hakika ya shirika la hisa ni kwamba kila mshirika ndani yake amekubali tu, na kukubali pamoja na kukubali

haichukuliwi kuwa mkataba kiSheria. Bali hakuna budi kuwepo kutaka kupidia maneno yanaomaanisha kutaka wala sio kukubali. Kisha ije kukubali kwa maneno yanaomaanisha kukubali. Kwa hivyo hatambuliwi mtu yoyote aliye sahihisha maandishi ya shirika kama (*mujeeb*), bali kila mmoja atambuliwa kama mwenye kukubali. Shirika litakuwa limesimama juu ya kukubali bila kutaka kwa hivyo haijasimama.

Warasilimali huita maandishi ya shirika yaani nidhamu yake jina la mkataba, na husema: ‘Mkataba umepita.’ Amma kiSheria, maandishi haya hayatambuliwi kama mkataba. Bali mkataba ni kutaka na kukubali baina upande mbili, kwa hivyo shirika la hisa halitambuliwi kama mkataba kiSheria.

Isitoshe, mkataba huu haujakusanya mwafaka juu ya kusimamia amali ya kimili kwa ajili ya faida, bali mwanzilishi au mwandishi amewafiki juu ya kulipa mali katika mradi wa kimili. Kwa hivyo iko tupu ya msingi wa makubaliano juu ya kusimamia kazi. Bali ilioko ndani yake ni mtu mmoja kujifunga kibinafsi kulipa mali tu pasina kuhimiza kazi katika kujifunga hivi. Na kwa sababu kusimami kazi ya kimili ni lengo katika shirika wala sio kushirikiana tu, mkataba kukosa makubaliano juu ya kusimamia kazi hubatilisha mkataba. shirika haliundwi kwa kukubaliana juu ya kulipa mali kwa kukosekana makubaliano juu ya kusimamia amali ya kimili, na kwa hayo shirika ni batili pia.

Yaweza kusemwa maandishi ya shirika yamekusanya sampuli ya amali ambayo itasimamiwa kama kazi ya kutengeneza sukari, biashara nk kwa hivyo imetokea makubaliano juu ya kusimamia amali ya kimili. Jibu lake ni kuwa sampuli ya amali iliotajwa ni kazi shirika litasimamia, lakini haijatokea makubaliano juu yake kutoka upande za washirika. Wao wamekubaliana juu ya kushiriki na shuruti za kushiriki tu, na kuwacha usimamizi wa amali kwa shakhsiya wa kikanuni ambayo itakuwa ndio shirika baada kubuniwa kwake. Kwa hivyo, haijatokea makubaliano baina ya washirika juu ya wao wenyewe kutenda amali ya kimili.

Juu ya hayo, shirika katika Uislamu hushurutishwa kuwepo mwili yaani kuwepo mtu mwenye kutasarruf kwani maana ya mwili katika shirika, biashara, kuajiri na yaliosalia katika mikataba ni mtu mwenye kutasarruf wala sio kiwiliwili au juhudi. Kuwepo mwili ni kiungo cha kimsingi katika kusimamishwa shirika. Mwili ukiwepo, shirika husimama na ukikosekana katika shirika, shirika halisimami wala halibuniwi kimsingi. Hakuna mwili kattu katika shirika la hisa bali kimakusudi hutenganishwa na kiungo cha kuwepo mtu katika shirika, wala haipewi thamani yoyote. Kwani mkataba wa shirika la hisa ni mkataba baina mali tu; mali ndizo zinazoshirikiana bila wenyewe kuziimiliki. Mali hizi hushirikiana pasina kuwepo mwili wa mshirika pamoja nazo. Kupotea kuwepo mwili hujaalia shirika kutosimama, basi ni batili kiSheria kwani mwili ndio yenyewe kutasarruf na mali. Juu ya mwili pekee yake nido hutegemewa kutasarruf na mali; ikiwa hakuna mwili, hakuna tasarruf.

Amma kwa kuwa watu wenyewe mali (warasilimali) ndio wenyewe kusimamia kibinafsi kukubaliana juu ya kushiriki kimiali, na kuwa wao ndio wenyewe kuteuwa kikao cha usimamizi ambayo husimamia kivitendo kazi katika shiria, hino haidokezi kuwepo mwili katika shirika kwani makubaliano yao ni kufanya mali mshirika wala sio kuwa wao wenyewe ndio washirika. Mali ndio mshirika wala sio mwenye kuimiliki. Amma kuwa wao ndio wenyewe kuchagua kikao cha usimamizi, hino haimaanishi hao wanawakilisha wao bali kikao hicho huwakilisha mali zao wala hawawakilishi wao kwa dalili mwenye hisa ana kura kulingana na anachomiliki. Mwenye kumiliki hisa moja ana kura mora yaani wakili mmoja, na mwenye hisa elfu moja ana kura elfu moja yaani wakili elfu moja. Kwa hivyo hino ni uwakilishi juu ya mali wala sio juu ya mtu. Hino hudokeza ya kwamba kiungo cha mwili kimepotezwa na kwa kuwa imeundwa na kiungo cha mali tu.

Kwa hivyo, istilahi ya shirika la hisa hudokeza kwamba haimiliki shuruti za lazima ili kusimama shirika katika Uislamu.

Kwa sababu hakuna makubaliano ya watu wawili au zaidi, bali ni kujifunga na mapendekezo ya kibinafsi kutoka upande mmoja tu. Na hakuna mwili wenyе kusimamia tasarruf kwa sifa yake ya kibinafsi katika shirika, bali ni mali tu pasina kuwepo mwili. Kwa hivyo mkataba ya shirika la hisa ni batili kiSheria kwa upande huu, kwa hivyo shirika la hisa ni batili kwani shirika halijasimama wala haisimami juu yake istilahi ya shirika katiak Uislamu.

2:- Shirika ni mkataba kutasarruf na mali na kuzidisha mali kwayo ni kuizidisha kwa umilikaji. Kuzidisha mali ni kutasarruf ni tasarruf za kiSheria, na tasarruf zote za kiSheria ni tasarruf za kimdomo nazo hutokamana na mtu sio mali. Hakuna budi kuzidisha mali itokamani na mwenye kumiliki tasarruf yaani mtu wala sio mali. Shirika la hisa hufanya mali kuzidi kivyake bila mwili wa mshirika na pasina mtu mwenye kutasarruf anayemiliki haki ya kutasarruf; hufanya mali ndio yenyе kutasarruf kwa sababu shirika la hisa ni mali ziliojumuika na kupewa nguvu za kutasarruf. Ndio maana shirika huhisabiwa shakhsiya ya kimajazi inaomiliki kipekee haki ya tasarruf za kikanuni mfano kununua, kuuza, kuunda, kushtaki nk. Wala washirika hawamiliki tasarruf yoyote bali tasarruf ni khususi kwa shakhsiya ya shirika ilhali tasarruf katika shirika katika Uislamu hutokamana na washirika peke yao, mmoja akitasarruf kwa ruhusa ya wengine; wala mali ya shirika iliojumuishwa haina uzito wowote katika kutasarruf bali tasarruf imefungika kwa mtu mshirika. Kwa hayo, tasarruf zinazotokea katika shirika kwa sifa yake kama shakhsiya ya kimajazi ni batili kiSheria kwa sababu lazima tasarruf zitokamane kutoka mtu maalumu yaani kutoka watu maalumu, na mtu huyu awe mionganoni mwa wanaomiliki uwezo wa kutasarruf; na hino haihakikishwa katika shirika la hisa. Wala haisemwi hapa kwamba mwenye kusimamia kitendo katika shirika ni wafanyikazi nao ni wenyе kuajiriwa na warasilimali wenyе hisa. Na wenyе kusimamia idara ya tasarruf ni mudiri (meneja) na kikao cha usimamizi; nao wanawakilisha wenyе hisa. Haya hayasemwi kwani mshirika amefungika kibinafsi katika shirika, na mkataba wa shirika imetukia juu yake kibinafsi. Haimjuzu

ye ye kumwakilisha mtu kusimamia vitendo vya shirika wala kumuajiri mtu kusimamia amali za shirika kwa niaba yake, bali hulazimika kusimamia amali za shirika kibinafsi. Haiwajuzu washirika kuajiri wafanyikazi kuwasimamia, wala kuwakilisha kikao cha usimamizi kwa niaba yao. Isitoshe, kikao cha usimamizi haiwawakilishi wenyewe hisa bali ni huwaklisha hisa zao kwa sababu yenyewe kumweka katika idara ni kura alizozipata katika uchaguzi nazo ni kwa hisabu na mali zilizoshirikiana katika hisa wala sio kwa hisabu ya watu wenyewe kushiriki. Na juu ya hayo, meneja na kikao cha usimamizi haimiliki uwezo wa kutasarruf katika shirika kwa sababu tatu:-

Mwanzo: Kwa sababu wao hutusarruf kama wakili kwa niaba ya wenyewe hisa yaani washirika kwa kuchaguliwa na wao ilhali haimjuzu mshirika kujiwakilisha kwa sababu shirika limesimama juu ya nafsi yake. Kama haijuzu kuwakilisha mwenye kuowa kwa niaba yake—bali yajuzu kuwakilisha mwenye kufunga mkataba ya ndoa kwa niaba yake—kadhalika haimjuzu kuwakilisha mwenye kushiriki kwa niaba yake. Bali yamjuzu kuwakilisha mwenye kufunga mkataba wa shirika lakini si mwenye kuwa mshirika kwa niaba yake.

Pili: Wenyewe hisa yaani washirika wamewakilisha juu ya mali zao wala sio juu ya nafsi zao kwa dalili ya kuwa uchaguzi ndio hutambuliwa katika kuwakilisha; nayo hutambuliwa kwa hisabu ya mali wala sio kwa hisabu ya watu. Kuwakilisha hupitia mali zao wala sio nafsi zao.

Tatu: Wenyewe hisa ni washirika kimali tu wala sio washiriki kimwili. Na mshirika wa kimali hamiliki uwezo wa kutasarruf kattu, basi haisihi kwake kuwakilisha mwenye kutasarruf katika shirika kwa niaba yake.

3:- Kuchukuliwa shirika la hisa kuwa ni yenyewe kudumu huhalifu Shar'a. Shirika ni katika mikataba yalioruhusiwa kiSheria inaobatilika kwa kufa mmoja wa washirika, kuwa mwandazimu, kufungiwa kwake kutotasarruf na kuvunjwa na mmoja wa washirika ikiwa imeundwa na watu wawili. Lau imeundwa na

watu zaidi ya wawili, shirika huvunjwa kwa kifo, uwandazimu au kufungwa mshirika kutotasarruf. Lau mmoja wa washirika akiwa na warathi, huangaliwa. Ikiwa mrathi hajabalighi hawezi kuendeleza shirika, lakini akiwa amebalighi, anaweza kuendeleza shirika na mshirika mwenzake kumruhusu kutasarruf au mwenyewe aweza kudai kugawanya (shirika). Mshirika akifungwa haki ya kutasarruf (na mahkama), shirika huvunjwa kwa sababu ni lazima mshirika awe aweza kutasarruf. Kwa hivyo shirika kuwa ni ya kudumu na kuendelea kwake pasina kujali kuwa mshirika mmoja au kufungwa kwake haki ya kutasarruf hufanya shirika kuwa fisidifu kwa kukusanya sharti fisidifu inaohusika na umbo la shirika na **hakika asili** (*mahiya*) ya mkataba.

Ufupi wa maneno ni kuwa shirika la hisa haijasimama kimsingi kwani wenye kuiunda ni washirika wa kimali tu pasina kuwepo mshirika wa kimwili ilhali kuwepo mshirika wa kimwili ni sharti ya kimsingi kwani juu yake husimama shirika kama shirika; na akikosekana, shirika halisimami wala haliwezi kusimama. Na shirika za hisa hutimia kwao wao kwa kuwepo washirika wa kimali tu, na shirika hushughulika na kutenda kazi zake moja kwa moja pasina kuwepo mshirika wa kimali wala huyu mshirika wa kimali hapewi umuhimu wowote. Kwa hayo huwa ni shirika batili kwa kutosimamishwa kama shirika kiSheria. Kisha wale wanaosimamia tasarruf katika shirika ni kikao cha usimamizi nao ni wawakilishi wa wenye hisa yaani washirika wa kimali ilhali kiSheria haruhusiwi kujiwakilishia mtu kutasarruf katika shirika kwa niaba yake sawa sawa awe mshirika wa kimali au mshirika wa kimwili kwa sababu mkataba wa shirika imetukia juu yake kibinafsi basi ni lazima yeye asimamie tasarruf. Haruhusiwi kujiwakilisha au kumwajiri mwenye kusimamie tasarruf na kazi katika shirika. Ni mshirika wa kimali tu kiSheria asiemiliki tasarruf katika shirika wala haki ya kufanya kazi humo kama mshirika kattu; bali tasarruf katika shirika na kufanya kazi katika shirika imefungwa na mshirika wa kimwili sio mwengine. Pia shirika la hisa huwa ni shaksiyya ya kimajazi ya kikanuni ambao kinamiliki haki ya kutasarruf ilhali tasarruf kiSheria haisihi ila kutoka mwanadamu mwenye

uwezo wa tasarruf kwa kuwa ni mwenye akili aliye balighi au mwenye akili mwenye kukuwa karibu kubalighi. Tasarruf zote isiotokamana kwa sura hino ni batili. Kusingizia tasarruf kwa shakhsiyya ya kimajazi haijuzu bali hakuna budi kuelekeza tasarruf kwa mwanadamu mwenye uwezo wa kutasarruf. Kwa hayo shirika za hisa ni batili na tasarruf zao zote ni batili; na mali zote zinazochumwa kuzipitia ni batili ziliozochumwa na tasarruf batili zisizoruhusiwa kumilikiwa.

Hisa katika Shirika la Hisa

Hisa za shirika ni ukarasa za kimali zinazowakilisha bei/thamani ya shirika wakati inapothaminiwa wala haziwakilishi rasilimali ya shirika ilipoasisiwa. Hisa ni sehemu isiotengwa na umbo la shirika lakini si sehemu ya rasilimali yake; basi ni kama kitegemeo cha thamani ya mapato ya shirika. Thamani ya hisa sio moja bali hubadilika kulingana na faida au hasara ya shirika; wala sio moja katika miaka yote bali thamani yake hutofautika na kubadilika. Kwa hayo hisa haiwakilishi rasilamali iliolipwa pindi shirika ilipoasisiwa bali hisa huwakilisha rasilimali ya shirika inapouzwa yaani wakali fulani; basi ni ukarasa wa kipesa ambao bei yake hushuka pindi soko la hisa linaanguka na kupanda pindi soko limeinuka. Hisa baada shirika kuanza kazi hutengwa kutoka kuwa rasilimali hadi kuwa ukarasa wa kimali yenye thamani maalumu.

Hukmu ya kiSheria juu ya ukarasa za kimali ni kuzichunguza. Zikiwa zinakusanya mali halali kama pesa ya kikaratasi yenye kubadilisha moja kwa moja na dhahabu au fedha na mfano yake, kuiza au kuinunua ni halali kwa sababu imekusanya mali ya halali. Lakini zikikusanya mali haramu kama deni inaopatikana ndani yake mali ya riba, hisa za mabenki nk kuziuza na kuzinunua ni haramu kwa sababu imekusanya mali haramu. Hisa sa shirika za hisa ni (*sanadaat*) zinazokusanya mkusanya wa rasilimali halali na faida haramu katika mkataba batili na mu'amala batili pasina kutenganishwa baina mali asli na faida. Na kila (*sanad*) ndani yake ni thamani ya fungu la mapato ya shirika batili, na hizi mapato zimechumwa kwa mu'amala batili iliokanywa na Sheria basi huwa mali haramu. Kwa hivyo hisa za

shirika ya hisa hukusanya mali ya haramu basi hizi ukarasa za kimali—nazo ni hisa za mali haramu—haziruhusiwi kuziuza, nunua au kuamiliana nazo.

Imebakia suali juu ya yaliowafikia Waislamu ya kununua hisa za shirika za hisa, kushiriki kwao katika kuzianzilisha na kumiliki kwao hisa kwa sababu ya kushiriki kwao katika shirika hizi. Je vitendo hivi ni haramu kwao wao juu ya kwamba waliokuwa hawajui hukmu ya kiSheria pindi waliposhiriki, au walifutiwa fatwa na maSheikhe ambao hawakufahamu undani ya uhakika ya shirika za hisa? Na je, hizi hisi mikononi mwao ni mali zao na mali halali kwao wao hata kama zimechumiwa kwa amali zilizobatilishiwa na Sheria? Au ni haramu kwao wao au hawazimiliki? Na je, yawajuzu wao kuuza hisa hizi kwa watu au haijuzu?

Jawabu ya haya ni kwamba kutojua hukmu ya kiSheria sio udhru kwa sababu ni *fardh ‘ayn* kwa kila Muislamu kujifundisha hukmu za kiSheria yanaomlazimu yeye katika maisha yake ili atekelze vitendo kwa mujibu ya hukmu ya kiSheria. Lakini ikiwa hukmu hiyo ni mfano mwa hukmu ambazo kawaida hazijulikani na mfano wa mtendaji huyu, haadhibiwi kwa kitendo na kitendo chake ni sahihi hata kama hukmu ya kiSheria ni kwamba kitendo ni batili. Hii ni kwa sababu **“Mtume (SAW) alimsikia Mu’awiya bin Al-Hakam akimwitikia mwenye kuchemua ilhali alikuwa katika swala. Alipomaliza kuswali, Mtume alimfundisha kwamba maneno hubatilisha swala, na kumwitikia mchemuaji hubatilisha swala, lakini hakumuamrisha kuregelea swala”** (Muslim na An-Nisai wamesimulia maana ya haya kwa njia ya ‘Ata bin Yassar). Hii ni kwa sababu hukmu hino, nayo ni kuwa maneno hubatilisha swala, ni katika yale ambayo kikawaida haijulikani na watu kama hao basi Mtume alimpa udhru na kuhisabu swala yake kuwa sahihi. Na kuwa shirika za hisa ni haramu kiSheria ni mionganini mwa hukmu ambayo mfane wake haijulikani na wengi, kwa hivyo ujinga huu hupewa udhru. Basi vitendo vya wale walioshiriki ni sahihi hata kama shirika ni batili kama swala ya Mu’awiya bin Al-Hakam ambayo ilikuwa ni swala

sahihi. Na fatwa za maSheikhe pia huchukua hukmu ya kutojua kwa mwenye kufutiwa lakini mufti hana udhru kwa sababu hakujitolea kibidii katika kufahamu uhakika wa shirika za hisa kabla kutoa hukmu juu yake. Amma hawa washirika kumiliki hisa, hino ni umilikaji sahihi wala sio wa kibatili kwa kutojua kwao ubatili wake kwa kutojua unaopewa udhru. Basi ni mali halali kwao wao maadamu hukmu ya kiSheria imechukua vitendo vyao kuwa sahihi wala sio batili kwa kutojua kwao ubatili kwa kutojua unaopewa udhru. Amma kuuza hisa hizi kwa Waislamu, hino haijuzu kwa sababu ni karatasi za kimali ambazo ni batili kiSheria; uhalali wa umilikaji wake umekuja tu kighafla kwa sababu ya udhru uliotolewa udhru. Lakini lau ajue hukmu ya kiSheria ndani yake au abadilike kuwa mionganoni mwa wale ambao mfano wao sio mionganoni mwa wasiojua mfano wa hukmu hiyo, hapo itakuwa mali ya haramu isiouzwa au kununuliwa wala haipewa mwengine kumsimamia kuiuza.

Twarika ya kujikomboa na hisa hizi zilizomilikiwa kwa sababu ya kutojua hukmu yake ya kiSheria ni kwa kuvunja shirika au kuibadilisha kuwa shirika la Kiislamu. Au kumtafuta mtu asiyekuwa Muislamu anayehalalisha hisa za shirika za hisa, na kumwakilisha aziuze kwa niaba yake na kuchukua thamani yake. Kutoka Suwaid bin Ghafala “**kwamba Bilal alisema kwa Umar bin Al-Khattab: Wasimamizi wako wanachukua khamri na ngurue kama kharaji. Akasema: Musichukue kutoka kwao lakini wawakilishe kuziuza kisha chukueni thamani**” (Al-Ubaid ameisimulia katika *Al-Amwal*). Wala hakuna hata mmoja aliomkanushia Umar kwa haya ilhali ni katika yale yenye kukanushwa lau inakhalifu *Shar'a*, basi ikawa *ijma*. Khamri na ngurue ni mionganoni mwa mali za *Ahl al-Dhimma* wala sio mali za Waislamu. Basi walipotaka kuwapa Waislamu badala ya *jizya*, Umar aliwaamrishaa wasizikubali bali wawawakilishe kuwauzia kisha wachukue thamani yake. Na maadamu hisa ni mali mionganoni mwa mali za warasilimali wamaghariibi wala sio mali kwa Waislamu, lakini zimewafikia Waislamu ilhali haisihi wao kuzichukua bali watawawakilisha kuwauzia. Kama haki ya Waislamu ya *jizya* na kharaji imetukia juu ya khamri na ngurue, na Umar aliwaruhusu kuwawakilisha

maDhimmi kuwauzia, kadhalika hakia ya Waislamu katika hisa hizi inawaruhusu kuwawakilisha madhimmi wawauzie.

JUMUIYA ZA USHIRIKIANO (CO-OPERATIVE SOCIETIES)

Jumuiya za ushirikiano ni sampuli ya shirika za kirasilimali; ni shirika hata kama huitwa jumuiya za ushirikiano. Nayo ni ushirikiano baina jumla ya watu wanaokubaliana baina yao kusimama kwa ushirika kwa mujibu ya amali yao khasa.

Jumuiya ya ushirikiano katika sura yake ya kibiashara ya kikawaida hulenga kusaidia wanachama wake na kudhamini maslahi yao makhsusi ya kiuchumi. Na jumuiya za ushirikiano hukusanya shakhsiya ya kimajazi kwa shirika, na kwa hivyo kutofautiana na jumuiya nyengine kwa sababu jumuiya hizo hazilengi malengo ya kiuchumi. Jumuiya hufanya kazi kuzidisha faida ya wanachama wake wala sio maslahi ya wengine, inaolazimisha kujenga mahusiano yenye nguvu baina nishati zake za kiuchumi na hali ya uchumi ya wanachama.

Jumuiya ya ushirikiano huundwa na idadi ya wanachama ambao wanaweza kuwa saba, au wanazidi au kupunguka, lakini haiundwi baina ya watu wawili tu. Nazo ni sampuli mbili: Mojawapo ni shirika yenye hisa za kuanzilisha ambaye yawezekana mtu yoyote kuchukua sifa ya mshirika kwa kumiliki hisa hizi. Ya pili ni shirika bila hisa za kuanzilisha ambapo kujianganisha nayo ni kwa kulipa malipo ya kushiriki ya kila mwaka ambayo jumuiya jumla huipanga katika kila mwaka.

Lazima jumuiya ya ushirikiano imiliki shuruti tano:-

Ya mwanzo—Uhuru wa kushiriki katika jumuiya. Mlango wa kujiunganisha hubakia wazi mbele ya mtu yoyote kulingana na shuruti zile zile juu ya wanachama walotangulia. Na nidhamu za jumuiya, vikwazo nk za jumuiya zimfunge ye ye sawa sawa vikwazo hivi ziwe na maumbile ya kieneo kama watu wa kijiji au maumbile ya ma-“professionals” kama vinyozi.

Pili—Usawa wa washirika katika haki: Na haki muhimu zaidi ni kupiga kura, basi kila mshirika hupewa kura moja.

Tatu—Kupanga faida maalumu ya hisa: Baadhi jumuiya za ushirikiano hulipa washirika wa kudumu faidi maalumu ikiwa faida ya jumuiya itaruhusu hayo.

Nne—Kuregesha iliopatika katika faida ya kiziada ya uwekezaji (investment): Faida safi huregeshewa wanachama kwa mujibu ya kazi walizozifanyia jumuiya mfano ununuzi, au kutumia huduma za jumuiya na viungo vyake.

Tano—Uwajibu wa kuunda utajiri wa jumuiya kwa ya akiba inaowachwa kwa siku za mbeleni (reserve fund).

Kikao cha idara kinachochaguliwa katika mkutano jumla wa kila mwaka ndicho kinachosimamia tasarruf za shirika katika idara yake na kutekeleza vitendo vyake moja kwa moja. Kikao hicho chaundwa mionganoni mwa washirika kwa sharti ya kwamba kila mshirika awe na kura pasina kujali hisa zake. Mwenye hisa mia moja au mwenye hisa moja wana kura moja katika uchaguzi wa kiidara.

Jumuiya za ushirikiano ni sampuli nyingi: Nyengine ni jumuiya za ki-professional, jumuiya za utumiaji (consumption), jumuiya za ukulima na jumuiya za uzalishaji. Kwa jumla zao, imma ni jumuiya ya utumiaji inaogawanya faida kwa mujibu ya ununuzi au jumuiya ya uzalishaji inaogawanya faida kwa mujibu ya uzalishaji.

Hizi ndizo jumuiya za ushirikiano, nazo ni jumuiya batili zinazogongana na hukmu za Kiislamu kwa sababu zifuatazo:-

1:- Jumuiya ya ushirikiano ni shirika basi ni lazima ikamilishe shuruti za shirika ilioshurutishwa na Shar'a ili kusihi shirika. Shirika katika Uislamu ni mkataba baina ya watu wawili au zaidi wanaokubaliana kupitia kwayo kusimamia amali ya kimali kwa lengo la faida. Kwa hivyo hakuna budi shirika liwe na

mwili lenye hisa ili liitwe shirika kiSheria. Likiwa shirika halina mwenye kumiliki na kutasarruf ili asimamie kazi ambayo kwa ajili lake shirika limeundwa. Tukitabikisha haya juu ya jumuiya ya ushirikiano, tutapata haijatimiza kuwa shirika kiSheria kwa sababu shirika limesimamia mali tu wala halina mshirika wa kiwiliwili; bali mali pekee yake ndio iliotukia shirika juu yake. Haijapita mkataba kusimamia kazi, bali imepita mkataba juu ya kuweka mali maalumu ili iundwe idara itakao chunguza mwenye kusimamia kazi. Watu wanaoshiriki katika shirika hushirikisha mali zao tu; basi shirika ni tupu ya mwili. Kwa hivyo jumuiya haiundi shirika la kiSheria kwa kutokweko mwili inaoshiriki. Haitambuliki kuwa imeundwa kimsingi kwa sababu shirika ni mkataka juu ya kutasarruf na mali wala kutasarruf haitokea ila na mwili; basi ikikosa mwili, shirika haliwi la kiSheria na huwa ni shirika batili.

2:- Kugawanya faida kulingana na ununuzi au uzalishaji—sio kulingana na rasilimali au kazi—haijuzu kwa sababu shirika ikitukia juu ya mali basi faida hifuata mali; na ikitukia juu ya kazi, basi faida hifuata kazi. Imma faida hifuata mali au kazi au zote mbili pamoja. Amma kushurutisha kugawanya faida kwa mujibu ya yalionunuliwa au yariozalishwa, hino haijuzu kwa kuhalifu mkataba wa kiSheria. Kila sharti inaokanusha yanaolazimishwa na mkataba (wa kiSheria), au sio kwa maslahi ya mkataba na wala hailizimishwi nayo, ni sharti fisidifu. Na kugawanya faida kwa mujibu ya yanaonunuliwa au yanaozalishwa hukanusha yanaolazimishwa na mkataba kwa sababu mkataba kiSheria hutukia juu ya mali au kazi; kwa hivyo faida huwa kulingana na mali au kazi. Na lau faida hushurutishwa kulingana na yanaonunuliwa au uzalishaji, sharti hino ni fisidifu.

BIMA (INSURANCE)

Bima juu ya uhai, bidhaa, yanaomilikiwa au sampuli yoyote mionganoni mwa sampuli zake nyingi ni mkataba mionganoni mwa mikataba. Nayo ni mkataba baina shirika la bima na mwenye kutaka kuhifadhiwa kumlipia ridhaa ima juu ya kitu chenyewe kilichohasirika au thamani yake ikihusika na bidhaa au yanaomilikiwa, au kiwango cha mali ikihusika na uhai na mfano

wake. Hino ni pindi inapotokea msiba kwa muda maalumu kwa mukabala ya malipo fulani; na shirika hukubali hayo. Kwa mujibu ya kutaka na kukubali huu, shirika la bima huahidi kulipa ridhaa kwa mwenye kujihifadhi ndani ya shuruti maalumu zilizokubaliwa baina upande zote mbili, imma kile chenyewe kilichohasirika au thamani yake pindi msiba unapotokea au kiwango cha mali kilichokubaliwa. Mfano ikipotea bidhaa yake, kuharibika gari lake, kuchomeka nymba yake, kuibiwa anayoyamiliki, afe nk katika muda maalumu kwa mukabala ya mwenye kujihifadhi kuilipa kiwango maalumu ya mali ndani ya muda maalumu. Kwa hayo hubainika kwamba bima ni makubaliano baina ya shirika la bima na mwenye kujihifadhi juu ya sampuli ya bima na shuruti zake basi ni mkataba, isipokuwa kulingana na hino mkataba iliotimizwa baina yao—nayo ni makubaliano—shirika huahidi kutoa ridhaa au kulipa kiwango maalumu kulingana na shuruti walizozikubalia. Lau msiba yamsibu mwenye kujihifadhi kulingana na mada za mkataba, shirika hulazimika kutoa ridhaa ya kitu kilichopotea au thamani yake kulingana na bei ya soko, pindi msiba unapotokea. Shirika lina khiyari baina kulipa thamani au kumpa mwenye kujihifadhi, au mwengine, (mfano cha) kitu chenyewe. Hino ridhaa ni haki mionganoni mwa haki za mwenye kujihifadhi juu ya dhimma la shirika kwa kutokea tu kilichotajwa katika mkataba lau shirika inakinai kustahiki mwenye kujihifadhi au mahkama kuhukumu na hayo.

Imetungwa jina la ‘bima’ kwa hayo. Na bima yaweza kuwa kwa maslahi ya mwenye kuchukua bima au maslahi ya mwengine kama watoto wake, mke wake na waliosalia mionganoni mwa warathi wake, au mtu au jamaa yoyote alioichagua mwenye kuchukua bima. Kutumiwa jina na bima kwa maisha, bidhaa, sauti nk ni kwa lengo kupendeza mu’amala huu kwa watu; lau sivyo, kwa hakika hahifadhiwi uhai bali huhifadhiwa tu kufikia kiwango maalumu cha pesa kwa watoto wake, mke wake au waliosalia mionganoni mwa warathi wake, au mtu au jamaa yoyote iliochaguliwa na mwenye kuchukua bima ikimfikia mauti. Wala hahifadhi bidhaa, gari, mali nk bali anahifadhi kupewa ridhaa ya kitu chenyewe au thamani yake kimali lau

bidhaa, gari, mali au chochote anachokimiliki husibiwa na madhara au uharibifu. Basi kwa hakika ni dhamana ya kupewa yeye au mwengine kiwango cha mali, au kupewa ridha ikimtokea kitu kinachosababisha kupotea nafsi yake au mali yake, wala sio dhamana juu ya uhai wake au mali yake. Hino ndio hakika ya bima, na ubatili yake hudhihirika kwa sura mbili baada kuichunguza:-

Moja: Ni mkataba kwa sababu ni makubaliano baina upande mbili, na hukusanya kutaka na kukubali; kutaka kutoka mwenye kutaka bima na kukubali kutoka kwa shirika. Ili kusihi mkataba huu kiSheria, lazima ikusanye shuruti za mkataba za kiSheria; itasihi ikizikusanya na lau sivyo, haitosihi. Mkataba kiSheria lazima itukie juu ya kitu au manufaa; lau haitukii juu ya kitu au manufaa, itakuwa batili kwa sababu haitukii juu ya kitu ili kufanywa mkataba kiSheria. Hino ni kwa sababu mkataba kiSheria hutukia imma juu ya kitu kwa mukabala ya ridhaa kama biashara, kununua kwa malipo ya kutangulia, shirika nk au hutukia juu ya kitu pasina ridhaa kama zawadi. Au imma hutukia juu ya manufaa kwa mukabala ya ridhaa kama kuajiri, au juu ya manufaa pasina ridhaa kama kuazima. Hakuna budi mkataba wa kiSheria kutukia juu ya kitu. Mkataba wa bima sio mkataba juu ya kitu wala manufaa, bali ni mkataba iliotukia juu ya ahadi yaani juu ya dhamana. Ahadi au dhamana haitambuliwi kama kitu kwa sababu haitumiki au kuchukuliwa manufaa yake; wala haitambuliwi kama kwa sababu haifaidiki na ahadi yenewe sio kwa ujira au kuazima. Amma kupatikana mali kwa kutegemea ahadi hino, hino haitambuliwi kama manufaa yake bali ni athari ya mu'amala tu. Kwa hayo mkataba wa bima haichukuliwi kwamba imetukia juu ya kitu au manufaa basi ni mkataba batili kwa sababu haikusanyi shuruti ziliowajibika kukusanywa katika mkataba kiSheria ili kutimia kutambuliwa kwake kuwa ni mkataba.

Pili: Shirika lilitoa ahadi kwa mwenye kutaka bima kulingana na shuruti maalumu, basi ni sampuli ya dhamani kwa hivyo ni lazima itabikishwe juu yake shuruti ambazo Shar'a huzitaka hata iwe dhamana ya kiSheria; itasihi ikizikusanya na lau sivyo,

haitosihi. Na kwa kuregelea kwa dhamana kiSheria, yadhihirika yafuatayo:-

Dhamana ni kuunganisha jukumu la mwenye kudhamini (mdhamini) pamoja na jukumu la mwenye kulazimishwa na jukumu mwanzo katika kujifunga na haki maalumu. Hakuna budi kuwepo kuunganisha jukumu na jukumu, mdhamini, mwenye kulazimishwa na haki mwanzo na mdhaminiwa. Dhamana ni kufungwa na haki juu ya shingo la mtu pasina ridhaa. Sharti ya kusihi dhamana ni kuwepo haki mionganoni mwa haki za kimali iliowajibika au itakaowajibika. Ikiwa hakuna haki iliowajibika au itakaowajibika, basi dhamana haisihi. Hino ni kwa sababu dhamana ni kuunganisha jukumu pamoja na jukumu katika kulazimika na haki basi ikiwi mwenye kulazimika na haki hana jukumu juu ya shingo basi hakutokweko jukumu juu yake. Hino ni wazi katika haki iliowajibika. Amma katika haki ambao itakuja kuwajibika mfano mwanamume kumwambia mwanamke: ‘Olewa na fulani, nami nakudhamini mahari yako’, mdhamini ameunganisha jukumu lake pamoja na jukumu la mwenye kulazimika na haki kwa kulazimika yeze na yanaomlazimu yule, na kwamba kinachothibitika juu ya yule itathibitika juu yake. Imma ikiwa hakuna haki iliowajibika juu ya mtu, au haki ambayo itakaokuja kuwajibika, hakuna hakika ya maana ya dhamana kwa sababu hakuna kuunganisha jukumu pamoja na jukumu; basi dhamana haitosihi. Kwa hayo, ikiwa hakuna haki iliowajibika au itakaokuja kuwajibika kwa mdhaminiwa juu ya mwenye kulazimika na haki haitosihi dhamana. Kwa sababu ni sharti ya kwamba mwenye kulazimika na haki awe na mdhamini juu ya kitu lau chaharibika au kupotea, au mdhamini wa deni sawa sawa akiwa ni mdhamini kivitendo ikiwa haki imewajibika na kuthibitika juu ya shingo, au mdhamini kwa nguvu ikiwa haki itakuja kuwajibika na kuthibitika juu ya shingo. Ikiwa mwenye kulazimika na haki hana mdhamini wa kivitendo au kinguvu, dhamana haisihi kwa sababu kisichowajibika juu ya mwenye kulazimika na haki hakiwajibiki juu ya mdhamini. Mfano mtu akubali nguo kutoka watu, na mtu mmoja amwambie mwenziwe: ‘Mpe nguo yake nami ni mdhamini’, kisha nguo yaharibika. Je mdhamini

atadhamini bei ya nguo kwa ajili ya mwenye kukubali nguo? Jawabu lake ni kuwa lau nguo yaharibika pasina kitendo chake au madharau yake, mdhamini halazimiki na kitu kwa sababu kimsingi mwenye kulazimika na haki halazimishwi na chochote; na lau yule wa mwanzo halazimiki basi, ni akili zaidi kwamba mdhamini halazimishwi. Kwa hayo hakuna budi kuwepo haki iliowajibika juu ya mwenye kulazimika na haki kwa wengine, au itakaowajibika, hata dhamana isihi. Kuthhibitika haki juu ya shingo sasa hivi au baadaye ni sharti ya kusihii dhamana. Lakini si sharti kwamba mwenye kulazimika na haki ajulikanwe au mdhaminiwa ajulikanwe; dhamani husihi hata kama watakuwa hawajulikani. Lau mtu amwambia mwenzake: ‘Mpe dobi nguo zako’ na aseme: ‘Naogopa zitaharibiwa’ basi yeze amwambie: ‘Mpe dobi nguo zako nami ni mdhamini juu yake lau zitaharibiwa’ pasina kutajwa dobi, itasihi. Itabidi adhamini lau ampe dobi nguo zake kisha ziharibiwe, hata kama mwenye kulazimika na haki hajulikani. Kadhalika lau aseme: ‘Fulani ni dobi mhodari, basi mimi ni mdhamini wa dobi kwa kila mwenye kumwachia nguo kutoharibika’, itasihi hata kama mdhaminiwa hajulikani.

Dalali ni dhamana ni wazi katika kuunganisha jukumu na jukumu, na kwamba ni kudhamini haki iliothhibitika juu ya shingo. Na ni wazi kwamba kuna mdhamini, mwenye kulazimika na haki na mdhaminiwa. Na pia mwenye kulazimika na haki hajulikani, na kadhalika mdhaminiwa. Dalili hino ni yaliosimuliwa na Abu Dawud kutoka Jabir aliesema: “**Alikuwa Mtume (SAW) haswali juu ya mtu aliekufa akiwa na deni. Basi akaja maiti na akauliza: ‘Je, ana deni?’ Wakajibu: ‘Ndio, dinari mbili.’ Akasema: ‘Mswalie swahibu wenu.’** Basi Abu Qatada Al-Ansari akasema: ‘Ziko juu yangu, ewe Mtume.’ Akasema: Basi Mtume (SAW) akamswalia. Na pindi Mtume (SAW) akanusuriwa na ukombozi, alisema: ‘Mimi ni mbora kwa muumini kushinda nafsi yake. Basi mwenye kuwacha deni, kuilipa ni juu yangu. Na mwenye kuwacha mali, hino ni kwa warathi wake’ Hadithi hino ni wazi kwamba Abu Qatada aliunganisha jukumu lake pamoja na jukumu la maiti katika kulazimika na haki ya kimali iliowajibika

juu ya mwenye deni. Na ni wazi kwamba katika dhamana kuna mdhamini, mwenye kulazimika na haki na mdhaminiwa, na kwamba mdhamini alioidhamini kwa wote wawili ni kulazimika na haki juu ya shingo lake pasina ridhaa. Na ni wazi ya kwamba mwenye kulazimika na haki ni maiti, na kwamba mwenye kudhaminiwa ni mwenye kukopesha na alikuwa hajulikani wakati wa dhamana. Kwa hivyo hadithi imekusanya shuruti za kusihi dhamana, na shuruti ya kufungwa kwake kama mkataba.

Hino ndio dhamana ya kiSheria. Na tukipima ahadi ya bima juu yake—nayo ni dhamana bila shaka—twaona kwamba bima imekosa kila sharti ya kusihi na kusimama dhamana iliotajwa na Shar'a. Katika bima hakuna kuunganisha dhimma juu ya dhimma kattu. Shirika la bima halifungi dhima yake juu ya dhimma ya yoyote kujifunga na mali ya mwenye kudhaminiwa; basi hakuma dhamana na bima huwa ni batili. Katika bima mwenye kudhaminiwa hana haki ya mali juu ya mtu yoyote ambayo shirika la bima limejifunga nayo kwa kuwa mwenye kudhaminiwa hana haki ya kimali juu ya yoyote ili shirika la bima lije kumdhampuni. Basi ni tupu na kuwepo haki ya kimali na shirika haijajifunga na haki yoyote ya kimali ili kusihi kuitwa dhamana kiSheria. Pia ile shirika imejifunga nayo mionganoni mwa ridhaa au thamani au kulipa mali haijawajibika juu ya mwenye kudhaminiwa kwa wengine pindi inapofungwa mkataba wa bima, sio wakati ule au mbeleni, hadi kusihi dhamana. Shirika la bima imedhamini kisichowajibika sio leo wala kesho, basi dhamana haitosihi na kwa hivyo bima ni batili. Isitoshe, katika bima hakuna mwenye kulazimishwa mwanzo na haki kwani shirika la bima haimdhampuni yoyote anayestahiki haki juu yake ili kuitwa bima. Kwa hivyo mkataba wa bima imekosa kiungo cha kimsingi zilizolazimishwa na Sheria juu ya dhamana, nayo ni kuwepo mwenye kulazimika mwanzo na haki. Kwa kukosa mkataba wa bima yule mwenye kulazimika mwanzo na haki basi huwa ni batili kiSheria. Pia pindi shirika la bima inapoahidi kulipa ridhaa juu ya kitu kilichopotea, kulipa bei yake ikiharibika au kulipa mali pindi inapotokea ajali, imejifunga na malipo haya kwa mkabala ya mali. Kwa hivyo ni kujifunga kwa mkabala wa malipo, na hino haisihi kwa sababu

sharti ya dhamana ni kwamba iwe bila malipo. Kwa hivyo bima ilio na malipo ni dhamana batili.

Kwa hayo hudhihirika kiwango cha bima kukosa shuruti za dhamana iliotajwa na Sheria, na kutokusanya shuruti za kusimama dhamana na shuruti za kusihi kwake. Kwa hivyo ukarasa wa ahadi inaotolewa na shirika na kudhamini ridhaa, bei au mali ni batili kimsingi basi bima zote ni batili kiSheria.

Kwa hayo bima yote ni haramu kiSheria sawa sawa iwe bima juu ya uhai, bidhaa, kinachomilikiwa nk. Na sura ya uharamu wake ni kuwa mkataba wake ni mkataba batili kiSheria. Na ahadi inaopewa na shirika la bima kulingana na mkataba ni ahadi batili kiSheria, basi kuchukua mali kulingana na mkataba huu ni haramu nayo ni kula mali kibatili na huingia katika mlango wa mali za haramu (*suhrt*).

15 NJIA ZILIZOZUILIWA KUZIDISHA MALI NAZO

Shar'a ya Kiislamu imefunga kuzidisha mali kwa mipaka yasiojuzu kuyavuka. Na imezuia mtu kuzidisha mali kwa njia maalumu nazo ni:-

Kamari

Shar'a imezuia kamari kwa njia ya kukatikiwa, na imepima mali inaochukuliwa kupitia kwayo kuwa haimilikiwa (kiSheria). Asema Allah Ta'ala:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَامُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ
الشَّيْطَانِ فَاجْتَبَيْهُ لَعْنَكُمْ ثَلْحُونَ - إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقَعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةُ
وَالْبَغْضَاءُ فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدُّكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ }

“Enyi mlionamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu na kutazamia kwa mishale ya kupigia ramli (yote haya) ni uchafu katika kazi ya Shetani. Basi jiiepusheni nay\vyo ili mupata kufaulu. Hakika Shetani anataka kuwatilieni uadui na bugdha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari, na anataka kuwazuia kutoka kumbuka Allah na kusali. Basi je mutawacha?” [TMQ 5:90-1]

Uharamu wa ulevi na kamari imetiliwa mkazo na sura nyingi za mkazo ikiwemo kuanza sentensi na “*Innama* (bila shaka)”, ushahidi wa kuzifananisha na kuabudu masanamu, kuzifanya uchafu kama alivyosema Ta'ala:

{ فَاجْتَبَوَا الرَّجْسَ مِنْ الْأُوْثَانِ }

“*Jiepusheni na uchafu ya masanamu*” [TMQ 22:30] na kuzichukua kama kazi ya Shetani na Shetani haleti ila shari tupu, kuamrisha kuepukana nazo, na kufanya kujiepusha kuwa ndio kufaulu. Na ikiwa kuepukana ndio kufaulu, basi kutena ni kushindwa na hasara. Pia kutaja natija zake za uovu nayo ni kuchochea uadui na bugdha mionganoni mwa watu wa ulevi na kamari, na yanaofikisha katika kuzuia kutoka utajo wa Allah na kuchunga nyakati za swala. Na msemo Wake:

{ فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ }

“*Basi je mutawacha?*” [TMQ 5:91] ni mionganoni mwa ufasihi zaidi katika mkanyo kwani ni kama imesemwa: Imesomwa kwenu yaliomo ndani yake ya mbinu za kuepukana na kuzuia, basi je mutawacha baada ya mbinu hizi za kuepusha na kuzuia? Mionganoni mwa kamari ni karatasi za bahati nasibu pasina kujali sababu tofauti za kuicheza, na kadhalika rehani juu yam bio za farasi. Mali ya kamari ni haramu isioruhusiwa kumilikwa.

Riba

Shar'a imezuia riba kwa njia ya kukatikiwa pasina kujali kiwango chake kuwa ni kikubwa au kidogo. Mali ya riba ni haramu bila shaka, na hakuna mwenye haki kuimiliki bali hurudishwa kwa wenyewe ikiwa wanajulikana. Asema Allah Ta'ala:

{ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا لَا يَقُولُونَ إِلَّا كَمَا يَقُولُ الَّذِي يَتَخَبَّطُهُ الشَّيْطَانُ مِنْ الْمَسِّ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَمَ الرِّبَا فَمَنْ جَاءَهُ مَوْعِظَةٌ مِّنْ رَبِّهِ فَأَنْتَهَى فَلَهُ مَا سَلَفَ وَأَمْرُهُ إِلَى اللَّهِ وَمَنْ عَادَ فَأُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ }

“*Wale wanaokula riba hawasimami ila kama anavyosimama yule ambaye Shetani amemzuga kwa kumsawaa (wako mbioni tu, hawana kituo).* Haya ni kwa sababu wamesema: ‘biashara ni kama riba’ ilhali Allah amehalalisha biashara na kuharamisha riba. Na aliyefikiwa na mauidha kutoka Mola wake kisha akajizuia, basi kwake yeye ni yale (mali) yaliotangulia na

hukumu yake iko kwa Allah. Lakini wanaoregea (kula riba) basi hao ndio watu wa Motoni, humo watacaa milele” [TMQ 2:275]

Na asema:

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذُرُّوا مَا بَقَى مِنِ الرِّبَا إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ - فَإِنْ لَمْ تَفْعُلُوا فَأَذْنُوا بِحَرْبٍ مِنْ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَإِنْ تُبْتُمْ فَلَكُمْ رُغْوُسٌ أَمْوَالُكُمْ لَا تَظْلِمُونَ وَلَا تَظْلِمُونَ }

“Enyi mliaoamini! Mcheni Allah na wacheni yaliobakia katika riba ikiwa nyinyi ni waumini. Na kama hamutofanya, basi fahamuni mutakuwa na vita na Allah na Mtume Wake. Na ikiwa mumetubu, kwenu nyinyi ni rasilimali zenu; musidhulumu wala musidhulumiwe” [TMQ 2:278-9]

Sifa ya uhakika wa riba ni kuwa faidha hino anayeichukuwa mwenye kulipwa riba ni kutumia vibaya juhudi za watu nayo ni malipo pasina kutumia juhudi. Na kwa kuwa mali inaochukuliwa riba juu yake imedhaminiwa faida pasina kuwa na uwezekano wa hasara, hino hukhalifu msingi: “**Faida hufuata (uwezekano wa) hasara**” Hino ni kwa sababu kutumia mali kupitia shirika, musharaba na mkataba wa kuajiri shamba la miti kwa shuruti zake sahihi yajuzu kwani hunufaisha jamii wala haitumia vibaya juhudi za wengine; bali huwa ni mbinu kuwawezesha kunufaika na juhudi zao wenyewe. Nayo ina uwezekano wa hasara kama uwezekano wa faida kinyume na riba. Juu ya hayo, uharamu wa riba ni kupitia nasi (ya Sheria) wala nasi hino haipimwi kuwa na ‘illah; kisha Sunna ikaja kubainisha mali za riba. Lakini yaweza kutukia akilini kwamba mwenye mali atahifadhi mali yake pasina kuitumia kuwaazima wenyе haja nayo kutimiza mahitaji yao. Na haja hino ni muhimu kwa mwenye haji basi hakuna budi kuwepo mbinu ya kutimiza haja hizi. Na haja leo zimekuwa tofauti na nyingi hadi riba imekuwa ndio msingi wa biashara, ukulima na usanii wa viwanda. Kwa hivyo ma-benki yameundwa kuamiliana na riba, wala hakuna mbinu nyengine na kadhalika hakuna mbinu kutimiza haja ila kupitia wenyе kukopesha kwa riba.

Jawabu lake ni kwamba sisi twazungumza juu ya mujtama inaotabikisha Uislamu kwa uzima wake ikiwemo upande wa uchumi, wala sio juu ya mujtama ulivyopangwa kileo. Hino ni

kwa sababu mujtama wa kileo huishi kwa mujibu wa nidhamu ya kirasilimali ndipo ma-benki yamechukua umuhimu kama dharura ya maisha. Tajiri anayejiona mhuru katika umilikaji wake na uhuru kupitia utapeli, ukiribitima, kamari, riba nk pasina serikali kuhusika au kufungwa na kanuni, bila shaka mfano wa hawa huona kwamba riba na ma-benki ni dharura ya uhai.

Kwa hivyo ni lazima kubadilisha nidhamu ya uchumi leo kwa uzima wake ili kuwekwa mahala pake—kimsingi na kikamilifu—nidhamu na Kiislamu ya uchumi. Ikizolewa nidhamu hino na kutabikishwa nidhamu ya Uislamu, watu wataona kwamba hakuna dharura ya riba katika mujtama unaotabikishwa Uislamu. Hino ni kwa sababu mwenye haja ya mkopo ama aihitaji kwa ajili ya uhai au ukulima. Amma haja ya kwanza, Uislamu umedhamini uhai kwa kila mmoja wapo wa maraia. Amma haja ya pili, Uislamu umeidhamini kwa kumwazima mwenye haja bila riba. Ibn Hibban amesimulia kumpitia ibn Masoud ya kwamba Mtume (SAW) alisema: **“Hakuna Muislamu mwenye kumkopeshaa Muislamu mkopo mara mbili ila huwa ni sadaqa mara moja”** Kumpokesha mwenye haja na mandoub wala kukupeshwa sio makruh bali ni mandoub pia kwani Mtume (SAW) alikuwa akikopeshwa. Na madamu kuna kukopeshwa nayo ni mandoub kwa mwenye kukopeshaa na kukopeshwa, watu wataona kwamba riba ni mionganii mwa madhara makubwa zaidi juu ya maisha ya kiuchumi, bali itadhihirika kama ni dharura kujitenga na riba na kupanga vizuizi vikubwa baina yake na mujtama kupitia Sheria na mielekezo kulingana na nidhamu ya Uislamu.

Ikipotea riba, hakuna haja ya ma-benki yalioko leo. Bait al-Mal itabakia peke yeke ikisimamia jukumu la kukopeshaa mali bila faida baada kuhakikisha uwezekano kunufaika na mali. **Umar bin Al-Khattab aliwapa wakulipa wa Iraq kutoka Bait al-Mal ili watumia ardhi zao.** Hukmu ya kiSheria ni kuwapa wakulima kutoka Bait al-Mal inaowawezesha kutumia ardhi zao hadi kutoa mapato. Imam Abu Yusuf alisema: **“Na wasiojiweza hupewa yanaowatosheleza kutoka Bait al-Mal ili kufanya**

kazi nayo” yaani ardhi. Kama Bait al-Mal inavyowakopesha wakulima kwa ajili ya ukulima, pia hukopesha watu kama wao wanaofanya kazi za kibinafsi kiasi kinacho watosheleza. Umar aliwapa wakulima kwa sababu walikuwa na haja ya chenye kutosheleza nafsi zao kimaisha basi aliwapa chenye kuwatosheleza, kwa hivyo hakuwapa wakulima matajiri chochote kutoka Bait al-Mal kuzidisha mapato yao. Qiyas hufanywa juu ya wakulima kwa watu mfano wao walio na haja cha kutosheleza nafsi zao kimaisha. **Mtume alimpa mtu kamba na shoka ili kukata kuni kwa ajili ya kupata chakula.**

Kuwachwa riba haitegemei kuwepo mujtama wa Kiislamu, serikali ya Kiislamu au mwenye kukopesha mali. Bali riba ni haramu na ni lazima iwachwe pasina kujali kuwepo au kutokwepo serikali ya Kiislamu, mujtama wa Kiislamu au mwenye kukopesha mali.

UDANGANYIFU WA KUPINDUKIA KATIKA BIASHARA (AL-GHUBN AL-FAAHISH)

Udanganyifu kilugha ni kuhadaa. Hsema amemdanganya (*ghabanahu*) katika kununua na kuuza yaani alimhadaa na kumzidi. Kumdanganya mtu kibiashara ni kumpunguzia katika bei na mengine. Udanganyifu ni kununua kitu kwa bei kubwa zaidi, au ndogo zaidi, kuliko mfano wake. Udanganyifu wa kupindukia ni haramu kiSheria kwani hadhit sahihi imeamrisha kuwacha udanganyifu kwa njia ya kukatikiwa. Bukhari amesimulia kumpitia Abdullah bin Umar kwamba **mtu alimtajia Mtume (SAW) mwengine aliemdanganya katika biashara, nae akasema: ‘Ukifanya biashara, sema: Hakuna udanganyifu/kuhadaa (*khilaaba*).’** Na Ahmad amesimulia kutoka Anas “**kwamba mtu kwa zama ya Mtume alikuwa akifanya biashara lakini alikuwa na udhaifu katika ‘aqd yake yaani akili yake. Basi watu wake walimuata Mtume na kusema: ‘Ewe Mtume, mzuie kutasarruf kwani hufanya biashara ilhali ana udhaifu katika akili yake.’** Mtume (SAW) akamwita na kumkanya na biasahra, lakini akasema: ‘**Ewe Mtume, sina subira ya kuwacha biashara.**’ **Basi (Mtume) akasema: ‘Ikiwa huwezi kuwacha biashara,**

sema ---- (*hawiha*) na hakuna udanganyifu (*khilaaba*).” Na Al-Bazzar amesimulia kutoka Anas kwamba Mtume (SAW) **alikuwa akikanya biashara ya --- (*mukhafalaat*)**. Na *khilaaba* ni kuhadaa. Hadithi hizi zaamrisha kuwacha *khilaaba* yaani kuhadaa, na kuhadaa ni haramu; kwa hivyo udanganyifu ni haramu. Isipokuwa udanganyifu wa haramu ni udanganyifu wa kupindukia kwani ‘*illa* ya kuhamisha udanganyifu ni kuwa ni kuhadaa katika bei; wala haitwi kuhadaa ikiwa ni kiwango kidogo kwani hiyo ni umahiri katika kusikizana bei. Bali huwa ni kuhadaa ikiwa ni ya kupindikua. Udanganyifu ikidhirika, mwenye kudanganywa ana khiyari; akipenda avunje mkataba au akipenda aitekeleze. Yaani kuhadaa kukidhahirika katika biashara, yamjuzu mwenye kuhadaiwa kurudisha bei na kuchukua bidhaa akiwa ni mwenye kuuza, au arudishe bidhaa na kuchukua bei akiwa ni mnunuzi; wala hawezi kuchukua fidia yaani kuchukua tofauti baina bei ya kweli ya bidhaa na bei ambao imeuziwa kwani Mtume amempa khiyari baina kuvunja biashara au kuikataa tu sio tofauti. Daraqutni amesimulia kwamba Muhammad bin Yahya bin Hibban alisema: Mtume (SAW) alisema: “**Ukinunua, sema: ‘Hakuna kuhadaa’ kisha una khiyari ya siku tatu kwa bidhaa ulionunua. Ukiridhia, imiliki na ukikasirika, irudishe kwa mwenywewe.**” Hino hudokeza ya kwamba mwenye kudanganywa ana khiyari, lakini hino khiyari huthibitishwa kwa shuruti mbili. Mwanzo, kutojua wakati wa biashara, na pili ni ziada au upungufu wa kupindukua ambao watu mfano wake hawangeli kubali wakati wa mkataba. Udanganyifu wa kupindukia ni ule ambao wanabiashara huuchukua kama udanganyifu wa kupindukua; wala haupimwi kuwa ni thuluthi au robo. Bali huachiwa wanabiashara wa eneo wakati wa kupita mkataba kwani hiyo hubadilika kwa tofauti ya bidhaa na soko.

KUFICHA AIBU (*at-tadlees*) KATIKA BIASHARA

Msingi katika biashara ni kufunga waliohusika. Pindi inapotimizwa kuomba na kukubaliwa baina muuzaji na mnunuzi, na hupita kikao cha biashara, mkataba wa biashara umewafunga na ni lazima waitekeleze. Lakini kwa sababu mkataba wa mua’amala ni lazima kutimizwa kwa sura

inaoondosha khasama baina watu, Shar'a imekanya watu kuficha aibu katika biashara na kuifanya dhambi sawa sawa iwe kutoka muuzaji au mnunuzi. Yote ni haramu kwani kuficha aibu huweza kufanya na muuzaji au mnunuzi. Maana ya *tadlees* katika biashara ni muuzaji kuficha aibu baada kuijua, au kuficha aibu ili kumfichia mnunuzi, au kuficha bidhaa hadi mnunuzi adhanie ni nzuri. Na *tadlees* kutoka mnunuzi katika bei ni kutumia pesa za urongo, au kuficha aibu katika pesa kwa kujua. Bei hutofautika kwa tofauti ya bidhaa kwa ajili ya *tadlees*, na mnunuzi huweza kuvutiwa na bidhaa kwa sababu ya *tadlees*. *Tadlees* kwa sura zake zote ni haramu kwa sababu ya yaliosimuliwa na Bukhari kumpitia Abu Huraira kwamba Mtume (SAW) alisema: “**Musifunge maziwa ya ngamia na mbuzi au kondoo. Na mwenye kununua huchagua bora ya khiyari mbili baada kukamua maziwa. Akipenda atamiliki au akipenda amrurdish pamoja na pishi ya tende.**” Na ibn Maja alisimulia kutoka Abu Huraira kwamba Mtume (SAW) alisema: “**Mwenye kununua mnyama ambae maziwa yange yamefungwa ana khiyari ya siku tatu. Na akimrudisha, airudish pamoja na pishi ya tenda, sio ---- (sumaraa)**”; maana yake ni kurudisha bei ya maziwa aliokamua. Na pia Al-Bazzar amesimulia kutoka Anas ya kwamba Mtume (SAW) **alikanya kuuza muhafalaat**. Hadithi hizi ni wazi katika kukanya kufunga maziwa ya ngamia na mbuzi au kondoo, na kukanya kuuza *muhafalaat* nao ni yule asikamuliwa hadi matiti yake yaonekana makubuwa au hudhaniwa hutoa maziwa mengi; kwani hino ni kuhadaa na kuhadaa ni haramu. Mfano wa hayo yote ni kuficha aibu kwani hayo yote ni *tadlees* ilioharamishwa sawa sawa ikiwa katika bidhaa au pesa kwani ni udanganyifu. Haimjuzu Mwislamu kudanganya katika bidhaa au pesa, bali ni lazima abainishe ukweli ya aibu yaliyomo katika bidaa au pesa. Haimjuzu kudanganya katika bidhaa ili aipigie debe au kuiiza kwa bei kubwa zaidi, wala kudanganya katika pesa ili ikubaliwa kama bei ya bidhaa kwani Mtume (SAW) ameikanya kwa kukatikiwa. Ibn Maja amesimulisa kutoka Uqba bin Amir kwamba Mtume (SAW) alisema: “**Mwislamu ni ndugu wa Mwislamu. Wala haimzuzu Mwislamu kumuuzia nduguye biashara ilio na aibu ila baada kumbainishia.**” Na Bukhari

amesimulia kutoka Hakeem bin Hazzaam kwamba Mtume (SAW): “**Upande mbili waliofanya biashara wana khiyari madamu hawatengana. Wakiwa ni wakweli na wemabainisha, watabarikiwa katika biashara yao. Lakini wakificha na kudanganya, baraka ya biashara yao hufutwa.**” Na Mtume (SAW) alisema: “**Mwenye kudanganya si mmoja wetu**” (Ibn Maja na Abu Dawud wameisimulia kumpitia Abu Huraira). Mwenye kuchukua kitu kupitia *tadlees* na udanganyifu, haimiliki kwani sio katika njia ya kumiliki bali ni katika mbinu iliockanywa kumiliki nayo. Nayo ni mali ya haramu na mali ya *suht*. Asema Mtume (SAW): “**Haitoingia Pepo nyama iliotokamana na suht, bali Moto ina haki zaidi nayo**” (Ahmed ameisimulia kumpitia Jabir bin Abdullah). *Tadlees* ikitokea sawa sawa katika bidhaa au pesa, mwenye kudanganywa ana khiyari; imma aifute mkataba au kuitekeleza. Wala hana khiyari nyengine. Mnunuzi akitaka kushika bidhaa yenye aibu au yenye udanganyifu na kuchukua fidia, yaani tofauti baina bei yake bila aibu na bei yake ikiwa na aibu, hana khiyari hiyo kwani Mtume (SAW) hakumjaalia fidia. Bali alikhiyarisha baina mambo mawili: “**Akitaka, aimiliki au akitaka airegeshe**” (Bukhari ameisimulia kumpitia Abu Huraira).

Si sharti ya kwamba muuzaji aijue *tadlees* au aibu ili kuthibitisha khiyari, bali khiyari humtukia mwenye kufanywa *tadlees* kwa mujaradi ya kutokea udanganyifu sawa sawa muuzaji alijua au hakuju. Hii ni kwa sababu hadithi ni jumla, na hakika ya biashara ni kuwa kumepita kilichokanywa; tofauti na *ghubun* ambayo hushurutishwa elimu juu ya udanganyifu wa kupindukia kwani ikiwa hakuju basi hakika yake ni kwamba hajakuwa mdanganyifu hadi mwenye kudanganya kuwa ni khiyari. Kwa mfano, lau bei la soko lishuke na muuzaji asijue kisha hubainika kwamba ameuza bidhaa kwa bei kubwa kuliko mfano wake, hino haitambuliwa kama udanganyifu wa kupindukua (*ghubun*) wala mnunuzi hana khiyari; kwani muuzaji hakuju bei imeshuka ili kuchukuliwa kama mdanganyifu wa kupindukia.

Ukiritimba (*ihtikaar*)

Ukiritimba hukanya wa kila njia, nayo ni haramu kiSheria kwani hadithi wazi zimekuja kuikanya. Saheeh Muslim amesimulia kutoka S'ad bin Musayyab kutoka Mu'ammar bin Abdullah Al-'Adawi kwamba Mtume (SAW) alisema: "**Hakuna mwenye kufanya ukiritimba ila mwenye kukosa.**" Na Al-Athram amesimulia kutoka Abu Umama aliesema: "**Mtume (SAW) amekanya mtu kufanya ukiritimba juu ya chakula.**" Na Muslim amesimulia kuititia msururu wake wa wasimulizi hadi S'ad bin Musayyab kwamba Mu'ammar alisema: Mtume (SAW) alisema: "**Mwenye kufanya ukiritimba ni mwenye kukosa.**" Kukanya katika hadithi huonyesha amri ya kuwacha, na kukemewa mwenye kufanya ukiritimba kwa kuwa ni mwenye kukosa—na mwenye kukosa ni mwenye dhambi, mwenye kuhalifu—ni dokezo lenye kudokeza kwamba amri ya kuwacha ni ya kumatikiwa. Ndipo hadithi hudokeza uharamu wa ukiritimba. Mwenye kufanya ukiritimba ni yule anaekusanya bidhaa akingojea kupanda bei ili aziuze kwa bei ghali hadi watu huwa na dhiki kununua. Amma kuwa mwenye kufanya ukiritimba ni mwenye kukusanya mali akingojea ziwe ghali, hiyo ni kwa sababu maana ya neno '*'hakara'*' kilugha ni ---- (*istabadda*); ndipo hupatikanwa kwamba ---- *istibdaad* ni kuzuia bidhaa ili ziuzwe kwa wingi, na *ku-ihtakara* kilugha ni kuzikusanya na kuzizua ukingojea ziwe ghali ili ziuzwe kwa wingi. Amma kwamba ni sharti ya ukiritimba kwamba zifike hadi huwa ni dhiki kwa wanunuzi kununua bidhaa iliofanywa ukiritimba, hino ni kwa sababu hakika ya *ihtikaar* haitokei ila katika hali hino. Lau haijakuwa dhiki kwa watu kununua bidhaa, haijatokea kukusanya bidhaa wala kufanya ---- (*istibdaad*) ili kuuzwa kwa wingi. Kwa hayo si sharti ya ukiritimba kununua bidhaa bali mujaradi ya kuzikusanya akingojea ziwe ghali ili aziuze kwa wingi huchukuliwa ni ukiritimba, sawa sawa amezikusanya kwa kununua au kutoka mazao ya ardhi yake kubwa kwa kuwa mpweke katika mazao haya, au uchache wa kupandwa; au amezikusanya kutoka mitambo yake ili kuwa mpweke katika usanii huu, au kwa kuwa usanii huu ni wa uchache kama ilivyo hali katika ukiritimba za kirasilimali. Kwani wao hufanya ukiritimba wa usanii wa kitu kwa

kuangamiza mitambo yote ila zao, kisha wao hutawala soko. Haya yote ni ukiritimba kwani hutukia ndani ya maana kilugha ya ukiritimba; ukiritimba ni kufunga bidhaa, au kutouza, akingojea kupanda bei na kuuza kwa wingi.

Ukiritimba ni haramu katika kila kitu pasina tofauti baina vyakula vya kibinadamu, vya mifugo, au yasiokuwa vyakula; sawa sawa ziwe ni dharura kwa watu au bidhaa vya kistarehe. Hino ni kwa sababu maana ya ukiritimba kilugha ni kukusanya kitu pasina vikwazo, wala haikuja kwa maana ya vyakula, au ngano au dharura za watu. Bali vitu vyote, wala haisihi kuihusisha kwa maana tofauti nay a kilugha. Na udhahiri wa hadithi iliokuja kuhusu ukiritimba hudokeza uharamu wa ukiritimba katika kila kitu, kwani hadithi hizi zilikuja kwa upanda pasina vikwazo, na jumla bila kuhusishwa, basi hubakia kwa upana na ujumla. Amma yaliokuja katika baadha ya riwaya ya ukiritimba iliosalitisha ukiritimba juu ya vyakula mfano hadithi: “**Mtume alikanya ukiritimba wa vyakula**” na riwaya nyengine, kutajwa chakula haihusishi ukiritimba na chakula. Wala haisemwi kwamba kukanya kulikuja pasina vikwazo katika riwaya kadha lakini ikafungwa na chakula katika riwaya nyengine, basi hadithi zisiofungwa hubuniwa juu ya zile ziliofungwa; hayo hayasemwi kwani neno “chakula” lililokuja kwa riwana haitoshi kufunga riwaya pasina vikwazo bali ni kutajwa mojawapo ya vitu vingi ambavyo havijafungwa. Hino ni kwa sababu kuvua hukmu kutoka yasiokuwa chakula itakuwa mfano wa mafhum ya jina (*mafhoum al-laqab*) lakini mafhum hino haifai kutendwa kazi; mfano wa haya haitoshi kufunga wala kuhusisha. Yaani kutajwa chakula katika baadhi za riwaya za ukiritimba ni kutaja sampuli mmoja ya ukiritimba kama mfano juu yake, wala sio kikwazo kufnga ukiritimba wala sifa yenye mafhum ambayo yawezwa kutendwa kazi. Bali chakula ni ‘jina gumu’ ya maana fulani, yaani ni neno (*laqab*) wala sio sifa basi mafhum yake haitendwi kazi. Kinachofaa kuwa ni kikwazo au cheye kuhusisha ni kilicho na mafhum inaotendwa kazi; hino haipo hapa. Basi hino hudokeza kwamba riwaya zilizokanya ukiritimba, hata zile zilizotaja chakula, ni hadithi pana na jumla zinazokusanya ukiritimba wa kila kitu kwa upana

wake. Uhakika wa ukiritimba ni kutawala soko, na kulazimisha watu bei anaotaka kwa kufanya ukiritimba bidhaa alizonazo hadi watu halazimishwa kuvinunua kutoka kwake kwa bei ghali kwa kumkosa mwengine anaeziuza. Mwenye kufanya ukiritimba hulenga kupandisha bei juu ya Waislamu na hino ni haramu kwani Ma'qal bin Yasir alisema: Mtume (SAW) alisema: “**Mwenye kuingilia bei za Waislamu ili kuwazidi nguvu, ni haki ya Allah kumketisha kwa mfuga ('udhm) la Moto Siku ya Qiyama.**”

Kupanga Bei (*at-tas'eer*)

Mola amejaalia mtu kuuza bei yake kwa bei anaoiridhia. Ibn Maja amesimulia kutoka Abu Said aliesema: Mtume (SAW) alisema: “**Biaшara ni kwa maridhiano.**” Lakini kwa sababu serikali yamkinika kupanga bei za watu, Allah aliiharamisha kuweka bei fulani na kulazimisha watu kuuza na kununua kwa mujibu yake; ndipo kupanga bei imekanywa.

Kupanga bei hutokea pindi sultan au manaibu wake, au mwenye kusimamia mambo ya Waislamu, huamrisha watu wa soko kutouza ila kwa bei maalumu pasina kuzidisha ili kuzuia bei kuwa ghali, au kwenda chini yake ili wasidhuru wengine yaani kuzuia kuzidi au kupunguza bei ilioamuliwa kwa ajili ya maslahi ya watu. Kama serikali kuingia katika bei na kupangia bidhaa, au baadhi za bidhaa, bei maalumu kisha kuzuia watu kuuza kwa bei iliozidi au kupungua bei ilioamuliwa kwa kuona hilo ni maslahi ya jamii. Uislamu umeharamisha kupanga bei kikamilifu kwani Imam Ahmad amesimulia kutoka Anas aliosema: “**Bei zilipanda katika zama ya Mtume (SAW) basi wakasema: ‘Ewe Mtume, lau ungelipanga bei?’ Yeye akasema: ‘Hakika Allah ni Muumba, Al-Qaabidh, Al-Baasit, Ar-Razzaaq, Al-Musa'ir nami naomba kukutana na Allah pasina mtu yoyote kudai nimemdhulumu katika damu au mali.’**” Na Abu Dawud amesimulia kutoka Abu Huraira aliesema: “**Mtu alikuja na kusema: ‘Ewe Mtume, panga bei.’ Akamjibu: ‘Bali ziwache.’ Kisha akaja mtu na kusema: ‘Ewe Mtume, panga bei.’ Naye akamjibu: ‘Bali Allah ndio mwenye kuteremsha na kupandisha.’**” Hadithi hizi hudokeza

uharamu wa kupanga bei, na kwamba hiyo ni dhulma anaoshtakiwa hakimu ili kuiondosha; na hakimu akipanga bei, atakuwa na dhambi mbele ya Allah kwani ametenda haramu. Kila raia aweza kumshtaki hakimu huyu aliepanga bei kwa Mahkama ya Madhalim sawa sawa awe ni Khalifa au wali, ili Mahkama ihukumu na kuondoa dhulma hino.

Uharamu wa kupanga bei ni jumla kwa bidhaa zote pasina tofauti baina ngano na yasiokuwa ngano kwani hadithi zilizokanya kupanga bei hazina vikwazo, na ni jumla; wala hakuna kilijokuja kuihusisha na ngano au yasiokuwa ngano. Kwa hayo, uharamu wa kupanga bei ni jumla inaokusanya kila kitu.

Hakika ya kupanga bei ni kwamba ni dhara kubwa inaodhuru Umma katika dhurufu zote, sawa sawa ikiwa ni hali ya vita au ya usalama kwani hufungua soko la kisiri ambao watu hutumia kununua bidhaa ziliofichwa mbali na usimamizi wa serikali; hili ndilo soko linaloitwa ‘soko nyeusi.’ Ndipo bei hupanda, na matajiri ndio wataweza kuzimiliki sio masikini. Na pia kupanga bei huathiri kuzitumia na kuzizalisha, na huenda kusababisha janga la kiuchumi. Juu ya haya yote, watu ni wenyewe nguvu juu ya mali zao kwani kumiliki kwao humaanisha kwamba wana nguvu juu yake ilhali kupanga bei huwafunga mikono; na hino haijuzu ila kwa nasi ya kisheria, na hapa haikuja. Kwa hayo haijuzu kuwafungia watu mikono kwa kuweka bei maalumu ya bidhaa zao kisha kuwazuia kuizidi au kuipunguza. Amma yanaotokea ya kupanga bei katika zama za vita au misukosuko ya kisiasa, hino hutokea imma kwa sababu ya bidhaa kupotea sokoni kwa sababu ya ukiritimba au kwa sababu ya uchache wake. Ikiwa upungufu hutokamana na ukiritimba, Allah ameihamisha; na ikiwa ni kwa sababu ya uchache wake, Khalifa ameamrishwa chunga maslahi ya watu basi ni jukumu lake kuileta sokoni kwa kuileta kutoka pahala pake. Na kwa hayo atakuwa amezuia kupanda bei. **Katika mwaka wa ukamwe ilioitwa ‘mwaka wa --- (ramaada) pindi Hijaz tu iliposibowi na ukamwe kwa upungufu wa chakula mwaka huo hadi bei zilipanda juu kwa uchache wa chakula, Umar**

bin Al-Khattab hakupanga bei maalumu za vyakula bali aliamrisha kuletwa chakula kutoka Misri na As-Sham kufikia Hijaz: basi bei zikateremka pasina haja kupanga bei.